Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 22 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo. Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**:

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**:-

Randama za Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 86

**Kuhusu Soko la Wamachinga Dar es Salaam**

**MHE. MOHAMMED ALI SAID** aliuliza:-

Soko la Wamachinga lililopo Ilala Jijini Dar es Salaam lilitegemewa liwe limefunguliwa ndani ya mwaka 2009:-

Je, ni sababu ipi iliyokwamisha kufunguliwa na kuanza kufanya kazi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kukwama kufunguliwa kwa soko la Wamachinga Jijini Dar es Salaam kumetokana na kuchelewa kukamilika kwa ujenzi. Ujenzi wa soko hilo ulikuwa ukamilike na kukabidhiwa tangu Septemba, 2008 sababu ya kuchelewa kukamilika kwa ujenzi huo ni mabadiliko katika ubunifu wa mradi ambapo awali ilikusudiwa jengo liwe na ghorofa tatu.

Wakati Mkandarasi akiwa ameanza kazi ya kuchimba msingi, wadau mbalimbali walijenga hoja kwamba kuongezwe ghorofa katika jengo hilo hadi kufikia ghorofa tano.

Baada ya kukubaliana kuongeza idadi ya ghorofa ili jengo liwe na uwezo wa kuchukua wafanya biashara wengi zaidi iliazimu kufanya upya usanifu wa jengo na hivyo kuchelewesha kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mkandarasi kukamilisha ujenzi hatimaye jengo lilikabidhiwa rasmi kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tarehe 21 Me, 2010 tayari kwa matumizi. Kwa sasa Halmashauri ya Jiji inakamilisha matengenezo ya vizimba na kazi hiyo ikikamilishwa soko litafunguliwa na wafanyabiashara wataanza kazi rasmi katika jengo hilo.

Na. 87

**Hitaji la Magari Mawili ya Kubebea Wagonjwa –Sengerema**

**MHE. ERNEST G. MABINA (K.n.y. MHE. SAMUEL M. CHITALILO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Sengerema ina wakazi wengi na Majimbo mawili (Sengerema na Buchosa) lakini kuna gari moja tu la kubebea wagonjwa ambalo halitatoshelezi kuhudumia wakazi wote:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Wilaya ya Sengerema magari mawili zaidi ya kubebea wagonjwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MISTAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samuel Mchele Chitatilo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ina eneo la mraba lipatalo kilomita 8,817 na ina vituo vya tiba 60 ikiwemo Hospitali teule moja inayomilikuwa na Jimbo la Katoliki la Geita. Kati ya vituo hivyo vituo vya avya ni 8 na zahanati 51 na Halmashauri ina wakazi wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 600,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema haikuwa na gari maalum la kubebea wagonjwa tokea miaka ya nyuma. Huduma hii imekuwa ikitolewa magari ya kawaida mfano *Landcruiser Hard top* lililokuwa limetolewa na Shirika la *Oxfarm* kwa ajili ya huduma ya Mama na Mtoto. Mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema katika bajeti yake ilitenga shilingi milioni 84.0 kwa ajili ya kununua gari maalum la kubebea wagonjwa na liliweza kununuliwa mwezi Novemba 2008.

Gari hili lilitumika hadi tarehe 12 Juni, 2009 wakati lilipopinduka likifuata mgonjwa na kuharibika kabisa. Kwa kuwa lilikuwa limekatiwa Bima (*Comprehensice*) kutoka Shirika la Bima la Taifa, mchakato ulianza kwa kuwasiliana na Shirika la Bima na mazungumzo yanaendelea ili kupata gari lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Idara ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inayo magari mawili ambapo kati ya hayo moja linatumika kutoa huduma ya mama na mtoto na vilevile linatumika kabeba wagonjwa (*ambulance*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema iendelee kutoa kipaumbele kwa suala hili la ununuzi wa magari ya wagonjwa na kutenga fedha katika bajeti yake. Hilo ni jukumu la msingi la msingi la Halmashauri husika.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo lililoko Sengerema ni

sawasawa kabisa na tatizo lililoko Geita. je, Serikali inasemaje kuvipa gari la wagonjwa vituo vya afya vya Kasamwa, Nzera, Katoro na Geita kwenyewe?

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, atoe magari Sengerema aache Buchosa? Mheshimiwa Waziri majibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu nilisema kwamba tutanunua magari ya wagonjwa yapatayo 50 lakini kipaumbele kitakuwa kwa Wilaya mpya, Wilaya ambazo hazina kabisa gari ya kubebewa wagonjwa na Wilaya zile ambazo ziko pembezoni. Kwa hiyo, kipaumbele kitakuwa zaidi ya huko kuliko Mikoa au Wilaya ambazo ziko katika hali ambayo si ya pembezoni.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Tatizo la Buchosa ni sawasawa na Mwibara na uzuri ni kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba atatoa kipaumbele kwa Majimbo yale ya pembezoni na Jimbo la Mwibara liko pembezoni. Je, anatoa ahadi gani kwa ajili ya Jimbo la Mwibara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla ya Bunge lako kwisha nilete ile orodha ya Wilaya ambazo zitagawiwa magari hayo ili tuweze wote kuiona na tujue kwamba ni Halmashauri gani itapata magari hayo.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na mimi nina swali moja la nyongeza. Tatizo la magari ya kubebea wagonjwa ni tatizo lililopo katika nchi nzima kwa ujumla na kwa kuwa amesema ataleta orodha itakayoonesha magari yatakayosambazwa katika Wilaya lakini katika orodha hiyo nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie katika Wilaya ya Bagamoyo ina Majimbo mawili Chalinze na Bagamoyo. Gari ya wagonjwa itakayokuwepo katika Wilaya ya Bagamoyo kwa maana ya Makao Makuu ya Wilaya ni umbali wa kilomita kama 180 kati ya Bagamoyo na Chalinze. Je, wale wagonjwa watakaokuwa wanapata matatizo kwa ajili kusafirishwa Tumbi kuna uwezekano wa kupata gari lingine ambayo itakaa katika Jimbo la Chalinze?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu. Hiyo orodha italeta fitna tu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukishanunua yale magari tunapeleka katika Halamshauri mbalimbali, Halmashauri hizo ndizo zinazopanga kwamba ni kituo gani cha afya kiko pembezoni zaidi na tumefanya hivi kwa miaka yote na baadhi ya Halmashauri imefanya hivyo. Nimeshuhudia kwa Chamwino tuliwapa gari lakini wamepeleka kwenye kituo cha afya ambacho kiko pembezoni kabisa mwa

Chamwino. Kwa hiyo, ni Halmashauri yenyewe ndiyo itakayoamua kwamba gari hilo lipelekwe katika kituo gani cha afya.

Na. 88

**Matukio ya uhalifu kuongezeka – Mbozi Magharibi**

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME** aliuliza:-

Kwa kuwa matukio ya ujambazi, ghasia, mauaji na upotevu wa mali za watu kwenye Kata za Tunduma, Kapele, Nkangamo na Ndalambo zilizopo mpakani mwa nchi ya Zambia katika Jimbo la Mbozi Magharibi yanazidi kuongezeka kila siku, na kwa kuwa kutokana na uchache wa askari Polisi, uhaba wa vitendea kazi na ukosefu wa gari, askari Pollisi huchukua muda mrefu kufika au mara nyingine kutofika kabisa kwenye maeneo ya tukio na kufanya tatizo hilo kuwa kubwa kila siku:-

Je, Serikali itachukua hatua gani za dharura ili kupunguza matukio hayo ya uhalifu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dk. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zinazolikabili Jeshi la Polisi Wilayani Mbozi zikiwemo uchache wa askari na uhaba wa vitendea kazi, hali ya uhalifu katika Wilaya hiyo si ya kutisha ikilinganishwa na Wilaya nyingine za Mkoa wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla.

Aidha, takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba kutokana na kuimarika kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na wananchi, matukio ya uhalifu kutoka Wilaya hiyo yamekuwa yakipungua kwa miaka mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiendelea kutatua tatizo la usafiri katika vituo vya Polisi kadri Bajeti inavyoruhusu. Kwa sasa Kituo cha Tunduma kina gari moja(1) aina la *Land Cruiser Pick up* pamoja na pikipiki tano. Aidha, kituo cha Kamsamba kina pikipiki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya vyombo vya usafiri vituo huongezewa nguvu kwa gari la OCD Mbozi pamoja na pikipiki zilizopo Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wilaya ya Mbozi itaongezwa askari wapya wanaohudhuria mafunzo CCP Moshi pamoja na gari moja kwa ajili ya kuimarisha ulinzi.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Lakini kabla ya hapo naomba tena nichukue fursa hii kuwaelezea wale wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi ambao hadi jana walikuwa bado wananipigia simu za kuuliza kama kweli wamepata Wilaya.

Napenda niwathibitishie kwamba tumepata Wilaya na inaitwa Momba na kwa hali hiyo naomba kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi tushirikiane nao miaka mitano ijayo ili tuweze kuijenga Wilaya mpya ya Momba.

**NAIBU SPIKA:** Sasa mbona unatumia zaidi muda wako?

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kuleta hiyo *pick-up* moja hivi karibuni. Pia niwashukuru wafanyabiashara wa muji mdogo wa Tunduma kwa kuchangia hizo pikipiki tano ambazo zinasemwa ziko pale ambazo nami nilishiriki katika mchango huo. Kwa vile Wilaya ya Mbozi imegawanywa kuwa na Wilaya mbili.

**NAIBU SPIKA:** Unatoa hotuba sasa.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Je, hawa Askari watakaokuja wengine watapelekwa kwenye hiyo Wilaya mpya?

**NAIBU SPIKA:** Sasa msipongezane katika muda wa maswali na majibu. Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli hata sisi tuliwapongeza wafanyabiashara kwa mchango wao mkubwa walioutoa kwa zile pikipiki tano hilo ni jambo ambalo tunalitambua.

Pili nizipokee shukrani zake kwa kazi ambazo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inafanya na tatu hapana shaka kwa kuwa hii ni Wilaya mpya lazima katika hawa askari ambao watakuwa wamefuzu mafunzo yao kutoka Moshi Wilaya hii mpya itapata askari.

**NAIBU SPIKA:** Sasa kuna Wilaya mbili, Mheshimiwa Zambi, utasema mbona wenzangu watapata gari mimi je.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa swali moja la nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Lakini Wilaya ya Mbozi ni moja ya Wilaya kubwa katika nchi hii kwa sababu ina kilomita za mraba karibu 9,000. Lakini tatizo tulilonalo ni vifaa vya kufanyia kazi kwa askari hawa.

Pamoja na *commitment* ya Serikali kwamba itaongeza vifaa hivyo, inaweza ikawahakikishia wananchi wa Wilaya ya Mbozi kwa ujumla kwamba vifaa hivyo hasa pikipiki na magari vitaongezwa ili tuweze kukabiliana na hali ya ujambazi ambayo Mheshimiwa Waziri anasema siyo kubwa wakati sisi tunayotoka maeneo ya Mbozi tunajua kwamba Wilaya ya Mbozi ina matukio mengi ya Ujambazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara yangu inakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi.

Lakini hiyo hajawa sababu ya kwamba suala la ulinzi wa taifa letu limekuwa ni tatizo kubwa.

Tumekuwa tunajitahidi kadri tuwezavyo. Nataka nimhakikishie kwamba katika vifaa ambavyo tumeomba katika Bajeti hii hapana shaka tutafanya kila jitihada tuhakikishe kwamba hata Wilaya ya Mbozi inapata katika vifaa hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Benson Mpesya, atauliza swali hilo, au kwa niaba yake Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale

Na. 89

**Mbolea ya Ruzuku**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. BENSON MWAILUGULA MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kutoa mbolea ya ruzuku katika azma ya kuimarisha kaulimbiu ya kilimo kwanza katika Mkoa wa Mbeya:-

(a) Je, Serikali inajua kwamba baadhi ya mifuko ya mbolea ilikuwa pungufu kwa ujazo wa kilogramu kumi hadi kumi na mbili?

(b) Je, Kata ya Isanga iliyoko Mbeya Mjini ilipewa mifuko mingapi ya mbolea ya kupandia *(DAP)?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mawilugula Mpesya , Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tulizonazo ni kwamba Halmashauri ya Jiji la Mbeya haijapokea malalamiko yoyote kuhusu upungufu wa wa ujazo wa mifuko kutoka Kata zilizogawiwa vocha ya pembejeo yaani mbolea ya kupandia na kukuzia. Hivyo Wizara yangu inapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hili tutalifanyia kazi kwa nia ya kujiridhisha na pia kuhakikisha tatizo hili kama lipo halitokei tena.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Isanga ni miongoni mwa Kata zilizopaswa kunufaika na ruzuku ya pembejeo (2009/2010) kamati ya vocha ya Jiji la Mbeya iliipangia Kata ya Isanga kaya 12 kupata ruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha ambazo ni sawa na ekari 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kamati ya Maendeleo ya Kata ya Isanga iliamua vocha hizo zisigawiwe kwa wakulima kwasababu zilikuwa chache ikilinganishwa na mahitaji. Wizara yangu ingependa kuchukua fursa hii kueleza kwamba, mahitaji ya pembejeo za ruzuku ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali. Na tunashauri kwamba, wale wote wanaopata fursa ya kupata pembejeo hizo bila kujali idadi wazitumie ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya chakula.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:**Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu zuri lakini pia nilikuwa naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, mbolea hii imethibitishwa kwamba ilikuwa ni pungufu ni hatua gani Serikali imechukua kuwawajibisha wale waliosababisha mbolea iwe pungufu?

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba hakuna taarifa zozote

ambazo zimethibitishwa kuwa kuna mifuko ambayo ilikuwa imepungua. Lakini pia nimesema kwamba Wizara itahakikisha kwamba kama matukio hayo yapo basi hayatokei tena lakini kwa sasa hivi hatuna taarifa na hata Halmashauri ya Jiji la Mbeya halina taarifa hiyo.

Na. 90

**Upungufu wa Chakula Nchini**

**MHE. MARIAMU REUBEN KASEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu ina upungufu mkubwa wa chakula:-

Je, Serikali imejiandaa vipi kutatua tatizo hilo pale Wananchi watakapohitaji msaada wa chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mbunge wa viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula nchini kwa sasa ni nzuri kutokana na mvua nzuri zilizonyesha katika msimu wa 2009/2010.

Hata hivyo, mwaka 2008/2009 kulitokea hali ya upungufu wa nafaka uliofikia takribani tani 860,000 kutokana na ukame katika msimu wa uzalishaji wa 2007/2008.

Maeneo yaliyoathirika zaidi na ukame na upungufu wa chakula ni ya Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara pamoja na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa chakula nchini kama ifuatavyo:-

1. Kutenga mahindi kutoka wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa ( NFRA) ambayo yaliuzwa katika soko la kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya chakula.

2. Kutoa chakula cha msaada kwa watu walioathirika na upungufu wa chakula kwa kugawia bure au kuwauzia kwa bei nafuu ya shilingi hamsini kwa kilo.

3. Kuondoa kodi kwa waingizaji /waagizaji wa mahindi kutoka nje ya nchi ili kuhamasisha wafanyabiashara kuingiza mahindi nchini kwa lengo la kupunguza pengo la upungufu.

4. Serikali ilisitisha mauzo ya mazao ya chakula nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa chakula na kupunguza kasi ya kupanda kwa bei ya vyakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa hali ya chakula, unaohusu kutathimini na kutoa taarifa za uzalishaji wa mazao ya chakula na upatikanaji wa chakula.

Inapobainika kuwa kuna maeneo ya wananchi yenye upungufu wa chakula kutokana na na ukame au dharula nyingine, Serikali kupitia Kamati ya Taifa ya Uratibu wa Maafa *(TANDREC)* huchukua hatua muafaka kukabiliana na hali hiyo.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE**:Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Masasi na Nanyumbu kumekuwa na upungufu wa chakula wa mara kwa mara ambao unatokana na upungufu wa mvua ambao tunaupata.

Je, ni lini Serikali itapeleka miundombinu ya umwagiliaji katika bonde la mto Ruvuma kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi ili kuwawezesha wananchi hawa waweze kushiriki katika shughuli za kilimo kinachohusu umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili:Pamoja na mvua za kutosha tulizipata msimu huu kwa nchi nzima lakini yapo maeneo ambayo kumetokea mafuriko.

Je, Serikali hadi sasa imeshafanya tathimini katika maeneo hayo ili kuweza kuwasaidia wananchi hawa ambao mazao yao yameweza kusombwa na maji ahsante .

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Chakula na Umwagiliaji ni kama wako pamoja Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali hili kwa kasi zaidi, nguvu zaidi na ari zaidi kwa Mheshimiwa Kasembe kama ifuatavyo:-

Kama kawaida Serikali inatenga pesa za *DADPS* kwa ajili ya umwagiliaji kwenye *schemes* ndogo ndogo kwa hiyo, ninamshauri Mheshimiwa Kasembe aweze kushauriana na Halmashauri yake kuhusiana na kutenga fedha na kuhamasisha wananchi katika kuibua miradi midogomidogo ya umwagiliaji ili waweze kupunguza tatizo hili la umwagiliaji katika eneo hilo. Lakini pia Serikali ina *programme* mbalimbali katika ngazi za Taifa ambapo zinaweza zikaelezewa vizuri na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ambayo ina kidhi mahitaji hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tathimini hili limesahafanyika katika maeneo ambayo yalipata mafuriko na ndiyo maana kama mnakumbuka Serikali imekuwa

ikipeleka vyakula pamoja na misaada mingine katika maeneo yaliyoathirika hususani maeneo ya Kilosa, Same na maeneo kama hayo ya Masasi.

**MHE.GEORGRE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali hili miongoni mwa Mikoa iliyopatwa na ukame mkubwa na kuwa na njaa kubwa hakuitaja Dodoma.

Lakini nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwa kwa kipindi cha mwaka jana imetoa chakula kingi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma na tunaamini kabisa katika hali iliyojitokeza mwaka huu kwa sababu hali ni mbaya zaidi kuliko hiyo ya mwaka jana Serikali itaingiza katika takwimu Mkoa wa Dodoma kwamba na wenyewe ulikuwa na ukame na bado unaendelea na ukame zaidi ya ule wa mwaka jana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama Serikali tunapokea shukrani zake kwamba Mkoa wa Dodoma ulipata chakula kingi zaidi.

Niseme tu kuwa siyo Mkoa wa Dodoma ni kwamba Serikali imejitahidi kupeleka chakula nchi nzima kwenye maeneo ambayo yalikuwa na upungufu wa chakula na eneo lake alilosema kwamba mwaka jana kulikuwa na upungufu wa chakula niseme kwamba kunapotokea upungufu wa chakula katika maeneo yote tuna hakikisha kwamba chakula kile kinakwenda katika maeneo hayo, labda nikiri tu kuwa sikusikia sehemu ya pili vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Kasema kuwa mwaka huu una hali mbaya sana. Je, mtaweka tena chakula huko kwenye orodha mtawaingiza?Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Maafa**.**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, Ushirika na Masoko napenda nimuarifu Mheshimiwa Simbachawene kwamba kwa sasa tathimini ya hali halisi ya chakula nchi nzima inafanyika.

Taarifa ya mwisho itatoka baadaye mwezi Julai ili kuona maeneo gani yana uhaba wa chakula iwapo Mkoa wa Dodoma utaonekana kuwa una uhaba wa chakula basi kama tulivyofanya mwaka jana tutatenga chakula cha kutosha kwa ajili ya wananchi wenye upungufu wa chakula.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kuniapa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Tarafa ya Ngorongoro ambayo pia ni hifadhi ambapo kilimo cha aina yoyote hakiruhusiwi na mwaka jana wakati wa ukame mifugo ilikuwa kwa zaidi ya 100% na ni mifugo ambayo inategemewa na hawa wafugaji. Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kusaidia Tarafa hiyo kwa upande wa chakula kuhusiana na njaa iliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa wananchi ambao wana njaa nchini wanapatiwa chakula kwa *category* ya kusema kwamba wale ambao hawana uwezo kabisa watapatiwa chakula cha bure.

Lakini wale wenye uwezo kidogo basi watapatiwa chakula cha shilingi 50/= kwa kilo kwa maana hiyo sisi kama Serikali tutahakikisha kwamba wataalam kama hawajafika kwenye Jimbo lako Mheshimiwa Watafika ili waweze kufanya tathimini pamoja na Halmashauri ya Wilaya yako ili waweze kujua ni idadi ya watu wangapi ambao wana upungufu wa chakula kusudu hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba tathimini kubwa inafanyika kusudi maeneo yote nchini ambayo yana matatizo kama haya basi yaweze kusaidiwa chakula.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango wa stakabadhi ya mazao ghalani unafaa sana kuokoa wananchi pale wanapokumbwa na njaa na kwa kuwa Serikali mpango huo imeanzisha kwa baadhi ya maeneo.

Je, haioni kwamba kuna kila sababu ya kuanzisha mpango huu kwa nchi nzima ili iwe kimbilio kwa wananchi wanapo kumbwa na njaa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba stakabadhi za mazao ghalani zinasaidia sana hasa katika uhifadhi wa chakula na mazao mengine kusudi chakula kile kiweze kutumika wakati wa njaa ama kiweze kuuzwa na kuweza kama ni mazao ya biashara basi yaweze kuuzwa na kuwapatia wakulima bei zaidi.

Nadhani suala hili ni suala linaloweza kufanywa kwenye ngazi ya Mkoa yaani utawala wa Mkoa pamoja na Halmashauri za Mkoa ule na kuona umuhimu wa kuweka stakabadhi za mazao ghalani kwa mazao yale ambayo wataona kwamba yanafaa na yale ambayo yamesha idhinishwa na Serikali kwamba haya yanafaa kuwekwa katika huo mfumo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sasa tunaendelea na Wizara ya Miundombinu na sasa na Mheshimiwa Omari Shaaban Kwaangw' atauliza swali hilo.

Na. 91

**Ujenzi wa Barabara ya Dodoma- Babati**

**MHE. OMARI S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wakala wa barabara *TANROADS* Makao Makuu walitangaza Tenda Na. AE/001/2009- 10/HQ/W/61 inayohusu kujenga barabara ya Dodoma- Babati (km

258) kwa kiwango cha lami-loti 2; sehemu ya Bonga-Babati na sehemu ya kuunganisha Kondoa ( *Kondoa access road*) kwa jumla ya km 19.2:-

(a) Je, ni hatua gani ya ujenzi imefikiwa hadi sasa tangu kutolewa kwa tangazo?

(b) Je, sehemu Bonga- Babati ni kilomita ngapi kati ya jumla ya kilomita 19.2?

(c) Je, mradi huo utagharimu fedha kiasi gani na unatazamiwa kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunikaribisha hapa Bungeni nilikuwa safarini Kigoma na Rukwa nimerudi salama.Kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Shabani Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa ujenzi wa barabara ya Dodoma- Babati km.258) kwa kiwango cha lami umepangwa kutekelezwa kwa sehemu mbili kwa kuanzia. Ambazo ni Dodoma-Mayamaya (km.44), Babati- Bonga (km.19) na daraja la Kolo. Maandalizi ya ujenzi wake yapo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo.

Kwa sehemu ya Babati, Bonga mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 20 Mei, 2010 kati ya *TANROADS* na Mkandarasi aitwaye *China Henan International Cooperation Group Co. Ltd. (CHICO)*. Mikataba ya sehemu zilizobaki inatarajiwa kusainiwa baada ya kukamisha taratibu za manunuzi mwisho wa mwezi Juni 2010.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya kilomita 19.2 zilizoainishwa katika Loti Na. 2 iliyotangazwa, kilomita 16.2 ni za kutoka Babati hadi Bonga na kilomita 3 zilizobaki ni za kuunganisha mji wa Kondoa *(Kondoa Access Road).*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama halisi ya mradi na muda wa ujenzi vitajulikana baada ya mikataba ya ujenzi wa sehemu zote zilizotangazwa kutiwa saini.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika ninakushukuriu kwa kunipa nafasi naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niseme kwamba hili la kuwekwa *sign* kwa mkataba wa kati ya barabara ya Bonga na Babati ni faraja kwa wananchi wa babati lakini naomba niulize kwamba sasa baada ya mkataba huu kusainiwa mwezi mei, 2010. Je, ujenzi hasa unatazamiwa kuanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Babati tulipata tatizo la mkandarasi kufukuzwa Kampuni ya *WESSON* ilifukuzwa kujenga barabara ya Singe kwenda mpaka Kiteto na Olkesmeti sasa Mkandarasi huyo ambaye ameteuliwa *Chiko Company* ningependa kufahamu kwamba ana sifa na uzoefu gani ili na yeye asije akafukuzwa kama ilivyofukuzwa kampuni *WESSON* iliyoshindwa kujenga barabara ya Babati kwenda Kiteto na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Kwaangw' kwa kutambua juhudi za Serikali mpaka hapa tulipofikia kuhusu ujenzi wa barabara hii na niahidi tu kwamba kasi ya Serikali itaendelea kwa nguvu zaidi.

Kuhusu kuwa ujenzi utaanza lini kama nilivyosema kwamba Mkataba ulisainiwa tarehe 20 mwezi mei hivi sasa mkandarasi ina wezekana akawa kwenye hatua za mobilizationa lakini niseme tu kwamba mkandarasi huyu Chiko ambaye ameteuliwa ni yuleyule ambaye anajenga ile barabara ya kutoka Babati kuelekea Singida. Kwa hiyo, nadhani mitambo yake iko kulekule anaweza kuanza wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu sifa zake niendeleze tu haya amabayo nimesema. Kwamba makanadarasi huyu sasa hivi ndiye anayejenga barabara nyingi hapa nchi ikiwemo hiyo ya kutoka Babati kwenda Singida.

Kwa hiyo, ana uzoefu mzuri hatutegemei kwamba anaweza kufukuzwa kama yule wa mwanzo aliyefukuzwa ambaye kwa matatizo ya kutokuwa na uzoefu mzuri ilisababisha afukuzwe, lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Kwaang' kwamba makandarasi huyu ana uzoefu wa kutosha. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM SALUM FAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza na mimi niipongeze Serikali kwa jinsi ilivyokubali na kujitahidi kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara hii ya kutoka Dodoma kwenda Babati.

Swali langu ni dogo tu kwamba, ni muda mrefu toka Serikali imeanza kutoa majibu kwamba Mkandarasi amepatikana na kwamba mkandarasi huyu ataanza kazi wakati wowote na sasa ni zaidi ya miezi 3 au 4.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ni kuwa huo Mkataba huwa hauna utaratibu wa kuonyesha kuwa baada ya mkandarasi kutia *sign* na kukubaliana na Serikali inachukua muda gani ili aweze kuanza kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kutambua juhudi za Serikali kama nilivyosema

kwamba barabara hii hapa tulipofikia ni pazuri, na niseme tu huyu Mkandarasi ambaye Mkataba umetiwa sahihi juzi kama nilivyosema kwamba yupo *site* sasa hivi katika maeneo yale yale anaweza kuanza wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba katika kuingia mkataba na kuwekeana sahihi na Mkandarasi muda unaainishwa kabisa. Kwamba ni kipindi cha muda fulani ili kazi iweze kukamilika, kwa hiyo kinachoangaliwa ni kama atakamilisha katika muda ule unaooneshwa katika mkataba, ndiyo maana Serikali imeweka wasimamizi katika miradi yote ya ujenzi ili kuweza kufuatilia muda ambao tumekubaliana.

Na. 92

**Usafiri wa Ndege - Iringa**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI (K.n.y. MHE. STEPHEN J. GALINOMA)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali Na. 288 ilisema kuwa, huduma za usafiri wa ndege haziwezi kupelekwa Iringa kwa kuwa hakuna biashara; lakini pamoja na ukweli huo, wananchi wa Iringa hawawezi kushabikia biashara ambayo haipo na nina uhakika kwamba mara ikijulikana na kutangazwa kuwepo kwa usafiri huo, wafanyabiashara na watu wengi toka sehemu mbalimbali za Mkoa wa Iringa wataanza kuitumia huduma hiyo:-

Je, kwa nini Iringa isiunganishwe na njia nyingine za aina za anga kama vile Mbeya, Sumbawanga, Songoea na Miji Mingine ya Kusini kwa lengo la kuimarisha biashara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge la kuunganisha njia ya usafiri wa anga kati ya Iringa na Miji mingine kama vile Mbeya, Sumbawanga na Songea kwa lengo la kupata abiria na mizigo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali Namba 288 katika Mkutano wa Kumi na Mbili, changamoto kubwa ya kiwanja cha ndege cha Nduli, ni ukosefu wa abiria na mizigo ya kutosha ya kuvutia makampuni yanayofanya biashara ya usafiri wa anga, hapa nchini yaweze kupeleka huduma kwenye kiwanja hicho.

Kwa kuzingatia uimara na ubora wa Kiwanja cha Ndege cha Nduli na umuhimu kuunganisha Mji wa Iringa na Miji mingine kwa njia ya anga, Wizara na Serikali kwa

ujumla itaendelea kuyashawishi makampuni ya ndege kuangalia uwezekano wa kuunganisha njia ya Iringa na Miji mingine kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, Naibu Waziri amekuwa akijibu swali akitoa hoja kwamba hakuna biashara, Je, haoni kuwa kwa kujengwa kwa kiwanja cha Kimataifa cha Songwe Mbeya kinaipa umuhimu sana kiwanja cha Iringa ili kuunganisha biashara zake kwa sababu na njia ya ndege itakuwa ni njia hiyo, kuwarahisishia wafanyabiashara kuunganisha kwenda Mbeya na kwenda nchi zingine;

Je, anakiri hilo na mpango wake ukoje ili kukamilisha lengo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe ukimalizika hii rai aliyoitoa itajenga hoja zaidi. Lakini niseme kwamba hivi sasa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Songwe unakaribia kumalizika na kiwanja hicho kitakapokamilika kitakuwa na miundombinu ya kisasa na huduma za mafuta na hivyo kurahisisha usafiri wa anga kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na rai yake tunaizingatia.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza;

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, je atakubaliana na ushauri kwamba katika kulitazama soko la Iringa la usafiri wa anga, sasa alitazame upya kutokana na Mji wa Iringa kuwa na Vyuo Vikuu vitatu, Chuo Kikuu cha Mkwawa, Chuo kikuu cha RUCO na chuo Kikuu cha Tumaini, kwa hiyo usafiri wa wanaohusika na Vyuo Vikuu kuna uwezekano mkubwa sana wa safari ya anga inayounganisha siyo tu Irinmga na Mbeya lakini pia Iringa na Dodoma ambapo pia pana mahitaji ya usafiri unaohitajika kwa ajili ya huduma ya Vyuo Vikuu hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ndiyo maana tulisema kwamba katika kuhamasisha hawa wafanyabiashara wa anga au safari za ndege, misingi yote hiyo aliyoieleza itazingatiwa.

Kwa hiyo, nataka nikubaliane naye kwamba tutautazama wakati tunafanya hamasa hiyo.

Na. 93

**Huduma ya Kusafirisha Mizigo Midogo kwa Treni**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kabla ya kukodishwa kwa *TRC (TRL)* huduma ya kusafirisha mizigo midogo midogo parcel za abiria kwa kuunganisha behewa moja kati ya breki na behewa la kawaida ilikuwa haijasitishwa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuondoa behewa hilo ni kuongeza usumbufu kwa watumiaji wa huduma hiyo kati ya Tabora-Kigoma –Mpanda kusafirisha mizigo hiyo ya kawaida?

(b) Je, ni lini itarejesha huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya kupakia mizigo midogo midogo ya abiria kwenye behewa maalum (*Brake Van Boogie*) haikusikitishwa wakati wa ubinafsishaji wa *TRC*. Hali halisi ni kwamba hata kabla ya *TRC* haijakabidhiwa kwa mkodishwaji, mabehewa haya maalum yalikuwa machache. Hivi sasa kuna jumla ya mabehewa saba ya aina hii ambayo hayakidhi mahitaji halisi ya abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichokuwa kikifanyika wakati wa *TRC* ambacho kinafanyika sasa hivi na *TRL* ni kwamba, abiria hushauriwa kukusanya mizigo yao midogo midogo (*parcel consolidation)* na kuipakia katika behewa la kawaida la mizigo kisha behewa hilo hufungwa katika treni hiyo hiyo ya abiria ambayo msafiri husika husafiria. Hii humwezesha abiria kuchukua mizigo yake anapofika mwisho wa safari yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabehewa haya maalum kwa ajili hiyo, yatanunuliwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Hivi sasa, abiria wanashauriwa kupeleka mizigo yao mapema kwenye stesheni husika ili iweze kupakiwa mapema kwenye mabehewa ya mizigo na hatimaye mizigo yao ipakiwe kwenye treni watakazosafiria.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kurudisha usafiri wa reli ya kati ambayo ilikuwa ni kero kubwa sana. (*Makofi*)

Kwa kuwa, mimi ndiye ninayeitumia pamoja na watu wa Kanda hiyo tunaitumia reli kwa muda mrefu na kuona hali halisi sina sababu ya kushindana na Naibu Waziri pamoja na majibu yake mazuri.

Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kwamba wakodishaji hao huduma zote ambazo walikuwa wamezisisha kama vile magenge ya wasimamizi wa reli ambao vituo vyao vimefungwa. Je, iko tayari kuhakikisha kwamba Chuo cha Tabora cha Reli kinarudishwa ambapo wakodishaji hao wamesitisha huduma ya kuendesha Chuo Hicho?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme tu kwamba hawa wakodishaji anaowasema hivi sasa kama ambavyo tumeshatoa taarifa Serikalini kwamba Serikali imeshaondokana nao. Hivi sasa kinachofanyika ni Serikali inaendesha huduma hizi za shirika la reli mpaka hapo atakapopatikana Mkodishaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hizo huduma ambazo kwa kweli hazikuwa zimeondolewa isipokuwa zilikuwa zinasuasua kutokana na uendeshaji ambao ulikuwa hauridhishi, kwa vile Serikali inaendesha shughuli hizi mpaka atakapopatikana Mwendeshaji mwingine, itaendelea kuzingatia huduma zote za msingi ili kuhakikisha kwamba wananchi hawapati kero walizokuwa wakizipata. Lakini vile vile Chuo cha Reli Tabora Serikali itazingatia na kuendelea kutazama uwezekano wa kukiendeleza.(*Makofi*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:**Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru, kwa kuwa sasa hivi treni imeanza safari zake kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na inapotoka Dar es Salaam ikifika Tabora *buffet* inakatwa inaenda Mwanza, na sisi tunakwenda bila kula. Sasa hivi *buffet* ya kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma ipo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaulizwa kwamba wanamaliza chakula njiani mpaka kule hamna chakula!(*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru kwa kutambua kwamba sasa hivi usafiri wa treni umerejea katika reli ya Kati na ninaomba niwahakikishie wananchi kwamba huduma hizo zitaendelea kwa kadri itakavyokuwa tunasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukatwa kwa *buffet* kwenda Mwanza na Kigoma kwenda bila chakula, niseme tu kwamba kwa sababu kila kitu kinahitaji maandalizi na kujiwekea utaratibu unaostahili. Sasa hivi maadam tumeanza kuendesha

tutaangalia uwezekano wa kuwapatia chakula watu wanaokwenda Kigoma lakini hiyo itategemea na uwezo wetu na mipango kadri itakavyokuwa inawezekana.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kurejesha huduma za usafiri wa reli naipongeza, ninaamini kabisa kwamba Serikali itakuwa imejipanga vizuri ili huduma za usafiri wa reli kwenda Mpanda zisije zikasitishwa tena kwa ukosefu wa mafuta.

Ni kwa nini behewa la Daraja la Kwanza kwa gari linalokwenda mpanda halipo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo ulipokuwa unanikaribisha hapa Bungeni, katika safari yangu ya Kigoma na Mkoa wa Rukwa ilinifikisha pia Mpanda na nilipokuwa Mpanda nilipata fursa ya kutembelea kituo chetu cha reli Mpanda na nikataarifiwa kuwa huduma za reli huwa zinafanyika mara tatu kwa siku na kwa hiyo Serikali inafanya jitihada na hatuwezi kusitisha kwa sababu nia na azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunawapa huduma wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la behewa la first class ambalo sasa hivi halipatikani katika treni ya kwenda Mpanda, kwa sasa tutajaribu kuangalia tuone uwezekano huo ili wananchi wa Mpanda nao waweze kufaidika na huduma ya daraja la kwanza katika usafiri wa treni. (*Makofi*)

Na. 94

**Matumizi ya Fedha Kabla na Baada ya Bajeti**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA (K.n.y. MHE. HASSAN C. KIGWALILO)** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, uzoefu umeonyesha kuwa, kila mwisho wa mwaka wa fedha na kabla ya hotuba ya Bajeti Wizara mbalimbali hufuja fedha kwa matumizi mbalimbali kama semina na kadhalika, kwa lengo la kumaliza matumizi ya fedha za Bajeti husika:-

(a)Je, kwa nini Serikali haionekani kukerwa na matumizi ya aina hiyo yasiyo na tija yanayojirudia kila mwaka wa fedha?

(b)Kwa kuwa, utaratibu huo unatoa mwanya kwa Wizara hizo kutumia fedha nje ya makusudio yaliyoidhinishwa kwenye Bajeti ya Serikali. Je, Serikali inachukua hatua gani kuidhibiti hali hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote walionitumia salamu za pole kutokana na matatizo yaliyonikuta mimi na familia yangu, nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Jimbo la Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi matumizi yote ya fedha yanayofanywa na taasisi za Serikali yawe mwanzo au mwisho wa mwaka huzingatia mpango kazi *(Action Plan)* ya taasisi husika. Kwa kawaida utekelezaji wa Bajeti umegawanyika katika kipindi cha miezi mitatu mitatu ambacho kwa mwaka hufanya robo nne. Jukumu ambalo limepangwa na halijaweza kutekelezwa katika kipindi cha robo ya awali kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha, hutekelezwa katika robo inayofuatia baada ya tatizo la msingi kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, uandaaji wa Bajeti ya Serikali hufuata mfumo unaozingatia matokeo, ambayo hulazimu kuoanisha Bajeti na malengo ya taasisi husika. Aidha, majukumu yanayopaswa kutekelezwa huandaliwa na hatimaye kutumika kama kigezo muhimu wakati wa utoaji wa fedha za Bajeti. Kwa maana hiyo taasisi itakayotumia fedha kinyume cha ilivyoidhinishwa na Bunge, itakuwa imefanya kosa, kwa mujibu wa sheria za fedha inapaswa kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kutoa miongozo ya mara kwa mara juu ya matumizi ya fedha za Umma, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu hufuatilia kwa karibu zaidi, matumizi ya fedha za umma, kwa lengo la kuhakikisha kuwa yanafanyika kwa kuzingatia mipango kazi na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Kwa kuwa suala la matumizi ya fedha za Umma ni muhimu sana, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, swali la msingi linataja ufujaji wa fedha wakati wa Bajeti, na kwa kuwa Wilaya ya Kilwa ni moja ya Halmashauri zake ilikwenda kutengeneza Bajeti zake Mtwara kwa maelezo kwamba wanaenda kujichimbia ili wasisumbuliwe, na kwa kuwa kwa upande wangu mimi naona huu ni ufujaji wa fedha wanatafuta jinsi ya kuzitumia wakati wa mwisho wa Bajeti, na walitumia fedha zipatazo milioni nane.

Je, Serikali haioni kwamba huu ni ufujaji wa Fedha?(*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, kama katika

programu na *action plan* zao wameweka *very clear* kwamba watatayarisha Bajeti nne ya eneo ili wasipate hiyo *disturbance* ambayo yeye ameizungumza, hilo si tatizo.

Lakini kama halikuwepo awali hilo ni tatizo na linapaswa kuchukuliwa hatua. (*Makofi*)

Na. 95

**Hisa za Serikali kwenye Mashirika ya Umma**

**MHE. MWADIN ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inamiliki hisa kwenye Mashirika mbali mbali ya Umma ambayo kisheria yanatakiwa kila mwaka kulipia gawio Serikalini:-

(a) Je, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2007, ni Mashirika mangapi ambayo Serikali inamiliki hisa kwa asilimia 50 hadi 100 na ni mangapi inamiliki hisa chini ya asilimia 50?

(b) Je, ni Mashirika mangapi ambayo yametoa gawio kwa Serikali na kwa kiwango gani na mangapi ambayo hayajatoa gawio hilo tangu mwaka 2005-2007?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Jimbo la Wete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2005-2007, Serikali ilikuwa na Mashirika 152 ambayo inamiliki hisa kwa asilimia 50 na zaidi. Aidha, katika kipindi hicho hicho, Serikali ilikuwa inamiliki hisa chini ya asilimia 50 katika Mashirika 31. Mashirika ya Umma mengi ni yale yanayotoa huduma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, gawio hulipwa kutokana na faida ambayo shirika limepata katika mwaka husika. Kama shirika litapata hasara, wanahisa huwa hawalipwi gawio. Katika kipindi hicho, jumla ya mashirika ishirini tu 20 ndiyo yalitoa gawio kwa Serikali lenye jumla ya shilingi bilioni 78.4.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa yapo mashirika ambayo yanatoa huduma lakini pia yanatengeneza faida:-

(a)Je, utaratibu upi uliowekwa kuona kwamba mashirika haya yanatoa gawio Serikalini lakini yenyewe hayaathiriki kiufanisi?

(b) Kwa yale mashirika ambayo yanatengeneza hasara. Je, Serikali inatueleza ni sababu zipi ambazo zinapelekea haya kupata hasara na hatua zipi ambazo inachukua kuyahuisha Mashirika hayo? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mashirika yote yanayopata hasara utoe sababu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina jumla ya Mashirika 117 ambayo haya yanatoa huduma tu, hayatoi gawio kwa maana hayatengenezi ziada yoyote.

Kwa maana hiyo Mashirika haya huwezi ukaya-*clasify* katika kutoa gawio katika kutoa gawio kwenda katika Serikali. Suala la kwamba utendaji wa wakazi nataka niseme tu kwamba kama yanatengeneza hasara mimi sitaweza kuelewa ni sababu zipi za msingi kwa shirika moja moja zinazosababisha wao kupata hasara.

Lakini la msingi ni kwamba tuna mashirika 15 ambayo haya Serikali sasa hivi inajaribu kuyaboresha ili yaweze kufanyakazi kwa ubora zaidi.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu la msingi tumeelezwa jinsi Serikali ina hisa katika Mashirika mbalimbali. Na mimi nataka niseme Serikali vile vile ina hisa kwenye benki ya *Twiga Corporation, Twiga Bancorp* asilimia 100 lakini mpaka leo Serikali haijaweza kuipa mtaji wa kutosha Benki hii ili iweze kufanya biashara ya kibenki na kwa maana hiyo kuiletea faida Serikali.

Je, Serikali inasema nini kuhusu kutoiwekeza Benki hii kuwa na mtaji wa kutosha kupata leseni ya benki na kufanya kazi kwa faida? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Serikali ina mpango gani kuiwezesha Benki hiyo siyo kutokuiwezesha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi mwakajana tulieleza kwamba Serikali ina nia thabiti ya kuiwezesha Benki hii ili kuiongezea mtaji. Lakini unavyoelewa kupanga ni kuchagua, tumeingiza kuianzisha Benki ya Kilimo. Kwa hiyo, ule mtaji ambao mwaka huu tulitegemea kwamba tungewapa *Twiga Bank* tumeshindwa kupata mtaji wa kutosha tumeulekeza katika kuanzisha Benki ya Kilimo. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na hii benki tutaiwezesha ili nayo iweze kufanyakazi kwa ufanisi zaidi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu maswali yake alionyesha kwamba ni Mashirika 31 ambayo Serikali inamiliki chini ya asilimia 50 na kwa utaratibu uliopo sasa hivi Kamati ya Bunge ambayo inashughulika na hesabu za Mashirika ya Umma haina mamlaka kabisa ya kukagua hesabu za Serikali ambazo zina hisa chini ya asilimia 50 ya Mashirika yetu ya Umma.

Sasa matokeo yake ni kwamba katika maeneo hayo kunakuwa hakuna usimamizi wa kutosha wa rasilimali za nchi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anadhani ni lini hasa kwa kushirikiana na Bunge kutatengenezwa utaratibu ambao Kamati ya Bunge yenye majukumu ya kusimamia Hesabu za Mashirika ya Umma, zinakuwa na mamlaka ya kukagua hesabu ambazo Serikali ina hisa chini ya asilimia hamsini (50%)?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Mdee ni sahihi kabisa. Lakini hivi sasa kama ananitaka mimi nitoe uamuzi hivi sasa ni lini Serikali itatoa maelekezo nadhani hanitendei haki. Hili ni jukumu la Serikali lazima tupeleke kwenye Baraza la Mawaziri halafu Baraza la Mawaziri ndio liandae utaratibu mpya kwa sababu hivi sasa tunavyofanya ni kwa mujibu wa sheria. Lazima tufanye marekebisho katika sheria zetu tufanye vile vile marekebisho katika Kanuni. Namwomba Mheshimiwa Mdee wazo lake tumelipokea na tutalitafakari na tutatoa uamuzi hapo tutakapomaliza kupata maelekezo zaidi kutoka Baraza la Mawaziri. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali yetu imekuwa ni king'ang'anizi kwa kumiliki hisa katika Mashirika mbalimbali tuliyokuwa nayo. Na kwa kuwa Serikali hii hii imeshuhudia kiasi gani tulivyopata hasara katika shirika la Ndege, *Air Tanzania*. Je, hatuoni kwamba wakati sasa umefika wa Serikali yetu kuuza hisa zake kwa wananchi ili iondokane na biashara hii katika Mashirika haya na kuleta ile dhana ya maisha bora kwa kila Mtanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nikubaliane na Mheshimiwa Sanya kwamba yeye binafsi anakubali kwamba Serikali hii pamoja na yeye tunataka kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania. Nataka nikubaliane nayo hiyo. Lengo la Serikali ni kufikia huko. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Sanya kwamba Serikali yetu haifanyi king'ang'anizi. Serikali yetu kila inapofikia wasaa inaangalia ni shirika gani, inaangalia idadi gani ya hisa tuuze tena kwa *amount* ndogo kabisa Mheshimiwa Sanya. Hilo wazo lako ni zuri na tutalifanya kila itakapobidi tutauza hisa kwa Mashirika mbalimbali ili ile dhana ya maisha bora iweze kupatikana pamoja na wewe Mheshimiwa Sanya si una hisa katika *NMB* wewe? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, pia muda umekwisha, tuliongeza muda kutokana na muda ule uliotumika kuwasilisha Hati mbalimbali za Wizara. Kwa hiyo, tumetumia muda kama inavyostahili.

Waheshimiwa Wabunge, leo tunayo bahati ya kufikiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wamekuja kwenye kikao cha Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Kwa sababu kikao hicho kitaanza saa nane. Kwa hiyo, ameona ni vizuri akatumia muda huu kuja kushiriki nasi katika ukumbi huu katika kipindi hiki cha maswali. (*Makofi*)

Si mnafahamu tena, amechukua fomu ya kugombea Urais Zanzibar. Ameongozana na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Wazazi, Mheshimiwa Dogo Idd Mbaruk. Nani kama Mama. *(Makofi/Kicheko)*

Hao ndiyo wageni wetu kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sasa tuna wageni wengine wa Mheshimiwa John Chiligati. Tulipaswa kuanza na wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, lakini twende hivyo hivyo. Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Mkurugenzi wa *FES Tanzania* Ndugu Stephen *Globot wherever she is could you stand up. Thank you very much. Then* tunaye Meneja Miradi *Face Tanzania* Ndugu Amon Petro. Tunaye Msaidizi wa Mheshimiwa John Chiligati Kenneth Nollo na tunaye Ndugu Mbwana Kambangwa kutoka CCM Makao Makuu yeye ndiye kiongozi wa msafara huu. Ahsanteni karibu na kazi za FES katika nchi yetu tunazifahamu na tumekuwa nao *FES* miaka mingi. Kwa hiyo, tunaomba tu aendelee kufanyakazi na sisi. (*Makofi*)

Halafu ni maafisa 54 wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambao wapo Bungeni kwa ajili ya kusikiliza Hotuba ya Bajeti. Bila kuwataja majina yao wote wanakaribishwa. Lakini Mheshimiwa Stephen Wasira anao wageni wengine ambao kutoka Shirika la Maendeleo la Marekani *US-Aid* Ofisi ya Washington Marekani ambao ni Ndugu Thomas Hobgood-Mshauri na mwelekezi. Tunaye Jeanne Dowing, Mshauri na mwelekezi. Tunaye Ndugu Gray Saga Mshauri na mwelekezi. Karibuni sana tumefurahi kuwaona na tunaamini kabisa mnaendelea na kazi vizuri katika nchi yetu. (*Makofi*)

Aidha, Mheshimiwa Waziri Wasira leo ana wageni wengine ambaye ni Ndugu Charles Mwangwale, Katibu wa CCM Wilaya ya Bunda. Anaye Mheshimiwa Mohamed Muya, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Anaye Ndugu Sophia Elias Kaduma, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Pia anao Wakurugenzi wa Idara mbalimbali za Wilaya ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wakurugenzi Wakuu wa Bodi za Mazao na Maafisa Waandamizi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwa hiyo, namkaribisha kwa namna ya pekee Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, pamoja na watumishi wake wote. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tunao wawakilishi wa wakulima na viongozi wa taasisi za mazao ya bustani Tanzania *TAHA* na *HODECT* ambao ni Ndugu Jacqueline Mkindi, Mkurugenzi wa *TAHA*, tunaye na mwingine Jacqueline Laizer Mkurugenzi wa *HODECT*. Tuna Ndugu Frank Msigwa, Mkulima wa *Avocado* kutoka Njombe. Aisee mbona hukusema unakuja yuko wapi Msigwa. Ahsante sana. Tunaye Ndugu Kambarage Sanga Mkulima wa *Apples* kutoka Makete. Yuko wapi huyu sasa ndiyo mambo hayo. Tunaye Ndugu Beda Kusenga Mkulima wa *Apples* naye kutoka Makete. Kwa hiyo, mnafahamu tena Mkoa mpya mkiongeza *Apples* na *Avocado* na mchuchuma imefunguliwa basi biashara na soko liko kwa uhakika.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu ambao ni Ndugu Oloibon huyu ni *Chief* Lukunati Moroto wa jamii ya wafugaji Magindu ameambatana na na mwanae. Ahsanteni karibuni sana ni vizuri na nyie mkaja mkatusikiliza katika Bunge hili. (*Makofi*)

Halafu yupo Ndugu Mbilikani Ngumbikwa jamii ya wafugaji pia. Ahsanteni sana wafugaji. Sisi tumetunga sheria ya kuweza kuboresha ufugaji wenu. Kuna mgeni wa

Mheshimiwa Said Arfi ambaye ni Ndugu Luka Kapipi kutoka Mpanda ni mratibu Mipango na uhamasishaji Jimbo la Mpanda Kati CHADEMA. Ahsante sana karibu. (*Makofi*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mossy Suleiman Musa ambao wa kwanza ni Balozi Isaac Abraham Sepetu, Chairman wa *Rain boll Top Solution*. Huyu alikuwa Waziri wetu. Tunafurahi kukuona tena. Tuna Ndugu Bill Aii Mjumbe wa Bodi ya Kampuni hiyo, tuna Ndugu Chris Aii pia Mjumbe wa Bodi wa Kampuni hiyo. Tuna Ndugu Titus Okidi injinia wa kampuni hiyo. Tuna Ndugu Fedinandesi Savio, Mjumbe wa Kamati hiyo. Wapo wageni wao *Financiers* kutoka Canada nao Ndugu *Lenox Brown*, tuna Ndugu *Brown Global Verification* na Ndugu Tom Seru ni *Director*. Karibuni sana wote tunategemea mtakuwepo Dodoma na kuona yale tunafanya hapa na kujitahidi.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Juma Killimbah kutoka kijiji cha Susu, Iramba - Singida wamekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge ambao ni Ndugu Mariam Kiula Mkigi akiambatana na wajukuu wake Mariam Sarafina na Jonas. Ndugu Mariam Kiula yuko wapi na wajukuu wake? Tumefurahi sana na nyie wajukuu basi mmekuja kujifunza karibuni sana. Ahsante.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa George Simbachawene ambaye ni Mchungaji Daniel Masagasi kutoka Parish ya Pwaga Jimbo la Kibakwe. Mchungaji karibu sana. Nchi inaomba sana sala zenu katika nafasi tunapokwenda kwenye Uchaguzi Mkuu.

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Pindi Hazara Chana ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango wanaongozwa na Lillian Nyemele. Yuko wapi. Huyu Lillian Nyemele kabla ya kwenda kusoma huyu alikuwa Afisa Tarafa wangu mimi pale Njombe. Wengine amefuatana nao ni Annett Mayengela, Noel Leviva, Witness Mafwela na Ndugu Mazalia Macha. Karibuni sana nadhani wamemaliza Mitihani tunawatakia maisha mema na Hongeza kwa kufanya hiyo kazi.

Tuna Ndugu Magori John Nyerere, huyu ni Mjukuu wa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, yuko wapi, ahsante sana. Na wewe uko huko mipango, okay. Tuna wanafunzi 15 wa Chuo cha *St. John's* Dodoma, wakiongozwa na Matron wao Dr. Jean Kaningi, wako wapi wote wanafunzi wa Chuo cha *St. John's*? Ahsante sana. Karibu sana tunawakia masomo mema na muachane na makundi kwa sababu makundi yanakuwepo lakini mwisho wake kila mtu yuko peke yake. Mwisho tuna wanafunzi tisa (9) kutoka shule ya Sekondari Sangiti iliyopo Moshi. Wanafunzi wa Sangiti wote pamoja na walimu wasimame popote pale walipo. Nadhani wamekosa nafasi watakuwa mahali pengine. Tunawakaribisha wote. Wageni wengine wote tunawakaribisha Bunge ni watu wote mnakaribishwa bila hata kuomba *appointment*.

Shughuli za kazi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Hamza Mwenegoha anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa leo kutakuwa na kikao cha Kamati pamoja na Wageni kutoka Bunge la Rwanda. Kikao kitafanyika katika ukumbi wa Namba 227 ghorofa ya pili, jengo la

utawala kuanzia sasa hivi saa nne. Kwa hiyo, wajumbe wa Kamati hiyo mnaweza kuondoka hivi sasa. Kwa sababu tuna mgeni *President* wa *Senate* ya Rwanda.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Masoud anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati leo tarehe 22 Juni, 2010 saa saba mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Halafu Mheshimiwa Mwenyekiti wa *CPA*, Tawi la Tanzania, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya *CPA* Tawi la Tanzania kuwa leo saa tano asubuhi mtakutana na Rais wa *Senate* ya Rwanda katika ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Kwa hiyo, Kamati ile nyingine ya Uchumi na Fedha wanakutana na wageni hawa hawa lakini pia na *CPA branch* ya Tanzania watakutana na wageni hawa saa tano, chumba 219, tunaomba wajumbe wanaohusika, msikose kwa sababu tunakutana na wageni.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa watakutana leo tarehe 22 Juni, 2010 saa tano asubuhi katika ukumbi wa Msekwa kukamilisha kazi ya kujadili bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2010/2011, wote wanaomba kuhudhuria. Sasa kule kwenye ukumbi wa Msekwa mtakuwa Kamati mbili baada ya saa mbili, sasa hiyo mtafahamu wenyewe. Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi na ya wageni wetu yamekwisha, sasa tunaendelea. Kwa sababu kauli mbiu mwaka huu ni kilimo kwanza, tunamwongezea dakika tano. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi Kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Maji na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuipa umuhimu na kutoa msukumo wa pekee kwa Sekta ya Kilimo. Kama wote mtakavyokumbuka, tarehe 3 Agosti, 2009, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alizindua rasmi kauli mbiu ya Kilimo Kwanza wakati wa wiki ya maadhimisho ya sherehe za sikukuu ya wakulima ya Nane Nane yaliyoadhimishwa Kitaifa katika viwanja vya Nzuguni Mkoani Dodoma. Msingi wa maudhui ya azma ya Kilimo Kwanza, ni kukiri kwamba, haiwezekani kukuza uchumi wa Tanzania na kiwango cha kupunguza umaskini

kwa Watanzania walio wengi bila kuwekeza kwa kiwango cha kuridhisha katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ambaye amekuwa akifanya ziara Mikoani ambapo, kila mara anatenga muda kuona shughuli za kilimo na kutoa maagizo mbalimbali kuhusu kilimo endelevu na kinachozingatia utunzaji wa mazingira. Maagizo na maelekezo hayo yanazingatiwa katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme* – ASDP) ili uzalishaji katika kilimo uwe endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kutumia sehemu ya muda wake kushughulikia masuala ya Kilimo na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge na Ismail Jussa Ladhu, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, Taifa letu lilipotelewa na Mzee Rashid Mfaume Kawawa aliyekuwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu. Aidha, Bunge lako Tukufu lilipata msiba wa kupotelewa na Mheshimiwa Sigifrid Selemani Ng’itu, aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa. Nachukua fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia za marehemu hao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Maji na Mifugo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa waliokuwa wakiutoa na ambao wameutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011. Naishukuru kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya mwaka 2009/2010 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2010/2011 katika kikao chake kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 2 Juni, 2010. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Bunda, kwa ushirikiano walionipa kwa kipindi chote cha miaka mitano cha kuwawakilisha Bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo. Nawaahidi kuwa nipo tayari kuendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kutoa mchango wangu katika kupambana na matatizo yanayotukabili Jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza tena Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo na kukipa kilimo kipaumbele katika mipango Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha 2005 hadi mwaka 2010, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika iliendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005, na bajeti ya mwaka 2010/2011 ambayo imetambua nafasi ya Kimkakati ya Sekta ya Kilimo katika modenaizesheni ya uchumi wa kisasa. Ilani hiyo inaielekeza Serikali kuwafikishia wakulima, wafugaji na wavuvi vijijini maarifa na kanuni bora za kilimo, ufugaji na uvuvi ili waongeze tija na mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 18 Januari, 2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika alisisitiza wajibu wa Wizara katika kutekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 ambapo alitoa maelekezo yafuatayo:-

(i) Kutayarisha mkakati na mipango itakayowezesha kilimo kuwa cha kisasa chenye tija na kitakachowaletea wananchi maendeleo;

(ii) Kuhakikisha wakulima wanapata na kutumia zana bora, pembejeo za kilimo husussan, mbolea, mbegu bora na madawa ya kudhibiti visumbufu. Aidha, aliagiza kuwa na wakulima wenye ujuzi na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika;

(iii) Kuhakikisha kuwa wakati wote wananchi hawafi kwa njaa; na

(iv) Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia kila chanzo cha maji kinachowezekana – mito, maziwa, mabwawa, visima na maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza maagizo hayo ya Mheshimiwa Rais, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Kilimo ilianza utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) mwaka 2006/2007. Awamu ya kwanza ya programu hiyo itakamilika mwaka 2012/2013. Kupitia *ASDP*, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo ikishirikiana na Halmashauri kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Develoment Plans- DADPs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata zana na pembejeo bora, hususan mbolea, viuatilifu, mbegu na miche bora kwa wakati muafaka na kwa bei nafuu, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini kutoka tani 241,753 mwaka 2005/2006 hadi tani 302,000 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 76. Katika kipindi hicho upatikanaji wa mbolea yenye ruzuku uliongezeka kutoka tani 53,389 hadi tani 150,000. Aidha, fedha zilizotengwa kugharamia ruzuku ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 7.48 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 118 mwaka 2009/2010;

(ii) Upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka kutoka tani 10,477 mwaka 2005/2006 hadi tani 16,148 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 54.12;

(iii) Upatikanaji wa miche bora ya mibuni uliongezeka kutoka miche milioni 2.85 mwaka 2006/2007 hadi miche milioni 10.4 mwaka 2009/2010. Aidha, upatikanaji wa miche bora ya chai uliongezeka kutoka miche milioni 2.48 hadi miche milioni 11.5 katika kipindi hicho;

(iv) Kuongeza uwezo wa kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani katika vyuo vya kilimo nchini kutoka wataalam 650 mwaka 2005/2006 hadi wataalam 3,500 mwaka 2009/2010. Idadi ya wataalam wa ugani imeongezeka kutoka 3,379 waliokuwepo mwaka 2007/2008 hadi watalaam 4,439 mwaka 2009/2010. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya wakulima wa mfano wanaopatiwa mafunzo kupitia utaratibu wa shamba darasa iliongezeka kutoka wakulima 1,800 hadi wakulima 174,370 kwa kupitia mashamba darasa 6,711 na wamekuwa wakiwafundisha wakulima wenzao katika maeneo yao;

(v) Kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula kutoka tani milioni 9.66 mwaka 2005/2006 hadi tani milioni 12.825 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 33. Wananchi katika maeneo yaliyokabiliwa na ukame wamekuwa wakipatiwa msaada wa chakula au kuuziwa chakula kwa bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo; n

(vi) Eneo la kilimo cha umwagiliaji limeongezeka kutoka hekta 264,388 mwaka 2005/2006 hadi hekta 331,490 mwaka 2009/2010 ambapo jumla ya kaya 200,000 zimenufaika na ongezeko hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuhamasisha wananchi katika sekta mbalimbali kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika. Idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika iliongezeka kutoka wanachama 750,000 hadi kufikia wanachama milioni 2.2 na Vyama vya Ushirika kutoka 5,730 hadi 9,501.

Aidha, idadi ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) iliongezeka kutoka Vyama 1,875 hadi 5,344 sawa na ongezeko la asilimia 184.5. Idadi ya wanachama wa *SACCOS* iliongezeka kutoka 291,368 hadi 911,873 katika kipindi hicho sawa na ongezeko la asilimia 213. Akiba na amana za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 85.6 hadi bilioni 194.8 sawa na ongezeko la asilimia 127.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi bilioni 65.7 hadi shilingi bilioni 463.4 sawa na ongezeko la asilimia 605.3. Mikopo hiyo ilitolewa kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, biashara ndogo ndogo, ujenzi wa nyumba, elimu na matibabu. Ukuaji huo wa ushirika unachangia azma ya Serikali ya kuondoa umaskini na kuwaletea wananchi maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Serikali imekuwa ikiongeza kila mwaka kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo kuanzia mwaka 2005/2006. Bajeti ya Sekta ya Kilimo iliongezeka kutoka shilingi bilioni 233.309 mwaka 2005/2006, sawa na asilimia 5.78 ya bajeti yote ya Serikali hadi shilingi bilioni 666.9 mwaka 2009/2010 sawa na asilimia 7.2 ya bajeti yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kutekeleza Azma ya Kilimo Kwanza kupitia programu zake kuu za *ASDP* na *CRMP*. Maelezo ya kina nitayatoa wakati wa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo ni moja kati ya sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu licha ya mabadiliko yaliyotokea katika mfumo wa uchumi katika miaka ya karibuni ambapo sekta za madini, utalii na huduma zimekua kwa kasi. Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia ajira Watanzania zaidi ya asilimia 70 na inachangia wastani wa asilimia 95 ya chakula kinachohitajika nchini. Katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo ilikua kwa wastani wa asilimia nne na ilichangia asilimia 26 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa chakula uliongezeka kutoka tani milioni 9.66 mwaka 2005/2006 hadi tani milioni 10.77 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 103. Takwimu za Uwiano wa Kujitosheleza kwa Chakula (*Food Self-Sufficiency Ratio-SSR*) kwa kipindi hicho zinaonyesha kwamba Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 105.4 (Kiambatisho Na.1.) Hata hivyo kumekuwepo na maeneo ambayo yalikuwa na upungufu wa chakula kwa nyakati tofauti kutokana na ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuratibu hali ya chakula nchini katika kipindi chote cha mwaka 2009/2010 na imekuwa ikipokea taarifa za hali ya chakula kwa kipindi hicho kutoka mikoa yote nchini. Kwa ujumla, katika kipindi hicho, hali ya chakula nchini haikuwa nzuri kutokana na uzalishaji mdogo wa chakula uliotokea katika msimu wa 2008/2009 kwa mazao ya nafaka uliosababishwa na ukame.

Tathmini ya uvunaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2008/2009 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2009/2010 iliyofanywa mwezi Desemba 2009 ilionyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ujumla katika msimu huo ulifikia jumla ya tani milioni 10.77 ikilinganishwa na mahitaji ya jumla ya tani milioni 10.57 ya mwaka 2009/2010 na hivyo taifa kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 102.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tathmini hiyo ilionesha kuwepo kwa upungufu wa nafaka wa takriban tani milioni 1.3 uliotokana na uzalishaji mdogo wa mazao hayo wa tani milioni 5.2 ikilinganishwa na mahitaji ya nafaka ya jumla ya tani milioni 6.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, baadhi ya maeneo ya nchi katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka ya Arusha, Kilimanjaro,

Shinyanga, Manyara, Mara, Mwanza, Morogoro, Pwani, Tanga na baadhi ya mikoa inayopata mvua za msimu kama vile Dodoma, Lindi, Mtwara na Iringa yalikabiliwa na upungufu wa chakula kwa viwango tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwezi Septemba, 2009 na Februari, 2010, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wa Usalama wa Chakula ilifanya tathmini za kina za hali ya chakula katika mikoa hiyo. Tathmini ya mwezi Septemba 2009 iliyofanywa katika Wilaya 65 katika mikoa 16 ilionyesha kwamba watu 1,569,890 katika Wilaya 59 walikuwa wanakabiliwa na upungufu wa chakula kati ya mwezi Novemba 2009 na Januari 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, matokeo ya tathmini ya kina ya mwezi Februari 2010, yalionyesha watu 717,684 katika Wilaya 34 za mikoa tisa iliyofanyiwa tathmini walikabiliwa na upungufu wa chakula kuanzia mwezi Machi hadi Mei 2010 na hivyo kuhitaji chakula cha msaada. Ili kukabiliana na upungufu wa chakula katika maeneo yaliyoainishwa, Serikali ilitenga jumla ya tani 124,374.6 za mahindi kwa ajili ya kusambazwa kwa watu wenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 12 Juni 2010, jumla ya tani 100,991.3 za chakula zilisambazwa kwa walengwa na kiasi kilichobaki cha tani 23,383.4 kinaendelea kusambazwa. Serikali iliweza kukabiliana na upungufu huo wa chakula na kukifikisha kwa walengwa bila kuhitaji msaada wa wahisani kutokana na kuwa na akiba ya kutosha ya chakula kwenye maghala ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*National Food Reserve Agency-NFRA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, *NFRA* waliweza kuhamisha jumla ya tani 126,914.9 za mahindi kutoka kwenye maghala ya maeneo yenye ziada na kuyapeleka kwenye maeneo yaliyokuwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei za vyakula kwa wastani ziliendelea kuwa juu katika maeneo mengi ya nchi kuliko ilivyokuwa katika msimu uliopita au ikilinganishwa na bei za wastani wa miaka mitano iliyopita. Bei za vyakula ambazo huchangia asilimia 55.9 ya mfumuko wa bei zimekuwa juu karibu katika kipindi chote cha mwaka 2009/2010. Kwa mfano, kati ya mwezi Novemba 2008 na Novemba 2009 bei za vyakula ziliongezeka kwa asilimia 17.1 na kati ya mwezi Aprili 2009 na mwezi Aprili 2010 bei zilikuwa asilimia 9.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la kuendelea kupanda kwa bei za vyakula na upungufu wa chakula uliojitokeza, Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

(i) Ilitenga jumla ya tani 124,374.6 za chakula kutoka *NFRA* kwa ajili ya kusambaza kwa walengwa katika mwaka 2009/2010.

(ii) Kupitia *NFRA* ilinunua nafaka kutoka kwa wakulima kwa ajili ya kuhifadhi na kupeleka katika maeneo yenye upungufu wa chakula ambapo katika mwaka 2009/2010 jumla ya tani 73,672.7 zilinunuliwa.

(iii) Ilihamisha tani 126,914.9 kutoka katika maghala ya *NFRA* Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwenda katika Kanda zenye Mikoa iliyokuwa na upungufu wa chakula.

(iv) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya pote nchini ilitoa mafunzo ya hifadhi bora ya chakula kwa wananchi katika ngazi ya kaya ili wajiwekee akiba ya kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao. Aidha, Serikali iliwahimiza na kuwahamasisha wananchi kutumia vyakula mbalimbali, hususan visivyo vya nafaka pamoja na uchanganyaji (*blending*) wa nafaka na mazao yasiyo ya nafaka ili kupanua wigo wa matumizi na upatikanaji wa vyakula.

(v) Ilishauri mikoa kuhusu kuongeza upatikanaji wa chakula katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wafanyabiashara kununua chakula kutoka mikoa yenye ziada kwa ajili ya kupeleka kuuza kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula na wananchi kuuza sehemu ya mifugo yao kwa ajili ya kujipatia mahitaji yao ya chakula.

(vi) Ilisimamia kwa karibu upatikanaji wa chakula nchini ikiwa ni pamoja na kusitisha kwa muda mauzo ya mazao ya nafaka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwezi Mei na Juni 2010, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri ilifanya tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na utabiri wa hali ya chakula kwa mwaka 2010/2011. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonyesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani milioni 12.8 zikiwemo tani milioni 7.7 za mazao ya nafaka na tani milioni 5.1 za mazao yasiyo ya nafaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2010/2011, yanakisiwa kufikia tani milioni 11.4. Hivyo, Taifa linategemewa kujitosheleza kwa chakula kwa takriban asilimia 112. (kiambatisho Na. 2)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali hiyo nzuri ya chakula kuna baadhi ya maeneo (*pockets)* yanayotazamiwa kuwa na upungufu wa chakula. Maeneo hayo ni wilaya zote za Mkoa wa Dodoma isipokuwa Wilaya ya Kondoa. Maeneo mengine yako katika wilaya za Longido (Arusha), Iringa Vijijini (Iringa), Shinyanga Vijijini, Shinyanga Mjini, Meatu na Kishapu (Shinyanga), Kwimba (Mwanza), Manyoni (Singida), Ruangwa na Lindi Vijijini (Lindi), Nanyumbu (Mtwara) na Mwanga (Kilimanjaro). Wizara kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri husika itaendelea kufuatilia hali ya chakula katika maeneo hayo na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali nzuri ya uzalishaji wa mazao ya chakula pamoja na sababu nyingine, imetokana na unyeshaji mzuri wa mvua katika maeneo mengi ya

nchi na kuongezeka kwa upatikanaji na matumizi ya pembejeo zikiwemo mbolea, mbegu bora na madawa ya kilimo chini ya mpango wa Serikali wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima. Kutokana na hali hiyo nzuri ya uzalishaji wa mazao ya chakula, wananchi na wakulima wanashauriwa kuhifadhi chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya kwa lengo la kuboresha usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inahamasisha matumizi ya mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa wakulima ili wauze mazao yao na kupata faida. Aidha, Wizara inahamasisha na kutoa wito kwa wananchi na wawekezaji wa ngazi zote kuwekeza katika usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuyaongezea thamani na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya chakula ni nzuri Serikali itaondoa zuio la kusafirisha mazao ya chakula nje ya nchi. Wakulima na wafanyabiashara wanaotaka kusafirisha mazao ya chakula nje ya nchi watapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*WFP*) kuendeleza mpango wa kununua mazao kupitia vikundi na vyama vya wakulima ujulikanao kama *"Purchase for Progress"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) iliyotolewa mwezi Mei 2010 inaonesha kuwa katika mwaka 2010, uzalishaji wa nafaka duniani unatazamiwa kuongezeka kwa asilimia 1.5 kutoka tani milioni 2,251.5 mwaka 2009 hadi tani milioni 2,286.0 mwaka 2010, na unakadiriwa kufikia kiwango cha mwaka 2008 ambapo uzalishaji ulikuwa tani 2,282.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bei za mazao ya chakula katika soko la kimataifa zimeendelea kuwa chini ya viwango vya mwaka 2008. Hata hivyo, takriban nchi 29 duniani zinatazamiwa kukabiliwa na upungufu wa chakula na zitahitaji chakula cha msaada. Nyingi ya nchi hizo ziko katika kundi la nchi maskini zenye kipato kidogo za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara hususan nchi za Saheli za Afrika Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mavuno mazuri ya msimu wa 2009/2010 yanayotazamiwa kuimarisha hali ya chakula hususan miongoni mwa jamii za wafugaji katika nchi za Afrika Mashariki, baadhi ya nchi jirani hususan Burundi, Kenya na Uganda bado zinatazamiwa kuwa na maeneo yanayokabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, nchi jirani za Kusini mwa Afrika hususan Zambia, Malawi na Msumbiji zinatazamiwa kuwa na mavuno mazuri, hali ambayo itasaidia kuimarisha upatikanaji wa chakula ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2005/2006 na 2009/2010, uzalishaji wa mazao makuu asilia ya biashara ulikua na kupungua kwa viwango tofauti. Zao la chai liliongezeka kwa asilimia 20, kahawa asilimia 3.4, korosho asilimia 39.0, tumbaku asilimia 57.4 na pareto asilimia 39.3. Kwa upande wa mazao ya pamba na mkonge uzalishaji ulishuka kwa asilimia 28.7 na 39.6 (Kiambatisho 3).

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2005/2006 na 2009/2010 kazi ya kuziendeleza na kuimarisha bustani za kuzalisha vipando vya mazao ya matunda iliendelea. Bustani hizo ni Mpiji (Bagamoyo), Bugaga (Kigoma), Songa (Muheza), Igurusi (Mbeya), Malindi na Jaegetal (Lushoto). Mojawapo ya kazi zilizofanyika katika bustani hizo ni pamoja na kuagiza aina nne bora za vikonyo vya mazao ya matunda ikiwemo michungwa, miparachichi, matofaa (*apples*) na mananasi bora kutoka Kenya na Afrika ya Kusini kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mbinu za uzalishaji bora wa mazao mapya yenye thamani na soko la uhakika zilifanyika wakati wa maonyesho ya NaneNane, Siku ya Chakula Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Wiki ya Ushirika. Wizara pia iliendelea kuzalisha vipando bora vya mazao ya matunda, mboga na viungo katika bustani hizo na kuvisambaza kwa wakulima. Uzalishaji wa vipando bora vya miti ya matunda hususan miembe na michungwa uliongezeka kutoka wastani wa vipando 100,000 mwaka 2005/2006 hadi vipando 300,000 mwaka 2009/2010 kwa bustani zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya bustani umeendelea kuongezeka. Kwa mfano, uzalishaji wa matunda mbalimbali uliongezeka kutoka tani 931,475 mwaka 2005/2006 hadi tani 2,700,221 mwaka 2008/2009 na mboga kutoka tani 134,604 mwaka 2005/2006 hadi tani 157,921 mwaka 2008/2009. Mazao hayo yalizalishwa na kuuzwa katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikishirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kilolo na Iringa Vijijini katika Mkoa wa Iringa na Halmashauri za Wilaya za Mbeya Vijijini, Mbozi, Ileje na Rungwe zimeendelea kuwahudumia wakulima wa mazao ya matunda yanayostawi katika maeneo ya hali ya ubaridi hususan matofaa (*apples)* na maparachichi. Wakulima waliopatiwa miche bora ya mazao hayo mwaka 2007 sasa wameanza kuvuna.

Mavuno hayo yanaashiria mwanzo wa Tanzania kuzalisha matofaa yenyewe badala ya kuagiza matunda hayo yanayoweza kustawishwa kwa wingi na kwa ubora wa hali ya juu nchini. Walaji wa matunda hayo nchini wameyaelezea kwamba ni mazuri na yana ladha nzuri kuliko yale kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwezi wa Juni, 2010, shehena ya tani 20 ya maparachichi kutoka Tanzania iliuzwa kwa mafanikio katika soko la Ulaya (Uingereza) kwa faida. Hii inaashiria mwanzo wa Tanzania kuingia katika soko hilo na tathmini ya awali imeonesha kwamba kuna soko la uhakika la mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuzalisha vipando bora vya zao la zabibu na kuvisambaza kwa wakulima wa mikoa ya Dodoma, Mara na Kilimanjaro. Katika Mkoa wa Dodoma, Taasisi ya Utafiti ya Makutopora kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilisaidia uanzishwaji wa shamba la hekta 101

katika Kijiji cha Chinangali. Aidha, wakulima katika Kijiji cha Mtitaa katika Wilaya ya Bahi na vijiji vya Paranga na Mondo katika Wilaya ya Kondoa walipatiwa mafunzo na vipando bora vya zabibu. Wakulima 100 na wataalam wa ugani 48 walifundishwa kanuni bora za kilimo cha zabibu katika Vijiji vya Nyamuswa, Kamkenga, Sarawe,Mugeta, Kyandege, Kasuguti, Kyangetutya, Kibara, Kung'ombe na Nansimo, Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwahudumia wakulima kwa ufanisi, bustani ya miche bora ya zabibu yenye uwezo wa kuzalisha miche bora 60,000 imeanzishwa katika Taasisi ya Utafiti ya Makutopora. Viwanda vya kusindika mvinyo vya *CETAWICO, ALCO Enterprises* na Tanzania *Distillers* viliendelea kuzalisha mvinyo na vinywaji vingine vinavyotokana na zao la zabibu. Kwa ujumla viwanda hivyo vina uwezo wa kusindika lita milioni 3.4 kwa mwaka. Viwanda hivyo vinatoa mchango mkubwa katika upatikanaji wa soko la uhakika la zao la zabibu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inashirikiana na Halmashauri za Wilaya za mikoa ya Pwani na Lindi katika kuendeleza zao la maembe ambapo katika mwaka wa 2009/2010 ilizalisha na kusambaza miche bora ya miembe 20,000 kwa wakulima wa mfano katika Wilaya za Bagamoyo, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini, Kisarawe, Mkuranga katika Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi. Jumla ya wakulima 582 wanashiriki katika mpango wa kuzalisha maembe bora ambapo wamepatiwa jumla ya miche bora 28,000 inayotosheleza kupandwa katika eneo la hekta 465.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeshirikiana na Wadau wa Mazao ya Bustani kupitia Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani Tanzania *(Horticulture Development Council of Tanzania – HODECT)* kuandaa Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani Tanzania. Aidha, *HODECT* iliandaa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa wadau wa mazao ya bustani ambapo mkakati huo uliwasilishwa kwa wadau na kukubalika ili utumike kuandaa programu za kuendeleza mazao ya bustani utakaoainisha malengo ya uzalishaji wa mazao hayo katika kila Mkoa na Halmashauri. Uzalishaji wa mazao ya bustani ni kama inavyoonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 4.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtikisiko wa uchumi duniani uliotokea kwa takriban miaka miwili umeathiri sekta mbalimbali hapa nchini ikiwemo Sekta ya Kilimo. Kutokana na athari hizo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kunusuru uchumi zikiwemo za kufidia tofauti ya bei ya mazao kwa wakulima, kufidia hasara walizopata wanunuzi, kudhamini mikopo ya mabenki, kusogeza mbele muda wa kulipa mikopo na kutoa mitaji kwa wanunuzi waliothibitika kuathirika na mtikisiko huo. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilichukua hatua zifuatazo:-

(i) Ilitoa shilingi bilioni 20 zilizotumika kufidia bei ya wakulima wa pamba kwa shilingi 80 kwa kilo ya pamba iliyouzwa katika msimu wa ununuzi wa 2009/2010. Zaidi ya tani 250,000 za pamba zilinunuliwa;

(ii) Iliongeza uwezo wa Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*National Food Reserve Agency – NFRA*) kwa kutoa shilingi bilioni 35 zilizotumika kununua na kusafirisha chakula toka mikoa iliyokuwa na ziada ya chakula na kupeleka katika mikoa iliyokuwa na upungufu. Jumla ya tani 73,672.7 za mahindi zilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya *NFRA* katika maeneo yaliyokuwa na upungufu wa chakula;

(iii) Ilifidia hasara ya shilingi bilioni 9.3 kwa wafanyabiashara wa pamba waliothibitika kupata hasara kutokana na tofauti ya bei ya kuuzia pamba katika soko la dunia iliyosababishwa na mtikisiko wa uchumi duniani. Aidha, shilingi bilioni 5.3 zilitolewa kwa ajili ya kusogeza mbele muda wa kulipa mikopo iliyochukuliwa na wafanyabiashara kutoka benki za *CRDB* na *TIB*; na

(iv) Ilifidia wafanyabiashara wa kahawa shilingi bilioni 9.9 ambapo shilingi milioni 803.8 zilitumika kusogeza mbele muda wa kulipa mikopo iliyochukuliwa na wafanyabiashara kutoka benki ya *CRDB.*

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kunusuru uchumi liliratibiwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali. Muda wa mwisho uliowekwa na Benki Kuu kuwasilisha madai ilikuwa tarehe 15 Julai, 2009. Hivyo, madai yaliyowasilishwa baada ya tarehe hiyo hayakuweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano, Wizara iliendelea kufufua Vyama vya Ushirika vilivyokuwa vimeshindwa kuwahudumia wanachama wake kwa kuviwezesha kufanya biashara kwa kujitegemea. Vyama vilivyofufuliwa ni *MAMCU* na *TANECU* (Mtwara), *TAMCU* (Ruvuma), *ILULU* (Lindi) na *CORECU* (Pwani) kwa ajili ya zao la korosho na *SHIRECU* (Shinyanga) na *NCU* (Mwanza) kwa zao la pamba. Ufufuaji wa Vyama hivyo ulioanza mwaka 2007/2008, uliviwezesha kununua mazao ya wakulima na kuwapa bei nzuri. Aidha, ubora wa mazao yaliyouzwa kupitia vyama hivyo uliongezeka na hivyo kuvutia wanunuzi na kuongeza ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2005 na mwaka 2010, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia chaguzi za viongozi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi, Vyama Vikuu, Kilele na Shirikisho kwa lengo la kuhakikisha kuwa chaguzi hizo zinafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ushirika ya mwaka 2003 ambayo ni pamoja na kuwezesha wanachama wa vyama hivyo kuchagua viongozi waadilifu na wanaowajibika. Zoezi hilo lilifanyika kwa Vyama vyote vya Ushirika vya Tanzania Bara vyenye sifa ya kufanya chaguzi. Aidha, viongozi mbalimbali wa ushirika waliochaguliwa walipata mafunzo ya uongozi bora na uwajibikaji ili kuimarisha utendaji wao katika Vyama husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kusimamia chaguzi za theluthi moja ya wajumbe wa Bodi za Vyama Vikuu vya Ushirika ambao vipindi vyao vya miaka mitatu vilikwisha. Vyama Vikuu vya *KNCU*, *KCBL* na *VUASU* (Kilimanjaro), ILULU (Lindi), *KCU* na *KDCU* (Kagera), *NCU* (Mwanza), *SHIRECU* na *KACU* (Shinyanga), *WETCU* na *ICU* (Tabora), MAMCU na TANECU (Mtwara), *SONAMCU* na *TAMCU*

(Ruvuma), *LATCU* (Rukwa), *ACU* (Arusha) na *CHUTCU* (Mbeya) vilifanya Mikutano Mikuu ya uchaguzi, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huo umetoa nafasi kwa Vyama vya Ushirika kupata viongozi wapya wenye upeo zaidi katika masuala ya uendeshaji na biashara pamoja na kujenga ushirika unaozingatia maadili ya uongozi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika. Vilevile, kesi mbalimbali zilizovikabili Vyama vya Ushirika zilifuatiliwa kwa lengo la kulinda maslahi ya Vyama na ya wanachama wake zikiwemo kesi za *NCU, MOFACU*, Moria *SACCOS, ILULU SACCOS* na *CHUTCU*. Kesi baina ya *CHUTCU* na kampuni ya *TLTC* ilimalizwa nje ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2009/2010, ilikadiria kukusanya mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 1.1 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 10 Juni 2010, Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 1.4 sawa na asilimia 133.2 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho shilingi milioni 259.5 ni albaki ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 228.6. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 135.9 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 92.7 ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, Shilingi bilioni 2.5 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 90.2 ni fedha za nje. Aidha, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 55 kwa ajili ya mpango wa kunusuru uchumi kwa mchanganuo ufuatao:-

Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kufidia bei ya wakulima wa pamba kwa shilingi 80 kwa kilo ya pamba iliyouzwa katika msimu wa ununuzi wa 2009/2010; na shilingi bilioni 35 kwa ajili ya ununuzi na usafirishaji wa nafaka kupitia Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*National Food Reserve Agency - NFRA*). Bajeti ya Wizara ikijumuisha fedha zilizopatikana kwa ajili ya mpango wa kunusuru uchumi imefikia shilingi bilioni 283.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 10 Juni 2010, Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 177.8 kutoka Hazina sawa na asilimia 93.1 ya kiasi kilichoidhinishwa. Hadi tarehe 10 Juni 2010, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 171.0 sawa na asilimia 96.2 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 10 Juni, 2010, fedha za bajeti ya maendeleo zilizotolewa ni shilingi bilioni 65.7 na matumizi ni shilingi bilioni 62.9 sawa na asilimia 96.0 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa *ASDP*, Wizara za Sekta ya Kilimo zilifanya ufuatiliaji na mapitio ya utekelezaji wa

*DADPs* ngazi ya Wilaya na Vijiji. Matokeo ya mapitio na ufuatiliaji huo yameonyesha mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa katika utekelezaji wa *ASDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa eneo la umwagiliaji kutoka hekta 264,388 mwaka 2006 hadi hekta 331,490 mwaka 2009/2010 ambapo jumla ya kaya 200,000 zimenufaika na ongezeko hilo la eneo la umwagiliaji. Kutokana na kuimarishwa kwa skimu za umwagiliaji kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wastani wa uzalishaji wa mpunga katika skimu za umwagiliaji umeongezeka kutoka tani 1.8 hadi wastani wa tani 6.0 kwa hekta. Aidha, tija katika uzalishaji wa zao la mahindi kwa wakulima wanaoshiriki utaratibu wa ruzuku mbegu na mbolea umeongezeka kwa mahindi katika Wilaya ya Siha umeongezeka kutoka tani 0.7 kwa hekta mwaka 2006/2007 hadi tani 4.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine yaliyotokana na utekelezaji wa *ASDP* ni pamoja na kuimarika kwa miundombinu ya masoko na maghala vijijini ambapo jumla ya maghala ya kuhifadhia mazao 493, masoko 96, majosho 271 yalijengwa na 187 yalikarabatiwa, malambo 194 yalijengwa na 78 yalikarabatiwa na kilometa 469 za barabara za vijijini (*feeder roads*) zilijengwa. Ujenzi wa miundombinu hiyo umewawezesha wakulima kupata uhakika wa soko na kupunguza gharama za usafirishaji mazao na hivyo kuongeza kipato.

Aidha, jumla ya vituo 55 vya wanyamakazi na Vituo vya Taaluma vya Kata (*Ward Agricultural Resource Centres – WARCs*) 166 vilijengwa. Katika kipindi hicho, matrekta makubwa 81, matrekta madogo 2,154 na plau 1,321 zilinunuliwa kwa lengo la kupanua maeneo ya kilimo na kuongeza tija.

Katika kipindi hicho, mashine 1,852 za kusindika mazao zilinunuliwa. Kati ya hizo, zilikuwepo mashine 78 kwa ajili ya kukaushia kahawa, 64 kukamua mbegu za mafuta, nane (8) za kukamua matunda na 1,095 za kusaga na kukoboa nafaka. Zana hizo ziliwawezesha wakulima kuongeza ubora wa mazao na hivyo kuongezeka bei ya mazao hayo. Kwa mfano, katika Wilaya ya Mbinga bei ya kahawa iliongezeka kutoka shilingi 1,667 kwa kilo mwaka 2006/2007 hadi shilingi 2,288 kwa kilo mwaka 2008/2009 kutokana na ongezeko la ubora uliosababishwa na matumizi ya mashine za kusafisha na kukaushia kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya ziliwezeshwa kupata vyombo vya usafiri kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji na utoaji wa huduma za ugani. Jumla ya magari 100 na pikipiki 1,612 na baiskeli 3,389 zilinunuliwa ili kuboresha utoaji wa huduma za ugani. Kupitia mashamba darasa, jumla ya wakulima 761,452 walipata mafunzo ya kanuni bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu kwa lengo la kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa *ASDP* hususan taarifa

za utekelezaji wa *DADPs* ngazi ya wilaya na vijiji. Uimarishaji huo ni pamoja na kuweka Mfumo wa Kuchambua, Kuhifadhi na Kusambaza Takwimu za Kilimo (*Agriculture Routine Data Base System - ARDS*) kwa kutumia *Local Government Monitoring Database version 2-LGMD2.*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010, niliahidi kuwa nitaangalia uwezekano wa kuwa na waratibu wa *ASDP* katika kanda saba za utafiti. Napenda kulieleza Bunge lako tukufu kuwa waratibu wa *ASDP* wa Mikoa yote wameteuliwa badala ya kanda na kupatiwa hadidu za rejea. Aidha, wamewezeshwa kwa kupatiwa sh. Bilioni 2.62 kwa ajili ya kununulia magari na gharama ya uendeshaji. Halmashauri za Wilaya nazo ziliwezeshwa kupata vyombo vya usafiri kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji na utoaji wa huduma za ugani. Jumla ya magari 100 na pikipiki 1,612 na Baiskeli 3,389 zilinunuliwa ili kuboresha utoaji wa huduma za ugani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha wakulima kununua zana bora kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kuwezesha wakulima kupata zana bora kupitia *DADPs* inayotekelezwa chini ya *ASDP*. Hadi kufikia tarehe 30 Mei 2010, jumla ya matrekta makubwa 53 na matrekta madogo 2,154 yalikuwa yamenunuliwa na kukabidhiwa kwa wakulima katika Wilaya mbalimbali. Katika mpango huo wakulima wanachangia asilimia 20 ya gharama ya matrekta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project – DASIP)* katika mwaka 2009/2010, Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani – *DASIP* unaotekelezwa katika Halmashauri 28 za Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ulitekeleza jumla ya miradi 291 iliyoibuliwa na wananchi katika mikoa hiyo. Kati ya miradi hiyo, miradi 228 ni ya jamii na 63 ni ya vikundi inayolenga kueneza matumizi ya teknolojia na kanuni bora za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya jamii iliyoibuliwa ni pamoja na masoko 43, ukarabati na ujenzi wa malambo 22, madaraja 46, majosho 19, maghala ya kuhifadhia mazao 59, visima vifupi kwa ajili ya mifugo 14, miradi midogo ya umwagiliaji maji 10, machinjio 4, miradi 4 ya hifadhi ya mazingira na miradi 7 ya mashine za kusaga nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kuhusu uandaaji wa Mipango ya Biashara (*Business Plans*) katika kilimo yalitolewa kwa Wawezeshaji Ngazi ya Kata (*WFT*) 780 na wakulima wawezeshaji 771. Vilevile, mafunzo ya rejea ya mbinu bora za kilimo na ufugaji yalitolewa kwa Maafisa Ugani 721 na wakulima wawezeshaji 771. Mafunzo ya kilimo na ufugaji bora yalitolewa kwa vikundi 4,680 kwa kutumia mbinu ya shamba darasa. Vikundi hivyo vinaendelea kupata mafunzo hadi vitakapokamilisha mzunguko wa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vikundi vipatavyo 4,371 ambavyo vilihitimu mafunzo ya shamba darasa msimu uliopita vilipatiwa mafunzo ya kuandaa Mipango ya

Biashara, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya kilimo na ufugaji na tayari vimepatiwa ruzuku ya kuanzisha miradi ya kuvipatia mapato. Mafunzo shirikishi ya uandaaji *DADPs* na *VADPs* bora katika Halmashauri za wilaya 28 na vijiji 780 vilivyo katika eneo la mradi yalitolewa. Vilevile, mradi ulitoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 33 kutoka katika Halmashauri 28 na tano kutoka sektarieti za mikoa kuhusu uimarishaji *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP* mwaka 2009/2010 ulikuwa ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji ambao ulikuwa ukitekelezwa kwenye mikoa 10 ya Tanzania Bara. Taarifa ya kukamilisha utekelezaji wa mradi (*Implementation Completion Report – ICR*) imeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya tathmini ya matokeo ya mradi (*Impact Assessment*) imeonyesha kuwepo kwa ongezeko la tija kwa ekari kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali. Kwa mfano uzalishaji wa zao la mahindi uliongezeka kutoka wastani wa tani 1.4 hadi tani 2.3, mpunga kutoka tani 0.9 hadi 1.444, ndizi kutoka tani 2,109.3 hadi tani 2,797.3 na muhogo kutoka tani 330.2 hadi tani 883.5. Pia matokeo yameonyesha kuwa wakulima wana uwezo wa kupanga na kutekeleza *DADPs* ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya teknolojia za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto za kusimamia fedha na miradi ya *DADPs* kwani baadhi ya Halmashauri zinatumia vibaya fedha hizo na Halmashauri zinabakisha fedha nyingi baada ya mwaka wa fedha kuisha. Aidha, miradi mingi ya ujenzi wa miundombinu haikidhi ubora wa viwango vilivyokusudiwa. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuimarisha usimamizi wa fedha na miradi ya *DADPs* katika Majimbo yao kwani *ASDP* ndio njia pekee ya kumkomboa mkulima kwa kumwezesha kuwa na usalama wa chakula na kuongeza kipato. Wizara itashirikiana na OWM – TAMISEMI kuwapa waheshimiwa Wabunge taarifa zinazohusu mgao wa fedha za *DADPs* kwa wilaya husika ili wazifahamu na hivyo kuwawezesha kufuatilia utekelezaji kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji katika Ngazi ya Taifa, Wizara na Taasisi zake. Utafiti wa Kilimo katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kutoa huduma za utafiti kwa lengo la kubuni teknolojia bora za uzalishaji wa mazao ili kumwezesha mkulima kupata mavuno mengi na kuongeza tija na hivyo kumwongezea kipato na kumpunguzia umaskini. Teknolojia zilizobuniwa ni pamoja na mbegu bora zenye sifa za kutoa mavuno mengi, kuvumilia visumbufu vya mimea, magonjwa na hali ya ukame. Teknolojia nyingine zililenga kubuni kanuni bora za uzalishaji mazao, kutathmini rutuba ya udongo na mifumo ya kilimo na uchumi jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti iligundua na kutoa aina mpya 25 za mbegu za mazao na kuidhinishwa kitaifa kwa ajili ya matumizi ya wakulima. Mbegu zilizotolewa ni pamoja na aina nne za

mahindi ambazo ni UHS 5210 , UHS 5350, Selian H208 na Selian H308. Mbegu za UHS 5210 na UHS 5350 zilitolewa na kituo cha Utafiti cha Uyole ambazo zinafaa kulimwa kwenye maeneo ya ukanda wa juu (mita 1200 – 1600). Mbegu za Selian H208 na Selian H308 zilitolewa na Kituo cha Selian, ambazo zinafaa kwa maeneo ya ukanda wa kati (mita 600-1200). Mbegu hizo zina sifa za kustahimili ugonjwa wa milia (*Maize streak*) na ukungu wa mahindi (*grey leaf spot*) na zinatoa mavuno kati ya tani 8-10 kwa hekta na kukomaa mapema.

Katika kipindi hicho, kituo cha utafiti KATRIN kimetoa kwa mara ya kwanza katika nchi yetu aina 5 za mbegu za mpunga kwa ajili ya maeneo yenye miinuko (*upland*). Mbegu hizo ni Lulu, Ziada, Komboa, Faidika na WAB450-12BLB. Mbegu hizo zinauwezo wa kutoa mavuno kati ya tani 3-4 kwa hekta na zinakomaa kwa muda mfupi. Mbegu hizo zimependekezwa kulimwa katika maeneo ya Kanda za Mashariki, Ziwa, Kusini na Nyanda za Juu Kusini.

Kituo cha Utafiti Naliendele kilitoa aina 5 za mbegu za Karanga za Mnanje-09, Masasi-09, Nachingwea -09, Mangaka-09, na Naliendele-09 pamoja na aina moja ya mbegu ya ufuta ya Mtwara-09. Mbegu hizo zinatoa wastani wa tani 1.0 – 1.5 kwa hekta na kiwango cha mafuta zaidi ya asilimia 51 ukilinganisha na mbegu zinazotumika kwa sasa ambazo zinatoa asilimia 45. Vituo vya Utafiti Ukiriguru na Maruku vilitoa aina mpya 8 za mbegu za muhogo ambazo ni Rangi mbili, Meremeta, Mkombozi, Belinde, Kasala, Suma, Nyakafulo na Kyaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu hizo zina uwezo wa kustahimili magonjwa ya batobato kali (*cassava mosaic disease*) na michirizi ya kikahawia (*cassava brown streak disease*) na zinatoa mavuno kati ya tani 17 na 23 kwa hekta. Kituo cha Utafiti wa Miwa cha Kibaha kilitoa aina 2 za mbegu za miwa za N19 na N25 zenye uwezo wa kutoa mavuno kati ya tani 80 na 120 kwa hekta na zina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa "*smut*".

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilizalisha jumla ya tani 48.2 za mbegu mama (*Breeder's seeds*) na tani 38.9 za mbegu ya msingi za mazao ya chakula na biashara kwa ajili ya kutunza mbegu halisi na kwa matumizi ya kuzalisha mbegu ya msingi katika mashamba ya Wakala wa Mbegu za Kilimo - *ASA* na kwenye makampuni binafsi ya mbegu. Jumla ya vipingili 474,000 vya muhogo, vipandikizi 177,000 vya viazi vitamu na miche 13,600 ya mizabibu ilizalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** tathmini ya mbinu shirikishi za udhibiti wa visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao na tathmini ya madawa asilia na ya viwandani yanayofaa kutumiwa bila kuathiri mazingira zilifanyika katika vituo vya utafiti vya Naliendele, Selian, Ukiriguru, Uyole, Maruku na Ilonga. Matokeo ya utafiti huo ambao ulifanyika Lushoto na Arumeru yameonyesha kuwa wadudu marafiki Nondo Mgongo Almasi – (*Diamond back moth)* wana uwezo wa kudhibiti wadudu wanaoshambulia kabichi kwa asilimia 80. Vilevile, utafiti wa funza mwekundu (*Red bollworm*) wa pamba katika mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini umekamilika na matokeo yaliwasilishwa katika semina za wadau zilizofanyika katika Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau walikubaliana na matokeo ya utafiti huo kwamba kilimo cha pamba akiwepo funza mwekundu hakina tija. Hivyo, walikubali mazao mbadala hasa ya alizeti na ufuta yahimizwe kulimwa na walipendekeza semina kama hizo zifanyike sehemu nyingine. Aidha, matokeo mengine ni pamoja na matumizi ya mchanganyiko wa viuatilifu aina ya *Roundup* lita 4/hekta na lita 2 za *2,4-D Amine* ambayo yana uwezo wa kuangamiza aina mbili za magugu ya mpunga pori na majani mapana na kupendekezwa kutumika kwenye maeneo yanayozalisha mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti wa Udongo na Rutuba ya Ardhi katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Kituo cha Utafiti cha Mlingano kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilikamilisha uboreshaji wa ramani za rasilimali kilimo katika wilaya za Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini ikiwa na lengo la kuainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mpunga na mahindi. Aidha, taarifa za awali za udongo zimekusanywa na kutumika katika kuboresha taarifa za ekolojia za kilimo za kanda katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Vilevile, Wizara ilifanya utafiti wenye lengo la kuinua kiwango cha matumizi ya mbolea ya Minjingu katika Wilaya za Mbinga, Babati na Karatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi kutoka tani 1.5 hadi tani 4.0 kwa hekta. Vilevile, utafiti wa kuongeza matumizi husishi ya mbolea ulifanyika katika Wilaya ya Mbozi. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha ongezeko la uzalishaji wa zao la mahindi kutoka tani 0.7 hadi tani 4.5 kwa hekta. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilifanya tathmini za udongo katika Wilaya 10 za Mkoa wa Arusha na Kilimanjaro na mapendekezo ya matumizi sahihi ya mbolea ya Minjingu yalitolewa na kupelekwa kwenye Wilaya na Vijiji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa Mifumo ya Kilimo na Uchumi Sayansi Jamii, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilifanya tafiti za kuangalia faida inayopatikana katika kilimo kwenye ngazi ya wakulima vijijini (*farm budget*). Tafiti hizo zilizofanyika Nyanda za Juu Kusini zilionyesha kwamba mkulima aliyepandikiza miche ya mpunga na kufuata ushauri wa kilimo bora alipata nyongeza ya faida ya shilingi 1,018,000 kwa hekta ikilinganishwa na mkulima ambaye hakutumia mbegu bora na kupanda kwa kuzitawanya (*broadcasting*) alipata ongezeko la shilingi 695,500 kwa hekta.

Kwa upande wa mahindi mchanganuo ulionyesha kuwa mkulima aliyepanda mbegu bora na kutumia mbolea za viwandani alipata faida ya shilingi 1,034,200 na mkulima ambaye alipanda kwa kuweka nusu ya kiwango kilichopendekezwa alipata faida ya shilingi 201,500 kwa hekta. Matokeo hayo yanatumika kuwashauri wakulima katika kuchagua mazao ya kulima yatakayo wapatia faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha Vituo na Kuimarisha Uwezo wa Watafiti katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuimarisha Mifuko ya Utafiti na Maendeleo ya Kanda *(Zonal Agricultural Research Development Funds- ZARDEFs*) pamoja na mfumo wa *Client Oriented Research and Development Management Approach (CORDEMA*). Jumla ya tafiti 46 zilipitishwa na Kamati za Uendeshaji wa Utafiti katika

Kanda chini ya Mifuko ya Utafiti ya Kanda na kufikia tafiti 110 kwa kanda zote. Tafiti hizo zinalenga kutoa na kusambaza teknolojia kulingana na vipaumbele vya kanda na mahitaji ya walengwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilikarabati mifumo ya maji katika vituo vya utafiti vya Ukiriguru na Mlingano. Aidha, jumla ya nyumba 20 za watumishi zilifanyiwa ukarabati katika vituo vya Makutopora, Ukiriguru, Selian, Uyole, Naliendele, Tumbi, Ilonga na Maruku. Vilevile, Vituo 9 vya Utafiti vya Ukiriguru, Tumbi, Mikocheni, Uyole, Naliendele, Selian, Makutopora, Horti-Tengeru na Ilonga vilipatiwa samani za ofisi.

Katika kipindi hicho, jumla ya watafiti 53 waliendelea kupata mafunzo ya muda mrefu, kati yao 18 Shahada ya Uzamivu (*PhD*), wanne Shahada ya Uzamili (*MSc*.) na 31 shahada ya kwanza (*BSc*.). Katika kuimarisha ujuzi wa watafiti wa uchumi, Wizara ilitoa mafunzo kwa watafiti 30 yanayohusu utayarishaji wa bajeti za uzalishaji mazao (*farm budgets*) na uchambuzi wa takwimu kwa kutumia kompyuta (*SPSS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, watafiti 40 walipata mafunzo ya muda mfupi yanayohusu ushirikishwaji wa wakulima kuweza kutambua, kuchanganua na kuweka vipaumbele vya kutatua matatizo ya wakulima na hatimaye kufanya utafiti shirikishi. Watumishi 60 walipata mafunzo ya muda mfupi yanayohusu mbinu za kufanya utafiti, kuboresha upatikanaji wa habari kwa kupitia maktaba ya elektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, katika mwaka 2009/2010, mahitaji ya mbolea yalikadiriwa kufikia tani 385,000. Hadi mwezi Mei, 2010, jumla ya tani 302,000 sawa na asilimia 79 ya mbolea ikijumuisha mbolea za ruzuku zilikuwa zimepatikana. Aidha, hadi kufikia mwezi Mei 2010, Wizara ilitoa ruzuku ya tani 150,000 za mbolea ikiwemo mbolea ya kupandia tani 75,000 na mbolea ya kukuzia tani 75,000 sawa na asilimia 100 ya lengo. Mbolea hiyo iliwanufaisha wakulima 1,500,000 ikilinganishwa na wakulima 737,000 msimu wa 2008/2009. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezwa kwa bajeti ya ruzuku ya pembejeo baada ya kupata fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Usalama wa Chakula (*Accelerated Food Security Project*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa 20 ambayo ilinufaika na ruzuku ya mbolea ni Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Kigoma, Manyara,Tabora katika Wilaya za Sikonge, Urambo na Igunga; Mara katika Wilaya za Tarime, Serengeti na Bunda; Shinyanga katika Wilaya za Kahama na Bukombe; Kagera katika Wilaya za Chato na Karagwe; Mwanza katika Wilaya za Geita na Sengerema; Mtwara katika Wilaya ya Mtwara; Lindi katika Wilaya ya Lindi; Tanga katika Wilaya za Korogwe, Lushoto na Muheza; Dodoma katika Wilaya za Mpwapwa na Bahi; Pwani katika Wilaya ya Bagamoyo na Singida katika Wilaya za Singida na Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya *Citizen Network for Foreign Affairs* (*CNFA*) ilitoa mafunzo ya taaluma ya biashara, matumizi na hifadhi salama ya pembejeo za kilimo kwa mawakala (*Rural agro-dealers*) 2,702 wa pembejeo

za kilimo kutoka katika Halmashauri 53 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga, Manyara, Tabora na Tanga. Aidha, kati ya hao, mawakala 319 walidhaminiwa kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.23 kutoka benki ya *NMB*. Vilevile, Wizara imekamilisha rasimu ya kanuni za Sheria ya Mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu bora, katika mwaka 2009/2010, mahitaji halisi ya mbegu bora yalikuwa tani 30,000 ambapo upatikanaji wake ulifikia tani 16,148.2 kwa mbegu za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta sawa na asilimia 53.7 ya mahitaji halisi. Kati ya hizo, tani 2,855.5 ni albaki ya msimu wa 2008/2009, tani 6,894.3 zimezalishwa humu nchini zikiwemo tani 97.2 zilizalishwa na wakulima wadogo wanaozalisha mbegu za Daraja la Kuazimiwa (*Quality Declared Seed – QDS*). Uzalishaji wa *QDS* ulipungua ikilinganishwa na tani 300 zilizozalishwa katika msimu wa 2008/2009 kutokana na ukame. Aidha, jumla ya tani 6,395 za mbegu ziliingizwa nchini na makampuni ya mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Wizara ilitoa ruzuku ya mbegu bora za mahindi na mpunga tani 15,150 ikilinganishwa na lengo la tani 15,701 sawa na asilimia 96.5 ya lengo. Wizara pia ilitoa jumla ya tani 290 za mbegu za zao la mtama na tani 85.4 za mbegu za zao la alizeti kwa kutumia utaratibu nje ya vocha. Mbegu hizo zilisambazwa katika Mikoa ya Singida (alizeti) , Dodoma, Mara, Shinyanga, Mwanza na Tabora (mtama). Kiasi hicho cha mbegu kimenufaisha wakulima 121,011 katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency-ASA*) imeendelea kushirikiana na JKT na Magereza ili kuongeza uzalishaji na uenezaji wa mbegu bora nchini. Hadi mwezi Mei 2010, jumla ya tani 918 za mbegu bora za nafaka, mikunde na mafuta zilizalishwa na kusambaza kwa wakulima ikilinganishwa na lengo la tani 1,500. Kati ya kiasi hicho, JKT na Magereza kwa pamoja walizalisha tani 484 za mbegu bora. Vilevile, ASA walizalisha miche bora ya maembe 200,000 katika bustani ya Mpiji.

Mheshimiwa Naibu Spika,Kamati ya Taifa ya Mbegu (*National Seed Committee-NSC*) iliidhinisha matumizi ya aina 27 za mbegu mpya za mazao ya mahindi (6), mpunga (5), karanga (5), ufuta (1), muhogo (8) na miwa (2). Aina hizo za mbegu zitasambazwa kwa wakulima kuanzia msimu wa 2010/2011. Mbegu hizo zina sifa za kutoa mavuno mengi, kustahimili ukame, ukinzani dhidi ya magonjwa na kukomaa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, miche bora, katika mwaka 2009/2010, hadi mwezi Mei 2010, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (*Tanzania Smallholder Tea Growers Agency –TSHTDA*) walizalisha miche bora 11,500,000 (sawa na asilimia 95.8 ya lengo la miche 12,000,000) kwa utaratibu wa ruzuku. Vikundi vya wakulima wa chai viliongezeka kutoka 134 mwaka 2008/2009 hadi kufikia vikundi 167 mwaka 2009/2010. Aidha, hadi mwezi Mei, 2010, Taasisi ya Utafiti wa zao la Kahawa (*Tanzania Coffee Research Institute –TaCRI*) ilizalisha jumla ya miche bora ya kahawa 10,400,000 kati ya lengo la kuzalisha miche bora ya kahawa 13,000,000 (sawa na asilimia 80 ya lengo) na

kusambazwa kwa wakulima. Vilevile, vikundi vya wakulima wa kahawa viliongezeka kutoka 540 mwaka 2008/2009 hadi kufikia vikundi 695 mwaka 2009/2010.

Mheshimwa Spika, katika mwaka wa 2009/2010, jumla ya wakulima 576,710 kutoka katika Mikoa ya Shinyanga, Mara, Kigoma, Manyara, Mwanza, Singida, Tabora, Iringa, Morogoro na Pwani walinufaika na ruzuku ya madawa na mbegu bora za pamba tani 15,375 kwa utaratibu wa vocha zilitolewa. Ruzuku hiyo ilitsheleza *acre-packs* 4,653,900 katika eneo la ekari 1,537,500 za zao hilo. Aidha, jumla ya tani 148 na lita 153,395 za madawa ya korosho zilisambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Iringa, Pwani, Ruvuma na Tanga kwa mpango wa ruzuku nje ya utaratibu wa vocha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zana za kilimo katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo na kuhamasisha sekta binafsi kuingiza nchini zana hizo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wake. Uingizaji wa matrekta umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010 jumla ya matrekta makubwa 2,364 na matrekta madogo ya mkono 3,214 yaliingizwa na kuuzwa na makampuni binafsi. Aidha, katika mwaka 2009/2010, jumla ya matrekta makubwa 627 na matrekta madogo 2,219 yaliingizwa nchini kwa ajili ya kusambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliandaa na kusambaza katika Halmashauri za Wilaya 132 viwango vya kiufundi *(specifications)* vitakavyokuwa vinatumika kwa ajili ya ununuzi wa matrekta madogo ya mkono (*power tiller*) yenye 12-15Hp, matrekta (35-90Hp), plau, haro, vipandio na tela. Viwango vingine vya kiufundi vilivyoandaliwa ni pamoja na matrekta makubwa (100-150Hp) na zana zake, mashine za kusindika muhogo, kukamua mbegu za mafuta, kumenya karanga, kupukuchua mahindi, kupura mtama, kuvuna na kunyunyizia dawa shambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia ilitoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matengenezo madogo madogo ya matrekta ya mkono, mashine za kupanda na kuvuna mpunga kwa maafisa zana 40 na wakulima 104 katika Wilaya za Ulanga, Kilombero, Kilosa, Mvomero, Korogwe, Mkuranga, Rufiji na Nzega. Vitini vya matrekta madogo ya mkono vimeandaliwa ili vitumiwe na maafisa zana katika kutoa mafunzo kwa wakulima kuwawezesha kutumia kwa usahihi matrekta hayo. Aidha, maafisa ugani 16 kutoka Wilaya za Urambo, Uyui, Sikonge, Manispaa ya Tabora na Nzega walipata mafunzo kuhusu matumizi ya majembe ya palizi ya kukokotwa na wanyamakazi na wanaendelea kutoa mafunzo kwenye vikundi 10 vyenye wakulima 210 namna ya kutumia wanyamakazi katika palizi. Mafunzo yametolewa pia kwa vikundi 8 vya wakulima wilayani Mkuranga kuhusu mashine za usindikaji wa muhogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Ugani 65 wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya zana bora za kilimo hifadhi ambapo mashamba darasa 46 yenye wakulima 1,137 yameanzishwa katika Wilaya za Moshi Vijijini, Arumeru, Karatu, Babati na Hanang. Mashamba hayo yanatumika kufundishia wakulima kwa vitendo teknolojia mbalimbali kama vile matumizi ya majembe tindo ya kukokotwa na wanyamakazi (*rippers*), mashine

za kupanda bila kukatua (*direct seeders*) na mazao funika kama fiwi (*dolichos lablab*) na mbaazi. Matumizi ya zana hizo pamoja na mazao-funika yanapunguza mkandamizo wa udongo, kuongeza rutuba na kuwezesha udongo kuhifadhi unyevunyevu na kupunguza harubu ya kazi kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuendeleza Vijana katika Kilimo – *One UN Joint Programme* Wizara kwa kushirikiana na mikoa ya Lindi na Mtwara katika hatua ya awali (*pilot phase*) imevipatia vikundi 20 vya vijana seti 20 za mashine za kusindika muhogo na kupatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mashine hizo na uendeshaji wa usindikaji kibiashara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*Food and Agricultural Organization – FAO)* chini ya mpango wa *One UN Joint Programme*. Jumla ya matrekta madogo ya mkono 35 yalipelekwa katika mikoa hiyo na yatagawiwa kwa vikundi vya vijana kwa kutumia utaratibu wa kuchangia asilimia 20 ya gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa pembejeo za kilimo, katika mwaka 2009/2010, Mfuko wa Pembejeo ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Aidha, Mfuko ulikusanya marejesho ya madeni ya nyuma ya kiasi cha shilingi bilioni 3.7 na kufanya Mfuko kuwa na jumla ya shilingi bilioni 7.5. Mikopo ilitolewa kwa wakulima binafsi, wasambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo na zana za kilimo, vikundi vya wakulima, *SACCOS* kupitia Taasisi ya Dunduliza, Benki ya Biashara na Uchumi ya Mkoa wa Kilimanjaro, Benki ya Wananchi Mbinga, Benki ya Ushirika Kagera pamoja na Mifuko ya Pembejeo ya Halmashauri ya Wilaya ya Newala na Tandahimba kwa ajili ya kununulia na kusambaza madawa ya zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 31 Mei, 2010 mikopo iliyotolewa ilikuwa matrekta makubwa mapya 155 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.8, matrekta madogo 50 yenye thamani ya shilingi milioni 399 na ununuzi wa pembejeo za kilimo na mifugo zenye thamani ya shilingi bilioni 2.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi bora ya ardhi, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilikamilisha rasimu ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo (*National Agricultural Land Use Planning and Management Master Plan*). Mpango huo utawasilishwa kwa wadau mbalimbali nchini ili kupata maoni yao kabla ya kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine iliendelea kusimamia na kutoa ushauri wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo. Wizara ilishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kupitia mradi wa *Globally Important Agicultural Heritage Systems (GIAHS)* unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia *FAO*, iliainisha mifumo mbalimbali asilia ya kilimo na ufugaji endelevu katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Ruvuma ili kuiendeleza kwa misingi ya vigezo vya Kimataifa vya kuitambua rasmi kama urithi wa dunia (*World Agricultural*

*Heritage*). Mifumo asilia ya kilimo iliyopendekezwa hadi sasa ni “Kihamba” (*Chagga home – gardens*), “Ndiva” (*Pare ndiva system*) na “Ngoro” (*Matengo pits*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*ASA*) na Mamlaka ya Kuendeleza Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*), ilihakiki na kupima maeneo saba yaliyo chini ya Taasisi hizo kwa lengo la kupata hati ya kumiliki ardhi. Katika kipindi hicho maeneo yaliyohakikiwa ni pamoja na makao makuu ya Wizara na mashamba ya mbegu ya Msimba na Mbozi. Aidha, hatua za awali za kupima shamba la mbegu Bugaga zimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitoa mafunzo juu ya uandaaji Mipango ya Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kilimo na Mifugo (*Land Use Management Plans*) kwa wataalam 35 wa hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi na Maafisa Kilimo kutoka Halmashauri za Wilaya 35. Mafunzo hayo yalihusisha pia matumizi ya vifaa vya upimaji ardhi na mashamba (*GPS and Total Station*) kwa lengo la kuboresha takwimu za kilimo na matumizi ya zana nyingine kama *line level* kwa ajili ya kuhifadhi udongo na maji mashambani kwa njia ya kilimo cha matuta.

Wizara ilihimiza Halmashauri za Wilaya za Same, Lushoto, Korogwe, Morogoro na Mvomero kuibua miradi ya hifadhi ya udongo na maji mashambani kupitia *DADPs* ambapo mafanikio yameanza kupatikana kwa kutumia kilimo cha matuta ya ngazi. Kwa mfano, wakulima katika kata za Chome na Vunta Wilayani Same; Tarafa ya Mlalo Wilayani Lushoto na baadhi ya vijiji katika Wilaya ya Korogwe wana uhakika wa kupata mavuno na wanaweza kulima mara mbili kwa mwaka.

Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imeanzisha shamba darasa kwa ajili ya kueneza kanuni za kilimo bora pamoja na hifadhi ya udongo shambani. Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Wizara imetathmini athari za kimazingira zinazotokana na kilimo na mabadiliko ya tabianchi wilayani humo na kuandaa mkakati wa kuibua miradi yenye tija itakayotekelezwa kupitia *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya kuhifadhi mazingira katika kilimo, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendelea kuratibu, kudhibiti na kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuwa na kilimo endelevu. Tathmini ya athari ya shughuli za kilimo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mazingira zilifanyika katika Halmashauri za Wilaya za Urambo, Sikonge, Iramba, Singida Vijijini, Masasi, Newala, Same na Siha.

Tathmini hiyo ilibaini athari za uharibifu wa ardhi zinazotokana na matumizi mabaya ya pembejeo, mmomonyoko wa udongo kutokana na kilimo kisichozingatia hifadhi ya mazingira hasa katika miteremko milimani; ukataji misitu ovyo kwa ajili ya upanuzi wa mashamba, nishati na ujenzi wa nyumba; uchafuzi wa mazingira kutokana na viwanda vya usindikaji mazao na upotevu wa bioanuai.

Wizara kupitia mradi wa *Joint Programme on Environment* (*JP* 11) ilitoa mafunzo kwa wataalam na wahamasishaji wa maendeleo 114 kutoka Timu za

Wawezeshaji za Wilaya na Kata, pamoja na Madiwani katika Halmashauri za Wilaya ya Sikonge, Iramba na Sumbawanga juu ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (*Strategic Environmental Assessment*). Mafunzo pia yalitolewa kwa wataalam 45 wa kilimo, mifugo, mazingira na sheria kutoka Halmashauri za Wilaya za Bunda, Manispaa ya Musoma, Misungwi, Manispaa ya Songea, Songea Vijijini, Namtumbo, Mbinga, Arumeru kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ushauri wa kitaalam, huduma za ugani, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Huduma za Ugani ulioanza mwaka 2007/2008. Kupitia mkakati huo, hadi mwezi Juni 2010, jumla ya wataalam 1,802 walikuwa wameajiriwa katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini. Aidha, wanafunzi tarajali 1,999 ambao wamemaliza mafunzo kwa vitendo ya utoaji wa huduma za ugani kwenye wilaya za mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Kigoma, Tabora, Mara, Shinyanga na Morogoro wanatarajiwa kuajiriwa ifikapo mwezi Oktoba 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kueneza mbinu shirikishi jamii ya Shamba Darasa katika kueneza teknolojia sahihi za kilimo chenye tija kwa kutoa ushauri katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jumla ya Maafisa Ugani 11 walipata mafunzo ya mbinu za shamba darasa na wakulima 55 kutoka skimu 11 za kilimo cha umwagiliaji walipata mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha mpunga. Wakulima walionufaika walitoka katika skimu za Ulyanyama (Sikonge); Nkiniziwa na Budushi (Nzega); Igulubi (Igunga); Mkuti (Kigoma); Nyinda (Shinyanga); Ngeme (Kishapu); Buyubi (Maswa); Igogwa (Misungwi); Luchili (Sengerema); na Chereche (Rorya). Aidha, maafisa ugani 117 kutoka Halmashauri za Wilaya 56 za mikoa 10 walipata mafunzo ya ukufunzi wa shamba darasa. Mikoa hiyo ni Rukwa, Ruvuma, Kilimanjaro, Pwani, Morogoro, Singida, Tanga, Arusha, Manyara na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Juni 2010, jumla ya mashamba darasa 6,711 yenye wakulima 174,376 yalianzishwa katika Halmashauri zilizoko katika Mikoa ya Mara, Manyara, Dodoma, Tabora, Rukwa, Tanga, Mbeya, Kigoma, Singida, Mwanza, Arusha, Morogoro, Pwani, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Shinyanga na Iringa. Aidha, kupitia ruzuku za *DADPs* nyumba 16 za wataalam wa ugani zimejengwa na 10 zimekarabatiwa ili kuboresha utendaji kazi. Wizara inahimiza Halmashauri kujenga nyumba za wagani kwa kutumia ruzuku za *DADPs* na kushirikisha wakulima kuchangia ujenzi wa nyumba hizo.

Wizara pia ilitoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 930 kutoka katika Mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga, Mwanza na Kigoma ambao walifundisha wakulima wenzao 69,750 chini ya usimamizi wa wataalam wa ugani wa Vijiji na Kata. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilitoa mafunzo kwa watoa huduma binafsi 75 na wataalam 118 kutoka Halmashauri za Wilaya kuhusu utaratibu wa kutoa huduma kwa njia ya mikataba kwa kuzingatia Mwongozo wa Sekta Binafsi katika kutoa Huduma za Ugani kwenye Halmashauri. Watoa huduma 30

walioanza kutoa huduma binafsi tangu utaratibu huo ulipoanzishwa wanaendelea kutoa huduma hiyo kwa mikataba katika halmashauri mbalimbali za Wilaya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,**maadhimisho ya sherehe za Nane Nane yalifanyika kitaifa kwenye uwanja wa Nzuguni mkoani Dodoma na katika kanda zote za kilimo ambapo wakulima walipata fursa ya kujifunza teknolojia mbalimbali za kilimo, kubadilishana uzoefu, taarifa za upatikanaji wa masoko na kuzawadiwa kwa wale waliofanya vizuri. Katika maadhimisho hayo, mkulima bora kitaifa mwaka 2009/2010 alitoka katika Kanda ya Kati. Wengine waliozawadiwa walikuwa wakulima bora wa mazao ya pamba na chai. Vilevile, mafunzo kwa njia ya maonyesho ya sinema kuhusu kanuni bora za kilimo pamoja na utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo yalifanyika katika vijiji 124 kwenye mikoa ya Ruvuma, Iringa, Rukwa, Mbeya, Tabora, Kigoma, Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhimisho mengine yalihusu Siku ya Chakula Duniani ambayo yalifanyika kitaifa Wilayani Sumbawanga katika Kijiji cha Matai. Aidha, wakulima waliendelea kuelimishwa kuhusu mbinu za kilimo bora kupitia vipindi vya redio 52 vya Ukulima wa Kisasa, vipindi vya Luninga, vijitabu na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya kilimo kwa wataalam, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010, niliahidi kuwa Wizara itafundisha wanafunzi 2,400 wa ugani katika vyuo vyake vya kilimo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilifundisha wanafunzi 3,498 ngazi za Stashahada na Astashahada na kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wagani wanafunzi 1,999. Mafunzo kwa vitendo yalihusu kuwafundisha wakulima kanuni bora za kilimo, hususan matumizi sahihi ya pembejeo katika Wilaya 64. Katika kipindi hicho, Wizara pia ilifadhili mafunzo ya muda mrefu kwa wakufunzi 11 katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilichopo Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia iliandaa mtaala wa umwagiliaji maji mashambani (*Irrigation*) pamoja na kuhuisha mtaala wa kufundishia mafunzo ya kilimo cha mazao ya bustani (*horticulture*) ili kukidhi mahitaji ya wadau mbalimbali wa kilimo. Kazi zingine zilizofanyika ni pamoja na: kukarabati na kujenga miundombinu mipya na kununua samani kwa ajili ya vyuo vya Kilimo vya Mtwara, Maruku, Tumbi, Ilonga, Kilacha, Inyala na Uyole kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (*Japan International Cooperation Agency – JICA*), Wizara ilitoa mafunzo yanayolenga kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo cha umwagiliaji katika vyuo vinne vya *KATC* Moshi, Igurusi, Ilonga na Ukiriguru ambavyo viliendelea kutekeleza mpango wa kutoa mafunzo kwa wakulima katika skimu kumi (10) za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu zinazoshiriki mpango huo ni Chikuyu (Manyoni), Lumuma (Mpwapwa), Mwangeza (Iramba), Mlenge (Iringa), Naming’ong’o (Mbozi), Lekindo (Tunduru), Minepa (Ulanga), Njagi (Kilombero), Chomachankola (Igunga) na Rungwe Mpya (Kasulu). Aidha, Wizara ilichapisha nakala 2,100 za vitabu saba vya kiada na rejea vya fani mbalimbali za kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo**,** katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na wakulima iliendelea kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Visumbufu hivyo ni pamoja na kwelea kwelea, nzige, viwavijeshi, panya na maradhi ya mimea ambayo husababisha upotevu wa mavuno wa kati ya asilimia 30 na 40. Udhibiti wa nzige wekundu umefanyika kwenye mazalio yao ya asili katika Mbuga ya Iku-Katavi na Ziwa Rukwa ambapo jumla ya lita 3,775 za viautilifu zilitumika kudhibiti nzige hao kwenye eneo la ukubwa wa hekta 6,350.

Aidha, udhibiti wa ndege aina ya Kwelea kwelea zaidi ya milioni 73.2 ulifanyika katika mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Iringa, Morogoro, Mbeya na Dodoma. Ndege hao wana uwezo wa kuharibu tani 732 za nafaka kwa siku. Jumla ya lita 2,575 za kiuatilifu zilitumika katika udhibiti huo kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 1,445. Vilevile, panya walidhibitiwa katika vijiji 151 katika mikoa ya Manyara, Morogoro, Tabora, Lindi, Ruvuma, Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro na Mbeya kwa kutumia chambo chenye sumu kilo 13,898. Udhibiti wa viwavijeshi ulifanyika kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 36,395.2 kutoka mikoa 16 ya Tanzania Bara ambapo jumla ya lita 13,225 za viuatilifu na mabomba 1,350 ya kunyunyizia yalitumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, huduma ya utabiri wa viwavijeshi ilimarishwa katika maeneo yote ambayo huvamiwa mara kwa mara na viwavijeshi ambapo jumla ya mitego 100 ya nondo ilikarabatiwa. Aidha, Wizara iliendelea kuwajengea wakulima uwezo wa kuendeleza utabiri shirikishi katika vijiji 60 ambavyo vilipatiwa mitego ya nondo wa viwavijeshi ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa milipuko.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mafunzo ya mbinu mbalimbali za udhibiti husishi katika mazao ya mbogamboga, viazi, pamba, mahindi, kahawa, migomba yalitolewa katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Shinyanga. Jumla ya wakulima 333 na wataalam 72 kutoka mikoa ya Mara, Shinyanga na Mwanza walipatiwa mafunzo kuhusu udhibiti husishi *(IPM)* katika zao la pamba. Aidha, uzalishaji na usambazaji wa viumbe vya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao kibaiolojia uliendelea katika mikoa ya Pwani, Tanga, Morogoro, Arusha, Dar es Salaam, Ruvuma, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Kagera na Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumdhibiti nzi wa embe, mitego 6,625 ilisambazwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 2,208 katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani na Morogoro ambapo lita 13.3 za *Methyl Eugenol* zilitumika. Wizara kupitia taasisi ya *International Centre of Insect Physiology and Ecology (ICIPE )* - Nairobi Kenya iliingiza jumla ya wadudu 8,700 wanaodhibiti nzi wa maembe kibaiolojia. Pia Wizara iliiruhusu taasisi ya *International Institute of Tropical Agriculture (IITA)* - Benin kuingiza aina mbili za manyigu wa kudhibiti nzi mweupe anayeharibu mimea mbalimbali. Sanjari na hilo, Wizara iliiruhusu *Agro EcoConsultants* kuingiza aina tatu za wadudu walawangi wanaodhibiti visumbufu katika zao la maua aina ya waridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo pia yalitolewa kwa wakaguzi wa mazao 12 kutoka wilaya zote za mkoa wa Tabora. Mafunzo hayo yalihusika na jinsi ya kumdhibiti

nzi wa maembe kwa kutumia wadudu walawangi *(biological control agents)*. Aidha, jumla ya mbawakavu 5,000,000 kwa ajili ya kudhibiti magugu maji katika Ziwa Viktoria walizalishwa na kusambazwa katika mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya wakulima 83 na wataalamu 60 kutoka katika mikoa ya Shinyanga, Mara na Iringa walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu ili kupunguza athari zinazosababishwa na matumizi mabaya ya viuatilifu katika mazingira na kwa afya ya binadamu. Aidha jumla ya viuatilifu vipya 311 vilisajiliwa na kuingizwa nchini.

Kazi za kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayosafirishwa nje ya nchi ziliendelea kutekelezwa kwenye vituo vya mipakani ili kudhibiti ueneaji wa visumbufu vya mimea na kurahisisha biashara ya mazao ndani na nje ya nchi. Jumla ya tani 2,529,665.0 za mazao mbalimbali zilikaguliwa kabla ya kusafirishwa nchi za nje na tani 589,817.9 zilikaguliwa kabla ya kuingizwa nchini. Vyeti 4,773 vya usafi wa mazao na vibali 318 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa mazao ya kilimo, katika msimu wa 2009/2010, uzalishaji wa baadhi ya mazao makuu asilia ya biashara uliongezeka na mengine ulipungua. Mazao ambayo uzalishaji wake uliongezeka yalikuwa ni pamba asilimia 33.1; tumbaku asilimia 3.7; sukari asilimia 1.2 na pareto asilimia 121.3. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chai, mkonge, kahawa na korosho ulishuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali Na. 1 uzalishaji wa mazao makuu asilia ya biashara (tani). Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara asilia, tumbaku, katika msimu wa 2009/2010 uzalishaji wa tumbaku uliongezeka kutoka tani 58,702 mwaka 2008/2009 hadi kufikia tani 60,900 ikilinganishwa na lengo la tani 60,000 lililokuwa limewekwa. Ongezeko la uzalishaji wa zao la tumbaku lilitokana na upanuzi wa maeneo ya uzalishaji, matumizi ya pembejeo pamoja na kuzingatiwa kwa kanuni bora za kilimo cha zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2009/2010, uzalishaji wa chai ulipungua kutoka tani 34,165 mwaka 2008/2009 na kufikia tani 33,160 ikilinganishwa na lengo la kuzalisha tani 35,000. Uzalishaji wa zao la chai ulipungua kutokana na ukame uliyoyakumba maeneo mengi ya uzalishaji wa zao hilo. Sababu nyingine zilizosababisha kushuka kwa uzalishaji ni pamoja na mgogoro uliotokea kwenye mashamba ya chai ya Lupembe ambao ulisababisha jumla ya hekta 200 za zao la chai kutovunwa pamoja na mgogoro kati ya wakulima wa chai Rungwe na Chama cha Ushirika Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2009/2010, uzalishaji wa pareto uliongezeka kutoka tani 1,500 mwaka 2008/2009 hadi kufikia tani 3,320 ikilinganishwa na lengo la kufikia tani 4,800. Ongezeko hilo lilitokana na ongezeko la tija kutoka kilo 650 kwa hekta hadi kilo 700 kwa hekta kufuatia matumizi ya miche bora na vikaushio bora vya maua ya pareto. Vilevile ubora wa pareto uliimarika kutokana na kuongezeka kwa sumu kutoka asilimia 1.6 hadi 1.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2009/2010, uzalishaji wa pamba mbegu uliongezeka kutoka tani 200,662 hadi kufikia tani 267,004 ikilinganishwa na lengo la tani 250,000. Uzalishaji wa zao hilo uliongezeka kutokana na matumizi sahihi ya madawa ya kuulia wadudu yaliyotolewa kwa utaratibu wa ruzuku, kushindanisha wakulima wa pamba na kuwepo kwa mvua za kutosha katika maeneo yanayozalisha zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, uzalishaji wa sukari uliongezeka kutoka tani 276,605 mwaka 2008/2009 hadi kufikia tani 279,850 ikilinganishwa na lengo la tani 317,000 lililotarijiwa katika kipindi hicho. Uzalishaji wa sukari uliongezeka kutokana na upanuzi wa kiwanda cha *TPC*, kuongezeka kwa uwezo wa usindikaji katika Kiwanda cha Kagera *Sugar Limited* pamoja na upanuzi wa mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa katika msimu wa 2009/2010, uzalishaji wa kahawa ulishuka kutoka tani 62,345 mwaka 2008/2009 na kufikia tani 40,000 ikilinganishwa na lengo la kuzalisha tani 50,000. Aidha, kushuka kwa uzalishaji kulichangiwa na tabia ya zao la kahawa kupunguza tija katika msimu unaofuatia misimu ambayo uzalishaji ulikuwa mkubwa; ukosefu wa mvua wakati wa kutoa maua na kubeba matunda; uvamizi wa wadudu waharibifu waitwao vidung'ata wa kahawa (*Coffee mealy bugs*) katika Wilaya ya Mbinga; ugonjwa wa mnyauko fusari (*Fusarium wilt*) Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mkonge katika msimu wa 2009/2010 ulishuka kutoka tani 33,208 za msimu wa 2008/2009 hadi kufikia tani 26,363 kutokana na mdororo wa uchumi duniani ambao ulisababisha wakulima wa mkonge nchini kupunguza kiwango cha uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, uzalishaji wa zao la korosho ulishuka kutoka tani 79,068 na kufikia tani 74,169 kutokana na hali mbaya ya hewa, hususan kuwepo kwa ukungu uliofuatiwa na hali ya ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa mazao ya chakula**,** Wizara iliendelea kuratibu kazi na majukumu ya Taasisi mbalimbali katika Sekta ya Kilimo kwa lengo la kuhakikisha tija na uzalishaji wa mazao ya chakula unaongezeka katika ngazi zote. Kazi zilizofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuzijengea uwezo ngazi za mikoa na Halmashauri kusimamia kwa ufanisi zaidi usambazaji wa pembejeo zenye ruzuku ili kuwafikia walengwa kwa wakati na kwa bei nafuu. Pembejeo hizo ni pamoja na mbolea, mbegu bora (mahindi, mpunga, mtama, alizeti ) na viuatilifu.

(ii) Kuimarisha uwezo wa mikoa kuratibu utekelezaji wa *ASDP* kwa kuanzisha ofisi ya Mratibu wa *ASDP* katika ngazi ya Mkoa. Halmashauri za Wilaya zilijengewa uwezo wa kuandaa, kusimamia utekelezaji na kutathmini *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa mazao yanayostahimili ukame na ya nishati, katika kuendeleza mazao yanayostahimili ukame, hususan muhogo, Wizara ilishirikiana na Idara ya Magereza na JKT kuzalisha takriban vipando milioni 17 vya muhogo vyenye ukinzani dhidi ya ugonjwa wa batobato kali na magonjwa mengine ya muhogo ili kuwezesha upatikanaji endelevu wa vipando bora vya muhogo kwa wakulima. Vipando hivyo vilizalishwa katika Halmashauri za Masasi, Mtwara, Nachingwea, Korogwe, Bagamoyo, Serengeti, Sengerema, Kibondo, Urambo, Bukombe na Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tangu mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya nishati ilishiriki katika maandalizi ya maeneo ya kuzingatiwa katika Mwongozo wa Kilimo cha Mazao ya Nishati nchini. Maandalizi hayo yalihusisha Wizara za Nishati na Madini, Kilimo Chakula na Ushirika, Fedha na Uchumi, Katiba na Sheria, Maliasili na Utalii, Maji na Umwagiliaji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa la Mazingira (*NEMC*), Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Shirika la Taifa la Maendeleo ya Mafuta (*TPDC*) na sekta binafsi. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kudhibiti kilimo cha mazao ya nishati, Serikali ilichukua hatua ya awali ya kuagiza Wakuu wa Mikoa kuwa waangalifu katika kutoa ardhi kwa wawekezaji na kuhakikisha kuwa ardhi inayofaa kwa mazao ya chakula haitumiki kwa mazao ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa bodi ya nafaka na mazao mchanganyikoi, Serikali imeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa Sheria Na. 19 ya mwaka 2009 (*The Cereals and Other Produce Act 2009*). Lengo ni kuwepo kwa chombo cha kusimamia uendelezaji wa mazao ya nafaka na yasiyonafaka pamoja na biashara ya mazao hayo ndani na nje ya nchi. Kufuatia hatua hiyo, mchakato wa kujadili mwongozo wa kufanya bodi hiyo kuanza utekelezaji wa majukumu yake umeanza kwa kuwashirikisha wadau ili kujadili mwongozo na masuala mbalimbali kuhusu Bodi hiyo. Aidha, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo ameteuliwa ili kuwezesha Bodi hiyo kuanza shughuli zake mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji mazao ya bustani, mbegu za mafuta na viungo, uzalishaji wa mazao ya bustani, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010, niliahidi kuwa Wizara kwa kushirikiana na wadau na taasisi za *Horticulture Development Council of Tanzania* (*HODECT*), *Tanzania Horticulture Association* (*TAHA*) na *Cluster Competitiveness Program* chini ya *Tanzania Private Sector Foundation* (*TPSF*) itaandaa Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani *(National Horticulture Development Strategy*). Napenda kulieleza Bunge lako tukufu kuwa Mkakati huo umeandaliwa na kupitishwa katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wadau wa Mazao ya Bustani uliofanyika Arusha tarehe 31 Mei, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, uzalishaji na usambazaji wa vipando bora vya mazao ya bustani uliendelea katika bustani za Serikali za Mpiji, Bugaga, Songa, Malindi, Jaegetal na Igurusi. Jumla ya miche 200,000 ya miembe ilipandwa kwa ajili ya kubebeshwa tayari kusambazwa kwa wakulima. Mafunzo kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya viungo na matunda yalitolewa kwa wataalam wa bustani 30 kutoka katika Wilaya za Mikoa ya Tanga, Mbeya, Morogoro na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara inaendelea kuwatambua na kuwasajili wazalishaji binafsi wa vipando na mbegu za mazao ya bustani ili wazalishe vipando bora kulingana na Sheria ya Mbegu ya Mwaka 2003 *(Agricultural Seed Act of 2003).* Kwa mfano, msimu wa 2009/2010 katika Mkoa wa Dar es Salaam wazalishaji binafsi 25 walizalisha jumla ya miche milioni 1.7 ya mazao mbalimbali ikiwemo ya miembe, michungwa, parachichi, papai, migomba, mikarakara na mipera.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu za mafuta, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhimiza uzalishaji na usindikaji wa mazao ya mbegu za mafuta, hususan alizeti, ufuta, michikichi, karanga na soya kupitia *DADPs* katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuendeleza mazao hayo. Katika msimu wa 2009/2010, Serikali ilitoa rukuzu kwa ajili ya mbegu za zao la alizeti. Wizara imeendelea kuhimiza utaratibu wa kilimo cha mkataba. Kupitia utaratibu huo, Bodi ya Pamba Tanzania inashirikiana na *Tanzania Gatsby Trust* kuendeleza kilimo cha zao la pamba nchini ambapo makampuni ya kuchambua pamba yanashiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa zao la soya**,** katika mwaka 2009/2010, Wizara iliandaa mkakati wa kuendeleza zao la soya ili kuiwezesha nchi yetu kufikia lengo la kuzalisha wastani wa tani 750,000 za soya ifikapo mwaka 2020 kati ya tani milioni mbili zinazoweza kuzalishwa. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*SUA*) kupitia mradi wa *Tropical Legume II Project* (TLII) iliendelea kuhamasisha uendelezaji wa zao hilo, hususan kwa ajili ya utengenezaji wa maziwa ya soya. Kutokana na juhudi hizo, mashine ya kusindika maziwa ya soya itasimikwa Mikumi Wilayani Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika kilimo, katika mwaka 2009/2010**,** Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Kilimo la Taifa iliendelea kuainisha vivutio vya uwekezaji vya kodi na visivyo vya kodi katika kilimo kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika sekta hiyo. Jumla ya mapendekezo 50 ya vivutio vya uwekezaji vya kodi yaliwasilishwa kwenye Kamati ya Kitaifa ya Kurekebisha Mfumo wa Kodi ambapo vivutio vya msamaha wa kodi vilivyokubaliwa ni 16 kupitia bajeti ya mwaka 2010/2011. Kati ya vivutio hivyo, 9 vinahusu sekta mazao na 7 sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivutio vya msamaha wa kodi vilivyopitishwa ni pamoja na:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye usafirishaji wa mazao ya kilimo kutoka shambani hadi kwenye viwanda vya usindikaji kwa wakulima wenye kilimo cha mkataba wa miwa, mkonge na chai;

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Zana za Kilimo kama vile; kivuna nafaka (*combine harvester*), *pick up balers*, *hay making machinery* na *mowers* vinavyotumika mahsusi kwenye uzalishaji wa kilimo na mifugo;

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani katika usafirishaji wa maua kwa ndege kwenda nje ya nchi;

(iv) Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mabanda yanayotumika katika kilimo cha maua (*green houses*);

(v) Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uzalishaji wa bidhaa na huduma zitolewazo kwa wakulima waliosajiliwa au mashamba ya Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mashamba kama vile mitaro ya umwagiliaji, barabara za mashambani, ujenzi wa maghala au huduma nyinginezo za namna hiyo;

(vi) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye usindikaji na uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini;

(vii) Kusamehe unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya juisi za matunda na bidhaa za maziwa. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji na kuboresha thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vya juisi na maziwa hapa nchini;

(viii) Kurejesha utaratibu wa kutambua baadhi ya vifaa kama bidhaa za mtaji *(deemed capital goods)* kwa baadhi ya Wawekezaji kwa nia ya kuvipa unafuu wa Kodi.

(ix) Kuongeza kiwango cha ushuru wa kusafirisha nje Korosho ghafi kutoka asilimia 10 hadi 15 au Dola za kimarekani 160 kwa tani moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Lengo ni kulinda viwanda, kuongeza ubora na thamani ya korosho na kukuza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliendelea kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) na Baraza la Biashara la Taifa kuhamasisha uwekezaji kupitia Azma ya Kilimo Kwanza. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Benki Kuu iliendelea na mchakato uanzishaji wa Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa chakula, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu na taarifa za hali ya chakula nchini. Mafunzo yalitolewa kwa wataalam katika Halmashauri za Wilaya na Miji katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kuhusu ufuatiliaji wa hali ya mazao mashambani na hali ya chakula. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya tathmini za kina katika maeneo yaliyobainika kuwa na upungufu wa chakula ili kutambua kaya zenye upungufu, mahitaji yao ya chakula na kuchukua hatua kukabiliana na upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (*Tanzania Meterological Authority-TMA*) ilifanya *survey* na mafunzo ya mifumo ya ukusanyaji wa taarifa za mvua katika vituo vya kupima mvua katika mikoa yote nchini kwa ajili ya kufufua na kuanzisha vituo vinavyokusudiwa kuunganishwa katika mfumo wa kisasa (*Automation*) wa ukusanyaji na uwasilishaji wa takwimu na taarifa za mvua na mazao mashambani kwa ajili ya uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya chakula katika ngazi ya Taifa, katika mwaka 2009/2010, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*National Food Reserve Agency*-NFRA) ilipanga kununua jumla ya tani 165,000 za mazao ya nafaka zikiwemo tani 160,000 za mahindi na tani 5,000 za mtama. Hadi mwezi Mei 2010, *NFRA* ilikuwa imenunua tani 73,682.7 za mahindi yenye thamani ya shilingi bilioni 24.5, sawa na asilimia 46 ya lengo. Lengo la ununuzi halikufikiwa kutokana na fedha za ununuzi kutopatikana wakati muafaka.

Kiasi hicho cha ununuzi wa mahindi kikijumuishwa na akiba iliyokuwepo ghalani mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa ununuzi ya tani 89,842 za mahindi iliifanya *NFRA* kuwa na akiba ya chakula yenye jumla ya tani 163,525.2 za mahindi. Hadi tarehe 12 Juni 2010, *NFRA* ilikuwa imetoa tani 100,991.3 za mahindi kwa Idara ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa chakula na maafa mbalimbali na hivyo kubakiwa na tani 50,300.4 za mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya chakula na usindikaji Wizara ilitoa mafunzo ya teknolojia za hifadhi bora na matumizi ya mazao ya nafaka na mikunde katika halmashuri 17 za Mbinga, Tunduru, Namtumbo, Songea (V), Songea (M), Kilindi, Muheza, Korogwe, Mkinga, Handeni, Nachingwea, Kilwa Masoko, Lindi (V), Ruangwa, Mkuranga, Kibaha na Bagamoyo kwa wataalam wa kilimo 138 ili kupunguza upotevu wa mazao na kuongeza uhakika wa chakula nchini.

Wizara ilitoa mafunzo ya ujenzi wa maghala bora ya kuhifadhia nafaka na mikunde kwa wataalam 10 na wawakilishi wa vikundi vya wakulima 120 katika Halmashauri ya Iramba mkoani Singida. Aidha, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya usindikaji wa mazao ya muhogo, mboga na matunda katika Wilaya za Kasulu, Tunduru, Ruangwa, Bunda na Nachingwea ambapo jumla ya wawakilishi wa vikundi vya wakulima 340 na wataalam 23 walipatiwa mafunzo hayo kutoka katika mikoa ya Kigoma, Ruvuma, Lindi na Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilitoa mafunzo ya kuibua miradi kwa wawezeshaji 109 kutoka Halmashauri za Wilaya za Bahi, Mpwapwa, Chamwino, Karatu, Ngorongoro, Longido, Monduli, Simanjiro, Babati (V), Babati (M) na Kiteto ili kuwajengea uwezo wataalam wa wilaya hizo kuwa na mbinu za kuibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula katika ngazi ya kaya itakayoingizwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji (*VADPs)* na hatimaye kuingizwa kwenye *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurekebisha na kuhuisha sera na sheria, katika mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha uhuishaji wa Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 ili kuwa na Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2009. Aidha, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa Muswada wa Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*The Cereal and Other Produce Act, 2009*); kukamilisha miswada ya sheria mbalimbali za mazao na Sheria ya Korosho, Miswada hii ilipitishwa na Mkutano wa Bunge wa 17 uliofanyika kati ya mwezi Oktoba na Novemba, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, rasimu ya awali ya Sheria ya Kusimamia Rasilimali za Kilimo (*The Agricultural Resources Management Legislation*) imeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yao. Mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika na muswada wa marekebisho ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mimea (*Plant Breeders Right*) yamekamilika na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Kanuni za Kusimamia Sheria ya Mbolea na sheria mbalimbali za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sensa ya kilimo, Wizara za Sekta ya Kilimo kwa Tanzania Bara na Visiwani zikishirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar, ziliendelea na zoezi la Sensa ya Kilimo na Mifugo. Taarifa ya Sensa ya Kilimo inaendelea kuandaliwa na timu ya wataalam kwa kuandaa majedwali na uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa tayari kwa uchambuzi. Aidha, rasimu ya taarifa ya utafiti wa kufuatilia kaya (*Panel Survey*) imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni yao kabla ya taarifa hiyo kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu kabambe ya mageuzi na modenaizesheni ya ushirika (*Cooperative Reform and dernization program*). Kuimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilisimamia chaguzi za theluthi moja ya wajumbe wa bodi za Vyama Vikuu na Vyama vya Msingi vilivyokuwa vimefikisha muda wake wa uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003.

Wizara pia iliteua wajumbe maalum wa Bodi wenye uzoefu katika masuala ya uendeshaji wa ushirika husussan, katika benki *KCBL* na *TANECU* kwa lengo la kuimarisha uongozi. Aidha, *KCBL* ilijengewa uwezo kwa kupewa mhasibu mwenye sifa. Wizara ilitoa mafunzo kwa wajumbe wa Bodi za Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*TFC*), na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SCCULT*).

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kuhamasisha wananchi kuanzisha au kujiunga kwenye vyama vya ushirika. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ilishirikiana na wadau wengine kuhamasisha wananchi kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika kupitia mikutano mbalimbali ya ushirika, vyombo vya habari, na maadhimisho ya Kitaifa yakiwemo ya

Siku ya Ushirika Duniani na ya Nane Nane. Kutokana na jitihada hizo, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka milioni 1.8 mwaka 2009 hadi milioni 2.1 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika kupitia utekelezaji wa *CRMP*. Miongoni mwa vyama vipya vilivyoanzishwa ni Chama Kikuu cha Madini cha Tarime (*Tarime Mining Cooperative Union*) kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo, Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku wa Kigoma (*Kigoma Tobacco Growers Cooperative Union*) na Chama Kikuu cha Warina-asali nchini (*Tanzania Beekeepers Cooperative Union*).

Mheshimiwa Naibu Spika**,**Wizara iliendelea kuimarisha *SACCOS* ili zitoe huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi, hususan waliopo vijijini. Idadi ya SACCOS iliongezeka kutoka 5,332 mwaka 2009 hadi 5,344 mwaka 2010. Aidha, idadi ya wanachama iliongezeka kutoka 820,670 hadi 911,873 katika kipindi hicho ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.1. Katika kipindi hicho, hisa za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 33.5 hadi shilingi bilioni 36.7, akiba na amana za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 148.1 hadi bilioni 174.6. Vilevile, mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi bilioni 383.5 hadi shilingi bilioni 463.4 sawa na ongezeko la asilimia 20.8. Mikopo hiyo ilikuwa kwa ajili ya mitaji ya biashara, kilimo, ufugaji, ujenzi wa nyumba, karo za shule, ununuzi wa matrekta madogo *(power tillers*) na matrekta makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kueneza matumizi ya mfumo wa stakabadhi za maghala, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kueneza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Lindi na Pwani. Kupitia mfumo huo, Vyama vya Ushirika katika mikoa hiyo vimekusanya Korosho za wakulima zenye jumla ya kilo 73,359,109 ambapo wakulima katika awamu ya kwanza walilipwa asilimia 70 ya bei dira ya shilingi 700 kwa daraja la kwanza na shilingi 570 kwa daraja la pili na pia kulipwa malipo ya awamu ya pili ya asilimia thelathini baada ya mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Vyama vya Ushirika vya mikoa ya Lindi na Mtwara vililipa wakulima malipo ya ziada ya kati ya shilingi 50 hadi 350 kwa kilo ya korosho baada ya kukamilisha hesabu zao. Kutokana na utaratibu huo, baadhi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi vimewalipa wakulima kati ya shilingi 1,000 hadi 1,050 kwa kilo ikilinganishwa na bei waliyokuwa wanapata wakulima ya shilingi 200 hadi 350 kwa kilo kabla ya mfumo huu kuanza kutumika. Aidha, kutokana na kutumika kwa mfumo huo, wakulima wamehamasika kuongeza uzalishaji wa zao la korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa lengo la kupunguza gharama na kumwezesha mkulima kupata malipo mazuri zaidi chini ya mfumo huo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko pamoja na wadau wengine ilipitia upya gharama za ununuzi na uuzaji wa korosho. Maeneo ya kupunguza gharama ambayo yameainishwa ni pamoja na magunia, usafirishaji, usambazaji wa fedha, ushuru

wa vyama, kupuliza madawa, unyaufu, ushuru wa Wilaya, riba ya mikopo na gharama za mwendesha ghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika kuwezesha utekelezaji wa mfumo huo, Wizara ilisaidia katika upatikanaji wa mikopo toka vyombo vya fedha (*NMB* na *CRDB*) ambapo Vyama vya Ushirika vya Msingi 291 vilivyo chini ya Vyama Vikuu vya *MAMCU* na *TANECU* (Mtwara), ILULU (Lindi), *CORECU* (Pwani) na *TAMCU* (Tunduru) vilipata mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 38.7 katika msimu 2009/2010. Urejeshaji wa mikopo katika maeneo ya Vyama ni takriban asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufufua na kuimarisha vyama vya tumbaku, kuanzia msimu wa 2009/2010, Wizara ilielekeza kutenganishwa kwa shughuli za usambazaji wa pembejeo na ununuzi wa tumbaku ambapo Vyama vya Ushirika kwenye maeneo ya uzalishaji wa tumbaku vilipewa jukumu la ununuzi na usambazaji wa pembejeo na makampuni yalipewa jukumu la kununua tumbaku. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara iliratibu majadiliano kati ya benki za *CRDB* , *NMB* na Vyama vya Ushirika ambayo yalifanikisha upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 36 kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vilivyonufaika na mikopo hiyo ni *CHUTCU* (Mbeya), *CETCU* (Singida), *LATCU* (Rukwa), *KACU* (Shinyanga), *SONAMCU* (Ruvuma) na *WETCU* (Tabora). Hadi tarehe 17 Februari 2010, Vyama vya Ushirika vilisambaza kwa wakulima wa Tumbaku jumla ya tani 22,941 za aina mbalimbali za mbolea. Hii ni sawa na asilimia 100 ya mahitaji yao. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza ahadi yake ya kulipa madeni ya nyuma ya wakulima wa tumbaku kwa makampuni ya ununuzi wa tumbaku ya TLTC na AOTTL. Hadi tarehe 15 Juni, 2010, jumla ya shilingi bilioni 1.4 zilikuwa zimelipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kuimarisha uendeshaji wa *SACCOS* na Benki za Ushirika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 139 wa mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Dodoma, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Mara, Kagera, Mwanza, Shinyanga, Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Arusha kuhusu matumizi ya miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa *SACCOS* ili kuwaongezea uwezo wa uendelezaji, ukaguzi na usimamizi wa *SACCOS*. Mafunzo hayo ni sehemu ya usambazaji wa miongozo ya *SACCOS* ya Uhasibu (*Accounting and Financial Management Manual),* Ukaguzi (*Audit guideline*) na Ukaguzi wa kawaida (*Inspection guideline*) na Mfumo wa Taarifa za Menejimenti (*MIS guideline*). Miongozo hiyo itaviwezesha Vyama kuendeshwa kwa kuzingatia sheria, taratibu na viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika, katika mwaka 2009/2010, Wizara ilifanya ukaguzi wa Chama Kikuu cha *TANECU* na Vyama vya Msingi 212 katika mkoa wa Mtwara na Vyama vya Msingi 117 katika mkoa wa Lindi. Ukaguzi huo ulilenga kubaini hali ya uendeshaji wa Vyama husika na mapendekezo yalitolewa kuhusu hatua zinazostahili kuchukuliwa ili kurekebisha dosari zilizojitokeza katika uendeshaji wa shughuli za ununuzi wa korosho kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala.

Taarifa ya ukaguzi inaendelea kufanyiwa kazi na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wale ambao watabainika kuhusika na ubadhirifu wa fedha za wanachama. Kwa kutambua umuhimu wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), Wizara iliendelea kutoa ruzuku ili kuiimarisha utendaji wake. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya Vyama 1,722 vikijumuisha *SACCOS* 917, Vyama vya Mazao 720, Vyama Vikuu 14 na vyama vinginevyo 71 vilikaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha tume ya maendeleo ya ushirika katika mwaka 2009/2010, Wizara ilikamilisha maandalizi ya kuanzishwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo inategemewa kuleta msukumo mkubwa katika uhamasishaji, uanzishaji, uimarishaji na uendelezaji wa Ushirika nchini. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imetayarisha bajeti inayojitegemea kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa UKIMWI Wizara iliendelea kutekeleza jukumu la kupambana na kuzuia maambukizi ya UKIMWI miongoni mwa watumishi. Wizara ilitoa semina, vipeperushi na mabango yaliyohamasisha watumishi kujikinga na maambukizi ya UKIMWI. Katika kipindi hicho, watumishi walihamasika na wengi wao kujitokeza kupima virusi kwa hiari na watumishi 18 waliothibitika kuwa na virusi vya UKIMWI wamewezeshwa kupata matibabu na lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya jinsia, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ilifanya ukaguzi wa masuala ya jinsia katika Wizara (*Gender Audit).* Matokeo ya ukaguzi huo yatatumika katika kuandaa Mwongozo wa kuingiza masuala ya jinsia kwenye shughuli za kilimo. Aidha, mafunzo ya jinsia yalitolewa na chuo cha *ESAMI* kwa Wajumbe watano (5) wa Kamati ya Jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya rasilimali watu, katika mwaka 2009/2010, jumla ya watumishi 174 wa kada mbalimbali waliajiriwa ili kuongeza nguvu katika utoaji wa huduma katika Wizara. Aidha, wataalamu wa kilimo wapatao 1,014 wamepelekwa kwenye Sekretarieti za Mikoa na mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa ili waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kuwapandisha vyeo watumishi 432 katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma; kutoa mafunzo elekezi *(induction course)* kwa waajiriwa wapya 49 kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazotumika katika utumishi wa umma. Vilevile, Wizara iliendelea kufanya ukaguzi wa watumishi *(Human*

*Resources Audit)* ili kuwa na taarifa na kumbukumbu sahihi za watumishi wote wa Wizara waliopo kwenye orodha ya malipo ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma Awamu ya Pili *(Public Sector Reform Program Phase II –PSRP II)* kwa kutoa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi *(Open Performance and Appraisal System-OPRAS)* kwa wakufunzi watarajali *(Training of Trainers- TOT).* Aidha, mafunzo kwa wasaidizi wa kumbukumbu 20 yametolewa ikiwa ni pamoja na kuimarisha masijala kwa kuweka vifaa imara vya kuhifadhi kumbukumbu pamoja na kompyuta.

Wizara imeimarisha huduma za Serikali Mtandao kwa kuweka mawasiliano ya *internet* kati ya Makao Makuu ya Wizara na vituo vya utafiti vya Naliendele, Tumbi, Ukiriguru na Uyole pamoja na kuweka mtambo wa kisasa wa mawasiliano ya simu za ndani Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mpango wa mwaka wa 2010/2011 katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ya *ASDP* ambayo lengo lake ni kuimarisha usalama wa chakula na kupunguza umaskini. Aidha, katika utekelezaji wa *ASDP* Wizara itazingatia misingi iliyoainishwa kukidhi Malengo ya Milenia (*MDGs*), MKUKUTA II na Kilimo Kwanza ambayo yote yanalenga kukuza uchumi, kupunguza umaskini uliokithiri na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa na Wakuu wa Nchi za Afrika walipokutana Maputo Msumbiji mwaka 2003, na kupitisha Programu Kabambe ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Barani Afrika *(Comprehensive African Agriculture Development Programme – CAADP),* Wizara katika utekelezaji wa *ASDP* imekidhi vigezo vya *CAADP* na hivyo inatarajia kutia saini hati ya makubaliano inayodhihirisha kuwa Tanzania imekidhi vigezo vya *CAADP*. Utiaji saini unatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa mwezi wa Julai, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, utekelezaji wa Azma ya Kilimo Kwanza umeanza kuungwa mkono na sekta binafsi ndani na nje ya Tanzania kufuatia Mkutano wa Uchumi wa Dunia *(World Economic Forum)* uliofanyika Dar es Salaam, Tanzania tarehe 5-7 Mei, 2010. Kutokana na Mkutano huo, makampuni ya *Unilever*, *YARA, DUPONT, SAB-Miller, General Mills, Syngenta, Monsanto* na Shirika la *AGRA* yamekubaliana na Tanzania kuanzisha miradi mbalimbali ya kukuza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor Tanzania – SAGCOT*). Mkutano wa kwanza kwa lengo la kuandaa andiko la awali kwa ajili ya utekelezaji wa *SAGCOT* ulifanyika Dodoma tarehe 8 Juni, 2010 na kuhudhuriwa na wawakilishi wa sekta binafsi wa ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa programu ya kuendelezxa sekta ya kilimo (ASDP)mwaka 2010/2011, utakuwa ni mwaka wa tano wa utekelezaji wa *ASDP*. Programu hii aidha, inatekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi

(*Decentralization by Devolution – D by D*) kwa kupeleka karibu asilimia 75 ya raslimali za Sekta ya Kilimo wilayani na vijijini. Utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya wilaya utaendelea kutekelezwa kupitia *DADPs*. Ili kutekeleza sera hiyo Halmashauri zilipatiwa maelekezo ya kiasi cha fedha ambazo zitatengwa kwa kila Halmashauri ili zitumie katika matayarisho ya mipango na bajeti zao kwa mwaka 2010/2011 na kujadiliwa na Kamati ya Fedha ya Halmashauri husika na hatimaye kupitishwa na Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti za mikoa zimetengewa jumla ya shilingi bilioni 102.4 zitakazopelekwa kwenye Halmashauri kutokana na Mfuko wa Pamoja wa *ASDP* na *DASIP*. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 97.5 ni fedha za nje na shilingi bilioni 5.0 ni fedha za ndani. Kati ya kiasi hicho cha fedha za nje, *DASIP* itachangia shilingi bilioni 15.6. Aidha, ofisi za Waratibu wa *ASDP*, ngazi ya Mkoa zimetengewa jumla ya Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kusimamia, kuratibu na kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Wizara za Sekta ya Kilimo zimetengewa shilingi bilioni 56.9 na kati ya fedha hizo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imetengewa shilingi bilioni 21.7 zitakazotumika kuboresha huduma za utafiti, ugani, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, hifadhi ya mazingira, usalama wa chakula, kuanzisha kituo cha utafiti chenye ubora wa hali ya juu (*Centre of excellence*), huduma za ugavi na manunuzi, sheria, uratibu na ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika,kufuatia kumalizika kwa kipindi cha utekelezaji cha mradi wa *PADEP* ifikapo Juni 30, 2010 kazi kubwa itakayofanyika ni kuainisha uzoefu na mafanikio yaliyopatikana. Wizara itaendelea kutumia wataalam walioshiriki katika utekelezaji wa *PADEP* kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Vijiji. Miongoni mwa kazi zitakazofanyika ni pamoja na kutumia uzoefu wa *PADEP* katika kuimarisha vikundi na mitandao ya wakulima, kushiriki katika mafunzo ya ujasiriamali miongoni mwa wakulima na kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya *ASDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa uwekezaji katika sekta ya kilimo Wilayani (*DASIP*)katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo (*DASIP)* imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya 28 wa kuibua, kupanga na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji (*VADPs*) na Wilaya (*DADPs*) yenye ubora unaokubalika;

(ii) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa Wakulima na wataalam wa kilimo na mifugo ili kuwapatia maarifa na utaalam wa kuendesha kilimo bora cha mazao na mifugo. Aidha, mafunzo ya uimarishaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo pamoja na utafiti wa masoko kwa mazao ya kilimo na mifugo yatatolewa kwa wataalam na wakulima;

(iii) Kujenga miradi ya umwagiliaji 14 katika eneo la mradi;

(iv) Kujenga mfumo wa masoko utakaowezesha wakulima na wafugaji kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi; na

(v) Kuimarisha usimamizi wa miradi inayotekelezwa katika wilaya zilizo chini ya mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa kilimo, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kutekeleza Nguzo ya 4 na 8 za Kilimo Kwanza kwa kubuni teknolojia bora za uzalishaji wa mazao mbalimbali zinazolenga kumwezesha mkulima kupata mavuno mengi na kuongeza tija na hivyo kumwongezea kipato na kumpunguzia umaskini. Utafiti wa zao la mahindi utafanyika katika Vituo vya Utafiti vya Uyole, Selian, Ilonga na Ukiriguru.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa zao la mpunga utafanyika katika vituo vya KATRIN, Dakawa, Ukiriguru na Uyole. Aidha, utafiti wa zao la mtama na uwele utafanyika katika vituo vya Ilonga na Hombolo na utafiti wa zao la ngano utafanyika katika vituo vya Uyole na Selian. Vilevile utafiti wa mazao ya jamii ya mikunde utafanyika katika Vituo vya Utafiti vya Uyole, Selian na Ilonga; Utafiti wa mazao jamii ya mizizi utafanyika katika vituo vya Ukiriguru, Kibaha, Naliendele, Uyole na Maruku. Pia utafiti wa zao la ufuta na karanga utafanyika Naliendele, na alizeti utafanyika Ilonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao mengine yatakayofanyiwa utafiti na vituo vyake ni pamoja na minazi (Mikocheni), korosho (Naliendele), zabibu (Makutupora), mkonge (Mlingano), pareto (Uyole), miwa (Kibaha) na pamba (Ukiriguru na Ilonga). Katika tafiti hizo, Wizara itaendelea kutafiti na kutathmini vizazi mbalimbali kwa madhumuni ya kutoa angalau mbegu saba mpya za mazao zenye tija kubwa zaidi, kustahimili ukame, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi viwango vya ubora, na matakwa ya watumiaji wa mbegu hizo na kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao yatakayohusika ni alizeti, pamba, ufuta, kartamu, karanga, mahindi, mpunga, mtama, ngano, shayiri na jamii ya mikunde. Mazao mengine ni viazi, muhogo, migomba, mboga mboga, matunda na viungo. Aidha, mbegu mama kiasi cha tani 60 za aina mbalimbali za mazao zitazalishwa ili kukidhi mahitaji ya mbegu kwa ajili ya mashamba ya kuzalisha mbegu. Vilevile, Wizara itaendelea na utafiti wa bioteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kubuni na kutathmini aina tatu za mbinu shirikishi za udhibiti visumbufu na magonjwa ya mimea na mazao na kutathmini madawa ya asili na ya viwandani yanayofaa kutumika bila kuathiri mazingira na kwa gharama nafuu.

Aidha, kituo cha Taifa cha Kutunza Nasaba za Mimea (*National Plant Genetic Resource Centre-NPGRC*) kilichopo Taasisi ya Utafiti wa Viautilifu vya Tropiki (TPRI) Mkoani Arusha kitaendelea kukusanya na kuhifadhi vinasaba kwa kushirikiana na vituo vingine vya utafiti. Vilevile, tathmini ya njia bora za usindikaji na uongezaji wa thamani kwa mazao mbalimbali kwa ajili ya kupanua soko kwa mkulima itafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa udongo na rutuba ya ardhi, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Mlingano, Uyole, Selian na Ukiriguru itahakiki na kupendekeza teknolojia angalau tano za urutubishaji husishi wa udongo (*Integrated Soil Fertility Management options*) kwa kila ikolojia za kilimo zilizoko katika wilaya 53 ambazo zinapata ruzuku ya pembejeo.

Vilevile, Wizara itaendelea na utafiti wenye lengo la kutathmini, kuhakiki na kutoa mapendekezo juu ya viwango vya matumizi ya mbolea. Kituo cha utafiti cha Mlingano kitaendelea na kazi ya kuboresha ramani za rasilimali kilimo kwa kutumia teknolojia ya Mfumo wa Habari wa Kijiografia kwa ajili ya kuainisha maeneo ya uwekezaji. Kazi hii itaendelea kufanyika katika wilaya za Mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Lindi, Mtwara na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaendelea kufanya uchunguzi wa sampuli za udongo kwenye kituo hicho ili kuweza kubaini teknolojia sahihi za kilimo endelevu na maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mahindi na mpunga katika wilaya za Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini. Kazi hiyo itaendelea kufanyika kwa kuzingatia mkakati maalum wa kuufanya Mkoa wa Mororgoro kuwa ghala la Taifa (Fanya Morogoro Ghala la Taifa-FAMOGATA).

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki wa matumizi ya mbolea ya Minjingu pamoja na Minjingu Mazao utaendelea katika Kanda za Mashariki, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Jumla ya sampuli za udongo 3,000 toka kwa wadau mbalimbali zitachunguzwa na kutolewa ushauri kuhusu virutubisho vinavyopaswa kuongezwa kwenye udongo ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa mifumo ya kilimo na uchumi sayansi jamii, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kufanya tafiti za sayansi jamii na uchumi kuhusu matatizo yanayoathiri uenezaji mzuri wa teknolojia za kilimo. Tafiti hizo zitafanywa katika kanda za Kaskazini, Mashariki, Nyanda za Juu Kusini, Kati, Kusini, Magharibi na Ziwa. Aidha, Wizara itaendelea kutayarisha bajeti za uzalishaji wa mazao ya mahindi, mpunga, muhogo, mtama na pamba kwenye kanda zote ili zitumike kufahamisha watalaam wa ugani na wakulima gharama za uzalishaji na faida inayopatikana kwa kila zao. Wizara pia itafanya tathmini ya matokeo ya tafiti *(impact studies)* kwa zao la mahindi ili kutambua mchango wa utafiti wa mahindi katika kuongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha vituo na kuimarisha uwezo wa watafiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi watafiti kwa kukarabati baadhi ya nyumba za kuishi wafanyakazi katika vituo vya Selian (nyumba mpya 1), Maruku (2) Makutupora (2), Naliendele (4), Ukiriguru (3), Tumbi (3), na Ilonga (4) na kukarabati mifumo ya maji katika vituo vya Naliendele na KATRIN. Katika kipindi hicho, barabara iendayo kituo cha utafiti Uyole kutoka barabara kuu ya Dar Es Salaam - Tunduma itaendelea kufanyiwa matengenezo (Kilomita mbili). Aidha, Wizara itanunua magari nane ambayo yatasambazwa katika vituo vya KATRIN (2), Ukiriguru (1), Mlingano (1), Naliendele (2), Ilonga (1) na HORTI Tengeru (1) pamoja na kuongeza vitendea kazi ambapo kompyuta 70 zitanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza uwezo wa watafiti, Wizara itatoa ufadhili kwa watafiti 52 kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu, kati ya hao 15 ni Shahada ya Uzamivu (*PhD*.), 11 Uzamili (*MSc*.) na 26 Shahada ya kwanza (*BSc).* Vilevile, mafunzo ya muda mfupi yatatolewa kwa watumishi wapatao 250 kulingana na fani zao ikiwa ni pamoja na watafiti, madereva, wasaidizi wa ofisi na makatibu muhtasi. Katika kipindi hicho, watafiti sita waliokuwa wakipata mafunzo ya *MSc*. watahitimu masomo yao na kurudi kwenye vituo vyao vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** chini ya mfumo wa usimamizi wa rasilimali na utafiti unaowalenga wadau yaani *Client-Oriented Research Development and Management Approach* (CORDEMA), Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watafiti 310 katika vituo 17 vya utafiti ili kuwajengea uwezo wa kuandaa na kutekeleza tafiti zenye kutatua mahitaji yanayotokana na vipaumbele vya kanda na wadau wake pamoja na kusimamia rasilimali za utafiti ili kuleta ufanisi katika ugunduzi wa teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuboresha Mifuko ya Uta fiti ya Kanda (*Zonal Agricultural Research and Development Fund- ZARDEF*) mintaarafu ya kufanya tafiti za kilimo zinazolenga kutoa teknolojia sahihi za kutatua matatizo ya uzalishaji. Jumla ya tafiti 140 zitafanyika katika kanda zote saba. Katika kuhakikisha kuwa teknolojia nyingi zilizogunduliwa na watafiti zinawafikia haraka walengwa, katika mwaka 2010/2011, Vitengo Unganishi katika kanda saba za utafiti na ugani vitaimarisha mbinu za kusambaza teknolojia kwa kutumia nyenzo rahisi za kufikisha ujumbe kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kutoa simulizi 35 za mafanikio ya utafiti na ugani (*success stories*) kwa kanda saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mradi wa kuanzisha Kituo cha Ubora wa Hali ya Juu cha Utafiti wa zao la mpunga kwa kanda ya Afrika Mashariki na Kati (*Regional Rice Centre of Excellence*) utaendelea kutekelezwa chini ya Programu ya Afrika Mashariki ya Kuendeleza Tija ya Kilimo na Uzalishaji (*Eastern Africa Agricultural Productivity Programme*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu hiyo itatoa msukumo wa pekee wa kubuni na kuendeleza teknolojia za mpunga na kuhakikisha kuwa zinatumiwa na walengwa kwa wingi nchini na nchi za Afrika Mashariki na Kati ambazo ni wanachama wa Taasisi ya Kuimarisha Utafiti wa Kilimo Afrika Mashariki na Kati (*Association for Strengthening*

*Agricultural Research in East and Central Africa – ASARECA).* Kituo cha Utafiti cha KATRIN – Ifakara ndicho kitakachoongoza na kuratibu shughuli za utafiti kikisaidiana na vituo vyote vya utafiti katika kanda saba za utafiti, vyuo vya mafunzo ya kilimo na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa pembejeo, katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kugharamia ruzuku ya mbolea, mbegu bora, miche bora ya kahawa na chai pamoja na madawa ya pamba na korosho (Nguzo ya 4 na 7 za Kilimo Kwanza). Idadi ya wakulima watakaonufaika na mpango wa ruzuku itaongezeka kutoka wakulima 2,076,710 mwaka 2009/2010 hadi wakulima 2,576,710 mwaka 2010/2011 wakiwemo wakulima 2,000,000 kwa mazao ya chakula na wakulima 576,710 kwa zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa 20 ambayo itanufaika na ruzuku ya mbolea na mbegu bora ni Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Kigoma, Manyara,Tabora katika Wilaya za Sikonge, Urambo na Igunga, Mara katika Wilaya za Tarime, Serengeti, Bunda na Rorya, Shinyanga katika Wilaya za Kahama na Bukombe, Kagera katika Wilaya za Chato na Karagwe, Mwanza katika Wilaya za Geita na Sengerema, Mtwara katika Wilaya za Mtwara, Newala na Masasi; Lindi katika Wilaya za Lindi, Nachingwea na Ruangwa; Tanga katika Wilaya za Korongwe, Lushoto, Kilindi, Handeni na Muheza; Dodoma katika Wilaya za Mpwapwa , Bahi, Kongwa na Kondoa; Pwani katika Wilaya za Bagamoyo na Rufiji; na Singida katika Wilaya za Singida Vijijini, Manyoni na Iramba.

Hivyo, kiasi cha mbolea ya ruzuku kitaongezeka kutoka tani 150,000 za mwaka 2009/10 hadi kufikia tani 200,000 mwaka 2010/2011. Mbegu bora za mahindi na mpunga zitaongezeka kutoka tani 15,150 hadi tani 20,000 mwaka 2010/2011. Kwa upande wa zao la pamba mikoa itakayonufaika ni Shinyanga, Mara, Kigoma, Manyara, Mwanza, Singida, Tabora, Morogoro, Pwani na Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miche bora, katika kuongeza matumizi ya miche bora, Wizara itaongeza usambazaji wa miche ya kahawa kufikia miche 15,000,000 kutoka miche 13,000,000 mwaka 2009/2010 na chai miche 15,000,000 mwaka 2010/2011 kutoka miche 12,000,000 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mradi wa Kuongeza Usalama wa Chakula, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuelimisha wakulima katika mikoa yote itakayofaidika na ruzuku ya pembejeo za kilimo ili zitumike kama ilivyokusudiwa;

(ii) Kuelimisha Kamati za Vocha za Taifa, Mkoa, Wilaya na Vijiji ili kusimamia utekelezaji wa ruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha;

(iii) Kuendelea kuwasaidia wakulima wadogo wanaozalisha mbegu bora za daraja la kuazimiwa;

(iv) Kuongeza uwezo wa Taasisi 3 za Utafiti (Selian-Arusha, Ilonga-Morogoro na Uyole-Mbeya) wa kuzalisha mbegu mama;

(v) Kuimarisha Kituo cha Utafiti cha Mlingano kufanya utafiti wa Matumizi Husishi ya Rutuba ya Udongo; na

(vi) Kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya Msimba (hekta 150), Kilangali (hekta 200) na Arusha (hekta 50) yanayoendeshwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo (*ASA*) ili kuongeza uzalishaji wa mbegu za msingi na zilizothibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kama zifuatazo:-

(i) Kuimarisha Mamlaka ya Kudhibiti Matumizi bora ya mbolea hapa nchini (*Tanzania Fertilizer Regulatory Authority- TFRA*);

(ii) Kusimamia utekelezaji wa uzalishaji wa mbegu za Daraja la Kuazimiwa (*Quality Declared Seed-QDS*) kwa kutumia wakulima wadogo;

(iii) Kuendelea kuwapatia mafunzo na kuwaongezea uwezo mawakala wa pembejeo (*Rural Agro Dealers*) na kupewa dhamana ya kupata mikopo ya kununua pembejeo; na

(iv) Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora zilizozalishwa na ASA kutoka tani 918 za mwaka 2009/2010 hadi tani 2,000 katika msimu wa 2010/2011;

(v) Kuzalisha miche ya matunda 350,000 na vipando vya mihogo 25,000,000; na

(vi) Kuimarisha Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (*TOSCI*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa ruzuku ya pembejeo za mazao ya pamba na korosho. Zao la pamba litapata ruzuku ya mbegu bora tani 10,000 na madawa *acrepacks* 4,653,900 kwa ajili ya ekari 1,537,500. Utoaji wa ruzuku kwa zao hilo utafanyika kwa utaratibu wa vocha. Aidha, zao la korosho litapata ruzuku ya madawa lita 64,000 na tani 3,000 za madawa ya unga.

Mheshimiwa Naibu Spika, zana za kilimo**,** katika mwaka 2010/2011, Wizara itatoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga na matumizi sahihi ya matrekta madogo ya mkono kwa vikundi 40 vyenye wakulima 1,000 katika skimu za umwagiliaji 40 zilizoteuliwa kuendesha kilimo bora cha mpunga ili kuongeza tija na mapato. Wakulima hao watafundishwa kuendesha kilimo kwa kutumia zana bora za kilimo kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Arusha, Meru, Babati, Karatu, Hanang, Moshi Vijijini, Same, Kilindi, Mvomero na Kongwa itatoa mafunzo kwa wakulima kuhusu matumizi ya zana bora za kilimo hifadhi. Aidha, vikundi 10 vya wakulima vitawezeshwa kuanza kutumia teknolojia mpya ya matumizi ya mashine za kupanda bila kukatua "*direct seeders*" zinazovutwa na matrekta madogo ya mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itashirikiana na Halmashauri za Kibaha, Kisarawe, Rufiji, Mkuranga, Bagamoyo, Mtwara Vijijini, Masasi, Nanyumbu, Lindi Vijijini na Ruangwa kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima na wakulima wadogo katika usindikaji wa muhogo, korosho na ukamuaji wa mbegu za mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya kushirikisha vijana katika kuendeleza kilimo**.** katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kiufundi kwa Halmashauri za Wilaya na wakulima juu ya matumizi bora ya zana hasa matrekta madogo ya mkono. Mafunzo yatatolewa juu ya matumizi na matunzo ya matrekta madogo ya mkono na mashine za kusindika muhogo (*chipper, grater, presser na milling machine)* ikiwa ni pamoja na kuendesha kilimo kwa kutumia zana bora za kilimo na usindikaji kibiashara kwa vikundi 35 vya vijana katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) chini ya Mpango wa *One UN Joint Programme.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembejeo za kilimo, katika mwaka 2010/2011, Mfuko wa Pembejeo umetengewa kisasi cha shilingi bilioni 3.8 zitakazotumika kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo pamoja zana za kilimo. Mikopo itakayotolewa ni ya matrekta makubwa 62 na madogo 63. Mfuko pia umepanga kukusanya marejesho ya mikopo iliyoiva yenye thamani ya shilingi bilioni 5.6 ambazo zitatumika kutoa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo. Kutokana na marejesho yatayopatikana, Mfuko umepanga kutoa mikopo ya matrekta 100 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.8, matrekta madogo 117 yenye thamani ya shilingi milioni 819 na pembejeo za kilimo na mifugo zenye thamani ya shilingi milioni 485.5.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** mafunzo ya kilimo kwa wataalam, katika mwaka 2010/2011, Wizara itatoa mafunzo ya muda mrefu ya astashahada na stashahada kwa vijana 5,499 katika vyuo 15 vya Wizara na binafsi (Nguzo ya 8 ya Kilimo Kwanza). Mafunzo hayo yanalenga kuwaandaa vijana kutoa huduma za ugani kwa wakulima. Wizara pia itagharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wakufunzi 10 wa shahada ya kwanza, wakufunzi 8 shahada ya uzamili na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 60 katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya muda mfupi (*refresher/upgrading courses*) yatatolewa kwa wakufunzi 40 kutoka kwenye vyuo vya kilimo pamoja na kuandaa mtaala mpya wa Zana za Kilimo (*Agromechanization*) ngazi ya Stashahada.

Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (*Japan International Cooperation Agency – JICA*), vyuo vinne (4) vya Kilimo (*KATC*, *MATI* Ilonga, *MATI* Ukiriguru na MATI Igurusi) vitawezeshwa kupanua na kutoa mafunzo ya umwagiliaji katika skimu 12. Aidha, vyuo vingine vitakarabatiwa na kuboresha samani, vitendea kazi, vifaa na nyenzo za kufanyia kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za ugani**,** katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuimarisha utoaji wa huduma za ugani (Nguzo ya 8 ya Kilimo Kwanza) kwa wakulima kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuboresha uenezaji wa teknolojia katika kilimo kwa kutumia mbinu shirikishi jamii katika kilimo, ikiwa ni pamoja na matumizi ya Shamba Darasa ambayo imeonyesha kuwa na manufaa kwa wakulima ambapo mashamba darasa 6,000 yenye wakulima 150,000 yanatarajiwa kuanzishwa mwaka 2010/2011;

(ii) Kuimarisha mfumo wa kutumia mkulima kuwafundisha wakulima wenzake *(Farmer-to-Farmer Extension)*, kwa kutoa mafunzo kwa wataalam na kuusimamia. Pia Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wakulima kupitia vipindi vya redio, vijitabu, machapisho, vipeperushi, mabango na kuonyesha sinema vijijini kwa kuzingatia kanda za kilimo kupitia ofisi Kiungo za Mawasiliano za Kanda;

(iii) Kutoa ushauri wa kitaalam wa kuendesha shughuli za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama njia ya kudumisha viwango vya utoaji wa huduma hizo;

(iv) Kuhimiza Halmashauri za Wilaya kuwapatia wataalam wa ugani vitendea kazi vikiwemo magari, pikipiki na baiskeli, kuwajengea nyumba za kuishi, kujenga Vituo vya Taaluma ya Kilimo vya Kata na kutoa mafunzo;

(v) Kuwezesha vikundi vya wakulima 30 kutoka mikoa ya Rukwa, Iringa, Morogoro, Mbeya, Ruvuma, Kigoma, Mara, Shinyanga, Manyara na Tabora ili kuendesha kilimo cha kibiashara;

(vi) Kutoa mafunzo kwa vijana tarajali ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa ugani vijijini;

(vii) Kuratibu mashindano ya Kilimo na maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nane Nane na Siku ya Chakula Duniani; na

(viii) Kushirikisha na kuwezesha sekta binafsi na asasi zisizokuwa za kiserikali kutoa huduma za ugani kwa kuzijengea uwezo na kuboresha utoaji wa huduma hizo na kuanzisha jukwaa la watoa huduma ili kurahisisha uratibu wa utoaji huduma za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya k ilimo, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kukagua, kutabiri na kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea hususan, kwelea kwelea, nzige wekundu, viwavijeshi

na panya (Nguzo ya 7 ya Kilimo Kwanza). Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuwajengea uwezo wataalam wa ugani na wakulima wa kupambana na visumbufu vya mazao kwa kutumia teknolojia rahisi. Teknolojia hizo ni pamoja na matumizi ya udhibiti husishi (IPM), wadudu walawangi na mimea katika udhibiti wa visumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma nyingine zitakazotolewa na Wizara zinahusu kusimamia Sheria ya Afya ya Mimea ya Mwaka 1997 hususan, katika udhibiti wa uagizaji, usambazaji, biashara na matumizi ya viuatilifu, na huduma za karantini ya mimea na mazao yake yanaposafirishwa nje au yanapoingizwa ndani ya nchi. Wizara pia itaendelea kuimarisha huduma katika vituo vyake vya karantini ya mimea na mazao mipakani, bandarini na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya kuhifadhi mazingira katika kilimo**,** katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuratibu, kudhibiti na kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira katika kazi za maendeleo ya kilimo kwa kushirikisha Halmashauri za Wilaya ili kuongeza uzalishaji na kuwa na kilimo endelevu. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau na Halmashauri za Wilaya, itafanya tathmini ya athari ya shughuli za maendeleo ya kilimo kwenye mazingira katika Halmashauri 10 za mikoa ya Manyara, Dodoma, Pwani, Lindi na Iringa kwa lengo la kupata hali halisi ya hifadhi ya mazingira katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaendelea kuhamasisha jamii juu ya matumizi bora ya teknolojia endelevu za kilimo zinazozingatia hifadhi ya mazingira kwa kupitia maadhimisho mbalimbali kama vile sikukuu ya Wakulima Nane Nane, Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Chakula Duniani, Siku ya Ushirika Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na kwa kutumia vyombo vya habari. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam na timu za wawezeshaji kwa mikoa iliyotajwa pamoja na mikoa ya Mtwara na Morogoro kuhusu kilimo endelevu kinachohusisha hifadhi ya ardhi na mazingira na jinsi ya kukabiliana na athari zilizopo zikiwemo zile za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira (*VPO-DoE*), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) pamoja na wadau mbalimbali itatayarisha Mipango na Mikakati ya Kilimo ya Hifadhi ya Mazingira. Aidha, Wizara itaandaa Mwongozo wa Tathmini ya Athari za Mazingira zinazotokana na shughuli za kilimo kwa lengo la kuhakikisha kuwa shughuli za kilimo nchini zinafanyika kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira (Nguzo ya 7 ya Kilimo Kwanza).

Mheshimiwa Naibu Spika**,** hifadhi ya udongo na matumizi bora ya ardhi, Wizara itaendelea kutoa maelekezo ya kitaalamu kwa Halmashauri 12 zinazoathiriwa sana na tatizo la mmomonyoko wa udongo katika mashamba ya wakulima na jinsi ya kukabiliana na tatizo hilo kwa kutumia mbinu na teknolojia mbalimbali za hifadhi ya udongo na maji mashambani. Pia, Wizara itatoa mafunzo ya vitendo kwa wataalam wa kilimo kutoka Halmashauri 22 ili wawe na uwezo wa kuwapatia wakulima mbinu na teknolojia mbalimbali za kudhibiti mmomonyoko wa udongo mashambani kulingana na mazingira ya maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuendeleza matumizi ya teknolojia endelevu za kilimo mseto (za asili na za kisasa) zinazofaa kwa maeneo ya miinuko katika Halmashauri 15 kulingana na mazingira ya maeneo husika ili kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi na kuenea kwa jangwa. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Shirika la Chakula duniani (*FAO*), kuendeleza mifumo asilia endelevu ya kilimo mseto sehemu za miinuko chini ya mradi wa *Globally Important Agicultural Heritage Systems* (*GIAHS*) unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Sekretarieti za Mikoa, itashiriki kikamilifu katika kutambua na kupima maeneo yanayofaa kwa kilimo ili kuchochea kasi ya uwekezaji katika kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kupima ardhi ya vituo vya Utafiti, vyuo vya Mafunzo na Wakala wa Mbegu ili kupatiwa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam kwa maafisa kilimo katika Halmashauri 10 nchini juu ya tathmini ya rasilimali ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo. Vilevile, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na jinsi ya kukabiliana na athari zitokanazo na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa njia ya redio, luninga, mabango na vipeperushi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa maelekezo ya kitaalam kwa Halmashauri 12 kuhusu tathmini na ukusanyaji wa takwimu za ubora wa ardhi ya kilimo ili kuwapa wakulima maelekezo sahihi ya matumizi ya mbolea kulingana na mazingira ya eneo. Aidha, Wizara itatoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri 10 juu ya uandaaji na usimamizi wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ili kuwa na vijiji vya mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam kutoka Halmashauri 24 juu ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya kilimo ili kufanikisha uendelevu wa matumizi ya ardhi hiyo na kupunguza migogoro ya ardhi kwenye vijiji husika. Aidha, Ili kusogeza utoaji wa huduma za matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa Halmashauri za wilaya na vijiji, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vitano vya kanda vilivyokwishaanza kupatiwa wataalam kwa kuboresha mazingira ya kazi na pia kuongeza uwezo wa rasilimali watu na vitendea kazi kwa kanda zote saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa mazao ya kilimo, uzalishajhi wa mazao makuu ya biashara asilia. Wizara kupitia Bodi za Mazao makuu ya biashara asilia (Nguzo ya 4 ya Kilimo Kwanza) itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia uzalishaji na biashara ya mazao hayo hapa nchini. Katika kuhakikisha tija na uzalishaji wa mazao hayo inaongezeka Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya, Wizara itaendelea kuhimiza Halmashauri za Wilaya kuwezesha wakulima kuibua miradi ambayo itaingizwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2010/2011, Wizara kupitia Bodi za Mazao itasimamia ubora wa mazao ili yawe na ubora wa hali ya juu na hivyo kuuzwa kwa bei nzuri katika soko la ndani na nje. Mambo muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na kuelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kutunza mazao mashambani, kuyapanga katika madaraja wakati wa kuuza, kuimarisha huduma za ukaguzi wa mazao, kuhakikisha mazao yanauzwa katika vituo vilivyoidhinishwa na kuhimiza usindikaji wa mazao kabla ya kuyauza. Mategemeo ya uzalishaji wa mazao makuu ya biashara mwaka 2010/2011 ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 279,850 mwaka 2009/2010 hadi tani 317,000 mwaka 2010/2011. Ongezeko litatokana na kupanuka uzalishaji katika viwanda vya Kagera na *TPC* na wakulima wadogo wa miwa kuongeza uzalishaji kutokana makubaliano na Jumuiya ya Nchi za Ulaya kwa kutumia utaratibu wa mashamba makubwa *(block farming)*. Utaratibu huo utarahisisha upatikanaji wa huduma za ugani, pembejeo, uvunaji na usafirishaji wa miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa tumbaku unatarajiwa kuongezeka kutoka tani tani 60,900 mwaka 2009/2010 hadi tani 78,000 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo litatokana na kuwajengea uwezo wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo cha tumbaku, kuwapatia wakulima mbegu bora za tumbaku, ujenzi wa mabani mapya 10,000 ya kukaushia tumbaku ili kuongeza ufanisi wa ukaushaji na kupunguza uharibifu wa majani baada ya mavuno. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa tumbaku kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri ya tumbaku kwa kuhakikisha unakuwepo ushindani katika ununuzi wa tumbaku nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,**uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 33,160 mwaka 2009/2010 hadi tani 35,000 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo litatokana na uvunaji wa chai iliyopandwa miaka miwili iliyopita, ufufuaji wa mashamba yaliyotelekezwa, kutoa mafunzo juu ya kilimo bora cha chai, hususan kwa wakulima wadogo; kuimarisha ukaguzi katika mashamba ya chai na kuhakikisha kuzingatiwa kwa kanuni bora za uzalishaji wa chai. Aidha, utaratibu wa kuwatumia wataalam waliobobea wa huduma za ugani katika zao la chai utaimarishwa *(commodity specific extension services)* na kuhamasisha uanzishaji wa mashamba ya chai katika maeneo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pareto**,** uzalishaji wa pareto unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 3,320 mwaka 2009/2010 hadi tani 5,000 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo litatokana na kuwafundisha wakulima mbinu za kilimo bora cha pareto, kuzalisha na kusambaza tani 23 za vikonyo vya mbegu bora za pareto na kuwajengea uwezo wakulima kupunguza upotevu wa maua ya pareto baada ya mavuno kwa kufundisha mbinu bora za ukaushaji wa pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** uzalishaji wa mkonge unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 26,363 mwaka 2009/2010 hadi tani 35,000 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo litatokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji unaotokana na upanuzi wa mashamba katika misimu ya nyuma, kuanza kwa uvunaji wa mkonge wa wakulima wadogo katika mikoa ya kanda ya Ziwa na kuwawezesha wakulima wadogo kupata mashine za

kukobolea mkonge. Aidha, Bodi ya Mkonge itaendelea kusimamia usafi wa mashamba ili kuhakikisha tija na uzalishaji katika mashamba ya mkonge unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa pamba unatarajiwa kupungua kutoka tani 267,004 mwaka 2009/2010 hadi tani 260,000 mwaka 2010/2011 za pamba mbegu. Upungufu katika matarajio ya uzalishaji unatokana na athari za kudorora kwa uchumi duniani ambapo bei ya pamba mbegu ilishuka hadi kufikia shilingi 440.00 kwa kilo moja. Kutokana na sababu hiyo, baadhi ya wakulima wameendelea kuwa na wasiwasi na bei ya pamba na hivyo kulima mazao mbadala katika baadhi ya maeneo hususan maeneo yanayolima tumbaku katika Wilaya za Urambo, Uyui, Bukombe na Kahama. Sababu nyingine ni ukame uliotokea katika baadhi ya maeneo wakati wa kupanda zao la pamba na mashamba mengi kujaa maji kutokana na mvua nyingi zilizonyesha mwezi wa Aprili na Mei, 2010 na hivyo kuathiri mimea ya pamba mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili zinaonyesha kwamba bei ya pamba inaanza kurudi katika hali yake ya kawaida. Katika msimu wa ununuzi wa 2010 bei dira itakuwa shilingi 600 kwa kilo. Hata hivyo, ni matumaini ya Serikali kwamba kutakuwepo na ushindani utakaowezesha bei kupanda zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa kahawa unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 40,000 mwaka 2009/2010 hadi tani 60,575 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo litasababishwa na mibuni kuongeza uzalishaji katika msimu unaofuata msimu wa uzalishaji pungufu. Aidha, miche bora ya kahawa yenye ukinzani wa magonjwa ya mibuni iliyopandwa msimu wa 2007/2008 imeanza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaendelea kuhamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na Vyama vya Ushirika ili kurahisha utoaji wa mafunzo ya kanuni bora za kilimo cha kahawa na uzalishaji wa miche bora. Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa *(TaCRI)* kuzalisha na kusambaza miche bora ya kahawa milioni 15, kuendelea kuhimiza matumizi ya mitambo midogo ya kumenya kahawa mbichi vijijini kupitia *DADPs*, kupanua eneo lililopandwa mikahawa bora yenye ukinzani dhidi ya visumbufu vya kahawa, na kuhimiza unywaji wa kahawa nchini.

Aidha, Serikali imeiagiza Bodi ya Kahawa kuanzisha utaratibu wa kutangaza bei dira kama ilivyo kwa mazao mengine ili kuwapa motisha wakulima na kudhibiti uuzaji wa kahawa nje ya nchi kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa korosho unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 74,188 mwaka 2009/2010 hadi tani 121,070 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo litatokana na kuhimiza matumizi ya viuatilifu vya udhibiti wa visumbufu vya mikorosho kwa wakati unaotakiwa na kwa bei nafuu. Wakulima watapata mafunzo ya kilimo bora cha mikorosho na watahimizwa kufufua mashamba ya korosho yaliyotelekezwa Aidha, mfumo wa matumizi ya stakabadhi ya mazao ghalani utaendelea kutumika katika mikoa yote inayolima korosho nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji mazao ya bustani, mbegu za mafuta na muhogo, Serikali itaendelea kutunza bustani za miti Mpiji (Bagamoyo), Bugaga (Kigoma), Songa (Muheza), Igurusi (Mbeya) na Malindi na Jaegetal (Lushoto) kama vyanzo vya vikonyo na vipando bora vya mazao ya bustani (Nguzo ya 4 ya Kilimo Kwanza). Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuhamasisha na kuonyesha teknolojia bora za uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na ya bustani wakati wa maonyesho ya Nanenane, Siku ya Chakula Duniani, Wiki ya Utumishi wa Umma na Wiki ya Ushirika;

(ii) Kuainisha, kuwasajili na pia kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa vipando vya mazao ya bustani ili wazalishe kwa kufuata Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003;

(iii) Kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya bustani kwa kufuata kanuni za kilimo bora cha mazao hayo;

(iv) Kuratibu uzalishaji wa mazao ya bustani na mbegu za mafuta na kuhimiza kilimo hai kwa utaratibu wa kilimo cha mkataba;

(v) Kuandaa mkakati wa kitaifa wa kuendeleza mazao ya mbegu za mafuta; na

(vi) Kuandaa jukwaa la kitaifa kwa ajili ya kuendeleza mazao ya mizizi hususan muhogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika sekta ya kilimo, Wizara itaendelea kuratibu uwekezaji katika kilimo kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*Tanzania Investment Centre*- TIC), Baraza la Taifa la Biashara (*Tanzania National Business Council-TNBC*). Vilevile Wizara itashirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Benki Kuu kuendelea na mchakato wa kuanzisha benki ya kilimo nchini kwa lengo la kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa chakula na lishe, katika mwaka 2010/2011, Wizara itazijengea uwezo Halmashauri za Wilaya zilizoibua miradi inayolenga kutatua matatizo ya upungufu wa chakula kupitia *DADPs* kwa kutoa mafunzo kwa timu za wawezeshaji wa Halmashauri za Wilaya na kuendelea kuhimiza uibuaji wa miradi ya aina hiyo (Nguzo ya 4 ya Kilimo Kwanza). Jumla ya wawezeshaji 230 kutoka Halmashauri 20 za Mikoa ya Mbeya, Kigoma, Kagera na Shinyanga watapatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo mengine yatahusu masuala mchanganyiko ya Usalama wa Chakula hususan, matumizi ya teknolojia za *Geographical Information Systems* (*GIS)* na *Global Positioning System* (*GPS*) katika ukusanyaji na usambazaji wa takwimu na taarifa za mvua na hali ya mazao mashambani, hifadhi bora na matumizi ya mazao ya nafaka na mikunde yatakayotolewa kwa wataalam wa kilimo 200 kutoka

Halmashauri za Wilaya 40 katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Iringa na Tabora ili kupunguza upotevu na kuongeza upatikanaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mafunzo kuhusu teknolojia za hifadhi na matumizi ya mazao ya mizizi, mboga na matunda kwa watalaam 50 wa Halmashauri za Mikoa ya Mara, Kagera na Tanga na mafunzo ya ujenzi wa maghala bora ya kuhifadhia mazao ya chakula katika Mikoa ya Mbeya na Shinyanga kwa mafundi ujenzi wa vijiji na wataalam wa kilimo yatatolewa. Wizara itahamasisha na kuhimiza wananchi kuhifadhi chakula cha kutosheleza mahitaji ya kaya kwa mwaka mzima ili kuepukana na njaa. Halmashauri zilizoibua miradi ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi mazao kupitia *DADPs* zitapatiwa ushauri wa kiufundi wa namna ya kutumia maghala hayo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuhimiza matumizi ya mazao yasio ya nafaka na matumizi ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya nafaka kwa kuchanganya muhogo na nafaka kama vile mahindi na mtama na itafanya tafiti maalum zitakazochangia kuongeza uwezo wa kubuni mikakati ya kuboresha usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na upatikanaji wa chakula, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake katika kuratibu hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa kufanya savei mbalimbali za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula ili kubaini hali ya chakula nchini na kupendekeza hatua za kuchukuliwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini za kina katika maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula na kuishauri Serikali kuchukua hatua zinazostahili kwa kuzingatia maslahi ya wazalishaji na walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya chakula katika ngazi ya Taifa, katika mwaka 2010/2011, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*NFRA*) imepanga kununua kutoka kwa wakulima hapa nchini mahindi tani 140,000 na mtama tani 5,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 57.5 (Nguzo ya 6 ya Kilimo Kwanza).

Aidha, kazi nyingine zitakazotekelezwa na *NFRA* ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kama vile magunia, maturubai, dawa za kuhifadhia nafaka, ukarabati wa maghala na kuimarisha uwezo wa kiutendaji. *NFRA* pia itahamisha nafaka kutoka kanda za *NFRA* zenye ziada na kupeleka kwenye kanda zenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** usindikaji wa mazao ya kilimo, Wizara itawajengea uwezo wataalam wa kilimo wa Halmashauri za Wilaya kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya chakula, hususan yale ya nafaka, mikunde, muhogo, mboga mboga na matunda.

Aidha, mafunzo ya utayarishaji na matumizi ya mazao ya mtama, muhogo, mboga mboga na matunda yatatolewa kwa lengo la kupanua matumizi ya mazao hayo katika kuongeza uhakika wa chakula. Ili kuongeza soko na kupanua matumizi ya zao la

muhogo, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuwahamasisha wasindikaji wa mazao ya nafaka kuchanganya muhogo na nafaka kama vile mahindi na mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurekebisha na kuhuisha sera na sheria, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuandaa na kufanya mapitio ya sheria na kanuni za Sekta ya Kilimo ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya sasa au malengo ya kutungwa kwa sera na sheria hizo (Nguzo ya 4 ya Kilimo Kwanza). Wizara itakamilisha maandalizi ya Mwongozo wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kilimo ili kubainisha majukumu ya wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (*The Agricultural Inputs Trust Fund Act 1994*), kukamilisha maandalizi ya Sheria ya Kusimamia Rasilimali za Kilimo (*The Agricultural Resource Management Legislation)*; kukamilisha maandalizi ya kanuni za mazao; kukamilisha uanzishwaji wa Bodi na Mamlaka ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; kuhuisha Sheria ya Hifadhi ya Mimea (*Plant Protection Act, 1997)* na kukamilisha mapendekezo ya Sheria ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa UKIMWI katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi 18 wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata vyakula vyenye virutubisho pamoja na kuhudhuria kliniki kwa ajili ya matibabu. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya kilimo kuhusu mabadiliko ya tabia na mienendo kwa vijana ili kuwaepusha na maambukizo ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya jinsia kwa kuzingatia umuhimu wa kuhaulisha masuala ya jinsia katika kuendeleza kilimo nchini, Wizara itashirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa kuingiza masuala ya jinsia katika shughuli za kilimo (Nguzo ya 8 ya Kilimo Kwanza). Wizara itatoa mafunzo ya jinsia kwa wajumbe saba (7) wa Kamati ya Jinsia ya Wizara ili kuwajengea uwezo wa kuzingatia masuala ya jinsia katika kupanga na kutekeleza mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** maendeleo ya rasilimali watu, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaajiri watumishi 222 na kuingia mikataba na watafiti watakaostaafu mwaka 2010/2011 ili kuongeza nguvu kazi katika utoaji huduma na kupandisha cheo watumishi 234 katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma.

Wizara katika mwaka 2010/2011 inategema kuwapeleka wataalam wa ugani 2,743 katika ngazi za Kata na Vijiji watakaohitimu Mwezi wa Novemba, 2010 na hivyo kufanya idadi ya wataalam wa ugani nchini kufikia 7,182 sawa na asilimia 48.0 ya lengo la wataalam waliokusudiwa ili kuwa na mtaalam mmoja katika ngazi ya Kata na Kijiji nchini. Serikali itaendelea kupeleka wataalam wa kilimo kwenye Halmashauri za Wilaya

kwa kutegemea ikama itakayoidhinishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na pia mawasiliano na Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itatoa mafunzo elekezi (*orientation)* kwa waajiriwa wapya ili waweze kufahamu sheria, taratibu na kanuni zinazotumika katika utendaji wa shughuli za Serikali pamoja na maadili ya utumishi wa umma kabla ya kupewa majukumu; kuimarisha mfumo wa wazi wa upimaji utendaji kazi (*Open Performance Review and Assessment System-OPRAS*) kukamilisha na kuzindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) na kuendelea kufanya ukaguzi wa watumishi (*Human Resources Audit*) ili kuwa na taarifa na kumbukumbu sahihi za watumishi wote wa Wizara waliopo kwenye orodha ya malipo ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Vyama vya Ushirika ni vyombo vya kuwawezesha wananchi walio wengi nchini kupata huduma za kiuchumi na kijamii zinazochangia kukuza mapato yao na kupunguza umaskini. Hata hivyo, Vyama vya Ushirika vimekuwa dhaifu kiasi cha kushindwa kutoa mchango wake kikamilifu katika kuhudumia wanachama wake. Kwa kutambua hayo na kwa lengo la kuimarisha Vyama viweze kuwanufaisha wananchi wengi nchini, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kuanzishwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo hilo lilizingatia pia ukweli kuwa suala la Ushirika linahusisha sekta mbalimbali kama vile kilimo, fedha, viwanda, nyumba, usafirishaji, uvuvi, maliasili na madini. Kwa hali hiyo ilionekana ni muhimu kuwa na taasisi inayojitegemea katika kushughulikia masuala ya ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa kuunda Tume ya Ushirika ulitokana na sababu ya kihistoria ambayo inaonyesha kuwa tangu uhuru Idara ambayo imekuwa ikisimamia maendeleo ya ushirika imekuwa ikihamahama kutoka Wizara moja hadi nyingine na kusababisha kupata uzito mdogo wa vipaumbele katika kusimamia maendeleo ya Ushirika hasa katika maeneo ya uhamasishaji (*promotion*), usimamizi (*supervision*), ukaguzi (*inspection*) na elimu/mafunzo (*education/training*). Tofauti na Idara, Tume chini ya Wizara yenye dhamana ya ushirika ni chombo kinachojitegemea kwa ajili ya kusimamia maendeleo ya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia tamko la Mheshimiwa Rais la kutaka kuundwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Wizara imefanya matayarisho mbalimbali ili kuwezesha Tume kuanza kutekeleza majukumu yake. Muundo wa Tume pamoja na Ikama ya watumishi vimeandaliwa na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais. Vilevile, Wizara ilitayarisha maelezo ya kazi (*Job description).*

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Tume ya Ushirika itakuwa na wajibu wa kuhamasisha ujenzi wa ushirika unaokidhi haja na matakwa ya wanachama na jamii kwa kuendeleza utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika (*CRMP*). Katika mwelekeo wa sasa wa kukuza na kuendeleza Sekta ya Kilimo Tume itachangia katika kufanikisha utekelezaji wa

Kilimo Kwanza na kufanikisha utekelezaji wa *ASDP* ili kuongeza kasi ya kufikia malengo ya Milenia, *CAADP*, MKUKUTA II na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika**,**Tume ya Maendeleo ya Ushirika itasimamia utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Muundo wa Tume hususan kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu maendeleo ya ushirika nchini;

(ii) Kuwa mtekelezaji muhimu wa sera, sheria na kanuni zilizowekwa na Serikali ili kuendeleza ushirika nchini;

(iii) Kusimamia na kuendeleza maadili, misingi ya ushirika na uendelezaji wake pamoja na kusimamia manufaa yatokanayo na ushirika kwa wanachama wake na jamii;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika;

(v) Kujenga uhusiano baina ya Taasisi za Ushirika za ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuharakisha upatikanaji wa maendeleo katika shughuli za wanaushirika;

(vi) Kuchukua hatua zenye lengo la kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini;

(vii) Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa kuwezesha Vyama vya Ushirika kuibua miradi bora yenye manufaa kwa wanachama na wananchi kwa ujumla;

(viii) Kuweka mazingira yatakayowezesha kukua kwa ushirikiano baina ya Vyama vya Ushirika hususan katika nyanja za uzalishaji, masoko, mitaji, teknolojia na habari;

(ix) Kufanya tafiti mbalimbali zenye kuwezesha kubaini changamoto zinazokwamisha maendeleo ya ushirika na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yake; na

(x) Kuwezesha kuwepo kwa weledi na utaalam katika Vyama vya Ushirika kuhusiana na masoko na mlolongo mzima wa kuongeza thamani ya mazao ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Muundo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, shughuli za Tume zitasimamiwa na Makamishna ambao watateuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume. Mtendaji Mkuu wa Tume atakuwa Katibu Mtendaji na atasaidiwa na Makatibu Watendaji Wasaidizi sita pamoja na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Aidha, Tume itakuwa na Sehemu (*sections*) sita na vitengo (*units*) vinane.

Mheshimiwa Naibu Spika**,**katika mwaka 2010/2011, chini ya Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itatekeleza kazi kuu zifuatazo:-

(i) Kuhamasisha uanzishaji, uendelezaji na uimarishaji wa Vyama vya Ushirika nchini. Mkazo mkubwa utawekwa katika utoaji elimu, mafunzo, ushauri na uhamasishaji kwa wanachama, viongozi, watendaji na wananchi kwa ujumla vikiwemo vikundi vya vijana ili kuviwezesha vyama kuwa na wanachama wengi, vyenye nguvu kubwa za kiuchumi pamoja na utawala bora kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Kilimo Kwanza;

(ii) Kusimamia na kuimarisha uendeshaji wa *SACCOS* na Benki za ushirika kwa mbinu mbalimbali ikwemo kusambaza miongozo ya uendeshaji, kuendelea kudhamini watendaji wa *SACCOS* kupata mafunzo ya cheti yanayotolewa na *MUCCoBS* na kusimamia kwa karibu Benki za Ushirika;

(iii) Kusimamia na kuwezesha wakulima kupata masoko bora ya mazao yao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala na taarifa za bei za masoko;

(iv) Kusimamia na kuimarisha uongozi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika wa mazao hususan pamba, korosho, tumbaku na kahawa kwa kuvipatia mafunzo, ushauri, ufuatiliaji wa karibu wa shughuli zao ili Vyama hivyo viimarike na viweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuleta mageuzi ya kilimo chini ya Kilimo Kwanza;

(v) Kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa ndani wa Vyama vya Ushirika;

(vi) Kuendelea kuvipunguzia Vyama vya Ushirika mzigo wa madeni na kuviwezesha kufanya maboresho stahili;

(vii) Kuimarisha na kuwezesha Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

(viii) Kuimarisha utoaji wa elimu ya uendeshaji na usimamizi wa fedha katika Vyama vya Mazao na *SACCOS* ili viweze kutumia kwa makini rasilimali zilizopo kwa ajili ya Kilimo Kwanza; na

(ix) Kuwezesha Tume kutekeleza majukumu yake ya kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, naomba nichukue nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubelgiji, Uholanzi na Uswisi. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo:-

Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, WARDA, Rockfeller Foundation na Bill and Melinda Gates Foundation. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyo nayo. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi; Katibu Mkuu Bw. Mohamed Said Muya; Naibu Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Wakurugenzi, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara bila kukwama. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** maombi ya fedha kwa mwaka 2010/2011, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 253,355,014,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizo, shilingi 149,402,643,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 103,952,371,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi 3,416,709,000 ni fedha za ndani na shilingi 100,535,662,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, Tume ya Ushirika inaombewa jumla ya shilingi 6,564,566,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 100,000,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii nimewasilisha mezani nakala ya Randama ya Mipango ya Bajeti ya Wizara na Tume ya Ushirika kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Hotuba yake imeungwa mkono. Ni hotuba ya kupenda kusoma, mengi ameshindwa kusoma kutokana na muda. Lakini nadhani ni muhimu sana wanaopenda kujua habari zaidi wasome katika kitabu hiki. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa

majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Juni, 2010 Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es salaam ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, maoni na ushauri wa Kamati kwa makisio ya mwaka wa fedha wa 2009/2010 pamoja na malengo na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, ambayo yaliambatana na maelezo ya maeneo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati, Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ikiwa msimamizi wa Wizara hii, ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 kwa lengo la kuboresha sekta hii muhimu. Wizara imejitahidi kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wawekezaji. Katika kuhakikisha Serikali inaweka vivutio kwa wawekezaji, Kamati ilielezwa kuwa Serikali inatoa msamaha wa ushuru wa forodha kwa mashine na mitambo, msamaha wa kodi kwa malighafi zinazotumika kutengeneza bidhaa kwa ajili ya kuuza nje ya nchi pamoja na msamaha wa kodi ya mapato kwa kipindi ambacho mwekezaji anapata hasara hadi anapoanza kupata faida.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Benki ya Ardhi. Katika jitihada za kuhakikisha nchi inakuwa na Benki ya Ardhi *(Land bank)* Wizara ilieleza kuwa, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*TIC*) inaendelea kuainisha na kutenga ardhi hiyo. Aidha, mashamba ya Taasisi za Serikali kama JKT, Magereza na Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*) yataainishwa na kuwekwa katika Benki ya Ardhi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Halmashauri. Kamati ilishauri Wizara iajiri wahitimu wa vyuo vya kilimo katika Halmashauri ili kupunguza tatizo la wataalam, Wizara ilieleza kuwa mnamo mwezi Mei, 2010 tayari wahitimu 750 waliofaulu vizuri wameanza kupangiwa kazi katika Halmashauri mbalimbali nchini.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfumo wa Vocha. Kamati ilishauri ifanyike tathmini ili kubaini mafanikio na changamoto za kutumia mfumo wa vocha katika kutoa ruzuku ya pembejeo. Wizara ilieleza kuwa tathmini hiyo imefanyika na imeonyesha mafanikio na changamoto. Baadhi ya changamoto hizo ni: Mahitaji makubwa ikilinganishwa na ruzuku ndogo inayotolewa, usimamizi hafifu kwa baadhi ya maeneo, uwezo mdogo wa wakulima kuchangia na mitaji midogo ya mawakala na hivyo kushindwa kufikisha pembejeo kwa wakulima. Kamati inaendelea kusisitiza Wizara ijipange vyema ili kutatua changamoto hizo.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vijana. Katika kuhakikisha Wizara inawawezesha vijana ili washiriki katika Kilimo, Wizara ilieleza kuwa tayari wameanza hatua ya awali (*pilot phase*) kwa kushirikiana na Mikoa ya Lindi na Mtwara na imevipatia vikundi vya vijana mafunzo na seti 20 za mashine za kusindika muhogo. Jukumu hili ni kubwa na muhimu sana. Kamati inaona kwamba hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kuwawezesha vijana kujiajiri katiKa Kilimo. Kamati inazidi kusisitiza kwamba iandaliwe programu maalum ya kuwawezesha vijana kujiajiri katika sekta hii ambayo ndiyo sekta pekee yenye uwezo wa kuajiri vijana kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

(a) Kuchelewa kupatikana kwa fedha za utekelezaji wa baadhi ya shughuli za Wizara;

(b) Ukosefu wa mawakala wa kutosha wenye uwezo wa kufikisha pembejeo za kilimo katika maeneo ya vijijini;

(c) Mahitaji mengi ya wakulima kwa Mfuko wa Pembejeo wakati bajeti ya Mfuko huo ni ndogo;

(d) Upungufu wa chakula kwa baadhi ya maeneo kutokana na mafuriko na ukame; na

(e) Idadi ndogo ya Maafisa Ushirika ikilinganishwa na idadi ya Vyama vya Ushirika, hivyo kusababisha kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Fedha na Malengo ya Bajeti ya Wizara Kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011. Ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika chini ya Fungu 43 inaomba jumla ya shilingi 253, 335,014,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 149,402,643,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 103,952,371,000/= ni kwa Miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 13,557,864,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 135, 844,779,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo Sh. 3,416,709,000/= ni fedha za ndani na Sh. 100,535,662,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazoombwa na Wizara zinakusudia kutekeleza kazi mbalimbali, baadhi ya kazi hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza. Wizara itaendelea kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza kupitia *ASDP* na utekelezaji utakuwa kwa awamu ambao utahusisha nguzo ya nne inayohusu mabadiliko ya mfumo wa kimkakati, Nguzo ya sita inayoelezea Vivutio, Nguzo ya saba inayoelezea Viwanda na Nguzo ya nane inayoelezea Sayansi na Teknolojia na Rasilimali watu;

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa Kilimo. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara inakusudia kuendelea kutafiti na kutathmini vizazi vya mbegu tano mpya za mazao zinazotoa mavuno mengi, kustahimili ukame na zenye ukinzani dhidi ya magonjwa. Aidha, inakusudia kuboresha vituo na kuimarisha uwezo wa watafiti na kubuni na kuendeleza teknolojia ya zao la mpunga kupitia Mradi wa Kituo Mahiri cha Utafiti wa zao la Mpunga;

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Kuongeza uzalishaji wa chakula. Katika kuhakikisha nchi inakuwa na chakula cha kutosha, katika mwaka 2010/2011, Wizara itahakikisha inaendelea kuipatia ruzuku ya pembejeo Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Iringa, Ruvuma, Morogoro na Kigoma na baadhi ya Wilaya za Mikoa ya Mara (Wilaya za Tarime na Serengeti), Tabora (Wilaya za Sikonge na Urambo), Shinyanga (Wilaya za Kahama na Bukombe), Kagera (Wilaya ya Chato), Mwanza (Wilaya za Geita na Sengerema) na maeneo yenye miundombinu ya umwagiliaji iliyokamilika ya Mikoa ya Mtwara (Wilaya ya Mtwara), Lindi ( Wilaya ya Lindi), Tanga (Wilaya ya Korogwe, Muheza na Lushoto), Dodoma (Wilaya ya Mpwapwa na Bahi), Pwani (Wilaya ya Bagamoyo), Singida (Wilaya ya Manyoni na Singida), Mara (Wilaya ya Bunda) na Tabora (Wilaya ya Igunga), itanufaika na ruzuku ya mbolea na mbegu bora za mahindi na mpunga. Aidha, kuhimiza mikoa isiyopata mvua za kutosha kulima mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama, muhogo, viazi na uwele;

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo. Wizara imepanga kuendelea kugharamia ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa kuongeza idadi ya wakulima wanaonufaika kutoka wakulima 2,000,000 mwaka 2009/2010 hadi kufikia wakulima 2,500,000 mwaka 2010/2011. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 127.1 zitatumika kugharamia ruzuku ya pembejeo za kilimo;

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, Visumbufu vya mimea na mazao. Ili kuhakikisha inadhibiti visumbufu vya mazao na mimea, Wizara imepanga kuzalisha na kusambaza wadudu walawangi (*Biological control agents*) na kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani na wakulima kuhusu udhibiti husishi, kukagua mazao yanayoingia na kutoka nchini ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa pamoja na kutoa vibali vya mazao yanayosafirishwa nje ya nchi.

(f) Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Chakula. Wizara kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* imepanga kununua kutoka kwa wakulima wa hapa nchini mahindi tani 140,000 yenye thamani ya shilingi bilioni 58.37 ili kuhakikisha kunakuwepo chakula cha kutosha.

(g) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za Ugani. Wizara imepanga kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam wa kuendesha shughuli za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini kama njia ya kudumisha viwango vya utoaji wa huduma hizo na kutoa mafunzo kwa vijana tarajali ili kukabiliana na upungufu wa wataalam wa ugani vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati, changamoto na maeneo ya utekelezaji kwa mwaka 2010/2011, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti. Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Wizara hii bado ni ndogo na ndio maana inashindwa kuchangia kwa kiasi cha kutosha katika kukua kwa uchumi. Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 26 tu ya pato la Taifa licha ya ukweli kwamba Watanzania wengi wanaokadiriwa kufikia asilimia 80 wanajishughulisha na kilimo. Ukuaji wa Kilimo unashuka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2008/2009 Kilimo kilikua kwa asilimia 4.6, mwaka 2009/2010 asilimia 3.2 tu wakati idadi ya watu inakua kwa asilimia 2.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Bajeti inayotengwa kwa kilimo bado inaongezeka kwa kiasi kidogo sana. Mwaka 2008/2009 ilikuwa ni shilingi bilioni 440 sawa na asilimia 6.4, mwaka 2009/2010 shilingi bilioni 666.9 sawa na asilimia saba na mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 903 sawa na asilimia 7.7 tu ya Bajeti yote ya Serikali. Kamati inashauri ni wakati sasa Serikali kuamua kuongeza bajeti ya Sekta ya Kilimo kufikia angalau kiwango kilichokubaliwa na nchi za *SADC* cha asilimia 10 ya Bajeti yote ya Serikali ili sekta ya kilimo ifanye vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini dhana ya Kilimo Kwanza imekuja kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kijani na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa na cha kibiashara. Hata hivyo, wakati wa kupitia bajeti ya Wizara, Kamati imeona kwamba hakuna viashiria vya kuwapo Mikakati ya dhati kutekeleza dhana hiyo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Wizara zote zinazohusika na Sekta ya Kilimo, zipewe fungu la kutosha kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza katika nguzo zake kuu ili zianze utekelezaji huo mapema iwezekanavyo na ziwajibike ipasavyo kwa matumizi bora ya fungu hilo.

(ii) Serikali haina budi kuhusisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa kuhakikisha inawawekea vivutio muafaka kwani ikumbukwe Sekta binafsi inachangia kwa asilimia kubwa katika kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti. Ili nchi iweze kuendelea katika sekta ya kilimo ni lazima iwekeze kwenye utafiti. Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Serikali za kutenga kiasi cha shilingi bilioni 30 kwa ajili ya taasisi mbalimbali za utafiti nchini. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Kutokana na kiasi cha shilingi bilioni 30 kutengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika taasisi zinazohusika na tafiti mbalimbali nchini, ni vyema basi taasisi za utafiti za kilimo zikagawiwa fedha zake mapema ili zianze utekelezaji wake.

(ii) Serikali itenge fungu la kutosha kwa ajili ya utafiti wa kilimo ili kufikia azma ya Kilimo Kwanza kama ilivyoainishwa kwenye nguzo ya Nne.

(iii) Muundo wa utumishi wa watafiti uangaliwe upya na urekebishwe mapema iwezekanavyo na hii iende sambamba na kuboresha maslahi yao.

(iv) Vituo vya utafiti vitengewe fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vinapatiwa vitendea kazi bora na vya kisasa. Aidha, fedha zilizoelekezwa katika utafiti zitumike kama ilivyopangwa badala ya kutumika katika shughuli nyingine.

(v) Utafiti wa matumizi ya bioteknolojia ufanyike ili kutengeneza mbegu bora zenye vinasaba vya kuweza kustahimili ukame kwani bioteknolojia imeendelea kukua kwa kasi kubwa ulimwenguni na kuwa nyenzo kubwa katika kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo.

(vi) Serikali ihakikishe matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo, mbolea. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza wigo wa ruzuku ya pembejeo, pamoja na pongezi hizo Kamati bado inasisitiza yafuatayo:-

(a) Serikali iendelee kuongeza idadi ya wakulima wanaopata ruzuku kwani itasaidia katika kuongeza tija. Aidha, Serikali ihakikishe inafanya utafiti wa kutosha ili kuweza kutambua tofauti ya misimu katika kila Kanda au Mikoa ili mbolea ziwafikie wakulima wa mikoa hiyo kwa wakati;

(b) Viwanda vya Mbolea vianzishwe nchini ikizingatiwa kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na gesi asilia na *phosphates* nyingi ambazo ni malighafi muhimu;

(c) Gharama ya kuleta mbolea iliyofungwa kwenye mifuko kutoka nje ya nchi ni kubwa mno, ni vyema basi mbolea hiyo iingizwe nchini bila ya kufungwa ili ifungwe hapa hapa nchini kwa madhumuni ya kupunguza gharama na bei kwa wakulima;

(d) Ili wakulima wenye mahitaji ya kiwango tofauti waweze kupata mbolea kulingana na mahitaji yao ni vyema sasa kuwepo na mbolea zinazofungwa katika mifuko yenye kilo tofauti, mfano kilo 25, 10 na tano. Hii itasaidia wakulima kujitokeza kununua kulingana na uwezo wao; na

(e) Kutokana na wizi wa vocha za ruzuku ya mbolea, Serikali ihakikishe inajitahidi kudhibiti na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kufanya hujuma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu bora ni moja ya misingi ya mavuno mengi hivyo kuwawezesha wakulima kuzalisha chakula cha kutosha na kuhakikisha kunakuwepo usalama wa chakula. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(a) Serikali iache kutegemea kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi na badala yake mbegu za kutosha zizalishwe hapa nchini. Aidha, kwa mtu anayetaka kuingiza mbegu nchini yawekwe masharti ya kumtaka azalishe mbegu hizo humu humu nchini, hii itapunguza gharama za ununuzi wa mbegu kwa wakulima.

(b) Serikali ihakikishe usimamizi na uratibu wa ubora wa mbegu unafanywa kwa umakini na zile zisizofaa ziondolewe sokoni. Aidha, wakulima wapelekewe mbegu kwa wakati ili kuwadhibiti wafanyabiashara wanaowahadaa kwa kufunga mbegu zisizo na ubora unaostahili kwenye vifungashio vinavyotumika kwa mbegu bora.

(c) Serikali ihakikishe inawafuatilia kwa makini wafanyabiashara au wauzaji wa mbegu katika kuhakikisha kwamba, zina ubora unaotakiwa ili kuepuka Taifa kuingia katika maafa ya njaa.

(d) Serikali ihakikishe mashamba ya kuzalisha mbegu yaliyobinafsishwa na kupewa *ASA* kuzalishia mbegu yanatumika kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madawa. Kutokana na mazao mengi yakiwemo ya chakula na biashara kushambuliwa na wadudu waharibifu, Kamati inashauri Serikali iendelee kuongeza bajeti ya madawa ya mazao haya ili kuongeza uzalishaji. Aidha, utafiti wa kutumia viuatilifu vya kimaumbile uendelee ili wakulima wavipate kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na maendeleo katika sekta ya kilimo, suala la zana za kilimo haliepukiki, miaka ya nyuma nchi yetu ilikuwa ina viwanda vya kuzalisha zana za kilimo kama *UFI* na *ZZK*. Tangu viwanda hivyo vife, nchi imekuwa ikiagiza zana kutoka nje ya nchi ambazo zimekuwa na gharama kubwa sana na kukosa vipuri mara zinapoharibika na hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa wakulima. Kamati inashauri haya yafuatayo:-

(a) Serikali ifufue viwanda vya zana za kilimo ili kumpunguzia mkulima gharama za kununua zana hizo kwa bei ya juu. Aidha, zana kama matrekta ambayo mengi yanaingizwa nchini bila kuwepo na vipuri vyake ni vyema basi Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha vipuri hivyo vinapatikana mara matrekta hayo yanapoharibika na Serikali ihakikishe inaweka uwiano wa bei ya matrekta madogo kwa nchi nzima. Kwa kuwa wakulima wa kawaida hawamudu kununua matrekta hata madogo kutokana na bei kuwa kubwa, ni vyema basi Serikali ianze kuhimiza kutumia wanyama kazi badala ya kuendelea kutumia jembe la mkono ambalo halina tija katika kilimo.

(b) Serikali ihakikishe inafufua Kiwanda cha Zana za Kilimo cha Mbeya na badala ya kuagiza matrekta madogo, iwe inaagiza vifaa vya matrekta hayo na kuuunganisha kiwandani hapo.

(c) Serikali ihakikishe inafanya mazungumzo na kuweka mpango mkakati wa kujenga kiwanda kipya cha kutengenezea matrekta madogo ikisaidiana na Mataifa yaliyoonesha nia hiyo kama vile China, Vietnam, Indonesia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji. Ili kilimo kikue kwa kiasi kinachotakiwa ni vyema basi nchi iweke mazingira mazuri katika kilimo. Kamati inashauri kwamba:-

(a) Serikali iongeze bajeti ya Sekta ya kilimo kwa kadri itakavyowezekana;

(b) Serikali iweke vivutio kwa wawekezaji ili washawishike kuja kuwekeza katika mashamba makubwa;

(c) Serikali ipunguze urasimu ili kuwashawishi wawekezaji wengi zaidi;

(d) Serikali ihimize ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ili kuongeza thamani yake;

(e) Serikali ishirikikishe Sekta binafsi kwani inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa sekta hii; na

(f) Serikali iendeleze kwa kasi zaidi zoezi la kutenga maeneo kwa ajili ya benki ya ardhi ili kuwapatia wawekezaji mara tu wanapojitokeza kuendesha shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa mazao. Mazao ya Chakula, Kamati inaendelea kusisitiza uzalishaji wa mazao ya chakula upewe kipaumbele kwa kuongeza ruzuku ya pembejeo kwenye maeneo yanayolima mazao hayo. Aidha, kwa maeneo yenye ukame Serikali ihimize ulimaji wa mazao yanayostahimili ukame kama mtama, uwele na muhogo ili kujihakikishia chakula cha kutosha wakati wa ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazao mengine. Kamati inasisitiza Serikali ijikite katika kuhimiza uzalishaji wa mazao mengine mapya kama viungo, matunda, mboga na maua ambayo yatasaidia katika kuliongezea Taifa pato na kukuza uchumi wa nchi kwa kuhakikisha inawapatia mitaji na utaalam wakulima. Aidha, Serikali itumie Chuo cha Utafiti cha *KATRIN* katika kupeleka utaalam wa mazao ya viungo kwa wakulima na kwa kutumia taasisi zinazohusika, ifanye utafiti wa mbegu bora za maua na mboga mboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Benki ya Kilimo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fungu maalum kwa mwaka huu kwa ajili ya kuwapatia wakulima mikopo kupitia Dirisha la Benki ya Rasilimali Tanzania *(Tanzania Investment Bank)*. Pamoja na jitihada hizo, Kamati inasisitiza mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo uharakishwe ili wakulima waweze kufaidika na mikopo mikubwa na yenye riba ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za Ugani. Kamati inatambua umuhimu wa huduma za ugani katika kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija. Kamati inasisitiza huduma za ugani ziboreshwe kwa kuhakikisha kwamba maafisa ugani wanapatiwa mafunzo na wanatimiza wajibu wao wa kusimamia wakulima ili kuongeza

uzalishaji. Aidha, mashamba darasa yaanzishwe katika maeneo mengi zaidi ili wakulima wajifunze kwa vitendo na hivyo kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambacho Benki ya Kilimo bado haijaanzishwa kwani inasaidia kutoa mikopo kwa wakulima. Bajeti ya Mfuko kwa mwaka huu 2010/2011 ni shilingi bilioni 3.8 ambayo ni sawa na bajeti ya mwaka 2009/2010 ya shilingi bilioni 3.8 kukiwa hamna ongezeko lolote. Kamati inashauri Serikali iongeze bajeti ya Mfuko ili iweze kuwahudumia wakulima wengi zaidi, kwani maombi ya mikopo ya pembejeo ni mengi zaidi ikilinganishwa na fedha inayotengwa kwa ajili ya Mfuko huu muhimu. Maombi ni wastani wa shilingi bilioni nane kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kilimo cha Utalii. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii wa asili. Sehemu kama za Kitulo kuna maua yameota ambayo inasemekana hayalimwi sehemu yoyote ulimwenguni, Kamati inashauri Serikali kuendeleza eneo hilo ili kuwavutia watalii na hivyo kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu soko. Hivi karibuni Serikali imekuwa ikiwakataza wakulima wa mahindi na mpunga kuuza mazao yao nje ya nchi kutokana na hofu ya kukumbwa na njaa. Kamati inaamini kwamba ni wajibu wa Serikali kununua mazao ya kutosha na kuyahifadhi kwa ajili ya kusaidia wananchi pindi kunapokuwa na njaa. Kwa hiyo, sio vyema wakulima kubebeshwa mzigo huo ukizingatia wanafanya juhudi ya kujikwamua na umaskini kwa mitaji ya kukopa kutoka vyombo vya fedha lakini baada ya mavuno wanazuiwa kuyauza kwa faida itakayorudisha gharama za uzalishaji na kujipatia faida. Serikali haina budi kununua mazao ya wakulima kwa bei ya soko pale inapowakataza kuuza nje ya nchi. Aidha, kwa mikoa ambayo haina mvua za kutosha ni vyema basi Serikali ihimize kilimo cha mazao yanayohimili ukame kama mtama, muhogo na uwele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mazao ni muhimu sana katika kusimamia mazao yetu na kuhakikisha yanazalishwa kwa kiwango kikubwa. Ili Bodi hizi ziweze kufanya kazi hiyo vizuri ya kusimamia mazao husika ni lazima ziwezeshwe vya kutosha. Bodi nyingi bado hazitengewi fedha za kutosha hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kamati inashauri Serikali iendelee kuziongezea fungu Bodi hizi kulingana na mahitaji yao. Aidha, Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Teddy L.

Kasella – Bantu, Mjumbe; Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mjumbe; Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mjumbe; Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mjumbe; Mheshimiwa Janet Mbene, Mjumbe; Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mjumbe; Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe; Mheshimiwa Juma S. Omary, Mjumbe; Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mjumbe; Mheshimiwa Salum K. Salum, Mjumbe; Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mjumbe; na Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mjumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen M. Wasira; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dokta David M. David, kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote hiki. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Mohamed Muya na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Sophia Kaduma, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashilillah na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Pili Omari kwa kuihudumia vizuri Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yao, sasa nashauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Fungu 43 kwa mwaka 2010/2011 jumla ya Sh. 253, 335, 014,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Unaunga Mkono Hoja. Hotuba yako ilikuwa ni nzuri mpaka ukasahau muda, kwa hiyo tunakubali. Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hiyo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa tukiwa hai wenye afya na kujadili mambo muhimu yanayogusa maslahi ya umma wa Watanzania. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kukushukuru wewe binafsi na Naibu wako kwa kunipa fursa ya kuweza kuwasilisha mawazo ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2010/11, kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 99(7), toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru viongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kwa kutuongoza vyema katika kuhakikisha ushiriki wetu Bungeni kwa miaka mitano unatetea maslahi ya wananchi wote bila kujali itikadi za kisiasa. Kwa namna ya pekee nawashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Chambani kwa kuridhika na utumishi

wangu kwao na hasa wanachama wote wa *CUF* katika Jimbo la Chambani kwa kunipa ridhaa ya kuendelea kuwatumikia katika uchaguzi wa kura za maoni uliomalizika hivi karibuni. Naamini kwa uamuzi wao huo na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitarudi tena Bungeni mwezi Novemba 2010 kuendelea kuwatumikia kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu nitakuwa sijatenda haki kama sitotambua mchango na juhudi kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya watendaji wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika kujaribu kurudisha heshima ya kilimo na wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya umuhimu wake katika uchumi wa nchi na maendeleo ya Watanzania, kilimo kinastahili kupewa kipaumbele cha kwanza na cha kipekee kwa maana ya kutengewa pesa zaidi katika bajeti kama walivyosema baadhi ya viongozi mashuhuri duniani kuhusu umuhimu wa kilimo kama ifuatavyo:-

(a) “Kila kitu kinaweza kusubiri lakini sio Kilimo” (Pandit Jawaharial Nehru).

(b) “Viwanda na ukuaji wa uchumi wa kisasa haviwezi kufanikiwa bila maendeleo ya kuridhisha katika sekta ya kilimo na hasa kipindi ambacho nchi ni changa kiuchumi” (Yujiro Hayami).

(c) “Bila maendeleo ya Kilimo, ukuaji wa viwanda aidha, utadumaa au ukifanikiwa utasababisha kuyumba kwa uchumi na matatizo ya ukosefu wa ajira na umaskini yatajitokeza kwa kiwango cha hali ya juu” (Michael P. Tadaro). Bahati mbaya hivi sasa tunashuhudia propaganda za maneno ya kufurahisha wakulima ili wawe wepesi kukipa kura Chama Tawala, lakini hakuna mkakati thabiti wa kufikia huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya Utendaji wa Wizara kwa Mwaka 2006 hadi 2009. Huu ni mwaka wa uchaguzi, wakati tunakwenda kuomba tena ridhaa za wananchi lazima tuwaeleze 80% ya Watanzania wote wanaotegemea kilimo kwa maisha yao ya kila siku jinsi Ilani ya *CCM* ilivyoshindwa kutekeleza ahadi zake kuhusiana na kilimo. Ukurasa wa 23 wa Ilani ya *CCM* unasema “ Ili uchumi wa nchi yetu ukue kwa kiwango cha asilimia kumi ifikapo mwaka 2010, lazima kilimo kifikie ukuaji wa angalau asilimia 20 ifikapo mwaka huo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka 2010 uchumi umekuwa kwa wastani wa asilimia sita tu, na sio 10%. Kuhusu kilimo takwimu za ukuaji wa kilimo zinaonyesha kama ifuatavyo: Mwaka 2006 ni 3.8%, 2007 ni 4.0%, 2008 ni 4.6% na mwaka 2009 ni 3.2% .

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi ni wazi kuwa kilimo chetu kinasuasua. Sababu kubwa zinazotolewa na Serikali ni uwekezaji mdogo katika miundombinu ya umwagiliaji, barabara za vijijini, uwezo mdogo wa wakulima wadogo kumudu gharama kubwa za pembejeo za kilimo na mabadiliko ya tabia nchi (ukame). Hivyo sababu hizo ndio chanzo cha matokeo ya takwimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa madai haya ya Serikali ni mbinu mojawapo ya kukwepa majukumu. Kazi ya Serikali ni kuandaa mazingira ya uwekezaji wa ndani na nje, lakini takwimu zinaonyesha kuwepo kwa urasimu mkubwa katika utoaji wa maamuzi, jambo linalosababisha kupungua au kutokuwepo kwa uwekezaji wa kuridhisha katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuondoa urasimu na ukiritimba katika utoaji wa maamuzi, kwani siku zote watu makini hujali muda kuliko pesa, kwa dhana kuwa ukipoteza pesa utazipa baadaye lakini muda ukipotea huwezi kuupata tena. *"The time is not rubber"*. Aidha hoja ya matatizo ya soko haina msingi pia kwani tuna soko kubwa la Afrika ya Mashariki na *AGOA* lakini hatujayatumia ipasavyo. Mabadiliko ya tabia nchi si hoja ya msingi kwa nchi yenye mipango makini. Kama upungufu wa mvua ni hoja ya msingi, nchi kama Misri zingeishije? Ni aibu kuhusisha ukuaji wa kilimo na upungufu wa mvua wakati tuna mito mikubwa isiyo kauka kipindi chote cha mwaka kama vile, Rufiji, Malagarasi Kilombero na kadhalika yenye uwezo wa kumwagilia mashamba makubwa kwa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuwa hakuna fedha za kutengeneza miundombinu ya kilimo, ni hoja dhaifu sana kwani ukiangalia bajeti 2010/2011 posho*(non discretionary)* kwa Wizara, Idara na Mikoa ni takriban Tshs418,506,159,442. Na posho *(Allowance in kind)* ni Tshs. 32,386,367,790. Hii ni baadhi tu ya mifano ya posho mbalimbali kwenye bajeti yetu. Fedha hizi zingepunguzwa kwa asilimia 50 tu na kuwekezwa kwenye kilimo zingesaidia sana. Hapa hoja ya msingi ambayo Watanzania wanapaswa kuielewa ni udhaifu wa Serikali katika Mipango yake katika kupanga vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo Kwanza. Katika bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali ilikuja na Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza bila ya kuiingiza katika bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa utekelezaji wa Kilimo Kwanza. Serikali ilichota bilioni 40 kati ya bilioni 53 ya fedha za *EPA* kununulia mbolea na bilioni 10 kuziweka katika dirisha la *TIB* kwa ajili ya mikopo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitarajia kuwa bajeti ya mwaka huu itatengewa fedha za kutosha ili ioane na dhana ya Kilimo Kwanza. Ongezeko la 11% katika bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka shs. 228.5 bilioni mwaka 2009/2010 hadi shs.253.9 bilioni mwaka 2010/2011 ni kuwadanganya Watanzania bure kuwa tutaweza kufanya mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio kuwa tu, bajeti ya Kilimo Kwanza haionekani katika bajeti ya Wizara ya Kilimo bali pia katika bajeti za Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Viwanda na Biashara na kadhalika ambazo kwa pamoja zinafanya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana na kauli za wakulima wengi kuwa Kilimo Kwanza ilikuwa ni mbwembwe tu za kisiasa, kwani hadi sasa hakuna mkakati wowote wa utekelezaji wake ambao Serikali imeutayarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ASDP*, huu ni mwaka wa sita wa utekelezaji wa *programme* hii wa Tshs. 2.5 trillion kwa miaka saba (2006-2012) ili kukuza kilimo na kuleta Mapinduzi ya Kijani. Kwa lengo hilo Serikali inapeleka 75% ya fedha za miradi ya maendeleo ya kilimo kwenye Halmashauri za Wilaya na Vijiji. Jambo la kusikitisha ni kwamba *program* hii iliyozinduliwa kwa hamasa kubwa haina usimamizi mzuri wa fedha hizi, jambo linalosababisha kuishia mifukoni mwa wachache na ufanisi kuwa mdogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikisema kila mara kuwa *ASDP* ilianza vibaya *(wrong footing)* kwani watendaji waliona wao ndio wenye jukumu la kubuni miradi kwa niaba ya wananchi na hivyo wananchi kukaa na kungoja miradi ianzishwe bila ya wao kujishughulisha. Hili liliondoa haja ya wananchi kuchangia na hivyo dhana ya umiliki ilitoweka. Sehemu nyingine Miradi inaanzishwa kwanza baadaye ndio Kamati za usimamizi zinaundwa baada ya miradi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linathibitishwa na kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo wakati anatoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge juu ya utekelezaji wa Programu hii Dar es Salaam, April, 2007, kuhusu changamoto alisema, nanukuu "Uwezo mdogo wa Halmashuri kuibua miradi (*DADPS*) na kuandaa taarifa kunakotokana na upungufu wa wataalam katika Wilaya". Hii maana yake ni kuwa uibuaji wa miradi ni jukumu la watendaji wa Halmashauri zetu. Hivyo basi, dhana ya uchangiaji kwenye miradi itaanzia wapi kama waibuaji miradi ni watendaji wa Serikali na si wananchi? Kama msimamizi mkuu wa Wizara anaelewa tofauti na ukweli ulivyo watendaji wake watakuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo yanakuja kwanza kwa viongozi kuamini kuwa *ASDP* inawezekana kuleta mapinduzi ya Kijani, na baadaye wachukue maamuzi magumu katika utekelezaji. Miradi mingi imeshindwa na taarifa zinaletwa Wizarani, lakini hatujawahi kupata taarifa kuwa watendaji wamefukuzwa na kufunguliwa mashitaka kwa kusababisha hasara katika miradi. Hili tu linatosha kutueleza kuwa *ASDP* imeshindwa. Maana yake ni kuwa Serikali imeshindwa kutimiza ahadi yake kwa Watanzania na hivyo wananchi hawana haki tena kuichagua CCM mwaka ujao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji, Ilani ya Chama Tawala ya mwaka 2005 inasema kuwa ifikapo mwaka 2010 tutakuwa na eneo la hekta milioni moja za umwagiliaji, lakini hivi sasa sekta ya umwagiliaji ina hekta 331,490, lakini hata ifikapo 2015 eneo la umwagiliaji litakuwa ni hekta 600,000 tu. Ni wazi Ilani ya CCM sambamba na Serikali pia vimeshindwa hata kufikia malengo ya umwagiliaji, hivyo Watanzania hawana sababu tena ya kuchagua CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kuwa Serikali inaongozwa na Sera katika utendaji kazi wake na sio matamko ya kisiasa ya kutafutia kura kama vile ya Kilimo Kwanza. Kambi ya Upinzani inaelewa umuhimu wa Umwagiliaji, lakini tatizo kubwa ni

kwamba Wizara inafanya kazi bila ya kuwa na mwongozo (Sera). Kambi ya Upinzani inashindwa kuelewa ni kwa vipi Wizara inaundwa bila ya kuwa na Mwongozo wa utendaji kazi wake yaani Sera ya Umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa eneo la umwagiliaji mwaka 2005 lilikuwa hekta 264,388, mwaka 2008 likafikia hekta 289,245. Sawa na ongezeko la hekta 24,857 ambayo ni asilimia 8.6. Kwa kipindi hicho Bunge lako Tukufu limepitisha jumla ya Tsh. 597,301,121,600/- kwa Wizara hii. Je, fedha hizo zinalingana na ongezeko hilo la asilimia 8.6? Tuna imani Watanzania watatoa maamuzi sahihi kwa ulinganisho huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya mazao ya kilimo, kwa kisingizio cha usalama wa chakula, Serikali imekuwa haiwatendei haki wakulima kwa kuzuia kuuza nje mazao yao ya kilimo ambayo ndio chanzo cha mapato yao. Mfano ni wakulima wa mpunga wa Kata ya Nkulo, Mkoa wa Morogoro, wakati msimu mpya wa uvunaji unaanza hivi karibuni huku ghala zao zina tani 216 za mpunga wa msimu uliopita, baada ya Serikali kuzuia uuzaji nje ya nchi. Ikumbukwe kuwa wakulima hawa wana mikopo ya benki yenye riba kubwa wakati ucheleweshaji huu bei ilishuka toka Tshs.375/- kwa kilo hadi Tshs. 120/- kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Watendaji wa Serikali wanazuia wanunuzi binafsi ambao wanatoa bei nzuri kwa mazao yao na kulazimisha wauze kwenye vyama vya ushirika. Mfano ni wakulima wa ufuta Mkoa wa Lindi na wakulima wa Kahawa Mkoa wa Kagera. Kambi ya Upinzani inasema kitendo hicho cha Serikali si halali, si cha kibinadam na kinapingana na dhana ya ushindani wa soko na hivyo kinawakatisha tamaa wakulima kwa kuwazidishia umaskini wa kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro Kuwa Ghala la Taifa. Mwaka 2006 Rais Kikwete aliutangaza Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa, kwa lengo la kulisha nchi nzima. Tamko hilo la Mheshimiwa Rais lilikuwa na kila uhalali kwa kuwa Mkoa huo umebahatika kuwa na ardhi nzuri na mito zaidi ya 176 isiyokauka mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mshangao mkubwa tamko hilo zuri la Mheshimiwa Rais wetu limetiwa kapuni na hadi leo hii Morogoro ni ghala bila mazao. Hii ni kuwa watendaji wanampunguzia heshima Mheshimiwa Rais. Wetu na kuonyesha kauli anazozitoa ni porojo tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kilimo Hai, katika nchi zote za Afrika ya Mashariki Tanzania ndiyo nchi ambayo imekuwa na Chuo Kikuu cha Kilimo kikubwa na cha kwanza chenye wataalam wenye hadhi ya kipekee. Tatizo tunaloliona hapa ni kuwa ama wataalam hawa hawatumiwi vizuri au hatuna takwimu za wahitimu hawa katika fani mbalimbali za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajua kabisa madhara makubwa yanayosababishwa na matumizi ya muda mrefu ya mbolea kwenye ardhi. Pia inaelewa umuhimu mkubwa uliopo wa kutumia mbolea za mboji kwenye udongo.

Kambi ya Upinzani inauliza ni kwanini Serikali inakataa kuwashauri wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutumia mbolea ya mboji *(Organic Fertilizer)* wakati inaelewa kuwa udongo wa maeneo hayo umekwishaharibika na kuwa sumu na haufai kwa kuzalisha na kuvuna kwa tija bila ya kutumia mbolea za chumvi chumvi. Hivyo wakulima hawa tayari wamekwishakuwa watumwa wa mbolea hizi na watakapozikosa hawataweza kuzalisha kamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa mbolea ni eneo lenye siasa nyingi na ni eneo lenye rushwa kubwa. Tunasema hivyo kwa msingi kuwa, tunashindwa kuamini kuwa Waziri anayekuwepo anaelewa umuhimu wa mboji kwa kilimo chetu lakini anashindwa kuweka mpango mkakati wa matumizi ya mboji kwa wakulima na badala yake anajitahidi kutafuta makampuni ya kuleta mbolea za chumvi chumvi *(Inorganic fertilizers)* nchini, au anajitahidi kuona jinsi ya kutoa ruzuku kwa mbolea hizo zisilipe kodi na ili mbolea iwe nyingi kwa wakulima. Kwa nini tusitoe Ruzuku kwa mbolea za mboji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbolea *ya (Erth Food*) ni Mboji ambayo imethibishwa na taasisi zote zinazopima ubora na kuonekana kuwa haina matatizo, lakini mbaya zaidi toka mwaka 1997 ilipoingizwa hapa nchini, Serikali imeshindwa kuwatangazia wakulima watumie mbolea hiyo na kuwapa maelekezo Wagani kuwaelimisha wakulima umuhimu wa matumizi ya Mboji, hivyo wakulima kupata nafasi ya kuchagua mbolea ipi inafaa kwa kilimo chao. Hapa ndipo nasema Sekta ya Mbolea imejaa siasa na Rushwa ya Ajabu, Kwani Serikali inashindwa kumsaidia Mzawa kujiimarisha na badala yake inazisaidia Kampuni za nje kummaliza Mzawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilikwishakuwa na program nyingi za kuwapa fursa wakulima kujifunza jinsi ya kutengeneza mbolea zao za mboji kutokana na rasilimali zinazowazunguka na wengine walikwenda Zimbabwe kujifunza jinsi ya kutengeneza mbolea hizo. Hii ni kazi mojawapo ya wataalam wetu wa SUA, Je, mpango huo umekwenda wapi kwa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kilimo hai kinaweza kuleta mapinduzi ya haraka na hivyo Tanzania kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula na kuondokana na aibu ya kuomba chakula kwa wahisani. Tunao uwezo wa kuzalisha hapa nchini kama tukiwa makini zaidi.

Aidha, uharibifu wa maliasili-ardhi unaotolewa na mbolea za chumvi chumvi utaepukwa. Kwa njia hii yale yaliyomo kwenye sera, kuwa na kilimo cha kisasa na endelevu yatatekelezwa kwa vitendo. Kilimo kitapanuka kwenye sehemu za ukame kwa vile mbolea za mboji zinahifadhi unyevunyevu kwa muda mrefu na hiyo ni faida kubwa sehemu hizi zenye mvua haba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua jukumu lake la msingi la kutoa ushauri wa matumizi ya mbolea kutokana na aina ya udongo na aina ya mbolea inayotakiwa kama ni Mboji au chumvi chumvi na waache wakulima wachague aina ya mbolea wanayohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kaungalia upya msukumo inaoutoa katika matumizi ya Mbolea ya chumvi chumvi ili itoe msukumo kama huo kwa mbolea ya Mboji kwa mikoa ambayo matumizi ya mbolea za chumvi chumvi hayajaanza kuleta madhara kwenye udongo, kwani gharama ya kuirudisha ardhi uhai wake (*soil reclamation*) ni kubwa mno. Hivyo kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa yanayotushauri tutumie mbolea hizo za chumvi, wao kwenye nchi zao wamekwishaacha matumizi ya mbolea hizo ili wasifunge viwanda vyao na watu wao kukosa ajira wanatuletea sisi. Itafikia muda baada ya kujiimarisha kuacha kuzalisha mbolea hizo hivyo kuanza kutushauri upya tutumie mbolea za mboji (Ni kwa nini wataalam wetu wasilione hili na wakatoa ushauri kwa Serikali au 10% inaendelea kuiuza nchi yetu?)

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kemikali (mbolea za chumvi chumvi) kwa wingi yanaharibu afya za wafanyakazi wa shambani. Imegundulika ongezeko la saratani, matatizo ya kupumua na magonjwa mengine mengi kwa wafanyakazi wa mashambani hasa mashamba ya maua na mbogamboga wanakotumia sana madawa ya kemikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa Wizara haijachelewa kwani Kilimo Hai bado kina nafasi kubwa ya kukifanya kishamiri hapa Tanzania na huu ndio muda wa kuangalia jinsi viwanda vikubwa vya mbolea duniani vinavyofanya biashara ya kuendelea kuzifanya nchi zinazoendelea kuwa maskini, utajiri wetu ni ardhi yenye rutuba, njia pekee ya kuendeleza hilo ni kilimo hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Magugu Katika Kilimo, Magugu ni tatizo kubwa sana katika kuongeza uzalishaji kwenye kilimo, takwimu zinaonyesha kuwa katika nchi ya Ethiopia kwa mfano, magugu hupunguza mavuno shambani kwa asilimia 30 hadi 88%, wakati Zambia ni kati ya asilimia 43 hadi 63%. Hapa Tanzania katika Nyanda za Juu Kusini upotevu wa mavuno kutokana na magugu ni kati ya 50% hadi 100%. Hili linatokana kwa kiasi kikubwa na kazi ya palizi kuwa ni ngumu sana na kutokufanywa kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine tafiti zinaonyesha kuwa palizi zinapofanywa kwa wakati zinaongeza mavuno hadi aslimia 138%. Taarifa hii inakatisha tamaa kwa mkulima wa Tanzania ambaye anategemea jembe la Mkono na hana uwezo wa kuajiri vibarua na hakuna teknolojia nyepesi ya kufanya palizi zaidi ya kutumia madawa ya kuulia magugu *herbicides* ambayo ni hatari kwa udongo na mimea, lakini pia hana uwezo kifedha kununulia madawa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inauliza Serikali inawasaidiaje wakulima wetu katika kubuni teknolojia rahisi kupambana na tatizo la magugu na je,

Serikali inaziwezeshaje taasisi za utafiti kama vile *SUA, CARMATEC, SEAS* na kadhalika katika kubuni teknolojia muafaka kupambana na tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aliyoitoa hapa Bungeni mwaka 2006 alitoa takwimu zifuatazo ikiwa ni malengo ya Serikali kwa uzalishaji ifikapo mwaka 2010. Kwa mfano, kahawa lengo lilikuwa kuzalisha tani 120,000 lakini hali halisi hivi sasa ni tani 40,0000, korosho lengo lilikuwa kuzalisha tani 180,000 ifikapo 2010 lakini hali halisi sasa hivi ni tani 74.1 na tumbaku lengo lilikuwa ni kuzalisha 100,000 lakini halisi ni tani 60.9, pamba ni kuzalisha tani 800,000 lakini halisi ni tani 267,004.

Chanzo: Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika mwaka 2006/2007 na Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya uzalishaji yaliyokuwa yamewekwa ili kufikiwa mwaka 2010 inaonyesha kuwa sio tu hata nusu ya malengo hayo hayakufikiwa, lakini baadhi ya mazao kama Korosho na Pamba mwaka huu 2010 hayakuweza kufikia hata ule uzalishaji wa mwaka 2006. Huku ni kurudi nyuma badala ya kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitolea tafsiri takwimu hizi kuwa, mipango yote inayoletwa hapa kuombewa fedha na Serikali inakuwa haikufanyiwa upembuzi yakinifu na badala yake Serikali inalijaza Bunge matumaini tu na hivyo kupitisha mapendekezo ya Bajeti za Wizara hii. Hii ni hatari kwa nchi inayotaka kweli kuinua kilimo, vinginevyo miaka yote pesa zitaendelea kupotea na umaskini utaendelea kuota mizizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baya zaidi malengo yaliyowekwa mwaka 2006 yameachwa na mwaka huu wa 2010, Wizara imetoa malengo mapya. Tunaitaka Serikali itueleze ni kwa nini inatoa takwimu ambazo hazikufanyiwa kazi wakati watendaji wapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya matatizo ya kilimo cha Tanzania ni kukosekana kwa uwekezaji wa kutosha kutoka ndani na nje, katika nchi za wenzetu, kazi ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji ni ya Serikali na wala siyo ya Wawekezaji na pale ambapo kuna miundombinu wawekezaji wa maana huvutika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, katika kusaidia kilimo cha umwagiliaji mamlaka za mabonde Tanzania zinaweza kutoa mchango mkubwa kwa kutafuta fedha ili kujenga miundombinu ya maji katika mamlaka zao na kuikodisha miundombinu hiyo kwa wakulima na wawekezaji. Kambi ya Upinzani ina imani kubwa kama miundombinu itakuwepo basi Watanzania wengi watajihusisha na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa miundombinu ya kufanikisha kilimo cha umwagiliaji imesababishwa kwa kiasi kikubwa kilimo kuonekana kama adhabu

badala ya kuwa ajira kwa Watanzania. Dhana hii inaweza kuondoka kabisa kwa kuwahusisha vijana walio wengi kwenye kilimo kwa mapendekezo tuliyoyatoa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu nyingi zinaonyesha kuwa uzalishaji unaongezeka kutokana na kuongezeka kwa eneo la kilimo *(production is directly proportion to increased cultivated area).* Dhana hii ndiyo Serikali inayoisisitiza kuwavutia wakulima wakubwa kuja hapa nchini kulima mashamba makubwa makubwa kwa kutumia zana za kisasa katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inasema dhana hii si sahihi kwani kinachotakiwa ni uzalishaji wenye tija kwa eneo husika. Kwa kutumia kanuni sahihi za kilimo bora na uzalishaji utakuwa mzuri. Hivyo basi wakulima wadogo ndio suluhisho la kukiondoa kilimo chetu kutoka tulipo hadi kuwa cha kisasa na cha kibiashara kama kweli nyenzo muhimu zitazingatiwa na kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia mashine kubwa katika kilimo maana yake unaiweka ardhi katika hatari ya kuondokewa na rutuba yake ya asili na ile iliyoongezwa wakati wa kurutubisha mazao husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilikwishatoa ushauri katika hotuba zake hapo nyuma kuhusiana na fursa tulizonazo katika kilimo cha muhogo hapa nchini, lakini ushauri huo haukufanyiwa kazi na hivyo kupoteza muda mwingi kwa wataalam wetu kutafuta njia za kupunguza umasikini wakati suala lilikuwa ni kuwaunganisha wakulima na masoko yaliyo nje au ndani. Unga wa Muhogo una matumizi mengi sana ya viwandani mbali na chakula cha kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima waliofukuzwa Zimbabwe walielekea Nigeria na kwa sasa wamekuwa ndio wazalishaji wakubwa wa muhogo na zao hilo ni la pili katika kuingiza fedha za kigeni kwa nchi ya Nigeria nyuma ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kambi ya Upinzani inawaambia Watanzania kuwa mapinduzi ya kilimo yameshindikana chini ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi baada ya miaka 33 ya uongozi wake. Hivyo, asilimia 80 ya Watanzania wanaotegemea kilimo wana maisha magumu sana hivi sasa. Hivyo basi, ifikapo mwezi OKtoba, 2010 waiweke CCM benchi, ili Upinzani waongoze nchi hii na kubadilisha maisha ya Watanzania kweli kweli yawe maisha ya neema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi y a Upinzani inasema kuwa Mapinduzi ya Kijani yanawezekana kwa Viongozi Wakuu Serikalini kuamini kwa dhati kuwa inawezekana. Kilimo ni sawa na Udaktari hivyo basi haihitaji "*trial and error*" kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha ya binadam. Tanzania tatizo ni kuwa viongozi wenyewe hawaamini kuwa inawezekana na bado wanafanya majaribio katika kilimo. Tunawaomba wananchi wachague watu makini wanaoamini kile wanachosema, hukumu yao ni hapo mwezi Oktoba 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge na wananchi ndiyo niliwaambia hotuba za wakati huu zinafanana na hivyo ni wakati wa lala salama. Nashukuru sana kwa hotuba yako Waheshimiwa Wabunge tumepata wachangia wengi kama 17 lakini kutokana na dakika zetu zile kumi kumi tunaweza kufika mpaka saa 12, halafu Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ufafanuzi wa baadhi ya hoja hizi. Kwa hiyo kwa kuanzia nitamwita Mheshimiwa Nsazungwanko.

Halafu Mheshimiwa Dk. Mahenge, Mheshimiwa Anna Lubembe, Mheshimiwa Anna Malecela, Mheshimiwa Ludovick Mwanzila, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Guido Sigonda na Mheshimiwa Kayombo wanaweza kumaliza asubuhi hii. Lakini kwa sababu ya shughuli zingine tulizonazo nitamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndugai aweze kukalia kiti.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai)*
*Alikalia Kiti*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini kabla sijasema ninalotaka kusema nataka nimkumbushe tu Msemaji wa Kambi ya Upinzani aliyetoka sasa hivi kwamba kwa maneno yake ni dhahiri hicho Chama hakichaguliki maana hakina programu mbadala, wanakuja na mbwembwe na porojo ambazo wala hazieleweki. Kwa hiyo, ndugu yangu nataka kumkumbusha tu kwamba chama kinachochaguliwa ni chenye programu maalum na sio mbwembwe za kisiasa na wenzetu wanashindwa hata kuona hata moja ambalo limefanyika vizuri hivi inawezekana kweli wote msione hata moja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwashukuru sana viongozi wakuu wa nchi yetu, Mheshimiwa Rais, Dr. Jakaya Kikwete na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kugawa haya maeneo mapya ya utawala, kwa kweli tunawashukuru sana sisi ambao maeneo yetu tangu uhuru yalikuwa hayajagawanywa tumepata faraja mpya kabisa. Tunashukuru sisi watu wa Kigoma kupata Wilaya mpya tatu.

Kwa kweli ni jambo kubwa la kihistoria, tumepata Wilaya ya Buhigwe kule Kasulu, tumepata Wilaya ya Uvinza kule Kigoma Vijijini na tumepata Wilaya ya Kakonko huko Kibondo. Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunasema ahsante sana na hakika haya ni maeneo ambayo mmeyaibua, yalikuwa ni baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayaonekani lakini yalikuwa ni sehemu ya vikwazo kwenye baadhi ya maeneo kuendelea kwa sababu tulikuwa na maeneo makubwa ya utawala, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa namna ya pekee naomba pia niwashukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kugawa Jimbo langu la Kasulu, Mashariki sasa hivi navyozungumza nina Majimbo mawili, Jimbo moja ni Jimbo la Kasulu Vijijini na Kasulu Mjini na wale wanaojua maeneo yale ni kwamba kwa kweli imetusaidia sana na mambo kule yako poa kabisa. Wananchi wa Kasulu tunasema ahsante sana kwa yote mawili kwa kugawa maeneo ya utawala, Wilaya mpya na kupata Jimbo jipya la uchaguzi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nikukumbushe yale mengine ambayo nimekuwa nikikunong'oneza wewe na Mheshimiwa Waziri Celina, naomba muendelee kutukumbuka, tunaomba sana sana muendelee kutumbuka ili kwa kweli kuweza pia kufika mahali nchi ikaonekana ina usawa wa kweli hasa katika kugawana rasilimali chache tulizonazo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema mambo hayo ya utangulizi na pia naomba kwa namna ya pekee nimshukuru Rais kwa ziara yake ya wiki ya jana ambapo alikwenda Kigoma kwa mambo matatu tu, umeme, maji na barabara na sisi tumefarijika sana sana kwamba umeme sasa Kigoma mambo safi, umeme unajengwa Kasulu mambo safi. Sasa maji katika Mji wa Kigoma - Ujiji mambo safi na barabara ya lami kutoka Kidahwe hadi Kasulu sasa inajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa yote hayo, tunasema ahsante sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne kusema kweli kule kampeni mmeturahisishia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hotuba moja kwa moja ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 73 na 76 naona Mzee Cheyo ananikumbusha kilimo, sisi ni wakulima wa asili bwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa ule nizungumzie juu ya shamba la mbegu la Bugaga. Mheshimiwa Waziri na timu yake walitembelea pale Kasulu, shamba la Mbegu la Bugaga, ambalo tayari limeshakabidhiwa Wizara ya Kilimo tangu Mwaka jana Septemba, lakini nilikuwa naangalia kwenye kitabu cha *development* sikuona mahali popote ambapo shamba lile sasa au linakarabatiwa miundombinu yake maana shamba linafanya kazi, tunazalisha michungwa, tunazalisha migomba, tunazalisha utafiti wa mahindi, maharage, mbaazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielewe *exactly* ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa shamba la Bugaga na kitu gani kinafanyika. Mheshimiwa Waziri na timu yake, Katibu Mkuu wake ndugu Muya na Wakurugenzi, ningependa nipate jibu mahususi kwa sababu lile shamba ni la muda mrefu sana, wewe mwenyewe unajua, nilitaka kujua *exactly* ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya shamba lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pia nikumbushe Mheshimiwa Waziri alipokuwa pale kwenye shamba lile mwaka jana Septemba, tulimkumbusha umuhimu wa kupima eneo lile ili hatimaye tuweze kujua kama lote wanalihitaji au kipande kitabaki kwa ajili ya wakulima wengine. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi huo Mheshimiwa Waziri awe *specific* juu ya fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya shamba la mbegu la Bugaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 73 na 76 naamini wamesahau au ni *error* hawaku-*mention* mahali popote shamba la mbegu la Bugaga katika kurasa zote zile mbili, wametaja mashamba mengine lakini shamba la Bugaga na hakika umesahau kulitaja kwa sababu wewe mwenyewe ulifika na siku zote nikikuita kwamba wewe ni Mzee wa Bugaga, hilo jambo nadhani utalikumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nimkumbushe, mwaka jana alitembelea Chuo cha Kilimo cha Mbondo Kasulu. Mimi nilimsindikiza kama anakumbuka, tulishauriana mambo mengi na sisi kwenye *RCC* ya mwaka jana tumeshakabidhi Chuo kile kwa Wizara yako ya Kilimo lakini kwenye *Training Institute*, sioni mahali popote unapozungumzia Chuo kipya kinachofufuliwa, zamani kilikuwa cha kilimo, kinafufuliwa sasa, Waziri anajua. Eneo lile ni kubwa sana na tulikuwa tunaamini kwamba ile Shule ya Sekondari ya Kilimo inayoendelea pale ingeweza ika-*co-exist* pamoja na Shuo kwa sababu ni eneo kubwa sana. Kwa hiyo, ninaomba sana suala hilo nalo Mheshimiwa Waziri anipe majibu mahususi, ni mambo gani yanafanyika, kama ni ukarabati wa majengo, ujenzi, upimaji wa eneo na kadhalika ili tuweze kufahamu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nataka kuzungumzia hili suala la ruzuku ya mbegu na mbolea. Eneo hili mmefanya vizuri, Wizara hongereni sana. Mbegu imefika Kigoma na Kasulu kwa wakati lakini nina ushauri kwamba Wizara mfungue dirisha la kuweza kuangalia namna ya kutoa mikopo hii kwa wakulima Vijijini kupitia kwenye SACCOS zao au kwenye Vyama vya Ushirika katika maeneo yao. Wakati mwingine mbolea inafika wakati wakulima hawako tayari kulipia fedha *cash* yaani mkono kwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni juu ya *cooperative development.* Nimeshangaa kwenye Kitabu cha *Development*, ni fedha kidogo ambayo imetengwa kwa ajili ya *cooperative development* kwa maana ya *cooperative reform* na *modernisation*. Naishauri Wizara kuangalia namna ya kuanzisha *programme* na Chuo cha Ushirika Moshi ambacho sasa hivi ni Chuo Kikuu Kishiriki kwa ajili ya hii *cooperative development*. Mheshimiwa Waziri anajua Chuo cha Ushirika Moshi au Chuo Kikuu Kishiriki cha Moshi sasa hivi chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine, ndiyo mabingwa wa ushiriki katika nchi yetu. Ninashauri *strongly* kwamba eneo hili ni muhimu sana hasa ukizingatia kwamba nchi nzima sasa hivi tumeanzisha *SACCOS*, kwa kweli nafikiri ingesaidia sana katika maendeleo ya wananchi wetu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na baada ya ufafanuzi bila shaka nitaunga mkono hoja kwa kazi nzuri iliyofanywa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na baada ya Mheshimiwa Nsanzugwanko sasa ni Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge na atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe.

Mheshimiwa Dkt. Mahenge, karibu.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitamke kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, kutoa pongezi na shukurani nyingi sana, kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuridhia na kutupa Mkoa mpya wa Njombe na kwa kuridhia na kutupa Wilaya mpya ya Wanging'ombe. Wananchi wa Mkoa wa Iringa wamepokea uamuzi huu kwa furaha kubwa sana na haya ni maombi ya muda mrefu ambayo Awamu ya Nne imeonyesha kwamba inawezekana. Siyo uamuzi mdogo kuamua kuundwa kwa Mikoa mitatu kwa wakati mmoja, Wilaya nyingi kwa wakati mmoja, Tarafa na Kata, haya ni maamuzi yanayostahili shukurani za pekee kwamba kweli Awamu ya Nne inafanya kazi. Wananchi wa Iringa wanashukuru sana hususani Wilaya za Ludewa, Njombe na Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimwa Mizengo K. P. Pinda ambaye haya maombi ya kuundwa kwa Mkoa wa Njombe alianza kuyashughulikia alipokuwa Waziri wa TAMISEMI na hivi ameyahitimisha yeye mwenyewe ndani ya miaka hii miwili. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa upendo huo mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaungana na mapendekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba Mkoa huu uitwe kwa jina la Njombe na hata katika maombi yetu wakati wote tulikuwa tunaongelea Njombe kwa sababu sisi tuna historia kwamba tulikuwa chini ya Wilaya ya Njombe, ni wamoja nadhani hili la Njuluma liliingia tu kwa sababu ya utani kwamba kulikuwa na Chama cha Ushirika cha Njoluma lakini kimsingi tunaungana na Mheshimiwa Rais kwamba Mkoa ule uitwe Njombe na tunaendelea kushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi haitakuwa na mantiki kuita Njoluma baada ya kupata Wilaya nyingine mpya ya Wanging'ombe kwa sababu Njoluma maana yake Njombe, Ludewa na Makete, kwa hiyo, utakuwa unainyima haki kwanza huo Mkoa mpya kupanuka lakini pia utakuwa unawanyima haki wenzetu wa Wilaya mpya ya Wanging'ombe. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba sisi kwa pamoja tunaungana na Mheshimiwa Rais kwamba Mkoa huu uitwe Njombe kwa sababu kwa kweli tumefarijika sana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda upande wa hotuba ya Bajeti ya Kilimo, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na mimi mengi sana nitaongea kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa sababu hiki ni kikao cha mwisho, nadhani tunatakiwa tuseme yale ambayo tumeweza kufanikiwa kwa ushirikiano wetu pamoja Serikali ya Awamu ya Nne, Viongozi wa Halmashauri pamoja na wananchi. Kwa hiyo, katika sekta hii ya kilimo kwa upande wa Makete, Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Makete haikuwa na soko hata moja wakati wa Awamu ya Nne inakuja kwenye utawala wake leo hii nasimama hapa tayari Awamu hii ya Nne imejenga masoko nane, tumeweza kujenga masoko Ikuwo, Mfumbi, Matamba, Kata ya Kipagalo, Kata ya Ukwama, Tandala na pale Mjini Makete tumejenga masoko mawili. Kuna soko moja kubwa la Kimataifa ambalo

limegharimu zaidi ya shilingi milioni 500, hivyo hatuna budi kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa sababu haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwenye sekta hii ya kilimo, tumefanikiwa kujenga machinjio pale Wilayani Makete. Tumejenga machinjio ya kisasa sana na kubwa ambapo itasaidia wakulima kupeleka mifugo yao na kutoa huduma inayotakiwa katika suala zima la machinjio. Tumeweza kujenga machinjio katika Kata za Tandala, Matamba na tunaendelea kujenga machinjio katika Kata nyingine. Hii ni Awamu ya Nne iliyotekeleza haya ndani ya miaka hii minne na nusu na bado kwenye bajeti hii tunaendelea kuleta maendeleo mbalimbali kwa muda huu uliobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeweza kujenga majosho karibu kila Kata. Tumefanikiwa kupata mnada wa kwanza wa mifugo Makete uliojengwa na Serikali ya Awamu ya Nne pale Isapalano. Haya ni mafanikio makubwa ambayo tunadhani tuna kila sababu za kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa mafanikio haya makubwa. Tunasema ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanikiwa pia kwenye zao la Pareto, Wilaya ya Makete ni ya wakulima wakubwa wa zao la Pareto na kwa miaka kumi iliyopita, ule uongozi wa Awamu ya Tatu, zao la Pareto lilikosa soko. Alipokuja Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, alisema hakuna nchi inayoweza kuendelea kama haina zao la biashara na kwa hiyo aliahidi kurudisha zao la Pareto kwa kulipa soko lake. Lile zao tayari limesharudi na wakulima wameshaanza kulima na bei ya Pareto sasa hivi kwa ile *grade* nzuri inafika mpaka kwa kilo shilingi 1,500/=. Sisi tunashukuru lakini nadhani hapa labda la msingi ni kutoa hamasa kwa wananchi ili walime zaidi hili kwa sababu walikuwa wameshaKata tamaa baada ya lile soko kukosekana, wakawa hawawezi kulima Pareto. Kwa hiyo, sasa hivi ule muamko wa kwanza kulima, umepungua, naiomba Serikali iendelee kuwahamasisha wananchi waweze kulima Pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika Pareto, pendekezo langu basi ni vizuri Serikali ione namna ya kuanzisha kiwanda kingine ili kuleta ushindani kwa sababu sasa hivi Pareto bei yake inapangwa na mnunuzi mmoja wa kiwanda kimoja na kwa hiyo, hiyo bei inaweza kuwa haina tija sana kwa sababu hakuna ushindani. Tulikuwa na taarifa kwamba kuna kiwanda kinajengwa Mbeya labda Waziri atatufafanulia kama ni kweli na kama hivyo ndivyo basi tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwenye zao hili la Pareto, ni vizuri kuruhusu wanunuzi wengine wawe wengi ili waweze kuwafikia wananchi mbalimbali maana nilipokuwa nazunguka Vijijini, unakuta baadhi ya maeneo wanasema hawajafikiwa na hivyo wanakosa hamasa ya kulima Pareto. Kwa hiyo, tunaendelea kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kweli kwa mambo haya makubwa ambayo imeyafanya ndani ya miaka minne na nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia suala zima la mbolea kwamba mbolea imefika Makete kwa utaratibu ambao umeanzishwa na Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Ni utaratibu mzuri lakini labda la msingi tuiombe tu kwa Wilaya ya Makete,

tunayo mazao ambayo yanahitaji mbolea mara mbili kwa mwaka kama Viazi, kwa hiyo, kuleta mbolea mara moja inakuwa hazitoshi. Lakini la pili, tunaiomba Serikali kwa mazingira ya Makete, Jiografia ya milima na mambo mengine basi mbolea iweze kuharakishwa isije imechelewa wakati mwingine inakuja mwezi wa tisa wakati sisi kilimo cha Mahindi kinaanza mwezi wa sita. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itusaidie kuharakisha mbolea iweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni haya, naendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Kombani, kwa ushirikiano wao kwa namna ya pekee walivyoweza kusaidia tukapata Mkoa mpya na Wilaya mpya. Nadhani kazi ni kwetu sasa kuungana na wananchi kufanya kazi kwa bidii, maarifa ili tuweze kujenga Mkoa wetu mpya wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Binilith Mahenge na kwa orodha niliyonayo hapa anafuata Mheshimiwa Anna R. Lupembe na baada ya hapo anafuata Mheshimiwa Anne K. Malecela.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi siku hii ya leo ili niweze kuchangia Wizara ya Kilimo, Chakula na ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na uzima mpaka siku hii ya leo. Vilevile napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwanza, kwa kutembelea Mkoa wetu wa Rukwa kuanzia tarehe 17 – 19, amefungua miradi mbalimbali ambayo ilikuwa kero kwa wananchi hasa umeme na barabara. Wananchi wa Rukwa tulikuwa hatuna barabara nyingi za lami lakini sasa mwelekeo umekuwa mzuri, tumefunguliwa barabara za lami ambazo ujenzi wake utaanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nimshukuru Rais pamoja na Waziri Mkuu, kwa kutupatia Wilaya mbili ambazo ni Wilaya ya Kalambo na Wilaya ya Mlele. Ina maana Mkoa wa Rukwa sasa jumla yake kutakuwa na Wilaya sita. Tunaomba tuwashukuru sana Viongozi wetu kutambua na kuhakikisha maendeleo kwa wananchi yanafika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwenye hoja moja kwa moja. Naomba niipongeze Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya kuwafikia wakulima kwa urahisi kwa kujua na kutambua kuwa Tanzania yetu wakulima ni wengi zaidi kuliko wafanyakazi, wakulima ni 80% na wafanyakazi ni 20%. Wakulima wengi katika Mkoa wetu wa Rukwa, safari hii wamejitahidi sana kulima na mwaka huu tumepata mazao mengi kupita wakati mwingine, kwa jitihada hiyo ndogo ambayo imewafikia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Mkoa wa Rukwa ni wengi, lakini hamasa ni chache. Wanaopata huduma nzuri na bora ni wachache sana, wengi hawapati huduma nzuri na kwa ukaribu. Mkoa wetu wa Rukwa Jiografia yake kidogo sio nzuri na Mkoa wenyewe ni mkubwa na Maafisa Ugani ni wachache sana, unakuta Kata tatu Afisa Ugani mmoja na Kata nyingine hazina Maafisa Ugani mmoja, unakuta Kata nyingine hazina kabisa Maafisa Ugani. Sasa unakuta mambo mengi ambayo Serikali ilipanga kuyafanya wale wananchi wengine hawayapati wala kuyajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna hamasa kuwa wananchi wajiunge kwenye vikundi, wakijiunga kwenye vikundi watapata asilimia ya *Power Tiller* au asilimia ya matrekta. Ile hamasa wale wananchi hawaipati na wala hawajui kama kuna kitu gani ambacho Serikali yao imewapangia na wanatakiwa wapate nini kutoka kwenye Serikali yao. Sasa unakuta ukitoa hamasa kama wewe ni Mbunge kusema jamani Halmashauri zenu zimepewa maagizo kuwa mnunue *Power Tiller* au matrekta msogee pale kwenye Halmashauri zenu ili muende mkachukue *Power Tiller* na yale matrekta kwa 20% wale wakulima hawajui na wala hawaelewi ni kitu gani Serikali yao inafanya. Tunaomba Serikali kwa kazi nzuri inayofanya basi ile hamasa wale wakulima kule waliko wafuatwe ili waelezwe ni kitu gani Serikali yao inafanya. Ni vitu vingi vizuri ambavyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya kwa Awamu ya Nne na wakulima wamekuwa na imani kubwa sana kwa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi na wanaipenda Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Kusema kweli ukienda kule Vijijini ukisema *CUF* wengi hawajui *CUF* ni nini wanajua Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na juhudi kubwa na nzuri ambayo Serikali ya Awamu ya Nne imefanya, ninaomba Waziri wetu wa Kilimo, aweke mikakati ya kuwafikia wananchi kule Vijijini ili kuweza kuwapanga waweze kujua Serikali yao inafanyaje kuhusu *Power Tiller* na matrekta, Serikali imewawekea mambo mazuri ndani ya Halmashauri yao. Ninajua Waziri anasaidiana na Waziri Kombani kwenye TAMISEMI, basi mpange vizuri zile Halmashauri hata wale wafanyakazi kwani kuna wafanyakazi Idara nyingine kule Halmashauri hawana shughuli muhimu sana basi waende kule Vijijini kuhimiza au kuhamasisha wananchi wajiunge kwenye vikundi ili waweze kupata fursa zao za kupata *Power Tiller* na matrekta ili kilimo kizidi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo pamoja na vocha. Kama nilivyosema, wananchi wengi hamasa hawaipati, lakini Serikali safari hii imejitahidi kufikisha vocha mapema, Mkoa wetu wa Rukwa, Wilaya ya Mpanda, imefanya vizuri kwenye vocha lakini Wilaya nyingine hazikufanya vizuri sana wananchi wengi hawakupata vocha. Ninaomba Serikali kwenye upande wa vocha, wajipange vizuri, wananchi wengi wanataka fursa ya kupata vocha lakini hawapati. Sasa hivi ukienda kuita mikutano ya hadhara, ukiuliza wakulima mnapata vocha, wengi wanakwambia hatujapata vocha. Ninaomba Mheshimiwa Waziri kuhusu mambo ya vocha, mjipange vizuri wananchi wengine hawapati vocha kwa wakati na wala hawapati kabisa. Kuna Watendaji wengine si waaminifu, ndiyo tatizo mojawapo, Maafisa wako wa Ugani siyo waaminifu hawafikishi vocha hizo, wenyewe ndiyo wanachukua, wanafanya shughuli zao binafsi na kujifurahisha na nafsi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja kwenye Tumbaku. Sisi Wilaya ya Mpanda, tunalima Tumbaku sana na wananchi wa Mpanda ile Tumbaku inawanufaisha sana. Mimi kila siku huwa najiuliza, huyu mkulima wa Tumbaku anapata hela nyingi lakini kuna tatizo, akifika pale anahesabiwa, tulikukopesha mbolea na kadhalika, nusu ya zile pesa zake za Tumbaku zinabaki pale kwenye Vyama vya Ushirika. Sasa ukiuliza ni kwa nini hela ile inabaki au kwa nini wewe mkulima kama mkulima si una pesa, kwa nini usiende kununua mbolea wewe mwenyewe ukalima Tumbaku yako halafu ukaenda kuuza pale? Wanasema ile mbolea haipokelewi. Sasa tunaomba basi Wizara kama Wizara, huyu mkulima wa Tumbaku naye awe huru, anunue mbolea yake yeye kama yeye, akishalima yale makampuni yakienda pale, yanunue Tumbaku ya yule mkulima kama wakulima wengine ili yule mkulima apate nafuu au yule mkulima apate faida kubwa zaidi. Ni tatizo kubwa sana kuhusu Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi wa Tumbaku katika Mkoa wa Rukwa wanajitahidi sana kulima na Wilaya ya Mpanda safari hii wamelima sana na wamepata sana lakini kila siku unajiuliza mbona huyu mkulima wa Tumbaku haendelei? Haendelei kutokana na kwamba hela zote zinakwenda kwenye Makampuni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mathayo D. Mathayo na napenda kusema kwamba bajeti yao ya kilimo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme ukweli hata kama kweli kuna fitina basi ziwe na mipaka. Miaka yote mitano, wenzetu mnaona sisi hatujafanya kitu kweli? Basi ninaomba niwashushue kwa kuwaonesha yaliyofanywa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika Jimbo la Same Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama kuna kitu kilichofanikiwa ndani ya Jimbo langu la Same Mashariki, ni Kilimo Kwanza. Kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepiga hatua kubwa sana upande wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, Jimboni kwangu, nina maeneo ya milima na maeneo ambayo ni tambarale. Maeneo ya milimani, ninalima Tangawizi kwa wingi, ninalima Hiliki, Kahawa, Ndizi, Mbogamboga na kadhalika. Kata nne zilizo katika maeneo ya tambarale, ninalima Mpunga, Mahindi, Mbogamboga na vitu vingi sana. Lakini naomba niseme ukweli, mimi kwenye Jimbo langu silimi Miwa, kama ipo ni ya kutafuna tu, kwa

hiyo, nisingeweza kuwa Mbunge mwenye akili timamu kama nitawashawishi wananchi wangu watengeneze kiwanda cha sukari kwa sababu silimi miwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirudi kwenye agenda iliyonifanya nisimame, kiwanda kidogo cha Tangawizi kilichoko Mamba Miamba, kiwanda kile ni kiwanda cha wananchi wanaolima tangawizi Same Mashariki. Wananchi wale wameshirikiana na mimi baada ya kushawishiwa sana na Halmashauri yetu ya Wilaya ya Same, inayoongozwa na Mkurugenzi imara anayeitwa Iddi, naomba nimshukuru sana Mkurugenzi wa Wilaya ya Same kwa kuwa mbunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya sisi kuona tuna Tangawizi nyingi lakini tukiziuza kama zilivyo bei ni ndogo. Halmashauri ikatushawishi na mimi nikawashawishi wananchi tukaona tutengeneze Kiwanda kidogo cha Kusindika Tangawizi. Kiwanda kidogo kile tumekijenga wenyewe, mimi na wananchi wa Same Mashariki milimani, jengo lile likawa tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge ambaye sichoki, nikaenda, nikambembeleza Rais, kwanza, nikaanza kumbembeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, akakubali akaja akaweka jiwe la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais akakubali harambee ya kuchangisha ili tuweze kupata mtambo wa kusindika Tangawizi yetu. Rais akakubali na ninaomba kupitia Bunge hili, nimwambie ahsante sana. Tulipata zaidi ya shilingi milioni 300, hii ndiyo Kilimo Kwanza ambapo wenzetu watani wetu mnasema hakikufanikiwa, hiki ndiyo Kilimo Kwanza. Sasa baada ya kujenga lile jengo na ninaomba niwaambie ndugu zangu Wabunge, hamuwezi kujenga kiwanda bila ya kutumia wataalam. Kiwanda kile kimesimamiwa na wataalam wa *SIDO* na mtambo tunanunua kutoka *SIDO*, wakasimamia wenyewe, wakaleta ramani kiwanda kikajengwa. Tukakusanya shilingi milioni zaidi ya 300, naomba niwaoneshe mKataba huu hapa, tumeingia mKataba na *SIDO* yaani sisi wananchi wa Same Mashariki tunaolima Tangawizi tukishirikiana na Halmashauri ya Same, tukaingia mKataba na *SIDO* tarehe 21 Mei, 2010 kwamba waweke mtambo wa kusindika Tangawizi kwa gharama ya shilingi 88, 895,000. Mjue kwamba, Rais alitusaidia tukapata zaidi ya shilingi milioni 300, mtambo ule umetu-*cost* shilingi milioni 88 na hela kidogo. Kwa hiyo, katika mKataba huu, tumeelewana na *SIDO* kwamba, kazi ya kuweka ule mtambo iwe ni miezi minne. MKataba umeanza tarehe 4 Juni, 2010 watatukabidhi kiwanda kikiwa kina mitambo tarehe 4 Oktoba, 2010. Jamani hivi Kilimo Kwanza hakijafanikiwa hapo? Halafu wenzetu nyie hapo mbele mnasema nini? Kilimo Kwanza kimefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la ajabu basi kaeni vizuri niwaambie, leo hii tangu saa 11 asubuhi, Gazeti la Tazama, hili hapa, linazunguka milima yote, lina picha ya kile kiwanda, linasema kakibanda kakuku, hakana hata mtambo ndani, jamani nyie

watu wa magazeti muwe mnafanya *research* kwanza kabla hamjaandika mambo, ni aibu, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnaona yote ninayowaeleza hapa huu mKataba, nakala yake nilimpelekea Rais, maana ndiye anayekusanya pesa, nakala ya mKataba huu nimempelekea Waziri Mkuu, ndiye aliyeweka jiwe la msingi, nakala ya mKataba huu Kata zote 10 wanao, leo unawapelekea magazeti si wanakucheka. Mambo mengine jamani ni aibu, hili gazeti sasa ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jamani ninaomba niwaambie kitu kimoja. Ndugu zetu mnaotangaza nia, tangazeni nia kwa unyenyekevu, wewe unaenda kumtongoza mwanamke ili umuoe, unaanza kumwambia una makengeza, nywele zako zimenyonyoka, miguu iko upande, atakukubali? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyepiga picha hii ni kaka yangu aliyetangaza nia. Mimi nina *CD* yake akiwaambia Waandishi wa Habari, naomba niwaletee hicho kibanda cha kuku mkitoe kwenye magazeti. Alidhani anagombea na mwanamke ambaye ni legelege, hapana! Nilimrekodi yale maneno yake, ni yeye amewapelekea Gazeti la Tazama hii picha na nina vithibitisho. Mkitangaza nia, msiponde kazi za wenzenu, njooni tushindane kwa nguvu ya hoja lakini msizungumze mambo ambayo hayana maana. Leo Gazeti la Tazama limeingia aibu, wananchi tangu saa 11 haya magazeti wanayachana tu, wanayachana kwa sababu ni uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilimwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba atoe tamko la Serikali kuhusu haya magazeti, yanapuuzwa lakini haya mambo yatakuja kumwaga damu siku moja. Haya mambo si ya kupuuza, hakuna kitu kikubwa duniani ambacho hakianzii kwenye udogo. Hiki kitu mnakiona ni kidogo kuna siku kitakuwa kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwenye Jimbo langu Kilimo Kwanza kimefanikiwa. Mheshimiwa Wasira hongera, Mheshimiwa Mathayo hongera, Waziri Mkuu hongera na Rais hongera. Napenda kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mama hongera sana. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI**: Huyo ni Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nami naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kutembelea Mkoa wa Rukwa na kuweka mawe ya msingi kwa ajili ya barabara zetu na hususan barabara ya Sumbawanga Matai kwenda Kasaga na Matai kwenda Kasesha. Ni faraja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ndoto ya Jimbo la Kalambo kutamkwa kwamba sasa ni Wilaya mpya kama zilivyotangazwa Wilaya nyingine pamoja na uundaji wa Kata mpya karibu tisa pamoja na Tarafa na Vijiji. Shukrani zangu zimwendee pia Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kazi ambayo ameifanya. Asichoke kwa sababu tulikuwa tunamsukumasukuma hapa na pale lakini naona alikuwa imara na ametusaidia sana, Mungu awazidishie kwa sababu wananchi wa Jimbo la Kalambo ambao sasa wataitwa ni wananchi wa Wilaya ya Kalambo, wanawashukuru wote Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na TAMISEMI, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya mpaka tumeweza kufikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kupuuza mafanikio haya ambayo tumeyapata kwa Tarafa, Kata, Vijiji pamoja na Wilaya na ujenzi wa barabara ya lami ya Sumbawanga Matai kwenda Kasanga. Tunawashukuru sana, tunajua mtatusaidia ili Wilaya hii iweze kusimama na wala hakuna anayeweza kubeza mafanikio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri wa Kilimo, kwa kazi nzuri ya kutoa taarifa hii ya Wizara ya Kilimo. Kilimo Kwanza, kilipoanzishwa katika nchi hii miaka miwili hivi iliyopita, Mkoa wa Rukwa tayari tulikuwa tuna MAKIRU, ni Mpango Maalum wa Kuendeleza Kilimo katika Mkoa wa Rukwa na nimshukuru sana Mkuu wa Mkoa, Ndugu Ole Njolai, ambaye amesimama imara sana kuweza kuhakikisha kwamba MAKIRU inafanikiwa. Lakini tunahitaji msaada katika mambo mengi ya msingi hasa kuhusu pembejeo, zana za kilimo, dawa, Maafisa Ugani na mambo ya namna hiyo hasa utafiti ili wananchi wa Jimbo la Kalambo ambayo sasa ni Wilaya ya Kalambo, waweze kupata mafanikio makubwa zaidi ili waweze kupata bei nzuri ya mazao na kuweza kupata maisha bora kama ahadi ya Rais ilivyo katika Awamu hii ya Nne. Mkoa umejipanga vizuri sana kwa kupitia mpango huu wa MAKIRU, tunaomba Wizara isaidie pale ambapo MAKIRU haikuweza kuzingatia masuala fulani tu machache ili tuweze kufanikiwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kalambo ambayo sasa ni Wilaya ya Kalambo, kilimo cha mahindi kimeshamiri sana. Jimbo lote linalima mahindi, mahindi ndiyo msingi wa uchumi wa wananchi wote wa Jimbo la Kalambo na Wilaya hii mpya. Bado hatujapata utafiti wa kutosha katika Jimbo hili ili tuweze kupata mazao ya msingi yatakayoweza kuwasaidia wananchi katika Wilaya hii mpya. Ninachoomba, Wizara hii ya Kilimo tusaidieni kufanya utafiti kuhusu suala la ukulima wa Alizeti, Shayiri, Maharage, Karanga na mazao ya aina hiyo ili wananchi waweze kuwa na mazao mbadala badala ya kuendelea kutegemea mahindi peke yake ili waweze kujipatia bei nzuri na kuweza kujipatia maisha bora. Tuongezeeni Maafisa Ugani wa kutosha katika Vijiji ili waweze kusimamia vizuri suala la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *SACCOS*, tunazo *SACCOS* ambazo ni ndogo sana, hazijaweza kufanikiwa vizuri kwa sababu zina mtaji mdogo, tunaomba Wizara hii ituongezee Maafisa Ushirika ili *SACCOS* hizi ziweze kufanya vizuri na ziweze kukua, lakini uhamasishaji bado ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Soko la Kimataifa la Mazao ya Nafaka pale Matai, soko hili limejengwa lakini bado halijatumika vizuri. Suala la kuwekeza mazao katika ghala ili watu waweze kuuza mazao kwa bei nzuri nalo bado halijafanikiwa vizuri kwa sababu pana matatizo ya upotevu wa mazao katika ghala kiasi ambacho kinawakatisha tamaa wafanyabiashara na wananchi wanaowekeza pale. Tunaomba Wizara itusaidie kusimamia kwa karibu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mazao wakati huu wa msimu wa mazao tunapoanza inakuwa chini, wakulima wanalalamika. Mimi nimepita katika Jimbo lote, wanalalamikia sana, wafanyabiashara hawa wanakwenda kulangua mazao kwa wakulima kwa bei ya shilingi 10,000 kwa gunia, kitu ambacho kinasikitisha sana. Bei hiyo haiwezi ikamsaidia mkulima kuweza kulipia gharama ya uzalishaji wakati hata mbolea hakupata kwa sababu vocha zilichezewa na wale waliopewa jukumu la kusambaza mbolea hiyo. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha, tunaomba suala hili lizingatiwe ili watu ambao wanachezea wakulima waweze kuadhibiwa kulingana na makosa waliyoyafanya. Upotevu wa vocha unasikitisha sana, tunaomba sana Serikali ichukue hatua ili kuweza kujisafisha kwa sababu wananchi katika Jimbo la Kalambo kwa kweli wanasononekana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *SGR*, ninaiomba mwaka huu inaponunua mahindi katika Jimbo la Kalambo au katika Wilaya ya Kalambo sasa, izingatie ukumbwa wa maeneo katika Wilaya hii mpya. Wamekuwa wakinunua mazao pale Matai peke yake ambapo hapatoshelezi, watu hawawezi wakatoka Kasanga, wakatoka Mwimbi na sehemu za Mwazye kwenda kuuza pale Matai, wafanyabiashara wa kati ndiyo wanaopata fursa hiyo. Kwa hiyo, ninawaomba *SGR* mwaka huu ili wananchi waweze kupata manufaa, wafungue vituo katika Vijiji vifuatavyo, Mwimbi au Ulumi, Mwazye, Mkombo, Kaluko, Msanzi, Mkowe na sehemu nyingine ambazo tuna maghala ambayo yalijengwa zamani kidogo na wanaweza wakatunza mazao pale kwa muda halafu wakayasafirisha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii, ninaiomba sana Wizara ya Kilimo ihakikishe kwamba, inazingatia kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kalambo na Wilaya ya Kalambo ili waweze kulima zaidi ili kuchangia mazao katika Akiba ya Taifa ili kuwalisha Watanzania ambao wanapatwa na njaa kama ambavyo Wabunge wengi wamelalamika. Kule Kalambo kuna chakula kingi lakini tatizo ni usafirishaji kwa sababu barabara sio nzuri, lakini na pia wakulima wanapata bei ndogo na ndiyo mara kwa mara tunaomba Wizara itukubalie tuuze nchi jirani kama Kongo, Zambia, Burundi, ili tuweze kupata fedha za kutosha kuweza kulipia gharama za kilimo. Lakini zana za kilimo nazo zizingatiwe, wakulima wauziwe *power tillers* na matrekta ili waweze kulima zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Maafisa wote, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ludovick Mwananzila. Kama nilivyosema, naomba kutambua uwepo wa Mheshimiwa Spika, Samuel Sitta kwenye kiti chake pale. Tunafarijika sana tunapomuona humu Bungeni akiwa anakalia kiti chake cha Urambo Mashariki. Nimhakikishie tu kwamba kama akiomba kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo Kwanza, nitampa nafasi ya kipaumbele kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitatoa dakika moja kwa ajili ya Mheshimiwa Spika akitaka kuchangia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nataka kutumia nafasi hii, kuwashukuru sana wapiga kura wa Bariadi Mashariki, tumeshirikiana vizuri kwa miaka mitano na nitaomba tena miaka mitano ili tuweze kukamilisha mambo ambayo bado hatujaweka sawasawa ambayo ni pamoja na daraja la Gamalaha na Ukigwamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka kusema kwamba sisi watu wa Bariadi tumefurahishwa sana na kuwa na Mkoa mpya wa Simiyu na Wilaya mpya ya Itilima ambapo Makao Makuu ya Mkoa yatakuwa Bariadi na yale ya Wilaya yatakuwa ni Lagangabilili. Vitu hivi, wale ambao ni vuvuzela wanavyopiga kelele, waone haya, ndiyo maana ya uwakilishi madhubuti ambao unaleta mambo mazuri mazuri kama haya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamba. Mwaka huu bei ya pamba kama alivyosema Waziri ni shilingi 600 kwa kilo, mimi naona hii bei haitoshi, ukilinganisha na gharama za kulima kwenyewe na sasa tuna *Power Tillers*, tunaweka *diesel* ambayo bei yake iko juu, usafiri uko juu na mambo mengine. Mimi nafikiri bei hii inaweza kuongezwa kwa sababu Serikali imefanya kazi nzuri ya kuondoa kodi kwa wanaosindika mbegu, sasa kodi hakuna kwa hiyo ile badala ya kuifanya iwe faida yao afadhali kiasi hicho Mheshimiwa Waziri aseme hiyo iliyopatikana ipelekwe katika kuongeza bei ya wakulima, hakuna kodi kwa mashudu basi hiyo ipelekwe kwenye kuongeza bei ya wakulima. *Cess* tumepunguza kutoka 5 - 3 basi hiyo iliyobakia ipelekwe katika kuongeza bei kwa ajili ya wakulima. Mimi nina hakika bei hii ingepandapanda ifike shilingi 700/=, 800/= hiyo ndiyo itakuwa ni bei ambayo itaweza kusaidia angalau kupunguza gharama ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka kusema kitu kimoja kwamba Mheshimiwa Waziri mwaka jana ulituondolea kile kitabu ambacho fedha ilikuwa inakatwa na pembejeo tulikuwa hatupati lakini sisi wakulima wa pamba tunaendelea kukatwa fedha. Kuna hili Shirika la *Cotton Development Fund*, linapokokotoa bei yetu, linatoa fedha kidogo kutoka kwa bei ya wakulima. Pia huu mtindo wa *Cotton Development Fund* kuwa yenyewe ndiyo inaagiza madawa halafu inagawanywa na inatumia hiyo fedha ambayo imekatwa kwa wakulima, naona hii ni *double financing*. Kwanza wanatukata bei, wananunua madawa halafu wanakuja kutuuzia na wanachukua ruzuku kutoka Serikalini kwa mtindo wa vocha. Nashauri labda Waziri angeliangalia suala hili pia kama kuna njia kwamba hizi fedha zinazokatwa kwa ajili ya hii kitu ziweze kurudishwa kwa wakulima. Kama kuna haja ya *Cotton Development Fund* basi hii iwekewe fedha kutoka Serikalini kama vile tunavyoweka kwenye Mfuko wa Pembejeo, uwe Mfuko Maalum kwa ajili ya Pamba na mimi hilo nitaliunga mkono mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nafikiri kuna haja sasa ya kuangalia…
*(Hapa king'ora ya kuashiria hali ya hatari kililia)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *direction* yako tufanyeje au niendelee?

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja pia kuangalia sana jambo hili la mbegu bora. Waziri amesema kwamba wakulima watapata tani 10,000 za mbegu bora, hiyo mbegu bora inatoka wapi kwa sababu sasa hivi mbegu ile tunayoipanda tunapopeleka *ginnery* ndio mbegu ile ile tunayorudishiwa. Kuna wakati mmoja nilifikiri kulikuwa na watu ambao walikuwa wanataka kuwekeza katika kulima pamba ya mbegu tu kama vile tunapolima mahindi kwa ajili ya mbegu, kama utaratibu huu upo, ninashauri upewe msukumo unaowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika njia ya kupunguza gharama kwa wakulima wa pamba, lifikiriwe kama lililokuwa linafanyika kwa upande wa tumbaku, *contract farming*. Watu waambie kwamba nilimie pamba na mwisho wa mwaka huu nitakupa bei hii. Sasa hivi ametuahidi kuwa mwaka huu tungepata zaidi na mwaka jana tulipata tani 267,000 imeshuka imefika tani 260,000, ameorodhesha sababu nzuri sana lakini tatizo kubwa ni wasiwasi wa bei. Wakulima wakiweza kuambiwa kwamba mtalima na tutawapa kiasi hiki, ataikimbia pamba mimi ninavyojua. Sasa hivi watu wanaanza kulima choroko kwa sababu wanategemea soko la choroko la India lakini wale ndugu zangu wa India wakishiba choroko inateremka. Ilikuwa imeanza kwa bei ya shilingi 1,500 jana hapa nimeambiwa imeshateremka mpaka Sh.600/=. Haiwezekani kutegemea choroko, sisi watu ambao tunategemea pamba tuko zaidi ya milioni 10 tukiitupa pamba tutakuwa tumekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kupendekeza, kwa muda mrefu mno tumeitazama pamba na bei yake kwa kuangalia tu nyuzi ambayo Wazungu na masoko ya nje yanatuchukulia, nadhani mtazamo huu lazima ugeuke kwa sababu asilimia 66 ya pamba ni mbegu ya mafuta. Kwa hiyo, hata ukokotoaji wa bei isiwe kwa kutegemea asilimia 33 ambapo ni nyuzi peke yake, hii ni mbegu ya mafuta, ni mbegu ya mashudu na ni mbegu kwa ajili ya kulisha wanyama. Kwa hiyo, tukiwa na mtazamo wa namna hiyo, jambo hili litaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la usafi, mimi kama Mbunge napigania hapa bei iwe nzuri, mazingira yawe mazuri kwa wakulima wa pamba, nawaomba kabisa wakulima wa pamba kutokuwa na usafi wa pamba ni kuharibu bei ya pamba. Kwa hiyo, tujitahidi, tupeleke pamba iliyo safi na Serikali itusaidie kwa kutumia Bodi ya Pamba na kuhakikisha kwamba mizani yetu sio mizani ambayo inageuka kufuatana na siku, leo inapigwa inasoma hivi, kesho inapigwa inasoma hivi, tunapofanya hivyo tunawafanya wakulima wenyewe watafute njia za kuweza kuwapunja wale ambao wananunua. Kwa

hiyo, Bodi ya Pamba iamke, huu ndio wakati wa kuweza kusaidia wakulima. Hayo ya pamba yamekwisha na Mheshimiwa Waziri na yeye anatoka kwenye pamba, naomba awe mshabiki wangu ili tuhakikishe kwamba wakulima wa pamba wananufaika katika suala hili la Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza sio semina, Kilimo Kwanza sio maneno ya kutembea kila siku, Kilimo Kwanza ni mkulima apate bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mzee Cheyo hujaunga mkono hoja. (Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, mliposikia king'ora kinalia, ni kwa sababu baadhi ya Wasaidizi walipuliza dawa ya kurekebisha hali ya hewa huko *Speaker's Lounge*. Hii inaonyesha kwamba jengo letu vifaa vyake ni vya kisasa na vinafanya kazi. Kwa hiyo, hakuna wasiwasi wowote, ni jambo ambalo limesharekebishwa, tunaendelea na uchangiaji.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Niungane na wenzangu kwa kweli kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya na nawapongeza sana kwa kipindi chote ambacho tumekuwa nao katika Wizara hii. Lakini bila ya kuwasahau wananchi wa Jimbo la Mbarali, wapiga kura wangu, kwa kuweza kushirikiana nami ndani ya miaka mitano na hiki ni kipindi cha pili kwa maana kwa miaka 10 katika kuendeleza Jimbo la Mbarali na katika kuboresha kilimo. Hii Awamu ya Nne, tumeanza vizuri kwa Kilimo Kwanza, kwa hiyo, nawashukuru sana na ninaamini Awamu hii tena tutakuwa pamoja ili tuweze kuendeleza kilimo na tulete maendeleo katika Jimbo letu la Mbarali. Lakini napongeza wafanyakazi wote wa Halmashauri kwa sababu wamekuwa nami bega kwa bega wakiongozwa na Mkurugenzi wangu Ndugu Kagomba kwa kushirikiana na wananchi wa Mbarali katika kila jitihada za kuboresha kilimo ili waondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, mimi niipongeze sana Serikali kwa jambo walilofanya katika Wilaya ya Mbarali, nimpongeze na Waziri Mkuu kwa sababu aliamua kwa moyo wa dhati kutembelea Wilaya ya Mbarali maeneo yote yenye kilimo muhimu na akaweza kutoa changamoto sana na wananchi wamefarijika sana, namshukuru sana kwa ziara yake. Lakini kuja kwake kumeleta mambo mazuri sana. Mimi nilikuwa naungana kidogo na Mheshimiwa Anna Lupembe hapa, kuna mambo mazuri sana ambayo Awamu ya Nne imefanya, kwa mfano, kwenye pembejeo za kilimo. Kwa kweli Halmashauri nyingi, kama zilikuwa zinafahamu, inawezekana kati yetu sisi Wabunge wako hapa ambao hawajui nini maana ya kutoa *Power Tiller* za ruzuku kwenye kila Halmashauri. Maana yake mkulima au kikundi kichangie asilimia 20, asilimia 80 ifadhiliwe na Serikali, ni jambo muhimu sana, lakini nani amelifahamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala hili kidogo limekuwa ni kitendawili. Mambo mazuri kama haya, Waziri Mkuu amekuwa akiita labda Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, anakaa nao, anawaeleza, lakini wale wenzetu ni watendaji sisi wanasiasa tukiambiwa jambo kama hilo linakuwa ni zuri sana kwenda kulitangaza katika maeneo yetu ya uwakilishi. Cha msingi na wananchi wapewe elimu wajue kwamba Serikali imeandaa kitu gani kwa sababu ile ya vocha imewagusa moja kwa moja wananchi wote na wameipokea kwa dhati pale ambapo Watendaji wamefanya kwa nia njema kabisa, wananchi wameshukuru na wamepongeza. Lakini pale ambapo ujanja ujanja umetumika, imekuwa ni tatizo kubwa sana kwa sababu vocha hazienda kwa walengwa, watu wamechukua vitabu wameuza, wamechukua fedha zao, ina maana mlengwa hakuweza kupata, jambo hili inatakiwa lidhibitiwe katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie tu wenzangu kwamba sisi kama Halmashauri yetu ya Mbarali, tulichukua hilo zoezi la kuweza kufanya ukaguzi na Madiwani kwenye kila Kata na tukagundua udanganyifu huo upo na mkiudhibiti, hakika mtakuta kuna manufaa makubwa sana ya vocha. Lakini vinginevyo ni watu wachache sana wataweza kunufaika na zile vocha kwa sababu zina upungufu fulani, wakisaini watu wawili tu, mtu anakwenda benki anachukua fedha za kitabu kizima, sasa hiyo haifiki kwa wale walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na moja la kuchangia, nilikuwa namtania hapa Mheshimiwa Wasira kuhusu mashamba. Kumekuwa na malalamiko sana na juzi limezungumzwa na wenzetu wa Upinzani kuhusu mashamba yaliyouzwa. Mimi niko kwenye Kamati ya Mashirika ya Umma angalau tumefanya ziara kwenye mashamba ya Kilimanjaro na Mbeya. Tatizo lipo kwenye mipaka, yale makubaliano ya mauzo na eneo ambalo lilitakiwa liuzwe. Sasa naomba katika bajeti hii na Mheshimiwa Wasira kabla hajamaliza nafasi hii, kwa makusudi kabisa, kwa mfano wa pekee kabisa, aje Mbarali hasa shamba lile la Kapunga, aangalie ili tushirikiane kujua hivi kilichouzwa ni kitu gani? Zimeuzwa hekta zile 5,000 ulizotangaza au limeuzwa eneo lote hata lile ambalo halijaendelezwa? Huo ni mfano ambao naufahamu, lakini mifano ya maeneo mengine hakuna mipaka. Najua *PSRC* walikuwa ni Wakala, ninyi mliamua kuuza kama Wizara ya Kilimo, kama wenye dhamana lakini hamkuweka mipaka kwamba liuzwe kufikia wapi? Tumekuwa tukijadiliana hapa na pale, mimi ninachoomba, utume timu yako kwa sababu *CHC* tulishaongea nao wakawa tayari, lakini ni vizuri tukawa na mwenyewe muuzaji ili akaone hali halisi, kijiji kilichosajiliwa hakiwezekani kikauzwa pamoja na shamba, sio rahisi wananchi wakauzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilombero liko tatizo kama hilo, nako tumetembelea. Lakini ni vizuri kungekuwa kumeainishwa vizuri na tukajua, je, huyu mtu aliuziwa kitu gani, mipaka yake ni nini na muda wake kwanza wa kuliendeleza ukoje? Lakini swali lingine lilikuwa ni moja, hivi tulikuwa tunauza mashamba ili yafanywe nini? Lengo la Serikali lilikuwa ni nini? Hayo malengo yamefikiwa na je, walipewa muda gani wa kujitathmini wenyewe ili Serikali ijue kwamba huu muda uliopewa wa miaka mitano ulitakiwa ufikie kiwango fulani cha uzalishaj, kama hujafikisha basi yarudi kwa wenyewe

waweze kutumia au tutangaze tuuze kwa mtu mwingine mwenye uwezo zaidi, baadaye anahodhi ardhi, hafanyi chochote, anatumia vifaa vilivyoko pale, vikishazeeka anasema nimeshindwa. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine mashamba yameuzwa hayana hati na hizo hati zifuatiliwe zaidi maana inawezekana ikawa ni kigezo kimojawapo kwamba nimeuziwa lakini siwezi kuendeleza kwa sababu sijapata hati ya kumiliki hicho ambacho nimeuziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwa upande wa Bodi ya Mazao. Bodi za Mazao baada ya kuwafanya kwamba wasilipe zile ruzuku, kwa kweli imekuwa ni tatizo, haziwezi kujiendesha na nina wasiwasi na hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko, itapata matatizo hayo hayo kwa sababu ile ruzuku inayotoka Serikalini haiwawezeshi kusimamia zile kazi ambazo wamepaswa kusimamia. Kwa hiyo, ninaomba sana nalo hilo lisimamiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mashamba ambayo tayari bado yanasimamiwa na Serikali na ninaamini kabisa Kilimo Kwanza ni muhimu na ninaguswa sana kwenye mashamba ambayo bado hayajabinafsishwa na bado yanaendelezwa chini ya miradi ambayo miundombinu yake haijaendelezwa na bado inakufa. Kuna shamba moja kubwa sana la umwagiliaji ambalo awamu ya pili litaendelezwa tena kwa hekta 3,600, shamba la Madibira. Alikuja Mheshimiwa Rais pale ameliona na akasema awamu ya pili lazima liendelezwe. Lakini ukiangalia pale lilipo tayari limeshachakaa na ninaamini ikipita miaka miwili mtasema wananchi wameshindwa kulisimamia kwa hiyo liuzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu, kuna wafanyakazi kwa kweli wako pale wa Wizara ya Kilimo ambao wanasimamia mradi huo lakini hawana chochote, bajeti inayopelekwa ni kidogo sana. Kuna wakati hapa nilimwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri hapa swali la nyongeza, akanijibu kwamba ule mradi unaendelezwa na unaendelea vizuri sana. Nashauri kwamba ni vizuri tukaenda kwenye *site*, ukaona kitu kwa macho halafu ukajua ni kitu gani cha kufanya. Mimi naomba niwashauri kwamba kwa kweli hili shamba ni muhimu sana, limeleta mabadiliko sana kwa wananchi wa Mbarali na nafikiri kwa Wilaya nzima na Tanzania nzima, basi ni vizuri mkalione kwa sababu miundombinu inakufa na vinu vile ambavyo vimegharimu karibu shilingi bilioni 42 vitakufa halafu baadaye tutasema tunalibinafsisha. Sasa naomba muende mkalione, muone ni jinsi gani mnaweza mkaokoa shamba lile hasa kwa upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni zao la biashara. Kwetu Mpunga tunaita zao la biashara. Mwaka uliopita, Serikali ilileta mpango angalau kila Wilaya ianishe zao moja la biashara na zao la chakula ambalo lingetusaidia sana kwa kipindi hiki cha Kilimo Kwanza. Niseme kwa mfano Mbarali Mpunga sio zao la chakula kwetu lile ni zao la biashara na tumepata soko kwa kutumia stakabadhi ya mazao ghalani. Wakati namuuliza Waziri Mkuu hapa nilikuwa nasisitiza hilo kwamba mmefungia mazao ya chakula yasiuzwe maana yake mmetufanya sisi Mbarali tusipate mzunguko wa chochote kile kwa

sababu hatutauza Mpunga kama zao la chakula. Kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe, mnapoangalia soko la nje mturuhusu Mbarali tuendelee kuuza mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Estherina Kilasi, kama nilivyosema atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Sigonda. Lakini kabla sijamwita, kwa uendeshaji bora wa shughuli za hapa Mezani, wameshachangia Wabunge saba kutoka Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala na Mbunge mmoja toka Upinzani. Kwa hiyo, ili kuweka uwiano kidogo baada ya Mheshimiwa Dkt. Guido Sigonda, atafuata mchangiaji mmoja tu basi, katika orodha yangu wanafuata karibu Wabunge wa CCM wote, nitamnyanyua Mheshimiwa Said Arfi atuhitimishe kwa asubuhi ya leo.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nami niungane na wenzangu kuchangia hoja ya leo hii. Lakini kabla ya kuanza kuzungumza, wenzangu ambao wametangulia wameipongeza Serikali kwa kugawanya baadhi ya maeneo kwenye Majimbo yao na kwenye Wilaya zao. Nasikitika kwa kweli nina simanzi na sijafurahia kwa sababu wapiga kura wangu wa Jimbo la Songwe walikuwa na mategemeo makubwa sana kutokana na ahadi ambazo zimetolewa kuhusu kugawanya eneo lile la Jimbo la Songwe. Vigezo vipo, bahati mbaya haya matokeo yaliyotokea hivi karibuni, hakuna kilichofanyika kwa upande huo. Ninachotaka kusema tu ni kwamba ndugu zangu wananchi, wapiga kura wa Jimbo la Songwe, Serikali ni sikivu, inajua ina mipango, kwa hiyo nawaombeni muwe na amani, najua kabisa kutokana na usikivu wa Serikali ya CCM, jambo hilo litafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *observation* hiyo, nataka kusema tu kwamba kwa kweli hotuba ya Mheshimiwa Wasira zaidi imetugusa sisi kutokana na jinsi Wizara hii ilivyoshughulikia Jimbo la Songwe. Jimbo la Songwe lilikuwa nyuma sana kabla ya mwaka 2005 lakini ni vizuri nikakumbushia tu ili kusudi na wenzangu wa huko Jimbo la Songwe wasifikirie kwamba basi kule kukataliwa au kunyamaza kwa Serikali, ndio kwamba hatukupata chochote. Wizara hii mwaka 1995 zao la pamba lilisitishwa kulimwa kutokana na sababu za kitaalamu. Wananchi walisikitika sana nao wakaona kwamba sasa Serikali inatupeleka wapi lakini ulikuja uhamasishaji wa Serikali, ikatushauri tutafute zao mbadala. Tumeukubali huo msisitizo na bahati nzuri katika miaka miwili iliyopita zao mbadala tulilipata ambalo ni ufuta tatizo linalokuja ni kwamba hilo zao linalimwa kwa wingi hatuna soko. Sisi tulidhani kwamba Serikali baada ya kutuhamasisha vile basi ingeanza hata kufikiria namna tutakavyoweza kupata soko la kuuzia zao letu. Wako walanguzi ambao wanakuja kila wakati, kwa kweli inasikitisha. Tunaomba Wizara pamoja na kufanikiwa kulima zao hilo, tupatiwe soko la kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Songwe katika Wilaya ya Chunya kulikuwa na tatizo la usambazaji wa mazao tuliyokuwa tunalima kutokana na kukosa barabara. Programu ambayo ilibuniwa na Serikali hivi sasa katika maeneo yote ambayo tunalima, kuna barabara ambazo ni za changarawe ambazo ni kama lami. Hii ndio kazi Wizara hii imetufanyia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho lazima niwapongeze hawa viongozi wa Wizara, wakulima walikuwa wakiomba walipwe deni lao la pamba toka mwaka 1995, baada ya kuuza walikuwa hawajapata malipo. Hivi sasa ninavyosema fedha zimeshatolewa na wakulima hawa wameshaanza kupewa pesa zao. Naishukuru sana Serikali kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, niende sasa katika suala la Kilimo Kwanza ambayo ndiyo Sera yetu. Bonde la Songwe linafaa kwa kilimo cha kila aina, iwe masika hata kiangazi, ninaomba Wizara ilifikirie. Mheshimiwa Waziri alifika kule na alishindwa kumaliza lile eneo, picha ambayo amepiga pale alikuwa anakinga mkono usoni ili kusudi angalau aweze kuona mbele. Ni bonde ambalo ni zuri sana, ninaomba Wizara iliangalie bonde hili zaidi katika kusaidia wananchi wale ambao walikuwa hawajazoea kupata maendeleo kutokana na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyeiti, suala lingine ni uwezeshwaji wa hawa wakulima. Kwa sababu ni Kilimo Kwanza na Jimbo letu lina ardhi inayofaa kwa kilimo wakulima wawezeshwe. Sasa hivi hii sera ya kuleta matrekta, nimeona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna matrekta mengi zaidi ya 2000 yameingizwa nchini lakini nasema bahati mbaya kwangu mimi hakuna trekta hata moja ambalo limeletwa kwa ajili ya kukopeshwa, ni ka-trekta kako kamoja mtu alikokanunua kwa fedha yake. Ninaomba Mheshimiwa Waziri alifikirie suala hilo la kutuwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yapo mambo mengi ambayo yamezungumzwa, la mwisho ni taarifa tu ya masikitiko kwamba Jimboni kwangu sasa hivi kuna kipindupindu, mpaka hivi sasa ninavyosema, watu wanne wamekufa. Ninaomba ile Wizara inayohusika na tatizo hili, dawa na maji ndiyo tatizo kubwa. Kwa hiyo, ninaomba Wizara inayohusika ijaribu kuangalia kwamba huko Chunya tayari kipindupindu kimeingia, ni kiangazi lakini ni ajabu wamepata kipindupindu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nikushukuru sana kwa kubasara yako uliyoitumia na kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja tuliyokuwanayo hapa mbele yetu. Napenda nianze kwa kusema kwamba kucheza na mbegu ni njaa. Tuna tatizo kubwa sana katika nchi yetu katika eneo hili la mbegu bora na watu wachache ambao wana tamaa na kujilimbikizia pesa, wanawahadaa wananchi na wanauza mbegu zisizokuwa na ubora na kwa bahati mbaya sana Wizara inayohusika, haina mkakati madhubuti wa kusimamia na kuangalia viwango na ubora wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata kuambiwa kwamba kuna watu wanachukua mifuko ya *SEEDCO*, wanachagua mbegu zilizokuwa bora katika mbegu za kawaida zilizokuwa katika maghala yao, wanatia rangi ya kijani, rangi ya mkeka, wanarudi wanafunga mifuko hiyo na wanaiuza wakiamini kwamba wakulima wetu wataamini ni mbegu bora. Lakini hakuna hata mtu yeyote ambaye anadhibiti au anasimamia suala hili.

Suala hili ni hatari kubwa katika Taifa letu na hasa katika dhana hii ambayo tunaijenga ya Kilimo Kwanza kama hatutaweza kusimamia ubora wa mbegu ambazo wanauziwa wakulima wetu. Ndiyo maana mara nyingi tija haionekani kwa sababu mbegu hazina ubora unaotakiwa, hilo lilikuwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna urasimu mkubwa sana na uhaba wa rasilimali watu katika Wizara ya Kilimo na hili nalo litatukwamisha sana kufikia malengo ambayo tunakusudia ya kuweza kujitosheleza katika chakula na ili hiyo dhana ya Kilimo Kwanza iweze kukamilika. Nasema hivyo kwa sababu inachukua muda mrefu sana miradi ya kuweza kuchochea kilimo kikue na hasa kilimo cha umwagiliaji kutekelezwa. Ninafahamu yako mabonde mazuri sana kule Mpanda ambako tayari maandiko ya awali yameshawasilishwa Wizarani lakini mpaka sasa hivi utekelezaji wake karibu miaka minne haujaweza kuchukuliwa hatua yoyote. Hili linasababishwa na uhaba wa wataalam na hasa eneo la wataalam wa umwagiliaji. Hakuna Ma-*surveyors* wa kutosha, hakuna wataalam katika eneo hilo la umwagiliaji, kwa hiyo, ni vizuri sasa Serikali ikawekeza katika eneo la rasilimali watu ili angalau miradi iweze kutekelezwa katika wakati muafaka ili iweze kusaidia katika kuboresha na kubadilisha hali ya mahitaji ya Taifa hili ambapo sasa hivi ni Taifa ambalo linaenda kuomba chakula wakati linaweza kujitosheleza lenyewe. Ni vizuri Serikali ikaangalia eneo hilo kwa kuongeza rasilimali watu kwa maana ya wataalam na pengine uhaba huo wa wataalam ndiyo matokeo yake kunakuwa na urasimu mkubwa na ucheleweshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limekuwa na malalamiko makubwa sana ni mbejeo hasa mbolea ya ruzuku. Mbolea ya ruzuku imeleta matatizo makubwa sana, kumekuwa na ubadhirifu mkubwa sana na hata katika Mkoa wa Rukwa umetokea. Lakini ni vizuri kila tunapofanya makosa tukatafuta njia nzuri na sahihi zaidi ya kuweza kupunguza hii mianya ya ubadhirifu na wizi na kujitajirisha kwa watu wachache. Nilikuwa naangalia kwamba kuna haja gani ya kuwa na Mawakala wa Pembejeo na hususan pembejeo za vocha. Ni kwa nini Serikali inashindwa kutambua wakulima wake? Kama Serikali ingekuwa inajua wakulima wake basi ni rahisi kuwafikishia mahitaji yao kupitia Serikali zao za Vijiji ambazo zimetapakaa katika nchi nzima badala ya kuwatumia Mawakala. Nipende kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze sana aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Kanali Mzurikwao kwa kazi nzuri aliyoifanya kusimamia ugawaji wa pembejeo za vocha katika Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wake kwa sababu na mimi ni mjumbe katika Kamati ya Pembejeo aliamuru kwamba kabla ya kugawa ni lazima tuwe na Daftari la Wakulima. Kwa kuwa na Daftari la Wakulima, watatambulika na maeneo wanayolimia yatajulikana basi ubadhirifu na upotevu wa mbolea hautakuwepo katika nchi hii, itakuwa ni historia. Lakini kwa sababu hatuna utaratibu mzuri na madhubuti wa kuwajua wakulima wetu, ndiyo maana katika ubadhirifu, wameandikwa watu ambao wameshakufa na majina yao yako katika misalaba kwenye makaburi mbalimbali au watoto wadogo walioko migongoni wamepewa mbolea kwa kisingizio kwamba hakuna mtu anayefuatilia wala anayejali. Lakini ipo haja ya makusudi kabisa sasa Serikali ikajipanga vizuri kwa kuwatumia Maafisa wao wa Serikali wachache waliosambaa katika

kila eneo kuhakikisha kwamba wanajua wakulima wangapi waliopo katika maeneo yao na mahitaji yao, ni kiasi gani ili mbolea ipelekwe kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pamoja na matumizi mazuri na ongezeko kubwa la mbolea lakini bado ipo jitihada makusudi inatakiwa ifanywe ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na kuangalia ubora wa ardhi *(soil test).* Hii haifanyiki kabisa, ni watu tu wanajiwekea mbolea kwa sababu mbolea ya ruzuku imeletwa na mbolea ni rahisi, wanatumia mbolea bila kujua kwamba ardhi hiyo inahitaji mbolea hiyo au mbolea ya aina nyingine na kwa sababu tuna uhaba sana wa Maafisa Ugani katika maeneo yetu kwa hiyo wakulima wetu hawapati elimu ya kutosheleza juu ya matumizi sahihi ya mbolea na mbolea nyingine hazifai kabisa katika maeneo mengi ikiwemo mbolea ya Minjingu. Mbolea hii imeleta matatizo, wakulima wengi wamepiga kelele lakini ni kwa sababu hakuna *study* zilizofanywa juu ya ubora wa mbolea yenyewe na mahitaji ya ardhi ambako mbolea inakwenda kutumika. Kwa hiyo, eneo hili nafikiri ipo haja ya makusudi Wizara ikaangalia wanajipanga namna gani katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, ni kwamba kumekuwa na mpango wa makusudi wa Serikali wa kuhamasisha wakulima wakubwa wakubwa kuja kuwekeza katika nchi yetu. Inawezekana kwamba ni jambo jema lakini mimi niseme kwamba sikubaliani na hilo. Serikali hii ilikuwa iangalie ni namna gani sasa inaweza kuwasaidia wananchi wake kwa maana ya wakulima hao hao. *Study* nyingi zimefanyika pamoja na kwamba asilimia 80 ya Watanzania wanaishi Vijijini lakini wanaofanya kazi ya kilimo, *active farmers* hawafiki asilimia 34 na asilimia 56 ya watu wanaokaa Vijijini si wakulima, wanafanya kazi zingine tu, biashara ndogo ndogo na kadhalika. Sasa ni namna gani Serikali inaweza kuwasaidia watu hawa wote wakarudi kuja kufanya kilimo badala ya kuwaleta hao wageni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimalizie kwa kumtaka Mheshimiwa Waziri aniambie, nimeona ameianisha makampuni kadhaa ambayo yatakuja kuwekeza katika kilimo, juu ya hatma ambayo imekuwa ikiandikwaandikwa sana katika vyombo vya habari, juu ya makazi ya Katumba na Mishamo ambayo inasemekana Wizara ya Kilimo tayari imepata wawekezaji ambao watakuja kuwekeza katika kilimo kwenye maeneo hayo. Tunataka tupate uhakika watu wa Mpanda juu ya maeneo ambayo yalikuwa makazi ya Katumba na Mishamo kama ni kweli Wizara ya Kilimo imeshaingia mkataba na Wamarekani, sijui Waingereza ambao wanataka kuja kuwekeza katika kilimo kule Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Arfi. Waheshimiwa Wabunge mpaka sasa wachangiaji tisa wamechangia na uchangiaji wetu utaendelea jioni kama alivyokwishatoa mwongozo Mheshimiwa Naibu Spika ambapo jioni tutaanza na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na wengine ninahakika watapata nafasi katika

ule muda wa saa kumi na moja kamili hadi saa kumi na mbili. Kwa hiyo niliowataja ni vizuri wakawahi kufika.

Kwa kuwa tutaendelea jioni na hoja hii hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na muda uliobaki hautoshi kumpa mchangiaji yeyote yule, kwa hiyo, nachukua fursa hii kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili leo jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Jioni hii tutaanza na Mheshimiwa Gaudence Kayombo akifuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya kuweza kufika siku ya leo. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Serikali nzima kwa kuongeza maeneo ya Utawala, na kule Mbinga tumepata Wilaya ya Nyasa, lakini mimi pia nimepata Tarafa tatu, Kata 10 na hivyo kulifanya Jimbo la Mbinga Mashariki kuwa na Tarafa sita, Kata 34 na Vijiji zaidi ya 145.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wataalam katika Wizara hiyo na Watumishi wote katika Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayoifanya, haina ubishi. Ninawapongeza sana. Lakini pia pongezi zangu ningependa ziende kule Mbinga kwa Mwenyekiti wa Halmashauri na Madiwani kwa kuamua kugawa bure miche bora ya kahawa milioni moja katika msimu wa mwaka huu na miche 400,000 ya kahawa jambo ambalo litaongeza sana kilimo cha kahawa na kilimo cha korosho katika Wilaya yetu ya Mbinga. Ningependa kipekee kabisa nimshukuru Waziri Mkuu kwanza kwa kufikiria kuwalipa Chama cha Msingi cha Utiri fedha walizokuwa wanazidai kupitia Chama cha Ushirika cha *MBICU* kilichofilisiwa lakini pia kutoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kusaidia ununuzi wa madawa kupambana na vidung’ata katika zao la Kahawa kule Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia ningependa kuyashukuru Mashirika ya *TACRI* kwa kazi nzuri wanayoifanya Proffesor Terry na kijana wake Swai. Mbinga wanafanya kazi nzuri sana ya utafiti wa zao la kahawa. Lakini pia *TAHA* Dada Jackline na wenzake walifika Mbinga bado tunawatarajia tena wafike kufanya yale ambayo waliyasema. Nawashukuru pia *SGR* kufungua kituo cha ununuzi wa mahindi pale Kigonsera. Matarajio yangu ni kwamba mwaka huu pia wataendelea kule Mpepai ambako pia kuna nafaka nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia mambo hasa yanayohusu Mbinga. Pamoja na kwamba Wizara inafanya kazi nzuri kama nilivyosema na hivyo mimi nalazimika kwa kweli kuunga hoja hii mkono kwa utendaji wao mzuri wa kazi, lakini ningependa watoe haya madoa kidogo yanayowatia kasoro. Kwanza ni ruzuku ya

mbolea. Nimesoma katika kitabu cha Waziri ukurasa wa 37 unaelezea mazao ya pamba na korosho yanapata ruzuku ya madawa, lakini kule Mbinga Kahawa ni zao la biashara, lakini halipati ruzuku ya madawa na wale wakulima kila wakati wanalalamikia jambo hilo nilikuwa naomba Wizara ichukue jambo hili iliangalie na ilifanyie kazi ili na hawa wakulima wa kahawa wafaidike kama wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku iko kwenye miche, lakini kule Mbinga miche ile inatolewa bure na Halmashauri yao. Kwa hiyo, ili waweze kupata *share* kubwa ya keki katika Serikali Kuu, tungependa haya madawa ya kahawa na yenyewe pia yatolewe kwa ruzuku. Wako pia wakulima wa mahindi hawana uwezo wa kifedha. Katika hotuba ya Waziri inaonyesha wazi kabisa kuwa kuna nchi za kiafrika ambazo zitakuwa na upungufu wa chakula Tanzania ingeweza kufanya biashara na watu hawa. Kama sisi tutalima zaidi na njia mojawapo ya kulima zaidi ni kuwawezesha hawa wakulima ambao hawana uwezo wa kifedha wakaingia mkataba na Serikali ili waweze kulima na kuuzia Serikali na Serikali ikauzia hizi nchi, na hivyo, tutakuwa tumewezesha hawa wananchi ambao mara nyingi wanabaki nyuma kwa kisingizio kwamba hawana uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni ulipaji wa madeni ya wakulima ambao wanadai kupitia vyama vyao vya ushirika ambavyo vimekufa, vimefilisiwa au vimelala tu usingizi. Hapa napenda kuishukuru sana Wizara ya Kilimo na Serikali nzima kwasababu mwaka jana waliweza kulipa shilingi milioni 106 katika chama cha *MBIFACU*. Lakini kwa bahati mbaya na mimi sitaki kuingia katika sababu zilizofanya chama kilichokuwepo kabla ya *MBIFACU* na wakulima wake ambao walikopwa shilingi milioni 400 hawakulipwa. Mimi sitaki kuingia katika sababu, lakini ninamwomba Waziri kwamba hizi fedha wangelipwa hawa wakulima ili waweze kuona kuwa Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi ni nzuri hasa ukizingatia kwamba kipindi hiki tunachoelekea ni kipindi cha Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni ufufuaji wa Ushirika. Tulikuwa na *MBICU* ambayo imefilisiwa na mufilisi, pale ni Serikali lakini kazi anayofanya yeye ni ya polepole sana.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Samahani Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 68 Kanuni ya 140 inazungumza juu ya ukaaji ndani ya Bunge, kwa maelezo hapa ya kifungu cha 140(k).

**MWENYEKITI:** Hebu twende taratibu unasemaje?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 140(k)

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 140? Ngoja nifike huko. Ndiyo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinaelezea juu ya ukaaji Bungeni, kinasema kwamba kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni atakaa kiti cha kwanza akifuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri upande wa kulia. Inasikitisha sehemu hii iko wazi, ina maana hakuna msimamizi wa shughuli za Serikali katika kikao cha leo? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kutukumbusha. Mheshimiwa Hussein, tafadhali. Limerekebika hilo. Mheshimiwa Kayombo endelea na dakika zako zimezingatiwa. Asante sana Mheshimiwa kwa kutukumbusha.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikwa katika *point* ya tatu ambayo ilihusu ufufuaji wa Ushirika. Tulikuwa na Chama cha Ushirika cha Msingi pale kilikuwa kimelala usingizi, yako matatizo ya kiufundi, lakini tumepiga hatua kwa kiwango kikubwa tukishirikiana na Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Ningependa sasa Mheshimiwa Waziri atusaidie kutupelekea mtaalamu kule kama *Cheif Executive Officer* ili aanze kazi, kwasababu bodi imeshachaguliwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ni udhibiti wa visumbufu vya wadudu. Kule tumeingiliwa na vidudu vinaitwa vidung’ata katika kahawa. Naendelea kuomba msaada wa Wizara ili waendelee kutusaidia zaidi kuhakikisha tunazalisha kahawa nyingi zaidi.

*Point* nyingine ni kuhusu Bodi ya kahawa. Bodi ya kahawa imepata Mwenyekiti mahiri sana na Mkurugenzi mahiri lakini inahitaji msaada mkubwa zaidi wa Serikali hasa kuliwezesha kwa upande wa fedha. Lakini pia ningependa waharakishe kuandikisha wakulima wale wa kahawa katika Wilaya ya Mbinga na Wilaya nyingine. Lakini pia niliuliza swali Bungeni hapa kuhusu kupeleka madaraka yao katika Mikoa ili waweze kuonekana na walisema kuwa watafungua kanda katika maeneo hayo, lakini kwa bahati mbaya ofisi ya Kanda imepelekwa Songea ambapo hawalimi kahawa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa ninapendekeza na ningeomba sana *TCB* kupitia Waziri wafikirie kuihamishia ile ofisi Mbinga na watashirikiana vizuri sana na *TACRI* ili kuweza kuinua zao la kahawa kuliko kuiweka pale walipoliweka maana hata makao makuu ya kahawa imewekwa katika eneo la kahawa. Lakini pia ningependa watusaidie sana Bodi hii ya kahawa katika kupeleka wataalamu na wakaguzi wa kahawa kama Sheria ya kahawa ya mwaka 2001 inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* nyingine ambayo nilitaka kuongelea hapa ni usindikaji wa bidhaa. Hili limetiliwa mkazo sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini sasa mimi ningependa Serikali yenyewe ionyeshe mfano katika kuhakikisha kwamba usindikaji unafanyika.

Napenda kuongelea hapa hasa mazao ya nafaka kama mahindi. Badala ya Serikali kununua mahindi, napendekeza ianze kununua unga tayari kwa kupeleka maeneo yale ambayo yana uhaba wa chakula. Wapelekewe unga badala ya kupelekewa mahindi na hii itasaidia kuleta *employment* katika haya maeneo na pia ujasiriamali katika haya maeneo

kuliko haya maeneo yazalishe mahindi na yapeleke mahindi yaende yakasagwe katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudie tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii na wafanyakazi wote katika Wizara ya kilimo ningependa tu wazingatie maombi yangu hayo, hasa la kulipa wakulima wa MBICU na hili la kukufufua MBIFACU kwa kutupelekea mtumishi mmoja ambaye angeweza kuanza kazi. Tunataka kununua kahawa katika msimu huu mapema kuanzia mwezi ujao, akitupelekea atakuwa ametusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na ninashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri asubuhi ya leo.

Awali ya yote, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake nzuri. Lakini jambo la pili, leo nimesimama pia ili kwa dhati ya moyo wangu kabisa niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Mbozi Mashariki kwa kuniamini mwaka 2005 na kunipa Ubunge na mimi kuwa mwakilishi wao miaka mitano hapa Bungeni. Ninawashukuru sana kwa imani yao waliyoionyesha. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda mwishoni, wenzangu wamekuwa wakitangaza nia ya kugombea Ubunge na mimi naomba niwaambie wana Mbozi Mashariki kwamba bado nina nguvu, nina afya njema na akili ya kuwawakilisha hapa Bungeni. Kwa hiyo, ninawaomba waendelee kunipa imani. Mheshimiwa Rais jana alipokuwa anachukua fomu alisema sasa tutakwenda kwa kasi zaidi, nguvu, zaidi na ari zaidi na mimi naomba niwahakikishie kuwa tutakwenda hivyo hivyo maana mwaka 2005/2010 tumetekeleza mengi na mimi nina hakika katika kipindi kinachofuata tutatekeleza zaidi kwa ari kubwa, nguvu kubwa na kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi kwa wananchi wangu wa Mbozi na kutaka waendelee kunipa imani katika uchaguzi unaokuja, naomba nichangie katika maeneo machache sana. Kwanza nilikwishaandika asubuhi, sikuwa ninajua kama ningefikiwa, lakini kwa kuwa nimepata nafasi maalum, naomba nichangie mambo mengine machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, leo naomba nilete rasmi salamu na pongezi za wana Mbozi kwa Serikali kuwapelekea mbolea ya *DAP* kwa ajili ya uzalishaji wa mahindi kwa maana ya vocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 msimu uliopita tulipewa mbolea ya minjingu ambayo kimsingi iliharibu mazao ya wananchi na hususan mahindi. Nilisimama mbele ya Bunge hili kwamba Wananchi wa Mbozi wanasema mbolea ile hawaitaki. Ninaishukuru sana Serikali, ilisikiliza ombi langu ikaamua kuwapelekea wana Mbozi mbolea ya *DAP*. Ninafurahi kuliarifu Bunge lako na Watanzania wanaonisikiliza mwaka

huu kwamba tumezalisha mahindi mengi haijawahi kutokea. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wajiandae kuyanunua yale mahindi kufungua masoko, lakini pia waruhusu Wananchi wa Mbozi waweze kuuza mahindi yao popote pale watakapopata soko ilimradi Sheria na taratibu zitakuwa zimefuatwa, maana mahindi ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbozi peke yake tunaweza tukavuna tani milioni moja na kitu jambo ambalo halijawahi kutokea hata siku moja. Kwa hiyo, ninaomba Wabunge tunaposimama hapa mbele na kuleta mambo ya wananchi Serikali ione kwamba tunazungumza yale ambayo tunatumwa na wananchi wetu na siyo mambo yetu wenyewe, ingawa yapo mambo ambayo tunawasilisha kama Wabunge na kwa uelewa wetu. Kwa hiyo, ninaishukuru sana Serikalikwa hilo. Lakini nisisitize sana soko la Tunduma ambalo ni la Kimataifa tunaloendelea kujenga linachukua muda mrefu, ninaomba Serikali ichukue hatua kuona kwamba linafunguliwa na linaanza kufanya kazi ili wananchi wa Mbozi waweze kuuza mahindi yao lakini pia mazao mengine mchanganyiko yaweze kupata soko zuri zaidi na wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ambalo ninataka nilizungumze hapa ni suala la mbolea. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la mbolea na ni ukweli kabisa kuwa bajeti ya kilimo inaongezeka na imeongezeka kwa asilimia 35, lakini pamoja na kuongezeka huko bado tunahitaji mbolea nyingi zaidi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikatambua bado tunahitaji mbolea nyingi zaidi. Msimu wa mwaka jana wananchi wa Mbozi Kaya 51,000 ndizo zilizopata vocha, mwaka 2009/2010 ni kaya 80,000 zilizopata vocha kati ya kaya 120,000 zilizopo Wilaya ya Mbozi. Hii ina maana kwamba kuna *gap* ya kaya karibu 40,000 ambazo zinakosa mbolea katika Wilaya ya Mbozi. Hili ni kundi kubwa sana lakini pia utaratibu unaotumika kwa ajili ya kugawa mbolea ya ruzuku unaleta ubaguzi kidogo kwa wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanafikiri kuwa Serikali inawabagua pamoja na kuwa kuna Kamati zinazoundwa na wananchi wenyewe, lakini unaanza kufikiria nani apate na nani akose. Mimi nadhani hili linatuletea ubaguzi. Hebu Serikali ijaribu kuangalia utaratibu mzuri zaidi, ikiwezekana, basi tubane matumizi maeneo mengine. Kama tunaamua kutoa mbolea ya vocha, basi tuhakikishe kuwa ni wananchi wengi zaidi wanapata kuliko utaratibu wa sasa ambapo wananchi wengi wanaachwa nje maana tunaanza kutafuta vigezo ya kwamba wewe hujachangia shughuli za maendeleo, wale wananyimwa. Mimi kwa kweli nadhani siyo jambo jema, linaleta ubaguzi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine linalohusiana na hilo, naomba kuwe na uaminifu kwenye zoezi zima la usimamiaji wa vocha zenyewe. Wenzangu wamezungumza kuwa ulitokea wizi mkubwa sana kwenye vocha na nyingi sana zilipotea. Kule Mbozi zaidi ya vocha 3000 zilipotea. Kwa hiyo, kama tulipata vocha 81,000 maana yake zilizowafikia wakulima ni 78,000. Vocha 3,000 ambazo zinagharimu zaidi ya shilingi milioni 100 zimepotea na hivyo kuwasababishia wananchi ambao walistahili wapate, kukosa. Kwa hiyo, naomba Serikali ichuke hatua za kuhakikisha kuwa wale wote ambao walihusika kwa njia moja ama nyingine, kama ni watumishi wa Serikali, kuhakikisha kwamba hawa wanatupisha ili tutafute watu wengine ambao tunafikiri ni waaminifu zaidi wanaoweza kusimamia mbolea hiyo kuwafikia wananchi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Waheshimiwa Madiwani wameachwa katika Kamati zile, hawapewi mafunzo kuhusu zoezi lenyewe la usimamizi wa vocha. Lakini pia hata Wenyeviti wa Serikali za Vijiji ambao ndiyo mbolea zinakwenda kwenye vijiji vyao hawahusishwi kwenye Kamati hizo wao wenyewe. Sasa unapokwenda kwenye mikutano, mbolea imepotea au vocha zimepotea, Mwenyekiti anasema mimi sijui utaratibu uliotumika, na ukimwuliza Diwani naye anasema hajui, lakini Mtendaji wa Kata ndiye anakuwa Mwenyekiti Msimamizi wa zoezi lile. Sasa inamuwia vigumu sana Mheshimiwa Diwani pamoja na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji katika kusimamia. Naomba Serikali irekebishe utaratibu wa zoezi zima ili kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wanafaidika kwa maana ya kuimarisha usimamizi wa mbolea hii ambayo tunakusudia kuwapelekea wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri pia kwamba tutumie mawakala waaminifu. Tuna *TFA (Tanganyika Farmers Association)*, imefanya kazi nzuri sana katika nchi hii katika kuhudumia wananchi. Ningeomba ipewe uzito mkubwa kabisa wa kupeleka mbolea kwa wananchi, maana hawa wanafanya kazi kwa uaminifu sana na tukiwatumia, wanaweza kuhakikisha mbolea inafika kwa wananchi kwa asilimia mia moja. Kama watakuwa na tatizo, labda ni la kibinadamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni suala la Benki ya Wananchi. Hili limezungumzwa sana, limetolewa maelezo sana, lakini kama kweli tuna nia ya kukuza kilimo katika nchi hii, ninashauri Serikali iangalie upya masharti yaliyo kwenye Benki ya Wakulima. Bado ninashawishika kusema kwamba wananchi walio wengi asilimia 80 ya Watanzania wanaolima kama hatujaangalia masharti haya, hiyo asilimia 80 inawezekana ni asilimia tano tu au asilimia kumi ya wananchi vijijini ambao ndiyo wakulima wengi wanaoweza kufaidika na Benki hii. Maana nina hakika wengi hawataweza kutimiza masharti yale ambayo yanatajwa na Benki ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sharti mojawapo ni lazima upite kwenye *SACCOS*, lazima upite kwenye *VICOBA*, lazima upite kwenye benki, kwa nini kama huyu mwananchi mwenyewe ametimiza masharti yake na ana hati zinazostahili kwa maana ya masharti ya kawaida, kwanini anapewa sharti lingine la kupitia kwenye vyombo vingine? Mimi ninadhani huu utakuwa ni urasimu ambao hautakuwa na maana yoyote na benki itaonekana haimsadii mwananchi kwasababu kuna watu ambao wameanza kukopa na kuanza kulalamikia masharti ambayo yamewekwa na benki hii. Kwa hiyo, kama tunataka kweli kuwasaidia wananchi, wakulima wa Tanzania, naomba masharti haya yaangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumze kwa kifupi sana kuhusu kahawa. Mazao mengine ya biasahara yanapewa ruzuku, ametoka kuzungumza Mheshimiwa Kayombo hapa Mbunge wa Mbinga, Mbozi, tunalima kahawa, wananchi hawapewi msaada wa ruzuku kwa ajili ya dawa za kahawa. Naomba na wenyewe wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa hii na ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kwamba tuko hapa kuzungumzia maendeleo ya nchi yetu. Kwa kipekee kabisa, naomba niwashukuru wale wanawake wa Kilimanjaro walionifikisha hapa Bungeni na niendelee kuwaambia kwamba niko pamoja nao na tutaendelea kujitahidi kuwazungumzia na wao waendelee kutushikilia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na *team* yao yote. Kazi walizofanya ni nyingi na kitabu hiki kinajieleza kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba naanzia na pale walipozungumza kuhamasisha wananchi au kujiunga na Vyama vya Ushirika. Hii iko kwenye ukurasa wa 63, tarakimu zinajionesha ni jinsi gani mwaka huu wa 2009/2010 wengi wamejiunga kwenye Vyama vya Ushirika na *SACCOS* nyingi sana zimefunguliwa. Hili ni jambo zuri na niseme tu kiu hii ni kubwa na kasi hiyo itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu iliyonifanya nichangie ni kwamba ni jinsi gani kwa mwamko huo wa wananchi kuhamasika kuingia kwenye Vyama vya Ushirika, Serikali imejiandaa kuwa na Maafisa Ushirika wa kutosha katika kuandikisha vyama hivyo na kuandikisha *SACCOS* hizo? Kule Kilimanjaro ofisi ya Ushirika haijatosheleza, wale waliopo Mkoani hawatoshi kutembelea wenzao wa Wilayani na walioko Wilayani pia ni wachache sana na hiyo imekuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita nilisimama hapa Bungeni na kuzungumza shida tuliyopata kwa kuandisha *SACCOS* za akina Mama, lakini hatukupata ufumbuzi. Ninaiomba Serikali ituambie: Je, ni Maofisa Ushirika wangapi hadi sasa wameandaliwa kumudu hii kasi ya wananchi waliohamasika kujiunga na ushirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hilo na kuelezea jinsi gani Wizara hii imejitahidi kuhamasisha wananchi. Naomba niende pale ukurasa wa 100 fungu la 24 linalozungumzia Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Mheshimiwa Rais ametoa idhini ianzishwe Tume hii na ukisoma mpaka mwisho tumeelezwa pia kazi za Tume hii, lakini ni lini sasa sheria italetwa hapa irekebishwe ili Tume hii iweze kuanzishwa? Kwa sababu hapa nimeona tumeelezwa na nilipoingia kwenye vitabu sikuona kama Tume hii imetengewa fungu. Sasa sijui hii Tume imeshaanza kufanya kazi au tumeelezwa tu utaratibu uliopo kwamba Tume hii itakuwepo na itafanya zile kazi kumi zilizoainishwa pale! Jambo hili ni zuri, lakini sina hakika basi kwa kuanzishwa Tume hii ni kuongeza mzigo kwa wananchi au ni kuwapunguzia wananchi mzigo, kwa sababu kama walikuwa wamehamasika bila Tume, Tume itafanya nini hasa? Ni kumudu kazi za Kilimo Kwanza au ni ushirika ule ule ninaoufahamu mimi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma ushirika huu ulikuwa mzuri. Nikiri tu kwamba wazazi wangu walikuwa wanachama wa *KCU*, tulikuwa na *primary societies* kwenye Wilaya zetu, lakini hadi leo nilivyosimama, ushirika ule wa *KCU* sasa unakuwa tena kama unafufuka. Tatizo, niseme wazi kwamba ni uongozi. Kazi zilizoorodheshwa hapa sikuona hata moja inayozungumzia kwamba watashughulikia uongozi kwa kina. Nijuavyo Ushirika, ni watu waliokusanyika wameamua kufanya shughuli moja kwa pamoja ili waweze kupata manufaa au wawe na maendeleo ambayo yanaweza yakamudu nia zao wakaweza kusonga mbele kwa pamoja na kugawana au hasara au wakagawana mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Tume hii itaingiaje kule kuweza kurekebisha uongozi mbovu ambao umeua ushirika wetu kutoka kwenye *primary societies*, *SACCOS* na hata kwenye hivyo vyama vikuu vya ushirika? Naomba ikiwezekana jambo hili liangaliwe kwa sababu kama hatutabadili au hatutaelekeza watu wetu wakati wanachagua viongozi, waache kuangalia ni mtoto wa nani au ndugu wa nani, wachague viongozi wale ambao ni wanaushirika wanaoweza kufanya kazi hii, vinginevyo, bado hii itakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia mambo ya uongozi katika ushirika, nirudi sasa katika zao ambalo limetupeleka wengine shule na kutuletea maendeleo makubwa katika maeneo yetu na zao hili ni kahawa. Kahawa ukiangalia ilivyokaa katika Mkoa wa Kilimanjaro katika yale mashamba ya watu binafsi, hakika hairidhishi kwa sababu kahawa hiyo iko katika hali mbaya. Nashukuru sana hatua za Serikali kuweza kutuletea miche mipya kutoka *TACRI*, lakini haitoshi tu kuletewa miche kama hakuna elimu ya kutosha. Nasisitiza kwamba elimu inatakiwa ili watu wajue kwamba ile kahawa inaweza ikawabadilisha hali zao endapo itatunzwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukizungumzia maofisa Ugani. Ni kweli, lakini siyo wote, niseme tu kwamba Maofisa Ugani wengi wao wanasoma nadharia katika vitabu, lakini wao wenyewe hawana mashamba. Mimi niliwahi kumtembelea Afisa Ugani mmoja, yeye anakaa nyumba ya kupanga, nikakuta hana shamba wala hajawahi kulima kahawa, lakini yeye ndiye anayetufundisha sisi kahawa. Pia hakuwa na hamu pia kufanya ile kazi. Maofisa Ugani wakati wanapangiwa katika maeneo, wapangiwe yale maeneo ambayo wao wenyewe wana *interest*, nadhani itasaidia zaidi kuendeleza zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitoe rai kwa Serikali. Sasa tukishakuwa na Tume hii, isaidie kuunda ushirika wa akina mama. Popote pale ambapo wanawake watakuwa wanajiunga, wasaidiwe ili wanawake hawa waweze kutoa changamoto kwa wanaume. Mengi ya mazao ambayo yapo kwenye Ushirika ni mazao ambayo ni ya wanaume au ni ya mfume dume. Kahawa ni zao la wanaume, tumbaku hali kadhalika, chai na mengineyo. Sasa ingekuwa tunaweza tukabadilishana, dakika hii kule Kilimanjaro wanawake wakasimamia Kahawa na wanaume wakasimamia ndizi, nadhani mngeweza mkaona hayo mabadiliko. Ninaomba wakati Serikali ina ari ya zaidi wafanye hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kazi aliyofanya Waziri Stephen Wasira, Naibu Waziri – Mheshimiwa David Mathayo na timu nzima ya Watendaji wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ikiongozwa na Katibu Mkuu – Ndugu Mohammed Muya ni nzuri inayostahili pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote hapa ni mashahidi wa bajeti ya sekta ya kilimo kukua kila baada ya mwaka. Tunakumbuka wote tulianza na shilingi bilioni mia mbili thelathini na tatu mwaka 2005/2006, na leo hii tunaongelea bajeti ya shilingi bilioni 904/= ambayo inakwenda kwenye asilimia nane ya bajeti ya nchi ambapo mwaka 2005/2006 ilikuwa kwenye asilimia 5.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko hilo, bado tuna changamoto ya kuiongeza bajeti ya sekta ya kilimo kufikia vile viwango vya *SADC* na Umoja wa Afrika vya asilimia angalau 10 ya bajeti ya nchi. Mimi naamini kabisa, kwa uongozi tulionao tutafikia huko. Kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri katutaarifu kuwa mbolea ya ruzuku itaongezeka vile vile kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kutoka tani tulizokuwanazo laki moja na nusu kwenda tani laki mbili. Hii ni taarifa njema sana kwa wakulima wote nchini, lakini hasa wakulima wa Kyela ambao walikosa mbolea hiyo msimu uliopita. Walikosa kwa sababu mbili kubwa: Kwanza, ilikuwa ni suala la udokozi katika vocha, suala ambalo Wabunge wenzangu wengi wameliongelea. Sitataka kuliongelea zaidi. Lakini pili, Wilaya ya Kyela ilipeleka mahitaji pungufu Wizarani kwa imani kwamba Wakulima wa Kyela hawapendi kutumia mbolea kwa sababu tu mbolea iliyokuwa inaletwa Kyela ilikuwa inakaa sana madukani, mwisho inapelekwa Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema watalaam wetu walikuwa hawajaijua saikolojia ya wakulima wa Kyela, kwa sababu wakulima wa Kyela walikuwa hawakimbii mbolea, walikuwa wanakimbia bei ambayo ilikuwa kubwa. Mbolea ya kupandia, Sh. 58,000/= wapi na wapi? Halafu Kyela ni jirani na Malawi, wanaona wakulima wenzao wa Malawi mbolea hiyo hiyo Sh. 10,000/=! Ilikuwa hailipi ndiyo maana walikuwa hawanunui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipoingia na mfumo wa vocha na Serikali yenyewe imetumbukiza nusu ya gharama, ilikuwa ni lazima wakulima wengi zaidi wajitokeze kutumia mbolea. Namhakikishia Waziri kuwa Kyela tunahitaji mbolea, tena nyingi. Safari hii atuletee mbolea ya kutosha, wakulima 21,000 tu kama ilivyokuwa, hebu atuletee angalau wapate wakulima 50,000. Na ninamhakikishia safari hii vile vile, hadokoi mtu vocha hata moja. Pengine Kyela ipate Mbunge mwingine, Mbunge ‘mdebwedo’ kutokana na hizi propaganda za mafisadi zinazoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kupendekeza msamaha wa kodi wa zana mbalimbali za kilimo hasa Kivuna Nafaka*(combine harvester).* Ninasema hili kwa sababu mimi natoka sehemu ambayo kuna kilimo cha mpunga.

Nimeona wakulima wa Kyela wanavyopata taabu wakati wa kuvuna. Ukilima zaidi ya ekari mbili tatu, inabidi uite watu wengi wa kuwalipa kwa ajili ya kuvuna. Humo humo kunakosekana umakini wakati wa kuvuna, kunarukwa mpunga, humo humo kuna wizi. Mwingine anavuna anafukia chini ya majani ili usiku aje achukue. Kwa hiyo, ni hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili namwambia Waziri kuwa nitawahamasisha wakulima kadhaa Kyela kununua *combine harvester* na asisikitike akituona tunamgongea haraka sana mlangoni kuja kumwomba msaada. Yeye umekuwa msaada mara kwa mara, wakulima wangu wengi Kyela wamepata matrekta ya mikopo kupitia ofisi yake. Tunashukuru sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri kwa kuhamasisha uanzishwaji na uimarishwaji wa *SACCOS*. Lakini wakati Waziri anahamasisha uimarishaji wa *SACCOS*, viongozi wengine wanachochea kifo cha haraka cha *SACCOS*. Mimi ninayo *SACCOS* Kyela yenye wanachama wakulima 245, inaitwa Kimbalu *SACCOS*, iko Kasumuru *Boarder*, Mji unaokua kwa haraka sana. *SACCOS* hii imekuwa inakwenda vizuri sana mpaka mwaka jana viongozi tulipoanza kuiingilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya uelewe jinsi ambavyo mara nyingine viongozi tunayashika shati maendeleo ya wananchi na Waziri aweze kusaidia kwa sababu yeye anasimamia sekta hii ili kuweza kulitatua tatizo hili. Nieleze kwa kifupi kwamba tarehe 11 Oktoba, 2008 Kyela ilipata heshima kubwa kutembelewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete. Alipewa kazi nyingi za kufanya, ya kwanza ilikuwa kuzindua Maktaba moja nzuri pengine ni ya viwango katika nchi hii ambayo imejengwa na NGO ya Mango *Tree* ya Kyela. Lakini vile vile, kuzindua Jengo la *SACCOS* hiyo ya Kimbalu, na hilo jengo lilimaliziwa haraka haraka kwa wananchi kuambiwa na viongozi wa Wilaya kwamba kopeni popote mmalizie hili jengo ili Rais aje alizindue, na tunawaahidi mtapata mkopo wa shilingi milioni ishirini kutoka *NMB.* Kinachonisikitisha siku hiyo Rais wetu wa nchi tunayemheshimu sana, amesimama pale amepewa cheki kubwa imeandikwa milioni ishirini, wakakabidhiwa ndugu zangu wa Kimbalu *SACCOS*. Tena Rais mtu makini sana, akawauliza hivi hii cheki ni mkopo ama msaada? Wakajibu haraka haraka, ni msaada Mheshimiwa. Utatoka lini? Wakasema, haraka tu watapata. Mheshimiwa Rais ameondoka, wana *SACCOS* wamekwenda benki, wanaanza kuambiwa masharti, leteni dhamana, leteni hiki, mbona *balance sheet* imekaa vibaya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia Waziri kupitia kwako kwamba mpaka leo hii hawajapata hizo Shilingi milioni ishirini. Mimi inaniuma kwa sababu tunaelekea kwenye uchaguzi, ni lazima niwe mkweli hapa. Mwaka 2005 nilizunguka Wilaya nzima ya Kyela, wananchi waliniamini nikisema tunakuja na kiongozi mwenye Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya! Wananchi wa Kyela walimpa asilimia 90 ya kura, mwaka huu mimi nategemea Rais wangu apate zaidi ya asilimia 98 ya kura kwa sababu kipindi hicho alikuwa hajachangia Kyela. Sasa hivi kila kitu kikubwa kilichofanyika Kyela kina mkono wa Rais Kikwete, ametusaidia. Lakini sitaweza kukubali kura zikapungua kwa ajili ya upuuzi kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunataka kuheshimu kiongozi wa juu kwa njia gani? Huwezi kumkabidhi Rais akashika lile bango mbele ya wananchi, wanaamini wanalipwa, anaondoka mnaanza kiswahili kipya. Mnafikiri watamlaumu nani? Wanaweza kumlaumu Rais. Lakini siyo hivyo tu, mimi mwenyewe kura zangu za maoni ziko hatarini pale kwenye eneo la Kimbalu. Sitakubali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri anisaidie hili, tuokoe jina la Mheshimiwa Rais na *NMB* watoe hiyo shilingi milioni ishirini kwa Kimbalu *SACCOS*. Dhamana ni Serikali ya Wilaya. Kumkabidhi Rais wa Nchi hundi ndiyo *security* hiyo! Wanataka *security* itoke wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisaidiwe hili. Hawa watu wa Kimbalu *SACCOS*, Mwenyekiti wao, Makamu na Kamati yao ya Utendaji ya watu 15 walikuwa wanaandamana kuja hapa leo, nimewazuia. Nikawaambia nitaongea na Waziri, wakasema hatukuamini! Nikasema hamniamini tena Mbunge wenu? wakasema sasa tutajuaje umeongea naye? Nikawaambia, basi nitaongea Bungeni, wakasema tutakuona kwenye *TV* ndiyo tutaamini. Sasa nimeongea. Waziri sasa ni juu yako na mimi naelewa kabisa kwa sababu wewe ni mchapa kazi. Naunga mkono hoja nikijua utanisaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe mchango wangu. Nitazungumzia zaidi Jimbo langu la Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo, nataka kusema kwamba nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kwa kuwa na moyo wa utulivu hasa kwa kipindi hiki ambacho nilikuwa na matatizo kidogo ya macho, lakini wametulia, wamenisikiliza, wamefuata maelekezo yangu na nimefurahi sana. Sina lingine la kusema isipokuwa nasema ahsante sana na kadri siku zinavyozidi kwenda hali yangu inazidi kuwa nzuri na nategemea tena kutangaza nia wakati wowote kuanzia sasa hivi. *(Makofi)*

Mhehimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilitaka kuzungumzia kuhusu masuala ya Jimbo langu la Kilwa Kaskazini. Kuna korosho na ufuta kwa maana ya mazao mchanganyiko. Nianze na korosho ambayo tayari bodi zake zipo, kila kitu kipo, mambo ya stakabadhi ghalani tumeelewa, nimepiga kelele sana, watu wameelewa, lakini ufuta wenzetu wengine wengi hasa wa Jimbo la Kilwa Kusini wananipigia simu mimi mtu wa Kilwa Kaskazini, wananiambia mbona imekuwa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi elimu hii tunapewa watu wachache au watu wote? Maana yake hali inakuwa mbaya sana kiasi ambacho mpaka nasikia watu wanafanya maandamano kwa sababu eti CCM inaiba ufuta wetu. Vitu vya ajabu kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Korosho, mimi ningependekeza kungekuwa na wiki ya korosho, watu wale korosho, badala ya kuuza nje, tule korosho. Korosho zina

thamani kubwa sana katika mwili wa binadamu, na mkila korosho nadhani mtanenepa kama wengine walivyonenepa hapa. Lakini, kama mkiitelekeza korosho, mtajionea wenyewe, mtaambiwa mmeathirika, mmefanya nini na kadhalika. Kwa hiyo, ndugu zangu Korosho, korosho, korosho msiziachie jamani. Pengine popote wanapotaka kulima korosho, tafadhali walime korosho, korosho ni nzuri, korosho ni siasa, korosho ni kila kitu ninavyoona. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ufuta na mazao mchanganyiko. Mimi ninashangaa ni kwanini Serikali inaleta kigugumizi katika kuweka kanuni ya mazao mchanganyiko. Tumeweka hapa sheria ya mazao mchanganyiko ambapo ufuta, mbata, mhogo, mpunga, mahindi na machungwa yote ingekuwa inazingatiwa kwa kusema kweli Kilwa Kaskazini au Kilwa kwa ujumla, tungekuwa tumepanda juu sana, na hata tungekuwa tuna kitu cha kujivunia cha kwenda kuzungumza mbele za watu kwamba na sisi tunacho kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kanuni zinalegalega mpaka Bunge lenyewe ndiyo linaisha hili, jamani tunakwenda wapi? Halafu kuna mazao mengine ya matunda kama machungwa na ndimu. Kule kwetu kwa mfano kama Kipatimu, Chumo pale na Ndete sehemu zote zile ambazo wanalima haya mazao ya matunda, kusema kweli ile miche yake imezeeka sasa hivi. Walikuwepo Wazungu, wakapanda ile miche, lakini sasa hivi imeshazeeka. Lakini kama kungekuwa na Bodi ikaweka kanuni zake na wakatuletea mbegu mpya na tukaweza kufanya vitu vyetu sawasawa na mpunga ule tunaolima Kilimani maana yake wengine wote hapa mnalima mpunga kwenye mabonde, sisi kwetu tunalima mpunga kilimani na tunapata, na tunakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine tumepelekwa shule kwa mpunga huohuo, lakini Bodi hamna. Kanuni zinachelea sijui Mheshimiwa Waziri atatuambia nini kwenye suala hili? Mimi ninasema hivi, nitanukuu maneno ya Mwalimu kwamba: “uchumi tumeukalia”, na kweli tumeukalia maana yake kama tungeweza kurekebisha haya mambo *chap chap* sasa hivi tungekuwa mbali na mazao yote yangeweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hasa kwa wenzetu hawa nikiwaita, pengine watanisema vibaya, mavuvuzela. Hawa mavuvuzela, wanazungumza hayo hayo. Sasa ninasema tukae chini, tutulie, tuweke kazi mbele na tufanye kazi ili tuhakikishe mazao haya yanafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno hayo mimi ninaomba elimu, hasa elimu itolewe na wananchi waelewe na wajue maana ya kuuza ufuta, maana ya stakabadhi ghalani nini, yote haya yaelezwe ndipo hapo mtaweza kujua kwamba Kilwa nayo inachangamka kwenye mambo ya mazao na ushirika wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema kwamba naunga mkono hoja na nia ya kugombea jimbo langu la Kilwa Kaskazini iko palepale, labda Mwenyezi Mungu aamue vinginevyo. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dr. Samson Mpanda**,** natumaini mavuvuzela wamesikia kule Kilwa. Sasa namwita Mheshimiwa Lucy Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa *Senator* Basil Mramba akiwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia, sikujua kama ningepata nafasi. Nilipeleka mchango wangu kwa maandishi, lakini kwa sababu nimepata nafasi ya kuongea nitayazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri ambayo imefanyiwa *research* na nina uhakika kabisa kama Wizara ikitaka kuitumia itafanikisha haya mambo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Kilimo Kwanza kiweze kufanikiwa vizuri ni lazima tuachane kabisa na kilimo cha kutegemea mvua, tuanze na kilimo cha umwagiliaji. Kule *TPC* katika shamba la miwa, wanatumia umwagiliaji na ndiyo maana wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Ningependa Serikali itueleze ina mikakati gani ya makusudi kabisa kuhakikisha kwamba, kilimo cha umwagiliaji kinatumika badala ya kutegemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, lazima washirikiane na Wizara nyingine ili kuweza kufanikisha Kilimo Kwanza. Wizara nyingine hizo ni kama vile, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Nishati na Madini. Kwa Wizara ya Miundombinu *at least* waweze kutengeneza barabara za kule vijijini kwa changarawe ili wale wakulima waweze kusafirisha mizigo yao kuileta kwenye masoko kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko wakakikishe kwamba, wanaweza kuwasaidia wakulima ili wa-*process* mazao yao kule kule vijijini. Hii itasaidia vijana wetu wasikimbilie mijini, maana vijana wengi wanakimbilia mijini kwa sababu ya kukosa ajira, lakini kukiwa na viwanda kule kule vijijini watakuwa wanafanya kazi kule kule vijijini kwenye viwanda, watapata ajira na vilevile mabaki ya vile vitu ambavyo vimekuwa *processed* yanaweza yakatumika kwa mbolea na vilevile kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara ya Nishati, wakulima wanatakiwa wapate nishati ya uhakika vijijini. Iwapo Wizara ya Nishati na Madini, inapeleka umeme vijijini, basi ipeleke umeme wa uhakika. Kwa mfano, kwa sasa hivi kule kijijini kwetu *Old* Moshi kuna umeme, lakini umeme ule unawaka kama mshumaa, hauwaki, hauna nguvu na hauwezi kuwasha mashine yoyote. Kwa hiyo, Wizara ya Nishati na Madini, ikipeleka umeme vijijini, basi wahakikishe wanapeleka umeme wa uhakika ambao unaweza ukasaidia na kuwezesha mashine zitumike kwa ajili ya kutengeneza juisi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo wamepata Sh. 103,952,371,000/=. Kwangu mimi ninaona bajeti hii ni ndogo sana ukizingatia kwamba watu wengi (zaidi ya asilimia 80) wako vijijini na wale ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vijijini, bajeti hii itakuwa ni ndogo kwa sababu itahitajika elimu na maafisa ugani watatakiwa wawe wengi zaidi. Tunatakiwa kutafuta ni jinsi gani ya kuzalisha mbegu bora, utafiti na kadhalika. Kwa hiyo, mimi kwa ushauri wangu bajeti hii ingetakiwa iongezwe zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwuliza Waziri katika bajeti ya masuala ya Ukimwi, *World Bank* wamejitoa, ninaona hamna fungu lolote kwa ajili ya Masuala ya Ukimwi katika sehemu za kazi. Mimi nilitaka kujua, wao watatumia fedha gani kwa ajili ya elimu ya Ukimwi katika Wizara yao? Kwa sababu hapa hamna fungu lolote lililotengwa kwa ajili ya masuala ya Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu uliopita kule Mkoa wa Kilimanjaro kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa mbegu za mahindi, na sasa hivi sehemu nyingi Tanzania, watu wengi wanakula ugali, hata kule Kilimanjaro ambako tulikuwa tunakula ndizi, sasa hivi tunakula ugali.

Sasa nilikuwa nataka kujua: Je, Wizara inazo mbegu za kutosha kwa ajili ya kipindi kijacho? Kwa sababu mbegu zilikuwa ni matatizo, watu walikuwa wana vocha lakini walikuwa wakienda kutafuta mbegu hawazipati. Ningetaka kujua Mheshimiwa Waziri, atueleze wana mbegu kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbole ya minjingu, watu wa kule Kilimanjaro walikuwa wanakataa kuitumia kwa sababu walikuwa hawajui matumizi yake. Inachukua muda sana, zaidi ya miaka miwili ili uweze kuona matokeo yake kwa sababu ni mbolea ya asili. Mimi ningeshauri Wizara itoe elimu ya kutosha, ni muda gani unahitajika ili tuweze kutumia mbolea ya minjingu, na vilevile waeleze ni Mikoa gani inaweza ikatumia mbole ya minjingu na sehemu zipi ambazo zinaweza zikakubali mbolea ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi duniani kote watu wanatumia *organic food*. Sasa ningependa kujua kama Wizara imetoa elimu kiasi gani kwa watu kulima na kutumia vyakula asilia badala ya vile ambavyo ni *genetic modified* kwa sababu, hivyo vinauzwa kwa bei ya juu zaidi na wakulima wakiweza kuelimishwa wakaweza kulima vyakula ambavyo ni *organic* ina maana watapata faida zaidi. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba, inaelimisha wakulima ili waweze kutumia hizi mbegu ambazo hazitumii *artificial fertilizer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu uhifadhi wa mahindi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Watu wengi sana unakuta wamelima mahindi mengi sana ya kisasa, lakini mahindi yale hayachukui muda sana yanapohifadhiwa, yanakaa kwa muda mfupi sana halafu yanaanza kuharibika na hawana sehemu za kuhifadhia kwa sababu sehemu za kuhifadhia ni ghali sana, hawawezi ku-*afford* yale matanki ya kuhifadhia mahindi. Lakini kwa vile wanajikuta wana mahindi mengi, wanataka kuuza nchi jirani lakini wanazuiwa.

Mimi swali langu ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri: Je, atawasaidia wananchi wa Kilimanjaro ili wapate vifaa vya bei nafuu vya kuhifadhia mahindi yao? La

sivyo, basi waruhusiwe kuuza mahindi yao nchi jirani ili waweze kujikimu kimaisha, maana yake wanazuiwa. Unakuta mtu ana mahindi, anataka kuuza nchi jirani anazuiwa, lakini kwenye nchi yetu madini mnayaruhusu yaende nchi za nje, mkulima aliyelima kwa jasho lake ananyimwa kuuza mahindi yake. Ningependa nipate majibu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nilichangia kwa maandishi, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hajaunga mkono hoja!

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Waziri na wasaidizi wake wote kuanzia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine kwa hotuba nzuri yenye mambo mengi na programu nyingi ambazo zote zinalenga kuinua kilimo katika nchi yetu na kwa sababu hiyo kupambana na umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo kwanza ni kukumbushia kama nilivyokuwa ninafanya huko nyuma kwamba, bado mkulima anahitaji mbegu bora zaidi, utafiti zaidi, elimu zaidi na mafunzo zaidi. Ninasema hivyo kwa sababu ukisoma hotuba hii utaona mambo mengi, mengi, mengi yanayokusudiwa kufanywa, lakini jambo la maana ni kwenda kwa watu halisi *on the ground*, hali halisi *on the ground* iko namna gani. Sote tunakubaliana kwa mfano vocha imeanza kuonesha matumaini ya kumnyanyua mkulima, lakini bado hakuna vocha za kutosha maana hiyo ni bajeti na hakuna fedha za kutosha. Kwa hiyo, kama tumeshakubaliana kwamba vocha zinasaidia, basi kuweko vocha za kutosha. Sasa hivi siyo kila mkulima anapata vocha, na anayestahili kupata vocha ni mkulima masikini, lakini siyo kila mkulima masikini anapata vocha sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, kwa sababu kilimo chetu hiki ni cha mahindi na nafaka mbalimbali ambazo zimekuwa zikilimwa huko nyuma, kinachotakiwa sasa ni *modernization* kama inavyosemwa kwenye hotuba. *Modernization* maana yake ni kumfundisha mkulima *on the ground*, hapo alipo kwenye shamba lake ili aweze kutumia utaalam wa kisasa, uliotokana na utafiti wa kisasa na ili aweze kuongeza mazao maradufu, apate bei nzuri na awe na uhuru wa kuuza mazao yake anapotaka kuuza penye bei nzuri.

Nasisitiza hili kwa sababu ukweli hata mimi ninaelewa kwamba ni rahisi zaidi kuzuia mahindi kuuzwa nchi jirani kama walivyosema wenzangu waliotangulia, lakini mkulima anafaidikaje? Mimi nilifikiri sera nzuri ingekuwa Serikali inunue mahindi kwa mkulima kwa bei ya kimataifa badala ya kumzuia. Kama akipeleka Malawi, Mozambique, Kenya au Uganda kwa bei fulani Serikali basi inunue mahindi hayo kwa bei hiyo na iweke kwenye akiba au baadaye yenyewe ikauze nje, ili tupate fedha za kigeni badala ya kumzuia mkulima na papo hapo mkulima halipwi bei halali ya soko iliyoko. Pendekezo langu kubwa sana ni hilo kwamba Serikali inunue mazao badala ya kumzuia mkulima kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kaya. Pale kwenye kaya, na hizi kaya masikini ndipo tunapolenga. Tukitaka kujua kama tumefanikiwa kwenye kilimo ni kujua mkulima leo anatoa kiasi gani na anapata fedha kiasi gani kutokana na mauzo yake. Yaani baada ya miaka mitano tungepima tukasema tumeondoa umasikini ngazi ya kaya kwa kupitia kilimo kwa njia kadhaa, kadhaa, kadhaa na mwanzo ni utafiti.

Mimi ninashukuru nimeona programu nyingi sana hapa za tafiti za mazao mbalimbali, lakini utafiti lazima umfikie mkulima na ulenge soko la mkulima, uzalishaji zaidi na elimu kwa mkulima mmoja mmoja, siyo kiujumla hivi. Ni mmoja mmoja na aweze kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli tukifanya hivyo tungeweza tukafika mahali tukasema asiyelima asile. Unajua kwenye Biblia wanasema asiyefanya kazi asile? Mimi naweza nikasema asiyelima asile, asiyefuga asile, na asiyevua asile. Lakini, huyu hawezi kufuga wala kulima, wala kuvua vizuri kama hana teknolojia ya kisasa inayomuezesha kuzalisha vizuri zaidi, kuongeza mazao, kupata bei nzuri zaidi, na kutumia teknolojia ya kisasa katika njia zote za uzalishaji na usindikaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, angalau wataalam wako wanisikie kwamba, tatizo kubwa leo vijijini hamna mizani. Huko kwenye Mikoa kadhaa tunaanza kupambana na wale watu wanaotumia vipimo bandia kama lumbesa, sijui majina mbalimbali ya vipimo, wakulima wananyonywa sana huko vijijini kwa sababu hakuna vipimo. Hivi, ni kitu gani kinazuia mahindi na Mchele na Mazao yote haya kuuzwa kwa kilo? Mimi ninajua kinachozuia hakuna vipimo vya kutosha huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri anataka kumsaidia mkulima baada ya kumhamasisha na kumwezesha kama alivyoeleza kwenye hotuba yake, ahakikishe anauza mazao yake kwa kilo au kwa vipimo vinavyoeleweka ili aweze kupata fedha halali kutoka kwa Wafanyabisahara halali, badala ya utaratibu wa sasa ambapo wanadanganywa sana na wanakosa soko zuri la mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ninakuomba ni kuweko utaratibu wa kuivisha matunda. Naona sasa umeanza kuingia kwenye matunda na bustani. Sisi Rombo tuko kwenye orodha hiyo ingawa hatukuandikwa mahali, lakini kama unavyojua Rombo tuko kwenye orodha hiyo ya wakulima wa bustani na ninadhani ndiyo Wilaya pekee ya Tanzania ambayo ina mkakati mzuri unaoeleweka hata kwenye Wizara yako. Natumaini mwaka huu tutaendelea kufanya kazi pamoja na utatusaidia kama ambavyo umekwishaiahidi kupitia kwa Katibu Mkuu wako.

Lakini Mheshimiwa Waziri watu wanachimbia matunda kwenye udongo ili yaive mapema. Hii balaa imetoka wapi? Watu wanachimbia mapapai, machungwa na kila tunda tunalokula Dar es Salaam limezikwa kwanza, ndiyo baadaye linakwenda sokoni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna teknolojia za kuivisha matunda, teknolojia rahisi kabisa za kuivisha matunda. Kwanini wakulima wasifundishwe njia za kuivisha

matunda? Nimefurahi nimeona hapa kwamba, mtakuwa mnapima sijui size ya mazao kwa mfano, machungwa size fulani, lakini ninaomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie hili tatizo la watu kuchimbia chini matunda ndiyo yaive kwa pamoja wakati kuna teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na kumtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri kwa sababu mimi naona matumaini mbele kama tukiendelea kufanya bidii na kufanya haya ambayo tumesema tutafanya. Ahsante sana. (*Makofi*)

## MCHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa maeneo mapya ya utawala na kwa Mbinga, Wilaya mpya ya Nyasa, Tarafa tatu kati ya kumi na vijiji vingi.

Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, pamoja na wataalam na wafanyakazi wote wa Wizara hii, mnafanya kazi nzuri sana, hata hivyo yamo mambo kama saba yanayogusa Mbinga ambayo ningependa yashughulikiwe ili kazi nzuri mnayofanya isiwe na kasoro yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasoro hizo za kurekebisha ni zifuatazo, kwanza ni kuhusu ruzuku. Mazao ya biashara ya pamba na korosho yanapewa ruzuku ya dawa, kahawa ni miche. Wakulima wa kahawa wanaomba nao wapatiwe ruzuku katika dawa na mbolea. Kwa vile kwa wakulima wa mahindi wapo ambao hawana uwezo basi Serikali itoe ruzuku ya asilimia 11 kwa wale ambao hawana uwezo wa kifedha lakini wanaweza kulima kama vile Serikali inavyotoa chakula bure kwa wale waliopatwa na njaa na hawana fedha.

Kuhusu ulipaji wa madeni *MBICU,* tunashukuru kwa Serikali kulipa shilingi milioni 106 kwa wakulima wa mbinga lakini wakulima wa *MBICU* walioanza hawajalipwa shilingi milioni 400 isipokuwa Chama cha Msingi Uteri walishalipwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa wakulima watalipwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ufufuaji ushirika wa *MBICU*, tayari bodi imeundwa, Wizara inaombwa kuchagua wajumbe wawili na kupeleka wataalamu angalau wawili akiwemo mtendaji mkuu, hii ni ahadi ya Waziri Mheshimiwa Stephen Wasira toka mwaka 2008. Ni vyema jambo hili likafanyika ili *MBIFAZU* wanunue kahawa mwaka huu. Naomba sana msaada wako ushiriki kwa biashara ya kahawa, ni muhimu hasa *TCB* wanapochukua hatua thabiti za kunusuru zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bodi ya kahawa *(TBC)* iharakishe kuandikisha wakulima na suala la kutangaza bei ielekezwe. Lakini naomba ofisi ya Kanda iwe Mbinga kama *TACRI* na si Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wadudu – vifungate, naishukuru Serikali kupitia ofisi ya Waziri Mkuu kutoa shilingi milioni 100. Naomba Wizara itusaidie zaidi ili jambo hili lisijirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naitakia Wizara kazi njema na naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa kusimamia kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kwa ufanisi. Nampongeza pia Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu kadhalika watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya kwa lengo la kuinua kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kimechangia 26% katika Pato la Taifa na asilimia hiyo imetokana na baadhi ya mikoa kufanikiwa katika kilimo cha kisasa na kuwa na mvua za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kondoa ni moja ya wilaya zinazopata mvua za kutosha kwa mwaka, tatizo lililopo ni pembejeo mwaka jana wananchi walichangishana kwa ajili ya kununua *power tillers* kupitia halmashauri tatizo walillopata na *power tillers* kutowafikia kwa wakati. Halmashauri walijitahidi kufuatilia hata hivyo upatikanaji wa *power tillers* hizo ulikuwa wa kusuasua mno.

Naiomba Serikali kuangalia namna ya kuisaidia halmashauri zetu katika suala la pembejeo ili pembejeo ziweze kufikishwa kwa wakati kwa wakulima naipongeza Serikali kutoa ruzuku kwa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Dodoma walihamasishwa sana kulima mazao ya biashara kama vile korosho, alizeti, ufuta na kadhalika. Naiomba Serikali kutuletea maafisa ugani wa kutosha kwani wananchi wa Dodoma hawana ujuzi wa ukulima wa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi waliitikia sana kilimo cha korosho tatizo ni wataalamu wa kuwaelekeza hivyo wanalima zao hilo kienyeji bila utaalamu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutoa mafunzo kwa wawekezaji 109 kwa lengo la kuibua miradi yenye lengo la kutatua matatizo ya upungufu wa chakula katika ngazi ya kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa Dodoma ni kame kila mwaka hivyo upungufu wa chakula ni wa mara kwa mara. Naiomba Serikali mafunzo hayo yangefanyika kwa wilaya zote za mkoa wa Dodoma hivyo kutuwezesha mkoa wa Dodoma kutatua tatizo la njaa linalo wakabili wananchi wa mkoa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyama vya ushirika bado havina mwitiko mzuri kwa wananchi kuunda na kujiunga na vyama hivyo. Uhamasishaji wa wananchi kujiunga na vyama vya ushirika ni muhimu sana, naomba maafisa wahusika na uundaji wa vyama vya ushirika wawajibike ipasavyo katika kuwahamasisha wananchi kujiunga katika vyama vya ushirika. Wananchi walio wengi katika mkoa wangu bado hawajajua faida ya kujiunga katika vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejiandaa vipi kuhusu kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuwa na uwekezaji endelevu katika sekta ya kilimo na hivyo kufanikisha kauli mbiu ya Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo na maji ni uhai ni mashirikiano yapi yaliyopo baina ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maji na Umwagiliaji hasa ikizingatiwa kwamba Tanzania ina mito mingi isiyokauka pamoja na maziwa lakini ina upungufu wa mvua katika maeneo mbalimbali . Serikali inasema nini kuhusu hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati gani itakayohakikisha usindikaji wa mazao badala ya kuuza mazao kama malighafi ambayo yanawapatia wakulima kipato kidogo pamoja na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanda vya mbolea ili mbolea ya kutosha yenye bei nafuu na inayopatikana kwa wakati badala ya kutegemea mbolea kutoka nje ambayo inakuwa ghali na haipatikani kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaonaje kuandaa mazingira ambayo yatawawezesha wakulima mmoja mmoja ambao wametimiza masharti lazima wajiunge katika *SACCOS* au vyama vya ushirika?

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niwapongeze Mawaziri na watumishi wa Wizara ya Kilimo kwa kazi yao nzuri na uwasilishaji wa Bajeti, mahiri sana, nawapongeza sana.

Pili, naomba nizungumzie suala la ushirika, maafisa ushirika wa huko wilayani wamekuwa wagumu sana kuandikisha vyama vipya vya ushirika. Wananchi wa Mnero Miembeni wamekuwa wakiomba na kufuatilia uanzishwaji wa chama cha ushirika cha msingi. Aidha, afisa ushirika hatoi maelezo ya kuridhisha kwa nini hataki kuandikisha chama hicho. Wananchi wa kijiji cha Ntepecha nao wameomba sana kuandikisha chama cha msingi lakini nao hawajasikilizwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri alipatie ufumbuzi jambo hili maana ni kero kubwa kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa mafanikio makubwa katika juhudi zao za kufufua kilimo.

Mimi ni *conservative* kwenye kilimo, *Old Habits Die Hard* sijaona dosari yoyote kwenye kilimo cha plau na wanyama kazi na mfano ni huo kwamba maeneo ambayo yanatumia sana kilimo hiki wako mbele. Matrekta na *power tillers* waachiwe matajiri wanaoweza kufanya *service* na kuya-*maintain* kwa watu wengi hawana uwezo kuyatunza wala kuyahimili kikamilifu.

Nashauri plau nyingine na maksai wengi vitolewe kwa vituo mbalimbali hata ikiwezekana bure kwa kila familia. Treka moja la *horse power* 45 ni sawa na shilingi milioni 56. Hivi fedha zilitumiwa kununua plau na maksai je, ni familia ngapi zitapata na hakuna *service and maintenance?*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi bali napenda kutoa ushauri ufuatao, kwanza, hadi leo asilimia kubwa ya mbegu bora inaagizwa toka nje ya nchi, ukweli ni kuwa mbegu bora kutoka nje inaweza isiwe mbegu bora hapa Tanzania kwa sababu ya tofauti ya udongo, mvua, joto na mahali mbegu bora iliyoagizwa na hali ya Tanzania kitaalamu hali hii inaitwa *genotypex environment interation*. Naomba sana tujitahidi kutumia mbegu bora iliyozalishwa hapa nchini na sio kuagiza toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima itambuliwe kuwa ili mbegu bora iweze kukuwa na kutoa mazao mengi inahitaji mbolea ya kukuza na ya kupandia. Hata hivyo kuna wakulima wasiofahamu na hupanda mbegu bora lakini hawatumii mbolea, tunaomba wakulima wapatiwe elimu kuhusu umuhimu wa kutumia mbolea wakati wanapopanda mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya kilimo bora yameanza kujitokeza mfano mzuri ni kule baada ya ukame wa mwaka 2009 hakuna chakula kiliagizwa toka nje bali chakula kilisafirishwa toka mikoa uliyokuwa na njaa. Naomba wanasiasa uchwara wanaobeza kilimo kwanza tusiwakilize kwani kufanya hivyo tutakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupate mafanikio katika kilimo kwanza tutumie rasilimali zetu kujenga mabwawa ya umwagiliaji kununua mbolea na kulima hapa nchini mbegu bora na tupeleke maafisa ugani kuelimisha wakulima kulima kilimo cha kisasa na hapa ndio tutaondoa umaskini wa Watanzania walio wengi.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. Ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote. Wakulima waliopo vijijini ambao ni wadogo wadogo na ni wa kilimo cha kujikimu wanafaidikaje na kilimo kwanza?

Kwa kuwa wadau wa kilimo bado wana matatizo sana katika kutumia mbolea ya Minjingu, je, ni mipango gani ya elimu imeandaliwa? Jambo hili lilizungumziwa sana kwenye kikao cha *RCC* mkoani Kilimanjaro na leo hii naomba nitoe dukuduku langu kuwa bado wananchi wanakigugumizi kuitumia ukizingatia kuwa matokeo yake siyo ya papo kwa papo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri na ngumu wazifanyazo kuendeleza kilimo katika nchi yetu. Ni kazi ngumu na nzito kutokana na umuhimu wa kilimo na wingi wa watu wanaohitji kuongozwa katika sekta hii. Aidha, pongezi zangu nazitoa kutokana na ubora wa hotuba iliyotolewa, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongeza hizi ninayo machache ya kuchangia katika hotuba hii kama ifuatavyo; naipongeza Serikali kwa ujasiri wa kuamua kuongeza ruzuku ya shilingi 80/= kwa bei ya pamba ya mwaka jana, ongezeko hilo limeongeza ari kwa wakulima wa pamba mwaka huu, naamini ni zao hili la pamba kwa msimu huu lingekuwa chini sana bila ongezeko hilo. Ruzuku hiyo imekuwa mkombozi wa kilimo cha pamba hasa katika Ukanda wa Magharibi (Mwanza na Shinyanga), kinachosikitisha ni kuwa bado wapo wakulima ambao hawajalipwa, ni matumaini yangu kuwa wote wanaostahili Serikali kupitia mikono yake mirefu walipwe japo kwa kuchelewa.

Bei iliyotangazwa sasa inatia moyio japo hairudishi gharama halisi ya kilimo cha pamba, kwa bei hii bado mkulima na pamba hatofautiani sana na mtu achimbaye akiba yake kwa kuogopa kuibiwa. Hii ni kwa sababu mtu huyo siku atakapofukua sehemu akiwa na bahati mbaya aweza akakuta imeliwa na mchwa! Nashauri bei ya pamba mwakani itangazwe mapema ifikie kiasi cha shilingi 1,000/= hata ikibidi kwa fidia ya Serikali kwa njia ya ruzuku.

Mwisho namtakia kheri Mheshimiwa Rais wetu kwa safari ndefu aliyoianza hapa jana, naamini akijitahidi atafanikiwa kukipata na Mwenyezi Mungu amwezeshe kuiongoza nchi yetu kwa miaka mingine mitano ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa asilimia mia.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kupata nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara muhimu nikianza kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Ndugu Muhamed Muya na timu nzima inayomsaidia, hotuba ni nzuri sana na nina imani mtasimamia vizuri tu, tekelezeni kama mwaka jana usimamizi ni mzuri.

Ombi langu la mwanzo ni kuhusu Kilimo Kwanza, ili tufanikiwe tuangalie kwa makini na Bajeti izidishwe hasa katika zana za kilimo cha kisasa, tuwatoe wakulima kutoka jembe la mkono, wakopeshwe *power tillers* na *tractor* kupitia vyombo mbalimbali vya umma. Mfuko wa pembejeo bado mtaji wake hautoshi, Waziri nikuombe sana mfuko huu upewe pesa za kuwakopesha wakulima, mfuko huo ni muhimu sana kwa nini usifanywe kama mfuko wa barabara na mifuko mingine iliyopo hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waziri na timu yake katika Bajeti ijayo ije na mpango mkakati wa mfuko huu ambao sasa umeanza kuonyesha matunda chini ya Mkurugenzi Mkuu na timu yake hivyo mpeni ushirikiano wakati huo huo ukusanyaji wa madeni kwa wale waliokopa usisitizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mizani ya muundo wa sasa kutotakiwa Kanda ya Ziwa hasa katika ununuzi wa zao la pamba. Mheshimiwa Waziri atakumbuka mabishano yaliyojitokeza katika mkutano wa wadau mkoani Mwanza. Kwa sasa bado ni tatizo kubwa sana hasa kwa vyama vya ushirika vipatavyo 144 hivi, kila chama kinatakiwa shilingi 500,000/= jambo ambalo hadi sasa limekwamisha maandalizi ya msimu kutokana na kutopata pesa za kununua mizani hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu Waziri atoe ufafanuzi wa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri ni nzuri tuwaombee tu watendaji wajitume katika kulinda mali za umma ili Watanzania wafaidike na Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Katibu Mkuu na wasaidizi wake kwa kazi nzuri na kwa jinsi walivyoitekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Nawapongeza pia kwa hotuba nzuri yenye malengo mazuri ambayo hapana wasiwasi Wizara itayatekeleza mwaka huu wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kwenye maeneo machache yafuatayo; kwanza maagizo ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara mwaka 2005. Rais alisisitiza maeneo manne ambayo nayaona ndiyo dira ya kuimarisha sekta ya kilimo.Kuweka mikakati ya kuleta kilimo cha kisasa chenye tija hii ndiyo njia pekee ya kuondokana na lindi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni kuwapatia wakulima zana bora na pembejeo zikiwemo mbolea, mbegu bora, dawa za kilimo na kuwapatia wakulima masoko ya uhakika, hii ndiyo mikakati itakayokifanya kilimo kiwe cha kisasa.

Pili ni kuwa na chakula cha kutosha ndiyo kinga kwetu tusife njaa, tatu, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ndiko kutakakotuhakikishia kuwa hatutaathirika na mabadiliko ya hali ya hewa na kwamba mavuno yetu hayatakuwa ya msimu wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyoelezwa katika ibara ya 13 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni sehemu kubwa ya utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais kwamba Bajeti ya kilimo imeendelea kuongezeka kutoka asilimia 5.8 ya Bajeti nzima ya mwaka 2005 hadi asilimia 7.2 kwa mwaka 2009/2010 na katika Bajeti hii kilimo kimepangiwa shilingi bilioni 903 sawa na asilimia 7.8 ya shilingi trilioni 11.112, ni ushahidi tosha wa kilimo kuzidi kupewa umuhimu mkubwa na kusogelea lengo la Azimio la Maputo.

Kuhusu utafiti, naipongeza Wizara kwa kuendeleza utafiti wa mbegu bora na udongo, nchi zote zilizopiga hatua kwenye kilimo zimefanya hivyo kwa kutia uzito kwenye utafiti. Kwa hiyo, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuweka vituo vya utafiti wa mazao mbalimbali. Lakini utafiti unagharama kubwa, hatuhitaji tutegemee tafiti zetu tu nyakati zote, ni bora tushirikane na taasisi nyingine za utafiti Barani Afrika na Umoja wa Afrika pale Addis Ababa una dira kubwa ya kilimo na maendeleo vijijini, maliasilli na mazingira. Idara hiyo ina vitengo vya utafiti ambavyo tafiti zao zinatolewa bure kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UA* na *NEPAD* pia wameunda chombo kiitwacho *Forum for Agricultural Research in Africa (FARA)* ambacho kina ratibu matokeo ya tafiti mbalimbali na zinapatikana bure. Nashauri Wizara na vituo vya utafiti nchini vishirikiane na taasisi hizo mbili Barani Afrika ili tufaidike na matunda yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na naiunga mkono hoja.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri kabisa na yenye manufaa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu tena zenye pongezi zimuendee Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa maandalizi haya. Ushauri wangu ni kuhakikisha zana za kilimo zinapatikana kwa urahisi.

Pia mikopo kwa wakulima iwe rahisi zaidi na sasa najua hili litafanikiwa kwa sababu ya kuanzisha Benki ya Kilimo, swali langu ni kuwa tunapowatangazia Watanzania kuwa zana za kilimo kama *power tillers* hazina kodi mbona ukifikisha bandarini vifaa hivi *TRA* wanasema kodi katika tela ya *power tiller* inalipwa kodi? Ushahidi ninao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa tuhakikishe mbolea zinawafikia wakulima wakati muafaka. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Hotuba hii pamoja na maudhui yake kama yatatekelezwa ipasavyo italiwezesha Taifa letu kuweza kujitegemea kwa chadkula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kuipa kipaumbele Sekta ya Kilimo. Aidha, Kilimo Kwanza kama kauli mbiu ya Serikali imeweza kuhamasisha jamii kuthamini kilimo jambo ambalo hapo nyuma lilidhauliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Rufiji hasa Jimbo langu la Kibiti kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendeleza kilimo. Jitihada walizofanya, pamoja na mvua nzuri zilizonyesha, imeweza kulihakikishia jimbo hili, kutokuwa na njaa mwaka huu. Zao la mpunga limestawi sana na wananchi wengi wanaendelea kuvuna mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pembejeo za kilimo kama vile mbolea pamoja na zana za kilimo nazo tumepata kiasi. Tunataraji mwaka huu tutaongeza *power tillers* pamoja na trekta ili ziwasaidie wakulima hawa kupanua mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *sulphur* ambayo hutumika katika kupulizia mikorosho nayo pia imeanza kutolewa na wananchi wanataraji kupulizia mwanzoni mwa mwezi wa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani zangu, nizungumzie suala la upatikanaji wa pembejeo. Katika ukurasa wa 78 na 79 wanaelezea kuwa, pembejeo za zao la pamba zitapelekwa katika Mikoa 20 ya Tanzania Bara. Miongoni mwa Mikoa hiyo ni Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Rufiji, zao la pamba linalimwa kuanzia mwezi Mei mwishoni. Lakini jambo la kushangaza hadi sasa mbegu hizo hazijapatikana. Jambo hili litasababisha kwa kiasi kikubwa kutofikiwa kwa lengo

lililokusudiwa. Naishauri Serikali iharakishe upelekaji wa mbegu ili mvua hizi zinazoendelea kunyesha zitumike kustawisha zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mafuriko yaliyotokea katika vijiji vya Jaribu, Mpakane na Uponda hapo Aprili mwaka huu. Kwa kweli wakulima wa maeneo hayo wameharibiwa mazao yao kutokana na mafuriko hayo na kusababisha zaidi ya ekari 1000 za mpunga ziliharibika kabisa. Taarifa ya mafuriko hayo imetumwa Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, lakini hadi sasa bado hatua za kuwasaidia wakulima hao kama zilivyoombwa na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, bado hazijachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wazi kuwa taarifa hii ya maafa inaihusu Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini kwa kuwa Wizara hii ndiyo inayohusika na kilimo na chakula, ni vizuri ikafuatilia barua hiyo ili wananchi hao waweze kupewa chakula kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 81 unazungumzia suala la zana za kilimo pamoja na mafunzo kwa wakulima wadogo kuhusu uzindikaji wa muhogo, korosho na ukamuaji wa mbegu za mafuta. Kwa niaba ya wakulima wa Rufiji naishukuru Serikali kwa maamuzi hayo yaliyo katika ukurasa huo kifungu Na. 171. Kama Waziri atakuwa na nafasi, ningependa kujua ni wakulima wadogo wangapi watakaopatiwa mafunzo hayo ili kuhakikisha mazao ya wakulima yanakuwa bora zaidi na kupata fedha nyingi kwa kuuza mazao yaliyosindikwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimalizie kwa kuiomba Serikali kuwa ni vizuri ikawahamasisha wananchi kwa kuwapatia wakulima wa Rufiji mbegu bora za mazao hasa mpunga kwani mbegu wanazotumia wakulima hawa ni za miaka mingi kiasi ambacho hata inasababisha wakulima hao kupata mavuno machache. Mbegu hizi zipatikane kuanzia mwezi Novemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo chetu kiwe na tija na kuweza kuwakomboa wakulima wetu kutoka kwenye dimbwi la umasikini, ni lazima kibadilike toka kwenye kilimo cha kujikimu kwenda kwenye kilimo kinachozalisha ziada kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni lazima yafanyike ili kilimo chetu kiwe cha tija zaidi:-

(1) Tuondokane na kilimo cha mvua hadi mvua. Serikali itie mkazo katika uwekezaji kwenye miundo mbinu ya umwagiliaji.

(2) Tuondokane na waatumizi ya zana za jembe la mkono. Tuongeze matumizi ya wanyama kazi na plau, *power tillers* na matrekta. Lakini hatuna budi kuwa na mfumo endelevu wa upatikanaji wa zana hizi pamoja na vipuri vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuwawezesha wakulima wetu kupata mikopo ya muda mrefu kwa masharti nafuu. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha dirisha la kilimo kwenye Banki ya Rasilimali. Naishauri benki ya rasilimali, ikamilishe haraka taratibu za kutoa mikopo ya kilimo. Aidha, Serikali iongeze matumizi ya mfuko wa mikopo ya pembejeo na zana za kilimo kwa kuupatia mfuko huu fedha za kutosha kuwakopesha wakulima. Kaisi kinachotolewa mpaka sasa cha shilingi bilioni 3.2 kwa mwaka hakitoshi kukidhi mahitaji makubwa ya mikopo ya wakulima. Serikali iangalie uwezekano wa kuongezea mfuko huu kiasi kisichopungua shilingi bilioni 5.0 kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wanahitaji elimu na maelekezo ya mara kwa mara toka kwa wataalamu kuhusu jinsi wanavyoweza kuboresha kilimo chao kutoka kwa Maafisa Ugani. Naomba Serikali iongeze udahili na ufundishaji wa Maafisa Ugani ili waweze kuwafundisha wakulima wetu taratibu za kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utafiti wa Kilimo – Tumbi Tabora ni moja ya vyuo kadhaa vya utafiti wa kilimo hapa nchini. Serikali iangalie kwa karibu sana mahitaji muhimu ya vyuo vyote vya kilimo hapa nchini ili viweze kuwa na mazingira rafiki kwa wanafunzi wanaopitia katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wataalam wengi wa taaluma ya utafiti wanakaribia umri wa kustaafu. Ni lazima Serikali iwe na mkakati maalum wa kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FESTUS BULUGU LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa mnayofanya. Hotuba ya bajeti na bajeti yenyewe imeandaliwa kitaalam. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna aina mbalimbali za mbegu ambazo zimethibitishwa bado hazijasambazwa kutumika na wakulima, ambazo ziko bado kwenye makabati *(shelves)* za vyuo vya utafiti. Wizara kwa *kushirikiana* na COSTECH, itilie mkazo usambazaji (uwasilishaji) wa teknolojia na mbegu mpaya na bora za kilimo ambazo zinatoa mazao mengi, zinahimili ukame, zinahimili wadudu na kadhalika na hivyo kumpa mkulima faida zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bado ina fursa kubwa ya kuuza mazao ya chakula nje ya nchi, iwapo kuna uzalishaji wa mazao hayo wenye tija, wenye uhakika na endelevu. Jimbo la Magu limezalisha mpunga kwa wingi sana msimu huu na kwa kuboresha barabara hadi vijijini, bei ya mkulima hata aliyeko *remote*, anapata bei *almost*

sawa na yule aliyeko kwenye *main road.* Wanunuzi toka nchi za jirani wamefanya mkulima anufaike sana kwa bei kuwa juu kwa sababu ya kuwepo soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondolewa ushuru kwa mafuta ghafi ya kula yanayoagizwa toka nje ya nchi yameathiri bei ya mazao ya mafuta yanayozalishwa hapa nchini. Bei ya pamba kwa mkulima ingeongezeka zaidi iwapo kodi hii isingeondolewa. Wakulima wa alizeti, simsim, karanga na kadhalika wameathirika. Serikali ilitazame tena suala hili kwa maana ya kuirudisha kodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja na umuhimu wa haraka kuanzisha viwanda (kuhamasisha wawekezaji ama kupitia utaratibu wa *PPP*) vya kutengeneza pembejeo za zana za kilimo, mbolea, viatilifu na kadhalika. "*Import bill*" ya miaka miwili ama mitatu ingetosha Serikali kuwa *share* na wafanyabiashara binafsi kuanzisha viwanda hivi hapa nchini. Tutaendelea kuagiza nje mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kusindika mazao ya kilimo vinaongezeka kwa kazi ndogo sana. Msukumo uongezeke kupitia Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzisha kilimo cha *GMO* hapa nchini Serikali iangalie uwezekano wa kuingia kwenye uzalishaji mazao kutumia *GMO* kuongeza uzalishaji wa mazao kwa ajili ya kuuza nje ya nchi na matumizi ya ndani ya nchi. Wenzetu Afrika walioingia katika kilimo hiki wamewezaje? Labda tujifunze kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Jimbo la Songwe wamehamasishwa sana kilimo cha zao la ufuta. Tatizo lililopo ni ukosefu wa soko sehemu pa kuuzia matokeo ya kulanguliwa. Je, Serikali haiwezi kusaidia kuwapatia soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni kero kubwa sana kwa wakulima katika Jimbo la Songwe. Kero hii inasababisha mfarakano mkubwa kati ya wakulima na wafugaji. Serikali ingebuni mpango wa kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde la Ziwa Rukwa linafaa sana kwa kilimo chote cha masika na kiangazi. Ni vyema sehemu hiyo ikafikiriwa kuwezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi kama vile matrekta na pembejeo.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Waziri – Mheshimiwa Wasira, Naibu Waziri - MheshimiwaMathayo na watendaji wakuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri na mafanikio makubwa katika sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Wamefanya mengi mazuri, wanastahili pongezi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, napenda kuwashauri mchukuwe hatua madhubuti kuwalinda wakulima hasa katika kipindi hiki cha kuanza kuuza zao la pamba. Tahadhari ya kwanza iwe ni kuhakikisha kuwa bei ya pamba inaendana na soko lake *(market conditions)*, lakini pia kuhakikisha kuwa mizani inayotumika haiwapunji wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara itumie fursa hii kutangaza aina ya mizani itakayotumika, kwani kuna mkanganyiko mkubwa wakati soko la pamba linaanza rasmi mwezi wa Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutokana na hali nzuri ya Jimbo la Mwibara, napenda kufahamu ni *schemes* ngapi za umwagiliaji zimepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2010/2011.

**MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ludewa (Kata za Madope na Madilu) wamepiga hatua kubwa katika kilimo cha chai. Wakulima hawa walianza na vitalu vya chai zaidi ya 30 (na wakapata kitalu bora kitaifa – kijiji cha Mangalanyere). Kufikia mwanzoni mwa mwaka 2010, wananchi hawa tayari wamepanda chai karibu katika ekari 100. Ili tupate kiwanda cha kusindika chai, lazima kuwe na angalau ekari 500, na kutokanana na uwingi wa miche iliyoko kwenye vitalu na *speed* ya kupanuka kwa kilimo cha chai, tunatarajia kufikisha ekari za chai 500 ifikapo mwaka 2011/2012. Kwa vile inachukua muda mrefu kupata mwekezaji wa kiwanda (kama inavyokuwa Kilolo) ni lazima kuanza kuhangaikia kiwanda cha chai (Ludewa) sasa. Je, Serikali itatusaidiaji kupata mwekezaji wa kiwanda cha chai Ludewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya Wizara hii ya Kilimo mwaka 2009/2010 Wizara iliahidi kuhusisha Wilaya ya Ludewa katika kiwanda *"Agriculatural Land use Plan"*. Hii haikufanyika, badala yake imefanyika *TAM* kutokana na kilimo na mabadiliko ya tabia nchi. Je, matokeo yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaotegemewa kuhusu kuhakiki matumizi ya mbolea kwenye udongo na mazingira pamoja na tathmini ya kimkakati ya mazingira vifanyike Wilaya ya Ludewa kwa kuzingatia miradi ya chuma Linganja na Mchuchuma kuanza kutaadhiri sana ardhi na mazingara na kilimo cha Ludewa. Tunahitaji kujipanga vilivyo katika matumizi ya ardhi.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pembejeo zinazotolewa na Serikali kwenye kilimo ili uzalishaji wa mazao uongezeke kama bei za mazao hayo itakuwa ndogo na haina uhakiki, ari ya wakulima katika uzalishaji au ulimaji wa mazao hayo utapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sahihi kuwazuilia wakulima kwenda kuuza mazao kwenye bei nzuri kwa kisingizio cha usalama wa chakula. Ni vyema Serikali itafute njia nyingine ya kuwa na usalama wa chakula popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutegemea kilimo cha mvua hapa nchini ni hatari hasa ukitilia maanani mabadiliko ya tabia ya nchi. Serikali bado haijajipanga ipasavyo

kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Ushauri wangu kwa Serikali ni bora watafute mabonde makubwa yenye uwezo wa kuzalisha chakula kingi kuliko kufanya kidogo kidogo katika maeneo mengi ya umwagiliaji, mfano, bonde la Mto Rufiji kama lingetumiwa kwa uzalishaji wa mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira ni mtambuka na kilimo licha ya kuwa ndio tunapata chakula, lakini pia kilimo kinachofanywa maeneo mbali mbali hapa nchini kinaharibu mazingira. Mazingira yanachafuliwa kwa kutumia mbolea ya chumvi chumvi na aina ya kilimo kinacholimwa. Je, Wizara imejipanga vipi na suala zima la kilimo na mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haiwezi kuleta mapinduzi ya kijani bila ya kuwa na wagani wa kilimo pamoja na wataalam wengine. Wakulima wetu wengi hawaelewi kilimo bora kikoje. Je, Serikali imejipanga vipi kuhusu suala la wataalam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwa maandishi hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa tamko la Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa ili iweze kulisha nchi nzima kwani ardhi yake ina rutuba sana, maji mengi, Serikali ni vyema sasa ikatekeleza tamko hili kwa kuwasaidia zaidi wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara sasa iongeze masoko ya mazao ya kilimo. Hivi sasa kumekuwa na malalamiko ya wakulima kwamba masoko ni madogo na bei ya mazao yao haidhaminiwi. Ni vyema basi wakauza nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, stakabadhi ghalani ni kweli imeboreshwa, lakini bado kuna mapungufu. Katika zoezi hili marekebisho yanahitajika ili kusaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya ugani, Serikali imejipanga kuendeleza kutoa ushauri wa kitaalam wa ugani ni vyema ikafuatilia kwa karibu katika Halmashauri zetu kuona elimu inawafikia katika Serikali za Mitaa na tatizo kubwa ni ufuatialiaji kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni wakulima wa korosho walinufaika na upandaji wa bei ya korosho, lakini wakulima wanalalamika jinsi ununuzi huo unavyoendeshwa na kuleta usumbufu. Ni vema hatua zikachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea ya ruzuku, wakulima wamekuwa wakilalamika kuhusu namna ugawaji wa vocha unavyoendeshwa, hauridhishi na kuleta adha kwa wakulima eneo hili nalo ni tatizo ambalo ni vyema likatatuliwa.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** awali ya yote, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, napenda kuwasilisha hoja na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukanda wa kati kilimo chake hasa ni mtama kutokana na hali ya mvua kidogo, lakini wananchi/wakulima wanang'ang'ania kulima mahindi na sio mtama kwa tatizo kubwa la ndege wasumbufu (kweleakwelea). Tukiwahakikishia tiba ya tatizo hili, mtama utalimwa na njaa itakwisha kanda ya kati. Nashauri kituo cha ndege cha kunyunyizia ndege ya kweleakwelea kiimarishwe na kitoe huduma za haraka ili kurudisha imani ya wakulima wa mtama.

Tunashukuru kwa Wilaya ya Manyoni kuigizwa katika utaratibu wa vocha, ombi ni kwamba kutafutwe mtaalam wa kilimo Mkoani, Wilayani hadi Kata atoe elimu kwa wakulima kuhusu namna ya kutumia utaratibu huu, na pia kuunganisha vocha na vikundi vya *SACCOS* ili wakulima wanufaike. Msimu uliopita ufanisi huu haukufanikiwa kutokana na mkulima kutoelewa vizuri utaratibu huu ambao ni mpya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARTHA MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji. Mimi nitakuwa na mchango wangu kwa njia ya maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini masharti ya mikopo ya *tractor* na *power tiller* ni magumu na kusababisha wakulima wengi walioko vijijini hasa wanawake ambao ndio wajasiriamali kushindwa kupata huduma hiyo eti kwa sababu tu wanatakiwa wawe na ekari 50 zilizoungana na sio tofauti tofauti hata kama zinazidi?

Je, ni vigezo gani vilivyotumika katika baadhi ya maeneo kupata fedha za semina ya Kilimo Kwanza kuliko zingine? Kwa nini hazikuwa zote?

Kwanini kuna miradi mingi katika Wizara hii kiasi kwamba inachanganya? Kwanini isiunganishwe iwe ni kitu kimoja Mfano, *DASIP, PADEP, ASDP* na *DADPS*.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Wasira, Naibu wake Mheshimiwa Mathayo pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na maandalizi mazuri ya bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuondoa kodi katika mbegu za alizeti na mazao mengine, jambo ambalo litasaidia wananchi wa Singida walimao alizeti na kuwahamasisha walime zaidi. Aidha, mafuta ya alizeti yataongezeka na kuwanufaisha wananchi wengi, viwanda vya kusindika alizeti navyo vitaimarika. Hivyo, naendelea kuishauri Serikali ilinde viwanda vya ndani vya mafuta ya chakula kwa kudhibiti uingizwaji wa mafuta ya chakula kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tatizo la ndege waharibifu halijapatiwa ufumbuzi na linaathiri sana mazao ya wananchi. Hili ni tatizo la muda mrefu lakini Serikali

haichukui hatua za uhakika kuangamiza ndege hawa yaani Qulea Qulea na Silindu (ndege wa Kijani). Ningependa kupata maelezo, mwaka huu ndege iliyodaiwa kufika Wilaya ya Singida Vijijini lakini haikufika, wananchi sasa wanakata tamaa ya kulima na huku tunahimiza Kilimo Kwanza, hizi ni *contradiction*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Maafisa Ugani hawaendi vijijini bali wanang'ang'nia kukaa mjini. Katika Kata nyingi na vijijini kuna wananchi hawawafahamu Maafisa Ugani kwa vile hawaendi katika Kata na Vijijini. Naomba sana tatizo hili lipewe msukumo wa dhati vinginevyo Serikali haitaboresha kilimo licha ya kutumia fedha nyingi kuajiri Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ushirika haujaimarika Jimboni kwangu na moja ya sababu ni uhaba wa Maafisa Ushirika, wapo wawili tu Wilaya nzima. Nasisitiza Halmashauri yangu iongezewe Maafisa Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mpango wake wa kilimo, ukisimamiwa kwa dhati, uchumi wa Watanzania utaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali ili kuboresha kilimo na kuinua pato la mkulima, Serikali ifanye yafuatayo:-

(1) Kupeleka Wagani na kuwapatia motisha. Ni vizuri wataaam wa kilimo wanapomaliza Vyuo Vikuu, wapelekwe kwenye Kata lakini Serikali iboreshe maslahi yao ili wasiondoke. Serikali iamue kwa dhati kuwaboreshea mishahara, nyumba za kuishi na usafiri ili wasishawishike kuondoka na kwenda mjini.

(2) Masoko ya uhakika, Serikali iachane na mpango wa masoko huria, kwani haya ndiyo yanaua bei ya mazao yetu. Mfano zao la pamba wakati Serikali inanunua kupitia Vyama vya Ushirika, pamba yetu ilikuwa safi tena yenye thamani. Leo zao hili limepoteza maana baada ya kuachiwa soko huria. Pamba inauzwa mashambani, chafu wakati mwingine ina maji, matokeo yake inakosa bei katika soko la dunia.

(3) Serikali iweke utaratibu mzuri wa kununua mazao ya wakulima. Serikali inapofunga mipaka, mazao ya mkulima yanashuka bei. Katika Wilaya ya Bukombe, mahindi na mpunga ni mengi. Ni vizuri Serikali iache kununua kupitia *SGR*.

(4) Upelekaji wa pembejeo, naipongeza Serikali kupeleka pembejeo Bukombe. Ombi langu msimu wa kilimo Bukombe unaanza mapema, ni vizuri pembejeo hasa mbolea na mbegu zipelekwe mwezi wa tisa au kabla ya hapo. Hata hivyo, wananchi wa Bukombe walishauri pembejeo zianze kupelekwa wakati wa mavuno wakiwa bado na fedha za kununulia.

(5) Zana za kilimo, napongeza kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati wa kuhitimisha hotuba yake, alisema kila Wilaya iamue ni zana zipi zitumke. Ni vema waraka utolewe kwenye Wilaya wenye maelekezo hayo. Kimsingi Bukombe ningekuwa mimi, ningechanganya kununua *power tillers*, maksai pamoja na plau kwani *power tiller* moja inaweza kununua *pair* nne (4) au zaidi za maksai na plau zake. Natumia fursa hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara, kwa ujumla kwa kuleta pembejeo na kuboresha kilimo Bukombe

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, kwa kuwasilisha hotuba nzuri sana ambayo ina mikakati ya kutekeleza azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza. Vilevile pongezi hizi ziwafikie Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii, ninawaombea Mwenyezi Mungu awape afya, nguvu na mshikamano ili waweze kutekeleza maazimio yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa stakabadhi ya mazao ghalani nchini. Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la njaa maeneo kadhaa hapa nchini kwa sababu ya ukame ambao umekuwa unajitokeza katika baadhi ya maeneo. Kwa kuwa upo mpango wa Serikali kwa Wilaya kadhaa wa stakabadhi ya mazao ghalani, napenda kuishauri Serikali kutoa agizo kwa Mikoa yote kutafakari mpango huu ili iwe kimbilio kwa wananchi ambao wanaweza kupata janga la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya kilimo, kwa kuwa imeonekana vituo vya kilimo vilivyojengwa kwa lengo la kutoa elimu ya kilimo cha kisasa, kuweka mbegu, kuweka pembejeo na kadhali vimeongeza tija ya kilimo, ninaishauri Serikali kujenga vituo hivyo kila Kata kupitia fedha za Kilimo Kwanza ili kuongeza uzalishaji wa kilimo kwa kudhibiti njaa na kuongeza pato la Taifa kupitia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Maafisa Ugani, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi yake kubwa ya kuboresha kilimo nchini kwa mazao mbalimbali. Kwa kuwa imeonekana wazi kuwa maeneo mengi yenye Maafisa Ugani, wakulima wengi wamevuna mazao ya kutosha kupitia kilimo cha kisasa. Ninaiomba Serikali kusomesha Maafisa Ugani wa kutosha ili kila kijiji kiwe na wataalam wa kilimo kuliko maafisa hawa kuwa kwenye Kata, wanakuwa na maeneo makubwa, utoaji wa taaluma unakuwa mgumu. Hata hao Maafisa Ugani walioko Wilayani watolewe waende kwa wakulima vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ushirika, mkakati wa Serikali wa kurudisha Vyama vya Ushirika, ni mzuri sana kwani Serikali itaweza kuwasaidia wananchi wengi kwa wakati mmoja kama vile kuwakopesha fedha za kununua mazao na

pembejeo za kilimo. Serikali itoe mwongozo kwa kila Wilaya kuunda Vyama vya Ushirika ili waweze kupata misaada au mikopo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Serikali kwa kutoa fedha za kilimo kupitia mifuko mbalimbali mfano *ASDP*. Kumekuwepo na matumizi mabaya ya fedha hizi kwa baadhi ya maeneo, ninaomba kuwepo na usimamizi madhubuti ili fedha hizi ziwezekuwa na tija katika kutekeleza lengo la Serikali la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya pembejeo kwa wanawake, nakiri kuwa juhudi za Serikali katika kutekeleza lengo la Serikali la Kilimo Kwanza zinaonekana kwa kuwa wanawake wameonekana wako sambamba na akina baba katika kilimo na kwa kuwa wanawake wamekuwa waaminifu na makini, ninaiomba Serikali kutoa mikopo ya pembejeo kwa wanawake nchini ukiwemo Mkoa wa Singida kwani sijawahi kusikia mwanamke amekopeshwa pembejeo mfano trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha pamba, ninapenda kuikumbusha Serikali kuwa miaka mingi iliyopita Mkoa wa Singida ulikuwa unalima pamba sana lakini zao hili lilipotea kwa sababu ya kukosa soko la kudumu. Kwa kuwa zao hili sasa limeanza kulimwa na baadhi ya wakulima baada ya soko kupatikana, Serikali iwahamasishe wakulima wa Singida waanze kwa uwingi kulima pamba kwani ardhi ya Singida karibu Mkoa mzima ni nzuri kwa pamba. Hii itasaidia kuongeza uzalishaji wa zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaishukuru Serikali kwa niaba ya wakulima wa alizeti Mkoani Singida kufuta ushuru wa alizeti kwani ulikuwa ni kero kwa wakulima wa zao hili na wafanyabiashara wa zao la alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu, kwa hotuba ambayo ni fasaha na yenye kujitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu zaidi, katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji, ni kilimo endelevu ambacho kinaweza kuitoa nchi yetu katika matatizo ya kuwa na uhaba wa chakula. Katika kutekeleza kilimo hiki, napendekeza, skimu ndogo ndogo ziwe na lengo kuu kwa sababu skimu hizi hazihitaji gharama kubwa, kama miradi mikubwa ya umwagiliaji. Katika Wilaya yangu fursa ya kuwa na skimu za namna hii ni kubwa sana kutokana na mito 38 isiyokauka. Kama miundombinu ya umwagiliaji itasambazwa Wilaya hii, basi tutaweza kuzalisha chakula kingi hasa mpunga kwa kuvuna mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kilimo cha miembe, Serikali iweke mkazo wa kilimo hiki ili nchi yetu iweze kuwa moja ya wazalishaji wakubwa wa zao hili. Hali ya hewa ya nchi yetu ni nzuri kwa kilimo hiki na papatikane Maafisa Ugani wa zao hili tu. Kwa mfano, tatizo kubwa la kilimo hiki ni upuputikaji wa maua ya miembe kipindi cha kutoa maua. Ziko aina za embe ambazo bei yake ni zaidi ya dola moja kwa hiyo kama uzalishaji utakuwa mkubwa nchi inaweza ikauza nje zao hili na kuipatia nchi yetu fedha za kigeni.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia muda huu kuwa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Kilimo imepangwa vizuri sana. Wataalamu wa Wizara wameweza kuwapa mategemeo Watanzania kwa kuona umuhimu wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni tegemezi kwa kukuza uchumi wa nchi yetu. Hivyo basi ni vyema Serikali ianze mapema kufanya uhakiki wa zana za kilimo. Kuna upungufu mkubwa katika nchi yetu jambo ambalo hupelekea wakulima wetu kulima kwa kutumia jembe la mkono na kuvuna mazao yasiyoweza kumkuza. Ili kilimo kiweze kukuza uchumi wetu, ni lazima Serikali iongeze kasi juu ya kilimo. Kufanya hivi kutampa mkulima moyo. Kuongeza kasi ya kilimo maana yake ni kuwepo soko la uhakika, bei nzuri ya mazao, viwanda na kadhalika. Kufanya hivi Serikali itafikia lengo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu tuliyonayo kwa baadhi ya Mikoa haitomsaidia mkulima. Kuna baadhi ya Mikoa, barabara ni mbovu jambo ambalo hupelekea mazao ya wakulima kuoza kwa kukosekana usafirishaji wa kuyapeleka sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ndio chachu cha maendeleo katika nchi yetu. Kutokana na bajeti ya Wizara kuwa ndogo, ni dhahiri Wizara itashindwa kufanikisha azma yake ya Kilimo Kwanza. Kuna mambo mengi sana yanayohitajika ili kukuza kilimo. Ukitazama bajeti, utaona Wizara imebebeshwa mzigo mkubwa na hatimaye kufeli katika kufanikisha azma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinahitaji pembejeo, kujengwa kwa viwanda vya mbolea ni kitu muhimu, kwani kutaweza kusaidia wakulima, mbegu bora ni moja ya kukuza kilimo. Madawa ni muhimu sana kwani ndio moja wapo ya kunusuru mazao yetu yasiharibiwe na wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko haja ione umuhimu wa vijana wetu kuthamini kilimo. Mara nyingi vijana hukimbilia mijini. Hii ni kasoro. Kama Serikali ikamuondoa kijana ili kumuwezesha kiakili, kiuwezo, kielimu na kadhalika bado tutabaki na maandiko tu. Ni haki ya Serikali kuandaa jambo jema kwa maslahi ya mwananchi wake na pia kwa Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo, napenda kumpa hongera Waziri wa Kilimo na Naibu wake na pia wataalamu wake kwa umahiri wao wa kumsaidia mkulima wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb), Mheshimiwa Dr. David Mathayo David (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu Mohamed Muya na wataalamu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Tabora, ambapo hutumika kulima mboga, matunda na kadhalika, ningeomba Serikali iangalie jinsi ya kuwezesha wakulima hao wa Kata ya Pangale, (Sikonge), Kata ya Mishe, Itonjando, Tumbi, Ndeveluo ili waweze kulima kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamejitokeza wakulima wengi wa zao la Tumbaku na kusababisha pembejeo kupungua. Hivyo basi niombe Wizara na wataalam waangalie upya takwimu za wakulima katika Mkoa wa Tabora ili kusitokee upungufu wa pembejeo kama vile, gunia za kufungia tumbaku, mbolea, vocha, mbegu bora za alizeti na mtama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo pia kuna wakulima ambao hulima chakula, mahindi ambayo huhitaji mbolea katika kata nane (8) nazo ni Tumbi, Ndeveluo, Mishe, Uyui, Itonjande, Itetemia, Kakola, Malolo, hao nao huhitaji ruzuku kwa mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utafiti Tumbi – Tabora, ningeomba Serikali iangalie kuboresha huduma bora, kama vile ukarabati wa mabweni, nyumba za Walimu, pia *hall*, kwani haviridhishi, ukarabati wa miundombinu, kama vile upatikanaji wa maji ya uhakika, kupewa vitendea kazi kama vile pikipiki na gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na chuo maalum cha kutoa mbegu bora za Tumbaku, Tumbi, hivyo ni vema kutoa mashamba darasa, kwenye maeneo husika hasa wanakolima zao hilo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, janga la njaa, kwa Mkoa wa Tabora, kuna upungufu wa chakula katika Wilaya ya Igunga, Nzega kutokana na upungufu wa mvua kwa mwaka huu, naomba Serikali ifuatilie suala hili kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza pia kiangalie upya suala zima la kuwawezesha wagani hapa nchini, kupewa nyumba bora, vijijini kwani wagani wengi hapa nchini wanakaa mijini kutokana na ukosefu wa nyumba za kuishi vijijini. Kutokana na hayo niombe Wizara kwa nchi nzima iwakopeshe wagani hao vitendea kazi ili waweze kutembelea maeneo ambayo yako mbali na makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagani hao wapewe pia posho ya mazingira magumu hasa pembezoni mwa nchi, ili wawe na moyo wa kufanya kazi. Wapewe fungu maalum la kuanzisha Mashamba Darasa kwa kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru Serikali kwa kuunga mkono kilimo katika Mkoa wa Rukwa, kwa kuhakikisha kuwepo kwa “mbolea ya ruzuku”. Hata hivyo, inasikitisha kuwa Mawakala waliohusika kusambaza mbolea hawajawatendea haki wakulima wa Rukwa kwa kupeleka mbolea walikojua, Serikali isaidie watu hao kuadhibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba darasa nayo ni mafunzo makubwa kwa wakulima wa Rukwa. Ni wazi kuwa sasa tija imeongezeka.

Mkoa wa Rukwa unajitahidi kununua matrekta. Tunahitaji sasa nguvu kupata wataalam ili kilimo Rukwa kifanikiwe zaidi. Mchango wa Serikali wa matrekta Rukwa tunautambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa haujapata mazao ya kudumu. Tunaomba Wizara iwasaidie wakulima wa Rukwa kuimarisha mazao ya kudumu kama Mbono eneo la Mpanda na zao lingine la kudumu ili mashamba ya wakulima hao yawe ya kudumu na kupandishwa thamani, kama wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la mazao ya Rukwa bado ni tatizo. Naomba Serikali itafute namna Rukwa inaweza kuuza mazao yao yasikae yanalundikana maghalani, kwa kushirikisha wakulima wenyewe kutafuta masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nichukue nafasi hii muhimu, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalamu wa Wizara, Mikoa na Wilaya, kwa kazi nzuri wanayofanya katika kusimamia, kuratibu na kutekeleza azma ya kitaifa yenye lengo la kuongeza kasi ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kuwa, naunga mkono hoja. Baada ya pongezi hizo, napenda kuchangia/kutoa ombi na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Nguzo ya Kwanza ni Dira ya Taifa ya Kilimo Kwanza. 1.2 - Kilimo cha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa, kiwe cha kisasa na cha kibiashara, majukumu ni kuwaendeleza wakulima wadogo 2009 - 2015.

Wilaya ya Rorya inavyo Vyama vya Wakulima Wadogo 28, vyenye wanavikundi wanaume na wanawake 228. Naomba Mheshimiwa Waziri awatambue, orodha ya majina nitampatia. Lengo ni kuwaendeleza kuwa wakulima wa kisasa kwa kuwapatia nyenzo hususan pembejeo na mbegu bora.

Pili, Nguzo ya Tisa ni Miundombinu kwa ajili ya Kilimo Kwanza. 9.1 - kubaini mahitaji ya uendelezaji miundombinu kwa ajili ya Kilimo Kwanza kwa kujenga Miradi ya Umwagiliaji ya kutosha, kwa kulenga mazao ya kipaumbele, wingi wa mazao na mahitaji ya mahali pa uzalishaji.

Wilaya ya Rorya ina eneo lipatalo kilometa za mraba 9,472, ambapo kilometa za mraba ni maji na kilometa za mraba 2,220 ni nchi kavu, eneo linalofaa kwa kilimo ni kilometa za mraba 1,116 au hekta 111,600, ambapo eneo linalolimwa ni hekta 50,000 kwa mwaka wakati hekta 61,600 hazilimwi au hazijaendelezwa.

Kilimo cha umwagiliaji kilianza mwaka 2002 kwa Skimu za Bwawa la Chuna, Bwawa la Chereche, baadaye Bwawa la Irienyi, Bwawa la Baraki, ambazo zilikuwa zinazalisha tani 861 za mpunga kila mwaka. Mabwawa yafuatavyo ujenzi unaendelea/haujaanza: Bwawa la Rwangenyi; Bwawa la Nyathorogo; na Bonde la Kirogo – Mto Mori. Kukamilishwa ujenzi wa mabwawa haya, kutaifanya Wilaya ya Rorya kuwa na mabwawa saba na kuweza kuzalisha Tani 6,373 kwa mwaka badala ya tani 861 za mpunga kila mwaka.

Ninaiomba Serikali iweke kipaumbele katika kukamilisha ujenzi wa skimu tatu za umwagiliaji chini ya utekelezaji wa miundombinu kwa ajili ya Kilimo Kwanza.

Uendeshaji wa skimu nne za umwagiliaji chini ya washiriki wa kilimo, unakabiliwa na uhaba wa fedha, naomba Serikali ianzishe Benki ya Wananchi katika Mkoa wa Mara na Wilaya ya Rorya, kwa kujenga uwezo wa usimamizi wa Benki hiyo kwa ajili ya mikopo.

Wakulima Wadogo Wilayani Rorya ni wachache waliopata nafasi iliyoko *Lower Moshi* (Kilimi cha Umwagiliaji).

Mkoa wa Mara unahitaji kuwa na Chuo cha Kilimo na Kiwanda cha Zana za Kilimo kwa kushirikianana na Sekta Binafsi.

Mwisho, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa Wizara kupata mchapakazi hodari. Naomba majibu.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mafanikio ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza ni muhimu kufahamu yafuatayo:-

Kwanza, usimamizi wa namna ya Mapinduzi ya Kilimo ni tatizo kubwa. Vocha za pembejeo zilizotolewa bado huwezi kujua kutoka kwa waliopewa jinsi walivyoboresha kilimo au kupata tija, hakuna anayepima matokeo kutoka kwa kila aliyepewa vocha za pembejeo. Mikakati isiwe kutoa tu, muhimu ni kujua wanavyotumia kuleta matokeo.

Pili, *power tillers* zinazouzwa kupitia Halmashauri na Watu Binafsi zimeonesha matatizo yafuatayo:-

(i) Bei zake ni kati ya shilingi milioni 8 - 10 kutegemea maeneo, lakini taarifa zingine zinaonesha kuwa, mawakala hununua kwa kati ya shilingi milioni mbili (dola 1000 -1500) kutoka nchi mbalimbali; sasa gharama hizi za nini? Kama kweli Serikali inataka Kilimo Kwanza iondoshe mawakala na *power tiller*s ziuzwe kwa wananchi kwa bei ndogo isiyozidi shilingi milioni mbili.

(ii) Vipuri vya matrekta hayo na mengine na zana za kilimo zinatozwa VAT, msamaha uliotolewa unahusu mazao ya chai na miwa tu na ni kwa wakulima wakubwa.

Naomba maeneo haya yapate maelezo sahihi. Naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa hotuba hii yenye kuleta matumaini.

(i) Kuwepo Programu Maalum itakayopanga juu ya kupeleka nguvu nyingi katika Mikoa michache ambayo ina mvua za kutosha kwa kupeleka matrekta na vifaa vingine vinavyohusiana na kilimo kama Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Morogoro na Iringa. Kwa kuipatia Mikoa hii mitano uwezo wa kitaalamu, pembejeo na matrekta, kutasaidia sana kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo na Mikoa mingine kuwe na mpango kabambe wa kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, ambacho kitakuwa ni mpango wa muda wa kati na endelevu.

(ii) Dhana ya Kilimo Kwanza isiwe kwa Viongozi wa Kisiasa kuhimiza bali pia iwe kwa vitendo na dhamira ya dhati kwa kutekeleza yale yote yaliyoamriwa na kwa wakati.

(iii) Halmashauri zote ziwe na Mpango Mkakati wa Kilimo Kwanza kwa kuwa na bajeti ya kila mwaka ya kununua matrekta na kuratibu suala zima la kilimo.

(iv) Kuwe na motisha kwa kuwapatia vitendea kazi mabwana na mabibi shamba kama nyumba na vyombo vya usafiri. Kwa kufanya hivyo, kutaongeza kasi ya wataalam, hao kupenda kuishi vijijini na wakulima.

(v) Kuwe na mpango wa kuanzisha mashamba makubwa ya mazao ya aina mbalimbali ili kilimo kiwe cha kisasa.

(vi) Kuwe na Sera ambayo itamlazimisha kila Kiongozi wa Kisiasa awe na shamba la mfano lisilopungua eka tano ili wananchi waige na kupenda kilimo na pia itakuwa ni sehemu ya kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na Wasaidizi wake wote, kwa kazi nzuri katika miaka mitano. Kwetu sisi Tabora Kaskazini, miaka hii mitano imekuwa ya mafanikio makubwa kwa kuboresha vipato vya Wakulima wa Tumbaku. Natumaini mafanikio yaliyofikiwa yataendelezwa na kuimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tupewe ushirikiano zaidi Tabora Kaskazini (Wilaya ya Uyui), katika kuinua na kuimarisha kilimo mchanganyiko kikiongozwa na Kilimo cha Mahindi na Mpunga, kwa kuwasaidia wakulima wetu wapate pembejeo muhimu kama ilivyo kwa tumbaku. Tunahitaji mbegu bora za mahindi na mpunga (ruzuku pia), pamoja na huduma za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Viongozi na Watumishi wa Wizara ya Kilimo kwa kuibua Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri yafuatayo:-

(i) Mpango wa Kilimo cha Umwagiliaji na hasa katika maeneo kame yanayopata ukame na njaa ya mara kwa mara ambapo ipo mito inayotiririsha maji, mfano, Mto Manonga na Mabonde katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Mwanza.

(ii) Usambazaji wa Mbolea ya Ruzuku iwe kwa wakulima wote na hasa ikizingatiwa maeneo mengi yana ardhi iliyochoka. Naomba Wakulima wa Wilaya ya Nzega nao wapewe Mbolea ya Ruzuku.

(iii) Huduma za ugani ziwe kwa mgawo wa watumishi wa kilimo na mifugo angalau kila kijiji kiwe na wataalamu wawili.

Napenda pia kutumia fursa hii kufikisha kilio cha maombi ya Wananchi wa Nzega kuomba msaada wa chakula. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa hotuba yake iliyojaa changamoto nyingi za kutekelezwa ili kuinua uzalishaji wa mazao ya chakula nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uzalishaji wa mbegu za mafuta kama alizeti na ufuta na kadhalika uongezeke kwa kasi nchini, hadi kufikia kukamua mafuta mengi ya kukidhi mahitaji nchini, ni lazima Serikali ichukue hatua za kuwajengea wakulima mazingira ya kuwepo soko la uhakika.

Nchi yetu ina maeneo mengi na makubwa ambayo yanafaa kabisa kwa kilimo kikubwa cha mbegu za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwapatia wakulima soko la uhakika, naiomba Serikali iwashawishi wawekezaji watakaojenga kiwanda au viwanda katika maeneo yanayofaa na ambayo wananchi wenye makazi kuzunguka viwanda hivyo wawe *outgrowers* kama mfumo ulivyo katika mashamba ya miwa na viwanda vya sukari. Ikiwezekana, hata mwekezaji awe na eneo la kulima mbegu za mafuta ikiwa ni *Nucleus Estate* itakayopunguza *excessive risk* ya kupungua kwa uzalishaji wa mbegu kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kiwanda kikiingia mkataba wa uhakika na wakulima wanaokizunguka watahakikisha wanazalisha mbegu za mafuta kwa wingi kwa kujiamini kutokana na kuwa na uhakika wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali irejee kulikagua Shamba la Mpunga la Kihangali, Wilaya ya Kilosa, ambalo Serikali imetumia fedha nyingi sana kuikarabati mifereji ya umwagiliaji. Mitaro karibu yote na mabanio yameharibiwa na mifugo mingi ya wafugaji walioamua kuacha mifugo yao Kihangali. Kwa kuzingatia dhana nzima ya Kilimo Kwanza, naiomba Serikali ilipe suala hili umuhimu wa pekee ili kuwakomboa wakulima wa eneo hili na kudumisha uzalishaji wa chakula kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali italizingatia jambo hili. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuanzisha kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, kauli hii haitoweza kutekelezeka bila Serikali kuwa na mikakati ya kuhakikisha kilimo kinaondokana na kutegemea mvua, tujielekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji hapa ndipo tutayoana mafanikio. Je, Serikali ina mikakati gani kuhusu hili la umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakulima wengi wanakuwa wakilalamikia Mbolea ya Minjingu kuwa haifanyi kazi na wengi wanapendelea kutumia mbolea ya chumvichumvi, lakini hawajapata elimu ya kutosha kuhusu manufaa ya Mbolea ya Minjingu na inatakiwa ikae ardhini kwa muda gani ili ifae. Ninashauri itolewe Elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya Mbolea ya Minjingu matokeo yake ni baada ya miaka miwili na kadhalika au vinginevyo pamoja na faida yake. Vile vile wakulima wajulishwe ni mikoa ipi au maeneo gani wanaweza kutumia mbolea hiyo na kwa mazao gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha Wizara ya Maendeleo kutengewa Bajeti ya shilingi 103,952,371,000 hizi ni ndogo sana ukizingatia sasa hivi kila mahali ni umuhimu wa kilimo ili kutuletea maendeleo ukizingatia asilimia 80 ya Wananchi wa Tanzania wapo vijijini na ni wakulima. Patahitajika mafunzo mengi kuhusu kilimo cha kisasa. Itabidi Maafisa Ugani waongeze maendeleo ya mbegu na kwa za haraka. Je, kwa kiasi hicho haya yatatekelezeka?

Ninashauri kipindi kijacho Bajeti ya Wizara hii iongezwe.

Katika Bajeti hii wahisani *(World Bank)* wamejitoa kusaidia fedha kuhusu masuala ya UKIMWI. Je, Wizara imejipangaje na matatizo ya UKIMWI katika sehemu

za kazi au watatoa wapi fedha kwa ajili ya masuala ya UKIMWI katika Wizara hii? Ninaomba nipewe majibu ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Duniani pote sehemu nyingi kwa sasa hivi watu wengi wanapendelea vyakula vya asili *(organic food)* badala ya vyakula visivyo vya asili *(generic modified food).* Je, Tanzania tumejipangaje ili tuzalishe vyakula vya asili zaidi ukizingatia ndivyo vyenye bei ya juu zaidi katika soko ili tufaidike zaidi katika mapato ya fedha za kigeni *(Export)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuwanufaisha wakulima wafaidike inabidi Wizara zishirikiane; Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Viwanda na Wizara ya Nishati.

(i) Wizara ya Miundombinu; ihakikishe barabara za vijijini zinapitika angalau kwa changarawe ili wakulima waweze kusafirisha mazao yao kwa bei nafuu na pia kuweza kuyapeleka sokoni kwa urahisi.

(ii) Wizara ya Viwanda; pawepo na viwanda vya saizi ya kati ili matunda/mazao yawe *processed* kule kijijini. Hii itawapatia ajira vijana wengi na kuwazuia kukimbilia mjini na mabaki ya mazao yale yanaweza kutumika pale kijijini kwa matumizi mengine kama mbolea na kadhalika.

(iii) Wizara ya Nishati; ihakikishe umeme vijijini unapatikana kwa uhakika sababu hata vijiji vilivyobahatika kupata, umeme ni mdogo sana unawaka kama mishumaa. Umeme huu hautoshi kuendesha au kuwasha mashine kwa ajili ya kutengeneza *juice.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakulima wengi wamekuwa wakilima kwa wingi sana mahindi ya kisasa lakini storage ni matatizo; ni ghali sana, ukizingatia mahindi ya kisasa yanaharibika haraka sana. Tunaiomba Serikali iangalie ni jinsi gani matanki ya kuwekea mahindi yanauzwa kwa bei nafuu au wakulima kule Kilimanjaro waruhusiwe kuuza mahindi yao nchi jirani wapate faida badala ya kubaki na mahindi ambayo hawawezi kuhifadhi na mwishowe wanapata hasara.

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Kwanza, naipongeza Serikali kwa kuwa na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Pamoja na pongezi hizi, napenda kuainisha changamoto zifuatazo:-

(a) Ukosefu wa mbegu bora. Msimu uliopita wa mvua za masika palikuwa na uhaba mkubwa sana wa mbegu, hali hii kwa Wilaya ya Kibaha Vijijini imedhoofisha sana juhudi za wananchi kulima ipasavyo; ni vyema pawe na mpango mahususi wa kuhakikisha kuwa mbegu zinapatikana kwa wakati.

(b) Vifaa vya kilimo – *Tractors and Power Tillers.* Serikali iweke mkazo mkubwa katika ununuzi wa *tractors/power tillers,* kuweka vituo vya huduma za *tractors* hizo, upatikanaji wa vipuri. Sasa hivi kuna tatizo kubwa la vipuri vya *power tillers* hasa *tyres* zake zinapatikana kwa taabu.

(c) Elimu kwa Wakulima – Bado lipo tatizo la maafisa ugavi waliopo kuwa ni makarani wa ofisini zaidi kuliko mabwana/mabibi shamba. Muda mwingi unapotezwa katika kujaza madodoso, mikutano na *seminars*, badala ya kutembelea mashamba ya wakulima na kutoa elimu.

(d) Majeshi: Ni vyema kazi kubwa zaidi ikawekwa kuwapa uwezo JKT na Magereza walime kisasa. Kwa upande wa JKT, wakati umefika sasa kupeleka vijana wengi kwenye makambi ambako wanafunzwa kilimo cha kisasa na wakimaliza wapewe ruzuku ya *power tillers* katika vikundi watakavyoviunda.

Nawatakia kazi njema, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza sana Wizara kupitia Waziri wake, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti hii. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa, Serikali kupitia Bunge hili, ilitunga Sheria ya Kusimamaia Mazao Mchanganyiko. Sasa nataka kujua je, Bodi ya Mazao Mchanganyiko ilishaundwa na nini mafanikio yake hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Vyama vya Ushirika vilivyokuwa vinajihusisha na ununuzi wa kahawa kufa na vichache vilivyobaki kutofanya kazi kwa ufanisi, yalijitokeza makampuni mengi ya watu binafsi na vikundi mbalimbali kununua kahawa. Tatizo linalojitokeza sasa ni kubadilika badilika kwa bei ya kahawa kwa wakulima (Shambani). Kwa maoni yangu bei hizo kati ya shilingi 1200 hadi 1800 hupangwa makusudi kabisa na wanunuzi hao; hali hii huwaumiza sana wakulima. Naiomba Serikali kupitia Bodi ya Kahawa, ifuatilie suala hili, vinginevyo tutaendelea kuwaumiza wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuwapatia wananchi nafuu ya mbolea na mbegu kupitia utaratibiu wa vocha. Hata hivyo, jitihada hizo za Serikali zinakwamishwa na watumishi na mawakala wasio waaminifu, ambao huiba vocha hizo. Napenda kujua ni hatua gani zilizochuliwa na Serikali kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu kwa wale wote waliohusika na wizi/upotevu wa vocha hizo?

Nashauri kwamba, ili kukomesha tatizo hilo ni vyema wale wote wanaohusika kwa njia moja ama nyingine kupoteza vocha hizo wafukuzwe kazi, washushwe vyeo na kufidia upotevu wa vocha.

Pili, naomba Taasisi ya *Tanganyika Farmers Association (TFA)*, ndiyo itumike kama Wakala wa Serikali katika kusambaza vocha za mbegu na mbolea. Nina hakika hatua hizo zikichukuliwa na kusimamiwa vizuri, tutapunguza vitendo vya wizi wa vocha hizo.

Tatu, Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali wahusishwe kikamilifu katika zoezi zima la ugawaji wa vocha kuliko kuwaacha nje kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha tija kitawezekana tu kama utafiti katika Sekta ya Kilimo utaongezeka. Ni aibu kwa nchi yetu kuendelea kuagiza mbegu nje ya nchi. Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba, tunatumia karibu asilimia 75 ya mbegu kutoka nje. Ninashauri nguvu zaidi zielekezwe kwenye eneo la utafiti kwa kuvijengea vyuo vya utafiti uwezo kwa kuongeza wataalamu vifaa vya kazi kama vile gari na kadhalika. Aidha, bajeti ya vyuo hivyo ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa unafanya kazi nzuri sana, kwani unaweza kuwafikia wananchi/wakulima wengi nchini. Nawapongeza Viongozi wa Mfuko huo kwa dhati kabisa. Tatizo ambalo Mfuko unakabiliwa nalo ni bajeti ndogo; kutengewa shilingi bilioni tatu kwa mwaka, ni kiasi kidogo sana. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii, ione umuhimu wa kuuongezea Mfuko pesa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuamua kuanzisha dirisha la kilimo kupitia *TIB* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wananchi/wakulima. Hata hivyo, masharti yaliyowekwa si mepesi sana, inawezekana kabisa azma ya Serikali isifikiwe kwa wakulima wengi kushindwa kukopa kwa sababu ya ugumu wa masharti. Nashauri Serikali ipitie upya masharti haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kwa sasa tunaelekea Soko la Pamoja na tunaotegemea wanufaike na Soko hilo ni wananchi wetu, hasa ambao wako mipakani na wengi wao ni wakulima ambao watauza mazao yao ya kila aina. Je, Bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii inatosha?

Kilimo cha wananchi wetu ni cha jembe la mkono na siyo cha kitaalamu, wanalima tu na wamezowea kulima mazao ya chakula chao; je, ni mikakati ipi ya haraka iliyofanyika kutoa elimu kwa kuwatengea maeneo kitaalamu mapema ili na wao wafaidike na Soko la Pamoja, bila kufanya hivyo Mtanzania ambaye ni mkulima atafaidika tusije tukawa watu wa kubeba mizigo?

Kwa kuwa Mkoa wa Kagera ni Mkoa wenye neema ya mvua za mara kwa mara; kwa nini Serikali haiwapi kipaumbele wakulima wetu kwa kuwapatia elimu ya kilimo cha umwagiliaji pamoja na utaalamu wa kuvuna maji ya mvua? Mkoa wa Kagera, tulikuwa na bahati ya kutoombaomba chakula ila matatizo ni kukosa utaalamu pamoja na sasa tumeingiliwa na ugonjwa wa migomba na ndiyo chakula kikuu. Je, bila kupata utaalamu watu watakufa na njaa?

Tunaomba msaada wa pembejeo mapema. Hatuhitaji mbolea ya chumvichumvi kwa sababu inaharibu sana udongo. Wananchi wanalalamika sana wanasema afadhali kutumia mbolea ya samadi kuliko ya chumvichumvi.

Ningependa kujua je, katika matrekta yaliyoingia Mkoa wa Kagera na Wilaya zake wamepewa mangapi?

Ardhi ya kutosha tunayo ya kulima kila mazao, kwa kuwa sasa hivi miundombinu ni mizuri Uganda na Rwanda tusaidieni Wanakagera tuondokane na umaskini na tukuze uchumi wa nchi.

Chai na kahawa ni mazao ambayo Wananchi wa Mkoa wa Kagera wamekata tamaa kuyaendeleza, kwa sababu ya kushuka kwa bei ya mazao hayo. Tunaomba msaada wa Serikali.

Kilimo ni uti wa mgongo, isiwe hadithi iwe ni vitendo. Pamoja na hayo, Kilimo Kwanza isiwe kaulimbiu tu iendane na vitendo vyake, tuwe na kilimo cha kisasa kinachoendana na kaulimbiu hiyo.

Wakulima wa Kagera wanakata tamaa ya bei ya Zao la Kahawa; ni lini Serikali itaingilia kati Zao hili kama zamani bei ilivyokuwa nzuri na kutuondolea umaskini Wanakagera? Kahawa inakuwa tamu, bei inakuwa chini, kitu cha kushangaza Uganda wanauza bei yao inakuwa nzuri na wananunua Kagera, Vijiji vya Misenyi Karagwe. Je, kwa nini Serikali pamoja na Wizara isifanye utafiti wa bei hawa wanauza wapi penye bei nzuri na sisi tukauze huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kushika kalamu hii na kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakupongeza wewe, Naibu Spika, na Wenyeviti wako wote, kwa kuliendesha Bunge lako Tukufu, bila ya upendeleo wowote; Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii ya Kilimo na Ushirika, pamoja na kazi ngumu waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee ziende kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeleta kaulimbiu ya Kilimo Kwanza lakini Mheshimiwa Spika, bado Serikali haijajipanga vizuri, kwani Kilimo Kwanza kinataka maandalizi makubwa kama viwanda vidogovidogo, mbolea ya kutosha, masoko, miundiombinu na zana za kisasa za kulimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kama Serikali haijitahidi, lakini la kusikitisha ni kwamba, wananchi wanajitahidi kulima lakini wanakosa masoko na viwanda vya kusindika, matokeo yake mtunda yanaoza na wananchi wanapata hasara sana juu ya kadhia hiyo. Kwa hiyo, ile dhana ya Kilimo Kwanza inakosa *impact.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iendelee kujipanga vizuri ili haya mambo muhimu yanayolalamikiwa yapatikane. Kwa kukosa mambo haya, vijana wengi wanaondoka vijijini na kukimbilia mijini, kwani wanaona dhana hii ya Kilimo Kwanza haiwasaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wa ugani ni kidogo sana na hao waliokuwepo hawawafikii wakulima kutokana na kukosa motisha ya maisha yao hasa ukizingatia maisha ya vijijini ni magumu, hakuna umeme wa kutosha, hakuna maji safi na salama. Mtaalamu anasoma halafu anakwenda kijijini kwenye mazingira magumu, anashindwa kufanya kazi yake kwa uaminifu, anaripuaripua tu matokeo yake mambo yanakuwa siyo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali haijaona umuhimu wa utafiti, kwani watafiti wanajitahidi kufanya hivyo lakini Serikali haiko *serious* katika kuchukua utafiti huo na kuufanyia kazi, kwa vile watafiti wetu wanafanya vizuri basi Serikali iwape motisha wenye fani hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwasaidie sana wananchi kwa kuwapatia mbolea bora ili wapate kulima mazao yaliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Bajeti ya Kilimo. Aidha, ongezeko la Bajeti ya Kilimo ukilinganisha na Bajeti iliyopita ni jambo la kupongezwa sana.

Eneo la Mufindi katika mashamba ya chai, Zao la Biashara, wameomba wapewe vocha katika Zao hilo la Biashara. Miradi ya Halmashauri ya Kilimo ilenge kuongeza uzalishaji hususan maeneo ya njaa kama Ismani ambako kila mwaka hupelekewa chakula.

Ninashauri utafiti wa udongo na mbegu bora na vituo vya utafiti viwepo kila Jimbo ili iwe rahisi kwa wananchi kupata ushauri na huduma za kilimo. Maeneo mengi udongo umechoka hauzalishi mazao kama miaka ya nyuma. Maeneo hayo ni kama Idodi, Pawaga na Ismani; hivyo, jitihada za ushauri na mazao mbadala ni muhimu wananchi wakaelekezwa. Mfuko wa Pembejeo upange bajeti yake kila mkoa ili Mfuko usipelekee mikoa michache kunufaika na mikopo kama ya trekta na mikoa mingine kutonufaika kabisa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

- Tunaomba mbegu bora za alizeti katika Wilaya ya Kongwa, Zao la Alizeti na Karanga zinaweza kutukomboa kwa lishe na uchumi pia.

- Mfuko wa Pembejeo bado haujatoa mikopo ya matrekta makubwa kwa wakulima Wilayani Kongwa. Naishauri uhamasishaji ufanywe kwa vile wakulima wenye uwezo ni wengi.

- Mwaka huu 2010/2011 ni mwaka wa uhaba wa chakula Wilayani Kongwa, tunaomba chakula cha njaa, hali ya chakula siyo nzuri kabisa.

- Tunahitaji mbegu bora za mtama mapema mwezi Oktoba *latest.*

- Zana za kilimo; naomba jembe la kukokotwa na ng'ombe lisidharauliwe, yatengenezwe kwa wingi na yasambazwe. *Power tiller* peke yake siyo ufumbuzi ni vyema na *ploughs* zisambazwe sana hasa Mikoa ya Dodoma na Singida.

- Udhibiti wa viwavi jeshi uimarishwe vinachangia sana uharibifu wa mimea.

- Tunaomba Zao la Zabibu lipewe kipaumbele kwa kusambazwa katika Wilaya za Kongwa na Mpwapwa.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia hoja hii, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii. Aidha, nampongeza Waziri wa Kilimo, Naibu wake pamoja na Wataalamu wote waliohusika kuandaa Bajeti. Bajeti imelenga kwa uhakika kaulimbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu katika eneo la ugawaji wa mbolea. Jimbo la Mbeya Vijijini lina aina mbili za upandaji wa mahindi.

Katika Kanda ya Juu, yaani Tarafa ya Isangati na maeneo machache ya Tarafa ya Tembela, yana kilimo cha kiangazi bila kumwagilia au mvua *(Dry Farming)* ambako kilimo chake huanza mwezi wa sita mpaka wa nane, huo ndiyo wakati ambao wanaanza kupanda mahindi.

Kanda ya Chini, Kata zote zilizobaki Tarafa ya Usongwe na maeneo mengine ya Tarafa nilizozitaja hapo juu, kilimo huanza kama kawaida.

Mheshimwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie upya namna ambavyo mbolea au pembejeo zinaweza kuwahi kwa wakulima hawa wanaoanza kupanda mahindi mwezi wa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuwapatia mbolea Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Muumba Mbingu na Nchi, kwa kuendelea kunipa pumzi kwa kipindi chote nilipokuwa hapa Bungeni. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa Hotuba pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa namna mnavyohimiza Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo tunalo hapa nchini ni soko kwa ajili ya mazao yetu. Wananchi wanajitahidi sana kulima kwa kufuata kanuni za kilimo katika Jimbo langu la Tarime, mazao kama mahindi, ulezi, mtama na ndizi bila kusahau zao la kahawa ambalo bei zake huwa ni za chini sana. Ni kweli kwamba, tunaweza tukawa na Kilimo Kwanza na wananchi kwa bidii zao binafsi wakalima na kupata mavuno ya kutosha, lakini sehemu ya kuuza (soko) inakuwa shida; na pale wananchi wanapoamua kutafuta soko la kuuza nchi jirani ya Kenya, Serikali huzuia wananchi ambapo huleta kero kwa wananchi. Naishauri Serikali iwe na maghala ya kuhifadhia chakula, ambapo Serikali itakuwa inatoa bei nzuri kwa wakulima. Vile vile Serikali iwatafutie soko la kuuza kahawa Wananchi wa Tarime ili wapate bei nzuri kuliko kupata bei ya chini kutoka kwa wanunuzi binafsi ambao hutoa bei za chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kadiri inavyoendelea kutoa vocha kwa wakulima ili kilimo kiwe cha tija ili mkulima aweze kunufaika. Tatizo kubwa ni utaratibu wa kugawa vocha. Zoezi la kugawa vocha karibu nchi nzima halikufanyika vizuri; Watumishi wa Halmashauri pamoja na wafanyabiashara wanatumia vocha hizo kwa manufaa yao, ambapo wakulima hawakuweza kupata vocha licha ya kwamba, vocha zilikuwa chache sana kulinganisha na idadi kubwa ya wakulima. Naishauri Serikali itoe vocha za kutosha kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kuajiri wagani wa kutosha na kuwapeleka vijijini kwa wakulima ili waweze kutoa elimu ya kanuni bora za kilimo, kuna baadhi ya wataalamu ambao hawawajibiki kwa wakulima. Kazi ambazo zinafanywa na wataalamu hao ni kufanya biashara zao binafsi wala hata hawana mashamba ya mfano. Ni kweli kwamba, wamesoma na kuhitimu kama mabwana/mabibi shamba lakini wao wenyewe hawapendi kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo chetu kiwe cha tija ni lazima tuwe na watafiti wa kutosha na Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya tafiti mbalimbali kwa mazao ili wakulima waweze kupata mazao mengi kwa eneo dogo la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Tarime, wakulima wengi wamekuwa wanatumia mbegu za mahindi kutoka Kenya ambazo mavuno yake ni mazuri

kulinganisha na mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Naishauri Serikali ihakikishe kuwa tafiti za mbegu mbalimbali za mazao ziwe sahihi ambazo zinatoa mavuno mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za matreka ni za juu sana na bei zinatofautiana kutoka Halmashauri moja hadi nyingine; ni kwa nini bei huwa tofauti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu kama Benki ya Wakulima imeanzishwa na kama ipo au itakuwepo; napenda nifahamu kama wakulima wataweza kukopa kutoka kwenye Benki hiyo? Benki mara nyingi zina masharti magumu ambayo mkulima hawezi kuwa na sifa za kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali masomo ya kilimo na mifugo yafundishwe katika shule zote za sekondari ili baadaye tupate wakulima wasomi, ambao watalima kwa utaalamu zaidi. Lazima nchi iwe na wakulima wasomi kuliko kuwa na wakulima ambao siyo wasomi. Baada ya hao wanafunzi kumaliza elimu yao ya sekondari, Serikali iwape mkopo kwa ajili ya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe elimu ya mazao ya bustani (nyanya, vitunguu na viazi mviringo), ambayo ni ya muda mfupi na yana faida kubwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii. Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Kwa kuwa Kilimo Kwanza ni Mkakati unaotegemewa Kitaifa kubadilisha maisha ya Watanzania na kuleta maendeleo; na kwa kuwa wanawake vijijini ni wazalishaji wakuu na ndiyo waathairika wakuu wa umaskini; je, Serikali/Wizara ina mpango gani juu ya kuhakikisha kuwa wanawake vijijini wanapatiwa ardhi yao wenyewe angalau eka moja kwa ajili ya kuendeleza na kuinua kipato chao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawajengea kujiamini na kujiona kuwa wanathaminiwa na nchi yao pamoja na Serikali yao hasa katika kipindi hiki tunapoelekea kwenye uchaguzi ikizingatiwa kuwa wanawake ni wapiga kura wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo na wananchi zaidi ya asilimia 80 wanaitumia Sekta hii katika kujikimu na kujipatia kipato. Hivyo basi, lazima elimu ya kutosha itolewe juu ya jinsi ya kuondokana na kilimo cha kutumia jembe la mkono na badala yake wawezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana bora za kilimo, pembejeo na urahisi wa kupatikana miche bora na mbolea ya kutosha, pamoja na utafiti wa ardhi utawezesha kutoa tija ya kutosha, hivyo uzalishaji utaongezeka kuondokana na uhaba wa chakula

nchini. Wagani na watafiti waendelee kufanya majukumu yao ipasavyo, kuwasaidia wakulima katika shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji ni kilimo bora ambacho hutoa tija zaidi; hivyo, ipo haja rasmi ya kujielekeza zaidi katika kilimo hicho, kwani wakulima huathirika zaidi pale kiangazi kinapokuwa kikubwa na ukame kutokea na kuondolea tija wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ile mikoa ambayo mvua imekuwa ni tatizo kubwa, ipo haja ya kuwekeza kwenye kilimo cha mazao yanayostahimili ukame kama muhogo na mtama. Kwa ile ambayo mvua inanyesha mara kwa mara, Serikali iwekeze zaidi kuwapatia pembejeo stahili ili izalishe zaidi na zaidi ili kuondokana na tatizo la chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imejaliwa sana kuwa na matunda ya kila aina, lakini hupotea ovyo ovyo kutokana na kutokuwa na viwanda vya usindikaji, jambo ambalo wakulima hupoteza mapato makubwa. Ipo haja sasa ya kuanzisha viwanda vya usindikaji ili wakulima wapate kipato waweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tumbaku ni Zao la Biashara na huiingizia Serikali kipato kikubwa, lakini zao hilo lina hasara kubwa kwa ardhi na lina madhara makubwa kwa afya ya binadamu; hivyo, Serikali lazima iangalie upya kilimo hiki na mbadala upatikane ili kuondoa athari kwa wananchi lakini na tija kwa Serikali. Ahsante.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Hotuba ni nzuri na inajitosheleza. Kazi nzuri ya kukiendeleza kilimo. Malengo yaliyowekwa yanatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naitakia Wizara kazi njema na utekelezaji wa malengo mazuri kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti nzuri, inayolenga kuboresha maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuandaa hotuba nzuri. Zaidi, naipongeza Wizara nzima kwa utendaji mzuri na mafanikio makubwa waliyoyapata katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tumeshuhudia katika miaka hii mitano (2005/2006 – 2009/2010).

Bajeti ya Sekta ya Kilimo imeongezeka kutoka 5.78% - 7.2% ya Bajeti yote ya Serikali. Napendekeza kuwa, kiasi hiki bado ni kidogo, inabidi Bajeti iongezwe ili iendane na majukumu makubwa yaliyobebwa na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza.

Naipongeza Serikali kwa utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo. Ili kupanua kilimo na kutumia zana bora za kilimo, inabidi kuwe na mikopo mikubwa na ya muda mrefu na hii itashawishi watu na wadau wengi kuwekeza kwenye kilimo. Hivi hiyo Benki ya Kilimo ambayo ni tegemeo la wakulima wadogo na wakubwa itaanzishwa lini?

Kama hatua ya kukabiliana na athari za mtikisiko wa uchumi duniani, Serikali ilitoa fedha ili kuinusuru Sekta ya Kilimo, Mashirika, Vyama vya Ushirika na Makampuni yaliyohusika kununua na kuuza mazao kama pamba, kahawa na maua. Ili kufiia wafanyabiashara wa kahawa nchi nzima ni shilingi bilioni 9.9 tu zilitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni mengi Mkoani Kagera walileta maombi ili wapatiwe fidia, hadi leo wengi hawajapata na wala hawakupewa hata jibu la kuelezwa kwa nini hawakupewa fursa hii. Je; ni makampuni mangapi yaliomba; mangapi yalipata; na kwa nini mengine hayakupata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuhamasisha na kuanzisha SACCOS nyingi kiasi kwamba katika kipindi cha miaka mitano, wanachama ndani ya SACCOS hizi wameongezeka kwa asilimia 213.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaji ya SACCOS hizi imeongezeka kwa asilimia 127.5. SACCOS zinasaidia watu wengi lakini wanachama wengine wamepata matatizo, kwani wamekopa na wakashindwa kurejesha. Hii inasababishwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana elimu sahihi ya mikopo na ujasiriamali. Serikali iliahidi kutoa elimu hii; je, ni lini itaanza kutolewa kwa Wanachama wa SACCOS na kwa Uongozi wa SACCOS?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu rahisi kinachoweza kuwaondolea umaskini Watanzania walio wengi ni kilimo. Serikali imeainisha kilimo kama kipaumbele cha Serikali namba moja na kuonesha dhamira hiyo kwa kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Hivi leo hii nikienda vijijini huko Kagera na mikoa mingine ni kitu gani nitakiona kilicho tofauti kinachoakisi Kilimo Kwanza? Mbona mimi naona *Business as usual?* Nashauri Kilimo Kwanza izinduliwe kwa mapana, tuone watu wanaelimishwa kwa wingi, mashamba darasa mengi, matrekta mengi, kuhamasisha watu wabadilishe *mind set*, hapo Kilimo Kwanza tutajua imeanza tena kwa nguvu. Je, Serikali ina mpango gani wa uhamasishaji na uwezeshaji ili Kilimo Kwanza kianze kwa nguvu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa MKUKUTA *Cluster* I, ililengwa 2000 – 2005 kilimo kifikie 10% lakini kwa bahati mbaya nchi yetu ina mipango mingi lakini utekelezaji ni mdogo. Hivyo lengo halikufikiwa badala yake kilimo kilikuwa kwa 4.4% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia malengo ya Ilani ya CCM iliahidi (2005 – 2010) kilimo kitakuwa kwa 20%. Aibu ni kwamba hakikifia hata asilimia tano. Badala yake kimefifkia 3.9% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha tunajikita kwenye kauli mbiu tumesahau utekelezaji. Kauli mbiu ni nyingi sana zikiwemo zile za kilimo ni uti wa mgongo, siasa ni kilimo na zingine nyingi ikiwemo hii ya sasa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kilimo kimepewa kipaumbele lakini bajeti yake ya maendeleo ni ndogo ni Sh.103,952,371,000. Pesa za nje Sh. 100,535,662,000 na pesa za ndani 3,416,709,000. Je, ni kweli mafanikio ya kilimo yatapatikana kwa kutegemea pesa za nje kwa zaidi ya 80%? Ni dhahiri mafanikio yatakuwa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu ni ya wakulima kwa asilimia 80% maana yake ni kwamba kwa kushindwa kufikia malengo ya MKUKUTA na yale ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi maana yake Serikali ya Chama cha Mapinduzi imezidisha umasikini wa mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumkomboa mkulima ambapo kwa ujumla wake ni 80% ya Watanzania, ili ajira hiyo imnufaishe mkulima na iweze kuwavutia vijana pia ambao wameshuhudia babu zao, baba zao karne na karne wakitumia jembe la mkono soko la mazao hakuna hivyo kukata tamaa na kukimbilia mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhu ya tatizo hili la kilimo kudorora ni kufuata ushauri ufuatao:-

- Uboreshaji wa uzalishaji katika sekta ya kilimo;

- Kuwepo na utaratibu wa kutoa mikopo kwa wakulima wa kati na wale wadogo;

- Uwekwe utaratibu wa usindikaji wa mazao hapa hapa nchini na kuacha kuuza mali ghafi;

- Miundo mbinu ya barabara vijijini itengenezwe ili bidhaa zifike sokoni.

- Miundombinu ya reli nayo iboreshwe ili mazao ya biashara na chakula yasafirishwe kirahisi ili barabara zetu zisiharibike;

- Umeme ufike vijijini ili kuwe na uwezekano wa kuwa na viwanda vidogo vidogo ili iwe rahisi kufanya *processing* ya mazao kabla ya kufikisha sokoni, mfano kubangua korosho na kadhalika;

- Maafisa Ugani wasomeshwe kwa wingi na wapatiwe vitendea kazi na Serikali ihakikishe wapo mashambani;

- Nchi isitegemee kilimo cha mvua peke yake, bali umwagiliaji uzingatiwe; na
- Serikali itueleze lini itatekeleza ahadi yake ya kufikia hekta milioni moja kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyosema ya (2005 – 2010)? Maana sasa

hekta za umwagiliaji ni 331,490. Imeshindwa hata kufikia nusu, yaani 2010, bado 668,510? Hii ni aibu hebu tuache maneno tutekeleze.

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya Wizara na Taasisi zake kwa hotuba nzuri sana na kazi nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la faraja kubwa sana kwamba pamekuwepo maendeleo na ukuaji takribani katika maeneo yote isipokuwa chai, mkonge na kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa zana za kilimo naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutumia matrekta makubwa na madogo. Hata hivyo, kuna umuhimu na kuweka taratibu nzuri za kuagiza na kuweka bei stahiki kwa matrekta, hasa madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulitunga Sheria ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Hii ilileta matumaini makubwa kwa wananchi lakini inasikitisha kwamba mpaka sasa bodi hiyo haijaanzishwa wala kutolewa mipango katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkazo kuwekwa kwenye maeneo ya jadi Iringa, Mbeya, Sumbawanga na Morogoro, ni vema maeneo mapya yakatupiwa macho chini ya Kilimo kwanza, hususan kwa umwagiliaji. Nafarijika kwamba Wilaya za Lushoto, Korogwe na Muheza zimeanzishwa kuwa miongoni mwa maeneo mapya yatakayofaidika chini ya msukumo huu. Napenda kushawishi Serikali iifikirie Wilaya ya Mkinga kutokana na ukweli kwamba Wilaya hii mpya ya pembezoni ina ardhi yenye rutuba nzuri na mabonde mengi yanayofaa kwa umwagiliaji na hatua nyingine za kuleta mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali kwa kuongeza shughuli za utafiti, mashamba darasa pamoja na kuongeza wageni na wataalam wengine. Naomba kwanza wataalam hawa pamoja na pembejeo zisirundikwe kwenye maeneo yanayopewa kipaumbele na sehemu mpya na za pembezoni zikakosa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana uamuzi wa kutoa fursa zaidi kwa wananchi kuuza mazao yao katika soko huria bila vikwazo kama ambavyo imekuwa mpaka sasa. Kwa msingi huu nashauri vizuizi vyote visivyo vya lazima viondolewe. Aidha, uimarishaji wa ushirika, mfumo wa stakabadhi ghalani, uwekezaji wa viwanda vya kusindika na kuongeza uwezo wa ghala ya Taifa (*SGR*) ukiimarishwa utasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote kwa kutuletea hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Wilaya ya Hai naishukuru sana Serikali kwa kutusaidia chakula cha msaada wakati tulipokumbwa na njaa. Pia tunaishukuru Serikali kwa kutupatia mbolea na mbegu za ruzuku ambazo zimesaidia kwa kiasi kikubwa, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hotuba hii katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu zana za kilimo. Hiki kilimo kwanza ili kiweze kufanikiwa tunahitaji tuwe na zana bora zaidi lakini bei zake ziwe na uhalisia kwa mfano *Power tiller* zinalanguliwa sana na hivyo kuzifanya kuwa ndoto kwa wakulima wadogo kuzinunua, ukweli wa bei zake unafahamika, *homework* ni kidogo na ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu mbolea, ni kwanini hadi hivi sasa bado hatujaanza kuzalisha mbolea hapa nchini wakati uwezekano upo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nizungumzie suala la mbegu. Nazidi kusisitiza umuhimu wa kuzalisha mbegu hapa nchini katika maeneo mbalimbali tuliyonayo hapa nchini mfano, katika mashamba ya Vyuo vya Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni, sumu au madawa ya mimea yanahitajika sana lakini ikiwezekana yazalishwe hapa hapa nchini ili kuepuka utapeli wa sumu au madawa yaliyo-*expire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni kuhusu kahawa. Naishukuru Serikali kupitia *TACRI* kwa jitihada zinazoendelea lakini nashauri bado elimu kwa wananchi inahitajika kuhusu miche mipya pamoja na uzalishaji wa miche kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali machache ambayo naomba majibu yake.

(a) Kama kweli tunataka kuwainua wakulima wetu ni kwa nini tunaendelea kuwazuia kuuza mazao yao nje ili hali gharama za uzalishaji ziko juu sana?

(b) Bodi ya Mazao Mchanganyiko ni lini itaanza kufanya kazi?

(c) Benki ya Kilimo; ni kwa nini hadi hivi sasa haijaanza?

(d) Ni hatua gani zimechukuliwa au zitachukuliwa ili kuwashawishi wakulima wakubwa kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza mchango wangu kwa kumshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi

wote wa Wizara kuweza kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza. Wakulima nchini wanafaidika na pembejeo zilizopatikana mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wananchi wa Wilaya ya Longido wanawashukuru sana Serikali kwa kuwapa chakula cha njaa wakati wa ukame 2009/2010. Wameona kwamba Serikali iko pamoja nao hasa wakati wa shida. Watu wangekufa sana, wanasema ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ukame wananchi wamekuwa maskini sana hawana chakula, wafugaji nao hawana mifugo imekufa kwa kiangazi. Ukame huo umesababisha njaa kuendelea kuwepo mpaka sasa. Ombi langu ni Serikali kufanya utafiti kuona kiasi cha watu ambao bado wana njaa na waweze kupatiwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kina ratiba yake ambayo huwezi kukwepa muda wa kuotesha, kupalilia hata kuweka mbolea. Kwa hiyo, Serikali izingatie wakati wa kuleta mbolea pamoja na pembejeo, mbolea iletwe kwa wakati bila kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jimbo langu la Longido kuna maeneo ya wafugaji, ambao hawalimi na maeneo ya wakuli. Napenda kueleza kwamba maeneo hayo serikali iwapatie pembejeo kuliko kuacha jimbo zima kwamba hakuna wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Nyanda za Juu ambayo Serikali inapeleka nguvu kubwa sana, kupeleka pembejeo ili walime chakula kinachotosheleza kulisha nchi nzima. Naomba ikumbukwe kwamba Mikoa ya Kusini bado ni mbali kupelekewa chakula au mbolea toka Songea hadi Arusha au Longido huko kaskazini. Kwa hiyo ni afadhali kuweka baadhi ya Mkoa wa Arusha kwenye Mikoa ya Ghala la Taifa kwani ni vigumu kusafirisha chakula toka Kusini mpaka Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi, naomba wakulima wadogo wadogo ambao hawana uwezo mkubwa wa kununua matrekta wapewe majembe ya kukokotwa na wanyama (maksai). Bado wakulima wadogo wadogo wapewe mikopo kwa ajili ya kununua hayo majembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hotuba ya Waziri.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja nataka kupata majibu mahususi ya hoja zifuatazo:-

(1) Shamba la mbegu la Bugaga – sasa chini *ya Tanzania Seed Agency (ASA),* nini kinafanyika 2010/2011 kama vile mikakati ya kupima eneo, kukarabati nyumba za wafanyakazi, vifaa/vitendea kazi, na kadhalika kuanza kazi ya utafiti.

(2) Chuo cha kilimo cha Mbondo, kilichopo Kasulu. Mheshimiwa Waziri Wasira alifika pale, *What is happening* kwa 2010/2011?

Ruzuku ya mbegu au mbolea kwa wakulima nchini. Pamoja na kazi nzuri ya kusambaza pembejeo hizo muhimu kwa kilimo. Ningependa kushauri (*strongly*) yafuatayo:-

(i) Sera hii tuifanyie marekebisho ili pia tuweke dirisha la kutoa mikopo ya pembejeo hizo kwa wakulima wetu wengi waliopo vijijini ambao ni kati ya 80 – 85%. Mikopo hiyo inaweza kupitia kwenye *SACCOS/CBO* zao na baadaye wakati wa mavuno basi *SACCOS* hizo zikalipia gharama zilizotolewa kwa mbegu au mbolea. Hii itasaidia sana kufikisha huduma hii muhimu na kurekebisha ujanja unaofanywa na Mawakala.

(ii) Yaliyotokea Mkoani Rukwa kuhusu pembejeo ya wizi au upotevu wa pembejeo yenye thamani ya Tsh.55.5 bilioni, ni fundisho tosha kwa Wizara na nchi. Ni dhahiri mikoa mingine ikiwemo Kigoma umekuwepo upotevu wa raslimali hii muhimu kupitia watendaji wasio na maadili na Mawakala.

(iii) Upo ushahidi kwamba wakati wa kilimo wakulima wengi wanakuwa hawana pesa (papo kwa papo) za kulipia mbolea au mbegu inapoletwa vijijini na Mawakala.

(a) Skimu ya umwagiliaji ya Rungwe Mpya – Kafulu.

(b) Skimu ya umwagiliaji - Titye.

(c) Skimu ya umwagiliaji - Msambara.

Naishauri mpango wa *JICA – page* 46 ishirikishe pia skimu zilizobaki (b – c). Aidha, chini ya *Irrigation Cooperatives,* Wizara isaidie Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ili kuzifanya *cooperatives* hizi zifanye kazi vizuri, mambo yafuatayo yanaweza kufanywa na Wizara au Halmashauri:-

(1) Mafunzo;

(2) Kujenga uwezo/vifaa vya kutendea kazi vyombo vya usafiri;

(3) Upatikanaji mbegu; na

(4) Huduma mahsusi za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Cooperative Development (Coop reforms)*:-

(1) Kwa nini hakuna kabisa fedha ya *development* 2010/2011.

(2) Wizara ya Kilimo iandae programu maalum na *MUCCOBS,* Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi katika hii *reform*. *MUCCOBS* ni *Authority* katika ushirika. Wizara ya Kilimo au TAMISEMI na hata Mifugo shirikianeni na *MUCCOBS to develop different progams*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Kilimo – *Mechanization Centres*. Nashauri sana Wizara kupitia Halmashauri ya Wilaya kusimamia sana vituo hivi vya kilimo, sioni unavyoweza kuzungumza *Mechanization* ya kilimo bila kusimamia vituo hivi na hatua kwa hatua, wakulima wetu vijijini wabadilike kutumia wanyama kazi, *power tillers* na trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila *centres* hizi *power tillers* zote zitasimama kwa marekebisho madogo madogo, *services* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kasulu tunazo *mechanization centres* kule, Mnzye, Kasulu Mjini, Nyenge na Makere, tusaidieni Halmashauri ya Wilaya, tuimarishe vituo hivi. Kwa kupata wataalam na mafunzo kwa vijana ili vituo hivi viwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amegusia suala zima la umuhimu wa utafiti katika kuleta maendeleo ya kilimo nchini. Ni dhahiri kwamba pasi na shughuli za utafiti kupewa kipaumbele inavyostahili hatutaweza kabisa kumkomboa mkulima wa kijijini, yule ambaye anatumia jembe la mkono, asiyefahamu jinsi ya utumiaji wa mbolea na namna ya uvunaji bora na uhifadhi wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya watafiti wengi wanaelekeza tafiti zao kwa kuongeza haiba ya kielimu (*academic performance*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawaelekezi tafiti zao kwa lengo la kumtatulia mkulima matatizo yake ya shambani. Ni ukweli usiopingika kwamba tafiti ni ghali mno kwa sababu zinatumia fedha nyingi pasi na kuiona faida ya moja kwa moja zitokanazo na tafiti hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo linaathiri shughuli za utafiti nchini ni kutokuwa na muunganiko wa Watafiti kutoka taasisi mbalimbali hapa nchini hali inayopelekea tafiti nyingi kurudiwarudiwa na hivyo kuigharimu sana Serikali pasi na kuleta tija inayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani umefika wakati kwa Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Lazima pawepo na mkakati wa makusudi kuweka taasisi moja tu hapa nchini ambayo itakuwa inaratibu na kusimamia tafiti zote zinazofanyika hapa nchini. Kwa kufanya hivyo tutaepusha kufanya tafiti ambazo hazina tija, kuratibu gharama za tafiti hizo. Lakini pia kuona kwamba tafiti zinazofanywa zimeelekezwa kutatua matatizo mbalimbali ya wananchi.

(b) Serikali itenge fedha za kutosha kugharimia tafiti kwa kuzingatia kwamba utafiti ni ghali sana na fedha nyingi zinahitajika. Kwa kufanya hivyo ni dhahiri kwamba watafiti wengi watavutiwa katika kufanya tafiti ambazo zina faida kwa nchi.

(c) Kuhakikisha kwamba matokeo ya tafiti zinazofanywa yanawafikia wakulima kule waliko. Maana yake ni kwamba sambamba na kuimarisha shughuli za utafiti basi pia shughuli za ugani nazo zinaimarishwa ili kwa pamoja waweze kuleta mapinduzi ya kilimo nchini.

(d) Maslahi ya Watafiti pamoja na Maafisa Ugani yaboreshwe ili iwe ni motisha kwao kuongeza juhudi ambazo hatimaye mkulima naye afaidike.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba kilimo kinaajiri karibu asilimia themanini ya Watanzania na takribani wengi wanaishi vijijini. Aidha, kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dhana nzima ya kuendeleza kilimo tumekuwa na kauli mbiu mbalimbali ambazo zimekuwa zinaletwa kwa nia ya kuimarisha kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na kauli mbiu ya siasa ni kilimo, chakula ni uhai na nyingi nyinginezo na sasa tuna kauli mbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na madhumuni ya kauli mbiu hizi ni kuleta mapinduzi ya kilimo ili tuweze kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara. Nchi hii ilitakiwa tujitosheleze kwa chakula na ziada kuuzwa katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika mazao ya biashara yaweze kulisha viwanda vya ndani. Kwa bahati mbaya malengo haya hadi hii leo hayajafanikiwa ipasavyo. Je, tumejikwaa wapi, nini tatizo letu. Nahitaji maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kupewa maelezo ni kwa kiasi gani kauli mbiu hizi zinazoletwa tangu tupate uhuru zinaoanishwa kwa manufaa ya mkulima. Kama hili halifanyiki basi tutakuwa na kauli mbiu za kila aina na za kila rangi lakini zitashindwa kutatua matatizo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima pamoja na kwamba wana vifaa duni vya kilimo na uchache wa mbolea lakini baadhi ya wakati wanazalisha ziada ya mavuno. Lakini kwa bahati mbaya kumekuwa na vikwazo kadhaa vinavyowanyima haki yao wakulima kuuza ziada ya mazao yao, jambo ambalo linawanyima fedha kwa ajili ya shughuli zao za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si busara hata kidogo kumlazimisha mkulima kuuza mazao yake mahali ambapo bei ni ndogo ilihali kuna sehemu ambapo akiuza mazao yake atapata bei nzuri itakayomwezesha kupata fedha za kutosha kugharimia shughuli zake za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iache kuwazuia wakulima kuuza mazao yao ya ziada sehemu ambayo mkulima anaamini atapata bei nzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Basil Mramba. Sasa muda haupo upande wetu kabisa, naomba nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Chakula na Ushirika, Dr. Mathayo David Mathayo. Mheshimiwa karibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah-wa-taallah* ambaye amenijalia uzima pamoja na afya njema na hivi sasa namaliza mwaka wangu wa tano kama Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini kunipa nafasi hii na napenda kumjulisha kwamba sasa ndio nimepata uzoefu mzuri zaidi.

Tatu, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa miongozo yake ya kila siku na Waziri wangu, Mheshimiwa Stephen Wasira. Kusema kweli amekuwa kioo changu cha kila siku. Nakushukuru sana Mzee Wasira, nimejifunza mengi kutoka kwako tena mengi mazuri kwa sababu wewe ni mcha Mungu, kwa hiyo, nimejifunza mengi sana kutoka kwako. Mwenyezi Mungu akuendeleze hivyo hivyo na uwe na nguvu hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa mimi na Waziri wangu tangu twende kufanya kazi katika Wizara hii. Lakini nisiwasahau waandishi wa habari ambao wamekuwa wanaandika habari nzuri kuhusiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kuelimisha umma kuhusiana na masuala mbalimbali ya kilimo.

Napenda kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Same Magharibi, kwa miaka mitano nimejaribu kuwatoa miiba mingi sana, kwa hiyo, nina imani hata wao watanitoa mwiba mwaka huu ili tuweze kuendelea kuwatelea maendeleo zaidi na ninaamini kabisa kwamba nitawaletea maendeleo zaidi na ninaamini kabisa kwamba nitawasaidia zaidi na zaidi kwa sababu sasa ndio nimepata uzoefu zaidi. Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu kwa sababu imekuwa inanipa *support* muda wote hasa nikiwa nje ya nyumba kwa maana ya kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nichangie hoja hii kama ifuatavyo:- Kwanza, niseme naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Orodha ile ya wachangiaji wote itasomwa na Mheshimiwa Waziri lakini mimi kwa kuwa nitakuwa najibu baadhi ama nachangia baadhi ya hoja, basi nitakuwa nawataja wale ambao wametoa hoja zao. Mheshimiwa Shally Raymond ameuliza kwamba sheria ya Tume ya Ushirika itapitishwa lini na Bunge?

Niseme kwamba itapitishwa Bunge lijalo na kwa bahati nzuri mwaka huu tumeshatenga fedha kwa ajili ya Tume na itafanya kazi zote zile, itasimamia kazi za ushirika ikiwa ni pamoja na ufufuaji wa ushirika, kurekebisha uongozi, kuhamasisha hata ushirika kwa akina mama ili akina mama waweze kujikomboa. Kwa hiyo, kazi zote hizi zitafanywa na Tume hii ni shilingi bilioni sita zimeshatengwa kwa ajili ya Tume ya ushirika.

Mheshimiwa Harrison Mwakyembe nimpongeze pia kwa shughuli yake nzuri, kazi yake nzuri anayoifanya kufuatilia masuala ya kilimo na sekta nyingine katika Jimbo lake, lakini napenda kusema kwamba katika *SACCOS* yake ya Kimbalu, mwaka 2005 iliomba mkopo *NMB* lakini kwa bahati mbaya masharti yale kidogo yalikuwa ni magumu kidogo.

Kwa hiyo, wakashindwa kupata mkopo ule kutokana na masharti, lakini Wizara itafuatilia suala hili ili tuweze kuangalia ni vipi *SACCOS* hii inaweza ikasaidika ili wananchi wale waweze kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mathias Chikawe amezungumzia kwamba Afisa Ushirika wetu aliyeko Nanchingwea anakuwa mgumu na wakati mwingine anakuwa haandikishi vyama vipya vya ushirika, napenda kusema kwamba Wizara itafuatilia suala hili na kuangalia kwamba wakati mwingine tutakumbushana majukumu ya kazi, lakini kama wananchi ndio ambao hawajatimiza masharti, basi wataomba watimize masharti kusudi waweze kuandikishwa kama vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Zambi pia amezungumzia masoko ya mazao na akashauri kwamba kuwe na vituo vya kutosha katika ununuzi na tunapenda kumjulisha tu kwamba wakala wa hifadhi ya Taifa pamoja na kwamba ina vituo vikubwa vya ununuzi wa mahindi, lakini bado itakuwa na vituo vidogo vidogo ikiwemo kile cha Mbozi kusudi waweze kununua mahindi ya kutosha wakati wa mavuno. Lakini pia tunahamasisha stakabadhi za mazao katika maghala ili kuweza kuwapatia masoko yenye bei nzuri wakulima wetu wanapovuna kwa kiasi kikubwa.

Serikali pia imeanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Najua Dr. Mpanda amelizungumzia hili kwamba kila anavyochangia kwenye Wizara ya Kilimo amekuwa analizungumzia suala hili la Bodi ya Mazao Mchanganyiko lakini nimhakikishie kwamba Bodi hii tayari tumeshateua Mtendaji Mkuu na wafanyakazi/watendaji wengi wadogo wadogo wanaajiriwa ili tuweze kuanza ile kazi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Kidawa Amedi Saleh ambaye ni Makamu Mwenyekiti pia wa Kamati ya Kilimo na Mifugo na Maji amesema kuna idadi ndogo. Suala hili pia limezungumziwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila kwamba kuna idadi ndogo ya maofisa ushirika ikilinganishwa na idadi ya Vyama vya Ushirika. Ni kweli lakini na sisi kama Wizara, kwa kweli tunawahimiza mamlaka inayohusika ambayo ni Halmashauri za Wilaya, Miji na Vijiji pamoja na Manispaa ili waweze kuendelea kuwaajiri maofisa ushirika angalau basi waweze kufikia kiwango ambacho kazi inaweza ikafanyika kwa tija.

Mheshimiwa Nsanzungwanko, amezungumzia kuanzisha programu ya kuendeleza ushirika kwa kushirikiana na *MUCOPS*, lakini napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa kwamba katika ile programu yetu ya ku-*modernize* ushirika inatekelezwa na wadau wengi kikiwemo Chuo Kikuu cha Ushirika na Masuala ya Biashara. Kwa hiyo, *MUCOPS* na yenyewe imejikita kweli kweli katika kuhamasisha ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakulima wa vijijini kuwezeshwa kupata mikopo ya pembejeo, wakulima hawa kupitia *SACCOS* amezungumza kupitia *SACCOS*. Niseme kwamba Kamati zile za Wilaya ambazo ndio kweli zinajua hizi *SACCOS* kwenye ngazi za Wilaya, basi hizi zinaweza zikateua *SACCOS* ambazo zina sifa, kwa maana ya kuwa na uongozi madhubuti, kuwa na kuweka *records* za vitabu vizuri na mahesabu yao na ziwe zimekaguliwa vizuri. Kwa hiyo, zile Kamati za Wilaya zinaweza zikateua baadhi ya *SACCOS* kwa ajili ya kupatiwa mikopo ya pembejeo. Hilo linakubalika kabisa.

Mheshimiwa Diana Chilolo ameomba kwamba Serikali itoe maelezo kwa kila Wilaya kuandaa vyama vya ushirika ili waweze kupata misaada au mikopo. Nadhani ni suala la kuhamasisha ushirika, kusema kweli ndio kazi tunayoifanya hiyo kuhamasisha vyama vya ushirika viundwe vipya, lakini wanachama pia waongezeke kwa vile ambavyo vimeundwa kusudi waweze kupata mitaji mikubwa na waweze kupata mikopo mbalimbali.

Mheshimiwa Emmanuel Luhahula - Mbunge wa Bukombe, amezungumzia suala la Serikali kwamba iweke utaratibu mzuri wa kununua mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika. Hili suala tunalihamasisha kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Diana Chilolo na ili kuweza kuimarisha ushirika, kusema kweli watatusaidia na hii *Cooperative Reforms And Modernization Program* inatusaidia sana na inazingatia uimarishaji wa vyama vya ushirika hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sigonda ameshukuru Serikali kulipa madeni ya mwaka 1995 kwa wakulima wa pamba Jimbo la Songwe. Kusema kweli hii ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama mnavyojua kwamba ni Serikali sikivu na ambayo inatekeleza ahadi zake kwa hiyo, ndio maana tukafanya hivyo.

Kuhusu Serikali kuwapatia soko la ufuta wakulima wa Jimbo la Songwe, tunashauri vyama vya ushirika wa ufuta vianzishwe kusudi viweze kufanya kazi hii kwa uzuri zaidi kwa sababu watakuwa wanafahamiana na watakuwa na *bargaining power* kama chama cha ushirika.

Mheshimiwa Kayombo - Mbunge wa Mbinga Mashariki amezungumzia wakulima MBICU kulipwa fidia. Kusema kweli kwa sasa Serikali mapitio ya awali ya

uhalali wa fidia umeshafanyika na kinachosubiriwa sasa hivi ni uhakiki wa Serikali ili mchakato wa kuomba fedha Serikalini ufanyike.

Pia Mheshimiwa Kayombo amezungumzia suala la Mbinga, kwa nini ofisi ya Bodi ya kahawa isiwe kule Mbinga? Nadhani ushauri huu tumeuchukua tutaufanyia tathmini kwamba ni kipi ambacho kitaleta manufaa zaidi kwa mkulima wa kahawa.

Lakini niseme tu kwamba kuna wataalam tayari ili kuongeza ufanisi wameshateuliwa wawili ambao wanakwenda kwa kila Halmashauri za kahawa ambao watakuwa wanawakilisha Bodi ya kahawa. Kwa hiyo, suala lake hilo tutaliangalia kwa umakini lakini pia ajue kwamba kuna wataalam hao katika ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufufuaji wa *MBIFACU* na kupatiwa wajumbe wawili, maandalizi ya kupata majina ya wajumbe watakaoteuliwa yanafanyika na suala la kupata wataalam wawili litafanyiwa kazi kama Mheshimiwa Mbunge alivyoomba na hasa hili litafanyika baada ya bajeti.

Mheshimiwa Bernadeta Mshashu amezungumzia kukosekana kwa elimu sahihi ya mikopo na ujasiriamali, kumesababisha mikopo ya *SACCOS* kutorejeshwa, Serikali iliahidi kutoa elimu hiyo, lini itaanza? Anauliza.

Ningependa kumjibu hapa Mheshimiwa Mshashu kwamba Serikali kwa kupitia *MUCOPS* imeshaanza kutoa mafunzo lakini mahitaji ya mafunzo haya ni makubwa sana, kwa hiyo, tutayafanya kwa awamu.

Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi amezungumzia kwamba Wizara iliahidi kuhusisha Wilaya ya Ludewa kuanda *Agricultural Land Use Plan* na anauliza hii haikufanyika na je, matokeo yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilikutana na uongozi wa Wilaya chini ya uongozi wa *DC* akiwemo *DED* na wataalam wake ikakubaliana utekelezaji utaanza mwaka huu wa fedha katika vijiji vya Nkomang’ombe, Kemelembe na Lifua. Kwa hiyo, suala hilo tayari limeshachukuliwa vizuri kabisa, asiwe na wasiwasi, kazi hiyo itafanyika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Shally Raymond suala lake la Tume nadhani nimeshalipatia majibu.

Mheshimiwa Daniel Nsanzungwanko ameuliza, kuna mpango gani wa kufufua chuo cha kilimo cha Mubondo? Mheshimiwa Daniel Nsanzungwanko napenda kukufahamisha kwamba mwaka huu tutafanya tathmini ya gharama za ukarabati wa chuo hicho, lakini ukarabati halisi kwa sababu kimekaa muda mrefu bila kutumika kwa kiwango kikubwa, ukarabati huo utafanyika mwaka 2011/2012 kusudi mafunzo yaanze mwaka 2012/2013. Kwa hiyo, suala hilo liko kwenye mipango yetu.

Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime amezungumzia umuhimu wa kutoa mafunzo ya bustani. Napenda kuwafahamisha kwamba Chuo cha Kilimo cha mboga, maua na matunda kilichopo Tenguru - Arusha kinatoa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Said Arfi anasema inachukua muda mrefu sana kutekeleza miradi ya umwagiliaji kutokana na uhaba wa wataalam wa umwagiliaji. Napenda kumfahamisha kwamba Chuo chetu kile cha Kilimo cha Igulusi, kwa sasa kinaandaliwa kusudi kiweze kufundisha na kutoa wataalam wa kati wa kazi hii ya umwagiliaji na tutaanza na ukarabati pamoja na kuajiri wakufunzi pamoja na kudurufu mitaala kusudi elimu iweze kutolewa vizuri katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua nafasi hii kushukuru tena kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nyingine tena ili niweze kutoa maelezo na majibu kwa baadhi ya hoja. Nimesoma hoja zote ambazo zimefika kwa maandishi, nimesikiliza zilizotolewa kwa kuzungumza, ni nyingi na kwa muda unaonipa pamoja na kusoma majina ya waliosema, mimi naamini muda huu hautoshi kujibu hoja zote.

Kwa hiyo, kabla hata sijaanza nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutazipitia hizi hoja, tutazijibu kwa kutoa kwa maandishi na tutawagawia Wabunge wote ili tuweze kujua na kuwa na *record* sahihi tulisema nini na Serikali inasema nini. Hiyo ndio itakayokuwa mfumo wa kujibu hizi hoja.

Kabla sijaanza kutambua wale ambao wamesema, ningependa na mimi nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini. Nimekuwa Waziri katika Serikali ya Rais Jakaya Kikwete kwa miaka mitano na katika kipindi hicho, amenipa majukumu makubwa na mengi, kwanza kama Waziri wa Maji; pili, nilikuwa Waziri wa kilimo; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa miezi mitatu na baadaye kilimo tena mpaka kufika leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninazo sababu zote za kuamini kwamba Rais alifanya hayo yote kwa imani na mimi. Nasema imani inazaa imani. Namshukuru sana Rais kwa imani yake kwangu. Baada ya shukurani hizo, niseme vile vile nawashukuru wananchi wa Bunda, wakati Rais ameniamini kwa miaka mitano na wao wameniamini kwa miaka mitano, na kwa kweli bila wao, hata Rais asingenijua wala kuniamini.

Kwa hiyo, kwa kweli pongezi za pekee na shukurani nazipeleka kwa wananchi wa Bunda ambao wameendelea kuniamini. Nilikuwa nao siku sio nyingi zilizopita, nimezungumza nao, wamenichangia pesa za kuchukua fomu na wengine wamenizawadia ng'ombe kwa kazi nzuri niliyofanya. Wameshusha sana *pressure* yangu na kunipa matumaini makubwa kwamba naweza kurudi tena katika Bunge lako Tukufu maana watu hawawezi kukupa ng'ombe wao bure bure tu bila sababu. Unajua watu wanapenda ng'ombe wao kweli, mpaka watoe lazima wana sababu.

Baada ya shukurani hizo, sasa niseme kwamba waliochangia kwa kuongea ni Waheshimiwa Wabunge 17 na halafu wamechangia Wabunge 57 kwa maandishi, halafu vile vile kuna Wabunge wanne walizungumzia kilimo chini ya Wizara ya Fedha na maelezo yao tunayo. Vile vile kuna Wabunge 13 walioongelea kilimo chini ya Waziri Mkuu. *Records* zote tunazo, tutaziandika na tutaziwasilisha kwao ili waweze kujua majibu hasa ya Serikali yanasema nini. Sasa kabla sijaendelea, niruhusu niwatambue waliosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Daniel Nsanzungwanko – Mbunge wa Kasulu lakini kabla ya Mheshimiwa Nsanzugwanko alikuwa ameongea Mheshimiwa Ali Khamis Seif – Msemaji wa Upinzani na Mheshimiwa Kidawa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya kilimo, Maji na Mifugo. Halafu yupo Dr. Mahenge – Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Anna Lupembe - Viti Maalum Rukwa na Mheshimiwa Anne Malecela – Mbunge wa Same Mashariki. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ludovick Mwananzila – Mbunge wa Karambo, Mheshimiwa John Cheyo – Mbunge wa Bariadi, Mheshimiwa Esterina Kilasi – Mbunge wa Mbarali, Mheshimiwa Dr. Gwido Sigonda – Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Said – Mbunge wa Mpanda Kati, Mheshimiwa Shally J. Raymond - Viti Maalum, Mheshimiwa Geofrey W. Zambi – Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Gaudence Kayombo – Mbunge wa Mbinga, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe – Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Dr. Mpanda – Mbunge wa Kilwa Kaskazini, Mheshimiwa Lucy Owenya - Viti Maalum na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David – Mbunge wa Same na Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Prof. Sarungi – Mbunge wa Rorya, Mheshimiwa Omar Kwaangw' – Mbunge wa Babati Mjini, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi - Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. James Msekela – Mbunge wa Tabora Kaskazini, Mheshimiwa Lucas Selelii – Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba – Mbunge wa Mikumi, Mheshimiwa Lucy F. Owenya - Viti Maalum na Mheshimiwa Dr. Msabaha – Mbunge wa Kibaha Vijijini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Godfrey W. Zambi tena, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Savelina Mwijage Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa

Mwijage huyo hatoki Kagera. Mheshimiwa Khadija Salum Ali Al-Qassmy, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa na sasa Mwenyekiti wa Bunge.

Pia Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimwa Charles Mwera, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Janet Mbene, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Brigadia Jenerali Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa *Architect* Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, tena aliandika Mbunge wa Kasulu, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mbunge wa Chonga, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Elietta Switi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mbunge wa Kibiti, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum. Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga, Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea, Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Madgalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mbunge wa Kwimba, Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa na Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi akaandika tena mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao ndiyo waliochangia. Kama kuna yeyote ambaye sikumwandika, itakuwa ni bahati mbaya na akinijulisha nitamsema. Baada ya kutambua, sasa ningependa nitumie fursa hii kutoa maelezo kidogo juu ya masuala ambayo yamejitokeza.

Kwanza ningependa nizungumzie masuala ya jumla na vile vile niwaombe Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili na lijalo ili tuweze kusaidiana na Serikali iliyopo sasa na ijayo katika kusimamia masuala yanayohusu kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *ASPD.* Huu ni mpango mkubwa ambao kazi yake kwa kweli ni kusaidia kuelekeza uwekezaji huko vijijini. Mimi nadhani tunaweza kufanikiwa sana, maana chini ya mpango huu fedha zinapelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya. Kwa mwaka huu tumepeleka shilingi bilioni 102 katika Wilaya zote nchini kwa ajili ya kuwekeza katika sekta ya kilimo. Mheshimiwa Basil Mramba atanisamehe nimepitiwa lakini Mheshimiwa Basil Mramba aliongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu tukiusimamia vizuri katika ngazi zote wakulima wetu watafanikiwa sana. Maana kinachokosekana huko vijijini kwa kweli na ambacho kinatufanya mara tunaenda kwenye ruzuku, mara tunaanzisha benki ni kwa sababu hakuna uwekezaji wa kutosha, hakuna dirisha ambalo linamwezesha mkulima wa Tanzania kupata mkopo kwa sasa. Mpango huu unawezesha wakulima, kwa mfano kwenye *power tillers* vikundi vya wakulima vinaweza vikatoa asilimia 20 tu ya thamani ya *power tiller* na vikapata kwa kutumia kulimia, huo ni mpango mzuri sana. Lakini fedha karibu asilimia 75 zinazotolewa kwenda huko kwenye Wilaya zinatakiwa zitumike kwenye umwagiliaji maji na sisi tunasema kwa kweli ukombozi wa nchi yetu utategemea zaidi umwagiliaji maji na huko vijijini wananchi wataelimishwa na wataanzisha miradi ya umwagiliaji maji kwa kutumia fedha hizi, mimi ninaamini ya kwamba matatizo yetu mengi yanayotokana na njaa yatapungua. Lakini ni kweli vile vile kwamba kila jambo jema huwa halikosi matatizo, bado tunayo matatizo ya usimamizi hapa na pale. Bado tuna matatizo ya kuwa na matumizi bila ya kulinganisha na thamani ya mali inayoingia katika miradi ile.

Mimi ningependa kusema katika hotuba yangu nimeeleza kwamba mwaka jana nilisema tupeleke mamlaka kidogo Mkoani tuwe na Ofisa Maalum ambaye anatembelea miradi ile, anatazama na kulinganisha thamani na suala hili lilikubalika na tumeteua Maofisa katika Mikoa yote 20 ya sasa. Hiyo mipya bado, lakini ya sasa ambako kutakuwa na Ofisa ambaye tumempa usafiri, tumwezeshe awe anaweza kutembelea ile miradi ya *DADPs* katika ngazi ya Wilaya na kujiridhisha kwa sababu binadamu tumezoea kuchunguzwa na kuongozwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tukiwa na mtu wa namna ile anafanyakazi, atasaidia sana. Lakini mimi ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kazi yetu ya kusimamia mwenendo na matumizi ya Serikali ni pamoja na kusimamia kazi za namna hiyo katika majimbo yetu. Kwa hiyo, mimi ni maoni yangu kwamba katika Bajeti zinazokuja na hata hii tungeweza tukatoa kila Wilaya ijue ni shilingi ngapi zimekwenda kwa ajili ya kazi hii ili Waheshimiwa Wabunge muwe na haki ya kwenda na kusema mradi huu uko wapi huu uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi naamini kwa kufanya hivyo tutakuwa tunasaidia sana wananchi waweze kujua kama fedha imekuja na miradi ni ipi, vinginevyo tutaendelea kuja hapa kila mwaka tunalalamika. Wale ambao wanazifuja,

hatua zinachukuliwa. Mlimsikia Waziri Mkuu aliienda akatimua watu wote kule Bagamoyo na hili linawezekana mahali popote. Lakini nafikiri hata kabla hujafika hapa, tunaweza tukazuia, maana kuzuia ni bora kuliko kutibu. Mimi naamini Waheshimiwa Wabunge tukishirikiana katika jambo hili tunaweza kuzuia na tunaweza vile vile tukahakikisha kwamba fedha zinazotolewa na Serikali zinawafikia walengwa. Fedha hizi zingine tunapewa na watu wengine wa nchi tu. Tutakuwa watu wa ajabu kusema kweli watu wa nje hawa wanatupa pesa zao halafu wanasema zote zimeliwa na mtu mmoja na yuko tu anaendelea kuishi vizuri bila taabu yoyote. Mimi sidhani kama hii ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegawana majukumu, kuna ngazi ya Taifa, tuna kazi ya kufanya. Tuna ngazi ya Wilaya ndiyo kubwa zaidi na ndiyo yenye fedha zaidi, kuna ngazi ya vijiji ambayo ndiyo yenye miradi inayogharamiwa. Kwa hiyo kila ngazi imepewa kazi chini ya mpango huu wa *ASDP*. Lakini yapo mafanikio vile vile yamepatikana. Rafiki yangu Mheshimiwa Khamis yeye alisema mpango huu hauna maana sana umeshindwa, lakini baadaye akatoka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakumsikiliza Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, angevumilia kidogo tu, nisingejibu, maana Mheshimiwa Dr. Mahenge alikuwa anajibu kwa kumweleza mafanikio, hatua kwa hatua, maghala mangapi, masoko mangapi yamejengwa, majosho mangapi yamejengwa. Haya mambo yote yako kila sehemu, lakini tunahitaji kujiimarisha zaidi. Lakini rafiki yangu Mheshimiwa Khamis simlaumu, najua tumegawana kazi hapa, wengine kazi yetu ni kusimamia mambo yafanyike, wengine kazi yao ni kukosoa tu. Hii kazi ya kukosoa unajua ni rahisi kidogo zaidi kuliko ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana mtu kufanya mambo makubwa, lakini kukosoa unaweza ukaamka tu ukasema hakuna lolote, si umeamka na umesema si basi. Kwa kuwa unalipwa hiyo hakuna tatizo. Maana na wewe umekuwa umetimiza wajibu wako. Hivi kweli bila kusema hivyo ungelipwa kwa nini hasa? Lakini ukweli ni kwamba mpango huu ni mzuri na una matunda yanayoonekana, matatizo yapo, lakini hiki kitu kinafanya kazi vizuri sana ni *source* ya *investment* kwa miradi midogo midogo ya wakulima vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hilo sasa niseme kidogo juu ya vocha, maana nalo limesemwa sana. Mpango wa vocha una historia, ulianzwa na Serikali ya Awamu ya Tatu mwishoni mwaka 2003/2004 ndivyo walivyoanza na ilikuwa makampuni yanapeleka pembejeo mikoani, yanakwenda yanauza yanarudi mikoani na ushahidi kwamba tumeuza. Lakini hakuna *document* inayoonyesha wamemuuzia mkulima gani. Kwa hiyo, wakileta ile *certification* tunalipa maana tumeyatuma yana gharama, mbolea ni yao na kuna gharama ya kusafirisha, wanafika kule. Lakini matatizo yaliyojitokeza ni kwamba manung'uniko yalikuwa ni kwamba mbona mkulima huyu tunayemlenga hapati hiyo mbolea ikawa ni makampuni ndiyo yanayopata faida kwa mfumo ambao kwa kweli huwezi kuthibitisha kama kweli mbolea imemfikia mkulima? Tukasema hapana tujifunze dunia ya wenzetu wanafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaenda Malawi, tukaangalia wanavyofanya mfumo wa vocha tukasema na sisi tunaweza tukaanza vocha, wao walikuwa wanatumia mbolea tu, sisi tukaongeza na mbegu. Sasa Malawi wanataka kuja kujifunza kwetu tumeingizaje mbegu. Maana mambo haya ni kujifunza hakuna mtu aliye na *formula* yake peke yake. Kwa hiyo, tumefanya na utaratibu wetu ni kwamba kunakuwa na Kamati kwenye kijiji, wakati wa awali tuliingiza wote hawa, walikuwa wanasema Mwenyekiti hatumshirikishi, mwanzoni tuliingiza Wenyeviti, lakini Wenyeviti wakaanza kuonekana tutawafunga waishe. Tukasema tuondoe Wenyeviti tuweke Kamati lakini iwe chini ya Serikali ya Kijiji ili Mwenyekiti awe msimamizi wa ile Kamati, ndivyo tulivyofika hapa. Tukaweka Kamati Wilayani na Kamati iko Mkoani ya kuhakikisha kwamba kazi hii inafanyika. Mimi ninaamini hii ni kazi nzuri na imefanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini najua vile vile yapo matatizo, nayakubali na mimi nataka niseme, mahali ambapo usimamizi wa Wilaya umekuwa nzuri matatizo hayakutokea, mafanikio ni dhahiri. Tuna Wilaya nyingi tu za mfano, hata Rombo kwa Mheshimiwa Basil Mramba pale, kuna ushahidi kwamba hakuna fujo iliyotokea na mahindi Rombo ile imetoka kwenye *deficit* ya njaa mwaka jana mpaka sasa inategemea kupata ziada kwa mfumo huo huo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi hii kitu kinafanyika vizuri. Lakini juzi tumepata fursa ya kuzungumza na Wakuu wa Wilaya wote chini ya Uongozi wa Rais na tumekubaliana kwamba jambo hili lazima lisimamiwe na uongozi wa Wilaya na kama makosa madogo madogo haya yadhibitiwe ili mfumo huu uweze kufanya kazi na uzalishaji uongezeke na tumepanua sana mfumo huu. Kuna watu walikuwa wanasema tunapeleka hiyo ruzuku kwa mikoa sita. Hapana, ukisoma kwenye hotuba yetu utaona hata mwaka huu tumeongeza Wilaya katika Mikoa ambayo ilikuwa haifikiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tuliweka Wilaya zaidi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, kwa mfano Shinyanga tuliweka kule Ushirombo katika Wilaya ya Bukombe na mafanikio ni makubwa Bukombe na mimi nataka kumuaahidi rafiki yangu Mheshimiwa Emmanuel Luhahula mwaka huu tutanunua ziada ya mahindi Bukombe kuyapeleka kwenye maghala ya Shinyanga ili Bukombe iwe ndiyo ghala la chakula la Mkoa wa Shinyanga pamoja na sehemu ya Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza, tumepeleka Sengerema na Geita kwa sababu hali ya hewa ni nzuri na mazao yale yanastawi. Kagera tumepeleka Chato pamoja na Karagwe. Tumepeleka katika Wilaya nyingi na mwaka huu tunapeleka katika Wilaya za Kusini, Wilaya chache za Mikoa ya Mtwara na Lindi na Pwani vile vile tutachukua Wilaya mbili na Mkoa wa Tanga. Nia yetu kwa kweli ni kuzalisha chakula kila mahali na kupunguza gharama ya kusafirisha chakula kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Badala yake watu waweze kujizalishia chakula chao pale mahali walipo.

Mimi naamini mpango huu ni mzuri, tuuunge mkono, lakini tuwe na *interest.* Namshukuru Mheshimiwa Said Arfi, alikuwa anasema yeye mwenyewe ni mjumbe wa Kamati ya Pembejeo pale katika Wilaya ya Mpanda na amethibitisha kweli Wilaya ya Mpanda ilifanya vizuri. Madudu yalifanyika tu katika Wilaya ya Sumbawanga. Sasa

mambo haya yote ni matunda ya dhambi sasa huko wamekosea. Lakini mimi ninaamini tutajifunza kule. Lakini nataka niwaambie wale waliokosea kwamba hawezi kuishi salama tu, haiwezekani. Vyombo vya dola vipo na vinaendelea na uchunguzi kule Rukwa na mimi naamini mahali popote ambapo madudu yamefanyika hatua zitachukuliwa. Shabaha yetu ni kufanya kweli ili wananchi wafaidi fedha inayotolewa chini ya mpango huu ambayo tunasaidiana na Benki ya Dunia kwa ajili ya kusaidia kuzalisha chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo linahusu stakabadhi ghalani. Limezungumzwa na Naibu Waziri. Hili kwa kweli ndilo jibu lingine zuri sana ambalo linaweza likawasaidia wakulima. Kwa ufupi hii kazi inafanyika vipi, ni kwamba wakulima wale wakianzisha mfumo wa stakabadhi ghalani wanakuwa na mkataba na benki kwamba mazao yao watayahifadhi katika ghala maalum. Benki inayafanya mazao yale yanakuwa ni mazao yaani ni *collateral* ni dhamana na benki inatoa fedha, inawapa sehemu ya fedha ya matumizi lakini mazao yanabaki ya kwao. Yanakaa pale yanasubiri bei, bei zitakapokuwa nzuri mazao yale yanauzwa, tena yanauzwa kwa mnada na soko likiwa zuri sana bei ikawa nzuri mkulima anafaidi. Kwa hiyo, huu ndiyo mfumo wenyewe. Umefanya kazi kwenye korosho. Ninaamini kwamba watu wa kule Kusini wanaupenda. Ndiyo maana wameamua na ufuta nao uingie kwenye mfumo ule pamoja na kwamba mfumo wenyewe usifikiri kuwa unakubalika kwa urahisi sana.

Mimi tulipouanzisha nilienda Masasi, nikakutana na wakulima wa korosho. Lakini kulikuwa na wanunuzi wa kati ambao hawapendi huo mpango. Kwa kutumia demokrasia yao waliniambia wewe Waziri unapinga soko huria. Mimi nikawaambia mimi nimesoma uchumi, lakini sikukutana na soko huria linalofanana na la kwenu hili la kuibia mkulima mpaka anataka kufariki. *(Makofi)*

Mimi soko huru nililosoma ni la mashindano na kwamba ushindani ule unazaa bei nzuri kwa mwenye mali, ndiyo niliyosoma, lakini la kwao lile ni soko holela. Mkulima wa korosho alikuwa anapata shilingi 300/= sasa hivi tumemtoa kwenye shilingi 300/= anapata mpaka *average* ya shilingi 1,000/=. Hivi hasa tufanyaje, maana hutuwezi kuumba mbingu na nchi, sisi hatuna uwezo huo. Sisi tuna uwezo wa kufanya mambo yakaleta faida. Rafiki yangu Mheshimiwa Khamis huwa tunakutana, anayajua vizuri mambo haya ila kazi yake ndiyo inamlazimisha kusema haya anayoyasema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizi bwana ukipewa inakuwa ngumu sana. Sasa liko suala la bei ya pamba imesemwa na marafiki zangu wawili. Kwanza imesemwa kama kawaida na Mheshimiwa John Cheyo na Mheshimiwa Charles Kajege jirani yangu. Wote wamezungumza bei ya pamba. Mimi najua na mimi natoka kwenye pamba na mimi Mbunge wa wakulima wa pamba, kwa hiyo, ukiondoa kofia yangu ya Uwaziri nabaki Mbunge wa Bunda na nina wajibu wa kuona na wao wanapata hata nikiwa Waziri, maana ni Waziri wa Serikali ya CCM ambayo inatetea maslahi ya wakulima wale wale. Kwa hiyo, ni kofia mbili zenye kazi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bei hatupangi Serikali, nataka wananchi wote wajue hivyo, inapangwa na soko, lakini Serikali sisi ni *referee.* Hakuna mpira unaochezwa bila *referee*. Sisi Serikali kupitia Bodi tunasema hawa wawakutanishe wanunuzi na wauzaji wazungumze waambiwe *figures.* Wanapewa taarifa juu ya hali ya mwenendo wa bei ingawa bei huwa haisimami mahali pamoja inashuka na kupanda. Sasa juzi juzi hapa wamekutana Shinyanga na wakazitazama hizo bei pamoja na gharama za kununua mazao hayo *genuine cost transportation* ya kutoa pamba iliko mpaka kufika bandarini ndiyo wakafikia kwamba shilingi 600/= ziwe ndiyo ya kuanzia. Narudia ni bei ya kuanzia siyo bei ya msimu mzima na kwa sababu soko huria ni la mashindano. Matumaini yangu mimi ni kwamba sasa wataanza kushindana kuanzia tarehe 28 na matumaini yangu ni kwamba bei itapanda zaidi ya shilingi 600/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo ninavyowategemea. Kwa hiyo, nawaomba wanunuzi wote wa pamba waache kufanya makubaliano washindane na kwa sababu uzalishaji umeshuka kidogo mashindano yatakuwa makali. Kwa sababu kila mmoja atataka kupata nyingi zaidi. Kwa hiyo, mimi naamini bei hii itakwenda zaidi ya shilingi 600/= inaweza kufika huko shilingi 700/= alikokuwa anasema Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niyaseme hayo mambo makubwa tu ambayo yamesemwa. Baada ya maelezo hayo sasa nitapitia pitia kidogo kwa sababu mpaka hapo utakapopiga kengele. Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, imetoa mawazo mazuri sana; wala sina haja ya kuyarudia kwa sababu wao ndio huwa tunashauriana na mawazo ambayo wameyatoa hapa yamesomwa na Mheshimiwa Kidawa Khamis Salehe, ni mawazo mazuri kabisa na sisi tunayachukua. Muundo wa utumishi wa watafiti unashughulikiwa, wakulima wanaopata pembejeo na ruzuku tuwaongeze; kila mwaka tunawaongeza, haya ndio masuala yaliyosemwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya mbolea vijengwe; jambo hili tunalishughulikia na tunataka kuona kwamba kweli vinajengwa. Mbolea inayoagizwa nchini isiwe kwenye mifuko ili kupunguza gharama; tunakubali, tumekaribisha mmoja wa wazalishaji wakubwa wa mbolea, tumempa eneo pale bandarini ajenge mfumo ambao utakuwa unaleta mbolea na kuiweka kwenye vipimo palepale na wataanza hiyo kazi hivi karibuni. Tuache kutegemea mbegu za kuagiza; nakubaliana kabisa na Kamati na maelezo mengine mazuri sana ambayo wameyasema.

Kambi ya Upinzani na yenyewe imetoa mawazo; tutayafanyia kazi baadhi ya mawazo ambayo wameyatoa, lakini vile vijembe tu ndivyo ambavyo sivikubali, ni lazima niiambie hii Kambi kwamba vile vijembe vya kusema CCM imeshindwa sasa wao ndio waje, kwa kweli hii ni ndoto ya mchana; kwa sababu hawatatushinda hata wafanyeje na kauli mbiu yetu ni kwamba ushindi 2010, ni lazima. Hilo ndilo jibu la hayo yote uliyoyasema. Mambo haya yamejibiwa kwa vitendo na kwa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani marafiki zangu wa Upinzani wamesikia na ninamshukuru sana Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, amenisaidia katika kujibu

yale mengine mengi ambayo yamesemwa na pamoja na kukueleza ndugu yangu wa Bugaga kule Kigoma, ambaye alitaka kujua *specifically* tunafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia kule kwenye shamba letu la mbegu, mwaka huu tunaanza na shilingi milioni 50 za kupima. Tunataka lile shamba lipimwe, liwekewe mipaka ili lipate hati, kwa sababu siku hizi bila hati watu wanaingia tu. Kwa hiyo, tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kuuza mazao nchi za nje ambayo yamesemwa na watu wengi; mimi nadhani hili tumeshalieleza vya kutosha. Ninachotaka kusema ni kwamba sisi ni Bunge la Jamhuri ya Muungano na Serikali ni ya watu hawa, kwa hiyo, ina pande mbili. Watu wakikosa chakula wanaiuliza Serikali chakula kiko wapi na wana haki ya kuuliza. Rombo walipokosa chakula, tuliwapelekea, walipokosa Longido, tuliwapelekea, Dodoma tumewapelekea na maeneo mengi kabisa. Wakati ule wale tuliokuwa tunawapelekea hawakusema mbona hamuwaruhusu kuuza nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa tatizo lao, ilikuwa ni kupata chakula, moja ya *responsibility* ya Serikali. Sasa sisi hatuzuiwi kuuza nje na wala hatuna sera ya kuzuia; mwaka huu tunazalisha tani milioni 7.7 za nafaka. Ukipiga mahitaji yote, tuna ziada ya kama tani laki nne hivi au nusu milioni. Kwa hiyo, tunawaambia wale wanaotaka kuuza nje, karibuni lakini mfuate utaratibu. Maana hakuna nchi ambayo watu wote wanauza, halafu anasema wakulima mnawazuia, bwana wee! Wakulima hawa tunawasingizia! Mkulima mdogo wa jembe la mkono hauzi mazao yake popote, anauza kwa mfanyabiashara na mfanyabiashara ndiye anayeuza nje. Sasa hilo nalo wala sio jambo baya kwa sababu ni amri ya biashara ya dunia. Kwa sababu kila mtu hawezi kwenda Kenya na wala kila mtu hawezi kwenda Zambia. Lakini tunataka kuwa na utaratibu ambao unamwezesha mkulima huyu kupata bei nzuri hata kwa huyu anayepeleka huko nje na wala tusidhani kwamba nje ndio *solution.* Maana juzi tuliruhusu watu wa Shinyanga wapeleke mpunga Kenya, tukawapa na vibali. Wakaenda Kenya wakakuta bei imeshuka, wakasema bei imeshuka; nikasema uzeni Tandale, maana soko ni soko na wala sio lazima liwe la nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani hili nalo tunakwenda nalo hivyo hivyo. Tunaruhusu wakati kuna ziada lakini wakati hakuna chakula kwa kweli Serikali ni lazima iwe na wajibu wa kuhakikisha kwamba chakula kinabaki nchini na watu wanakula. Kwa hiyo, wala lisionekane kama ni sera ya kukandamiza wakulima. Wakulima wale wale wakikosa chakula wanaiuliza Serikali, wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tarafa moja kule Tanga iliuza chakula chote Kenya, halafu ikatuambia sisi hatuna chakula; tukasema kimekwenda wapi? Wakasema tumekiuza chote Kenya kwa bahati mbaya. Sasa tungefanyaje, maana kulikuwa na mawili au tuwaache waone makosa ya kuuza nje au tuwape ili wajifunze na safari nyingine waweke akiba. Kwa hiyo, ni mambo ya namna hiyo, tunakwenda nayo taratibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sina uwezo wa kujibu hoja zote; uwezo ninao, ila muda tu ndio sina. Ungenipa muda hata wa saa mbili hivi, ningejibu kila kitu hapa, lakini sasa hili Bunge litalala hapa; kwa hiyo, kwa sababu muda hautoshi, nadhani sasa nikubali kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge, kwa michango mizuri. Mimi nataka kusema buku lote hili lina mawazo na hii hapa inaonekana kwamba Bunge hili lina utajiri mkubwa wa mawazo na sisi tuko tayari kuyasikiliza, tuko tayari kuyafanyia kazi ili tuweze kuleta mabadiliko katika nchi yetu. Labda niseme tu kwamba Kilimo Kwanza, tuko *serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tumei-*quote*, rafiki yangu Hamisi alikuwa anam-*quote* Gandhi Neru, lakini mimi nina kitabu hapa cha Kilimo Kwanza, kinam-*quote* Mwalimu. Sijui ni kwa nini hukum-*quote* Mwalimu, wewe unam-*quote* Neru tu, maana hata hapa kuna Neru wa hapa. Baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa majibu mazuri sana kwa hoja zilizo nyingi za Waheshimiwa Wabunge na hasa kwa kusisitiza ule msemo wa Chama cha Mapinduzi wa mwaka huu, kwamba 2010 ushindi.

**WABUNGE FULANI:** Ni lazima.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 43 – Wizara Ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Kifungu 1001 – *Administration and General* ……shs. 2,174,823,200/=

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina maswaia mawili madogo ya ufafanuzi.

La kwanza ni kwamba, nimeshangazwa kidogo na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu Chuo cha Kilimo cha Mbondo; kwamba Wizara iliyosheheni wataalamu kama hawa inahitaji miaka miwili, sio kufanya tathmini. Hilo jibu limenishtua na bila ya shaka watu wa Kasulu wameshtuka pia kwamba Wizara iliyosheheni wataalamu kama hawa, yenye Waziri mzoefu kama huyu, inahitaji miaka miwili kufanya eti tathmini kwa ajili ya kuanza kutumia Chuo cha Kilimo cha Mbondo. Nilikuwa nafikiri ni vizuri ningepata ufafanuzi juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la pili dogo, nadhani Kanuni zinaniruhusu, nishukuru hili dogo la shilingi milioni 50 kwa ajili ya shamba la kilimo cha Bugaga. Lakini nimkumbushe Mheshimiwa Waziri na timu yake kwamba hilo shamba sio kwamba halipo, lipo linaendelea; mimi nilidhani hiyo milioni 50 kwa ajili ya upimaji ni sawasawa, lakini liko suala kwamba kuna shughuli zinaendelea pale kwa kusuasua. Wana magari mabovu, wana nyumba ambazo ni karibu zinawaangukia, nilidhani kwa sababu ni kitu ambacho kinaendelea, nilikuwa naamini kabisa bila kutia mashaka kwamba kulikuwa na aina ya fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu iliyoko katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mimi nilitembelea Mkoa wa Kigoma na vilevile nilitembelea chuo ambacho Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko anazungumza na hicho chuo kilikuwa ni cha Wizara ya Kilimo huko nyuma, lakini kilibadilishwa na kuwa *Secondary School,* na wakati natembelea pale walikuwepo wanafunzi wanasoma. Wapo wanafunzi wa kawaida wa sekondari wanasoma pale, sio wanafunzi kwa maana ya kuwa ni Maofisa wa Ugani wa baadaye, ila wanasoma lakini vilevile masomo ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mkoa ulishauri ya kwamba kile chuo kirudishwe Wizara ya Kilimo, kimsingi mimi nilikubali, lakini Chuo hicho kimekaa nje ya Wizara kwa muda mrefu. Kwa hiyo, hatua ambazo tumezichukua ni kwamba kwa mwaka huu wa fedha tufanye tathmini, kwa sababu vile vile ni suala la Bajeti maana huwezi kukichukua tu mwaka mmoja ukafungua, wakati pengine huna pesa za kugharimia za kutosha; kwa hiyo, tunafanya tathmini lakini tunamuahidi ya kwamba katika Bajeti inayofuata baada ya hiyo tathmini ya miundombinu na kuona ni gharama kiasi gani zitatuwezesha kutengeneza, basi tutaingiza katika Bajeti ya mwaka unaofuata ili tuweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi wenyewe tunahitaji chuo kile, kwa sababu tunahitaji vyuo vya kufundisha maafisa ugani. Kama mnavyojua, tuna mpango wa kufundisha wengi tu na tunataka ifikapo mwaka 2012/2013 tuwe na Afisa Ugani katika kila kijiji na kila kata. Kwa hiyo, tunakubali tutachukua wajibu wetu kwa hiki chuo, lakini namuomba Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, atupe nafasi tufanye jambo hili. Tumeshafanya uamuzi ambao ulikuwa haujafanyika wa kukichukua, sasa tumefanya. Kwa hiyo, sasa atupe nafasi ili tuweze kutazama uwezekano wa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shamba la Bugaga, pale kuna shughuli za Wizara zinaendelea. Lakini tunayo mashamba mengi ya namna hiyo hapa nchini, lakini uwezo wetu wa kuyahudumia yote mara moja, sio mkubwa. Tunalo moja kule Mbozi ambalo tumelichukua lilikuwa ni la *NAFCO*, tunalo lingine Kilolo, tuna mashamba mawili Kilosa, tuna shamba lingine Arusha na kwa muda mrefu sana mashamba haya yalikuwa yameachwa; kwa mfano ukienda lile la Kilolo, ni pori kabisa. Lakini tunachotaka kufanya ni kwamba mashamba haya tuyaimarishe na kuyaimarisha ni

pamoja na kuyawekea miundombinu ya umwagiliaji maji ili yaweze kutumika kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu na miundombinu hii ni ya gharama, kwa hiyo, ndhani na hii nayo atupe nafasi tuende hatua kwa hatua, kwa maana mashamba hayo ni mengi na uwezo wetu wa kufanya yote kwa mara moja ni mdogo. Tunaanza na mashamba machache, halafu tunaongeza kila mwaka. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 43*, programu namba 10, *sub-vote 1001*, Kifungu 210100, sitaki kusema mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri nina imani kubwa sana tuliyonayo wananchi wa Mbozi kwake. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze wazi au atupe ufafanuzi baada ya maelezo yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 tulitoa malalamiko ya wananchi wa Mbozi kuhusu wizi wa vocha za ruzuku ya mbolea katika wilaya yetu na hususan katika kata za Chilulumo na Chitete katika Jimbo la Mbozi Magharibi, lakini tukaambiwa kwamba hakukuwepo na wizi wowote, kana kwamba hiyo haitoshi, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, tulitoa tena taarifa juu ya kutofikishwa kwa mifuko 100 ya mbolea ya ruzuku kwa kila kata katika kata hizo 26 pamoja na upotevu wa vocha za kutowafikia wananchi katika kata hizo. Je, Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Siyame, bahati mbaya sana nakupa nusu dakika umalizie.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa nataka kumalizia kwa kusema kwamba katika vijiji vyote hivi pamoja na kwamba baadhi ya vocha zilichukuliwa mpaka Mahakamani. Je, ni hatua gani sasa ambayo Wizara itachukua maana hata huko Mahakamani vocha hizo zimepotea?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa anazozisema ni kweli ziliwahi kusemwa hapa hapa Bungeni na tukaahidi kufanya uchunguzi; tukafanya lakini hakuna jawabu la maana ambalo tulilipata. Kwa sababu kama nilivyosema katika kujibu hoja, masuala haya yanapofanyika katika ngazi ya wilaya, ufanisi mkubwa zaidi unapatikana kama usimamizi wa wilaya ni mzuri. Wizara tuko mbali kidogo kuweza kujua ni nini kimefanyika katika kijiji gani. Kwa hiyo, suala hili tulilichunguza kupitia mamlaka zilizoko kule, lakini hakuna tulichokipata kwa ile ya kwanza aliyoisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ya pili ya vocha 3,000 anazosema zilipotea, tuliwasiliana na Mkuu wa Mkoa na kwa kweli sisi tulichukua hatua kwanza ili kuondoa wizi usitokee, tulifuta. Tuliziwasilisha zile namba zote za vocha kwenye benki ili kuhakikisha hazilipwi, kwa hiyo, kilichoibiwa ni karatasi sio pesa na benki ilisitisha malipo. Lakini watu wale walichukuliwa wakapelekwa Mahakamani, kwa sababu walikuwa wameonesha nia ya kutaka kuiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mahakama ikifika kule, Mamlaka yangu yanaishia hapo. Kwa sababu sasa inabidi wao wapate ushahidi na watoe hukumu kama

wanavyoona inafaa na Mahakamani kuna watu huwa wanashinda na wengine wanashindwa na kila mara wanaoshindwa huwa wanabaki wanalalamika, ndio maisha. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametokea kuzungumza akijibu hoja za masuala mbalimbali likiwemo pamoja na lile la soko huria la mazao. Hivi karibuni kule Mbozi nadhani na wilaya ya Mbinga ambako tunalima sana kahawa, kumetokea mkanganyiko mkubwa miongoni mwa wafanyabiashara na wakulima wa kahawa. Kuna wafanyabisahara ambao walikuwa wananunua kahawa ile mbichi (cheli), wakikoboa wao wenyewe. Lakini hivi karibuni ikatolewa taarifa na Mamlaka ya Bodi, ambayo viongozi wake Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi Mkuu Kumburu, walitembelea Mbozi, wakasema kwamba si ruksa kununua cheli, lakini walipokwenda Mbinga wakasema ruksa kununua cheli. Sasa wananchi hawa wakulima wa kahawa wakapata mkanganyiko mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni nini hasa kinachopaswa kifuatwe, ili wananchi wale wasiendelee kupata maelezo ya upande huu na kesho wanapata maelezo ya upande huu. Ahsante sana.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mkanganyiko analolizungumzia Mheshimiwa Zambi, ndio ninalisikia hapa. Lakini kama kweli Bodi imetoa maelekezo, Bodi ina wajibu wa kusimamia, ku-*regulate* zao la kahawa. Lakini katika ku-*regulate* inatakiwa iwe ina-*regulate* kwa kutumia Kanuni ambazo zina *apply* mahali pote. Sasa kama imetokea bodi ikasema Mbozi jambo lingine na ikasema Mbinga jambo lingine, namuomba Mheshimiwa Zambi atuachie tuwaulize kitu gani kilichotokea na kama tutaelewa vizuri tutatoa maelezo ambayo yatakuwa yanahusu zao mahali popote lilipo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*... .. .... .... .... sh.1,112,257,200/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* … … … … … sh.1,259,210,050/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 - *Agriculture Training Institute* … … sh. 4,874,807,700/=

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1004 programu hiyo lakini kifungu kidogo 230200 *Routine Maintenance and Repair of Buildings* zinaomba shilingi 12,000,000/= *issue topic* hapa inasema *Agricultural Training Institute* kwanza *institute* hizi ziko nyingi, sasa ningependa ufafanuzi wana *refer* kwenye *institute* ipi, *specifically* vilevile katika mchango wangu nilielezea kuhusu *Tumbi*

*Training Institute Agricultural Training Institute* hali yake si nzuri, shilingi milioni 12 tutafanyia nini jamani naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo; kusema kweli hizi fedha shilingi 12,000,000/= ni kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na majengo mbalimbali kule kwenye vyuo vya kilimo, ukarabati huo ni ule ukarabati mdogo sio ukarabati mkubwa kwa maana ya kujenga madarasa ama kujenga maabara ni ukarabati ule mdogo mdogo na nyufa na njia za kupitia na maeneo yanayovuja vuja, *maintenance*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*… … … … … … … sh.217,100,000/=
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*… sh. 366,250,000/=
Kifungu 1007 - *Information, Education and Communication*… … … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...sh. 300,000,000/=
Kifungu 1008 - *Legal Unit* … … … … … … … … … …sh. 258,750,000/=
Kifungu 1009 - *Management Information System Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... … … … … …sh. 211,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1010 - *Environmental Management Unit*...sh. 216,590,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilielezea kuhusiana na suala la makampuni yanayonunua tumbaku…

**MWENYEKITI:** Uko wapi?

**MHE. MAGDALENDA H. SAKAYA:** Samahani *sub-vote 1010,* kifungu kidogo 221300, nilipokuwa nachangia kwa maandishi nilielezea makampuni yanayonunua tumbaku mkoa wa Tabora yanatakiwa yashiriki katika kuhakikisha kwamba yanalinda mazingira na kwa utaratibu wanazofanya sasa hivi ni kwamba makampuni yanatoa mche mmoja wa mti katika mfuko wa mbolea lakini hakuna ufuatiliaji wowote unaofanyika kuona kwamba miche hii inakwenda kupandwa.

Kwa hiyo, unakuta kwamba mkulima akishachukua ile miche wakifika tu nje ya geti wanaitupa yote kwa hiyo, mazingira yanaendelea kuharibika huku miti inachomwa hakuna chochote kinachofanyika na Wizara ya Kilimo kuona kwamba ile miti inayochomwa kwa ajili ya kuchoma tumbaku inakuwa *replaced* na miche mipya, naomba maelezo kuhusiana na hilo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki alichokitaja Mheshimiwa Mbunge 221300, kinahusu gharama za majarida, vitabu na magazeti na vifaa mbalimbali vya mafunzo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Crop Development*…… … … …sh.104,256,593,600/=

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki naomba ufafanuzi kwenye *sub-vote 221500, Agricultural and Livestock Supplies and Services,* kwanza ufafanuzi wa kwanza ni kuhusu *title*, tunazungumzia Wizara ya Kilimo, sasa *Agricultural and Livestock Supplies* inanitatanisha. Halafu pili kinahusu nini hasa kifungu hiki?

**NAIBU WAZIRI KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kimeongezeka kutokana na ongezeko la wakulima watakaonufaika na ruzuku kutoka wakulima 1,500,000 kufikia wakulima 2,000,000 kwa maana ya mwaka huu wa 2010/2011 watapatiwa wakulimia 2,000,000 ruzuku pamoja na viuatilifu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Siraju Kaboyonga mara ya kwanza sikukubalia kwa sababu tulishakubaliana kwamba tunasimama mara moja tu, ahsante ni suala la utaratibu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 270500, Current Grant to Non-Financial Public Units such as Boards*, kwa mfano bodi ya pamba, kwanza nataka kutumia nafasi hii ili kujaribu kumshawishi Mheshimiwa Waziri afikirie ni jinsi watakavyooanisha watu ambao wanalima kwa ajili ya biashara kama chakula na *rules and regulations* kama za Waziri kusema msiuze hata kwa masoko ya nje, kwa sababu hili ni jambo ambalo ni la maana, hatuwezi tu tukaendelea kusema kwamba njoo ulime halafu useme aah, kama tuna njaa tutaamua unauza wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa nilitaka kusisitiza moja tu Mheshimiwa Waziri umesema kwamba ungependa tupate mbegu bora za pamba na umesema idadi kama ya tani 10,000 je, kuna mpango gani wa bodi ya pamba kuhakikisha kwamba tunapata mbegu ambazo ziko bora? Kuna mwekezaji yeyote ambaye labda atalima mashamba kadhaa na kuhakikisha kwamba tunarudi tena kama zamani *AR I, AR II* na *AR III?* Nimeshamaliza.

**MWENYEKITI:** Sijakusikia tuweke vizuri mambo haya, sasa hivi tusiingie sana kwenye masuala ya sera hapa sasa ni hatua ya ufafanuzi kwa jambo ambalo Mheshimiwa unaona kama halijakaa sawa sawa ili uweze kujua fungu hilo lina madhumuni gani tupo kwenye mambo ambayo ni *very specific* hivi sasa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa John

Cheyo nilivyomuelewa hapa alikuwa anazungumzia kwamba mwaka jana fedha zilikuwa shilingi bilioni nane, mwaka huu zimeshuka zimekuwa shilingi bilioni 7.9. Kusema kweli fedha hizi zimepungua kutokana na ufinyu wa Bajeti, hakuna lingine na hakuna sababu nyingine, ni kutokana na ufinyu wa Bajeti kwamba lazima tupunguze na kuongeza hapa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Hajanielewa kabisa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni la ufafanuzi tu ni *sub-vote* hiyo 2001 lakini *sub-vote 220100 Office and General Supplies and Services*, ukiangalia mwaka 2008/2009 zilitengwa shilingi 34,000,000/=, mwaka 2009/2010 zilitengwa shilingi 71,000,000/=, lakini mwaka 2010/2011 zimetengwa shilingi 1,227,852,400/= sasa hii *jump* imekuwa kubwa sana na ukiangalia *vote* yenyewe inahusu mambo kama ya manunuzi vile na huduma nyinginezo. Sasa kutoka shilingi 71,000,000/= mpaka shilingi bilioni moja, ningeomba Waziri pengine atoe maelezo ni vitu gani hasa ambavyo vimesababisha gharama kuwa kubwa hivyo.

**MWENYEKITI**: *Sub-vote* ni 220100 *Office and General Supplies and Services*, shilingi 34,090,266/= mwaka juzi shilingi 71,100,000/= mwaka huu shilingi 1,227,852,400/=, naomba ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa bei za vifaa na huduma mbalimbali ndiyo maana zimeongeza kutoka shilingi milioni 71 kufikia shilingi bilioni moja zaidi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Agricultural Mechanization*… … … .sh. 674,487,200/=
Kifungu 2003 - *Agriculture Land Use Planning and Management*… ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...sh. 316,300,000/=
Kifungu 2004 - *Plant Breeders' Unit* … … … … … … sh. 196,120,000/=
Kifungu 3001 - *Research Development* … … … sh. 13,519,145,300/=
Kifungu 4001 - *Cooperative Development* ... … … … ... … … sh. 0/=
Kifungu 5001 - *National Food Security*.….. … … sh. 19,449,208,750/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Kifungu 1001 - *Administration and General* … …  sh. 293,288,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning*… … … …… …sh. 4,189,926,000/=

**MWENYEKITI:** Hiyo ni *ASDP*.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni suala dogo tu la ufafanuzi. Mkoa wa Kigoma na wilaya za Kasulu, Kibondo na Kigoma sisi ni *recipient* wa fedha za *DADSP* sasa ukiangalia pale kwenye *sub vote* 1003 unaona kuna fedha za *DADSP* na kwenye malengo ya hotuba ya Waziri ukurasa wa 72 Mheshimiwa Waziri kama unazungumzia juu ya *development* ya *cooperative*s lakini kwenye *item* ya *cooperative* kuna *zero*, hakuna fedha mwaka huu sasa nataka kujua hiyo *link* maana yake ni nini ili tu nielewe maana ni vizuri Mbunge nikaelewa vizuri Mbunge nikaelewa vizuri je, ni hizi hela za *DADSP* zitakuwa *rolled over* kwenye *cooperative development* kwenye maeneo ya *DADSP* kwa sababu kwenye *development fund* ya *cooperative* kuna *zero* nilitaka kujua hiyo *link*, sasa naomba ufafanuzi tu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *vote 24* ambayo ni ya Kamishina wa *Cooperatives* ambayo tunaweza tukaipitia lakini ilikuwa wakati ule tunatoa kwenye Idara ya *Cooperative* sasa ina *sub-vote* yake inaitwa 24 ambayo inaitwa *Commissioner* ya *Cooperatives*. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 - *Agriculture Training Institute* … … sh. 1,100,000,000/=
Kifungu 1007 - *Information, Education and Communication*… … … … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...sh. 0/=
Kifungu 1009 - *Management Information System Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...sh. 80,000,000/=
Kifungu 1010 - *Environmental Mgt. Unit*… ... ... ... ...sh. 355,500,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Crop Development* … … … … sh. 84,861,485,000/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho cha *vote 2001*, nataka nisimame kwenye *sub-vote* 4486 *Agriculture Sector Development Program* nikitegemea kwamba kilimo cha chai hapa kama *crop* bila shaka ndiyo kinahusika kama ndivyo nilikuwa nimeandika kwenye maelezo yangu nilichangia kwamba sisi Ludewa tumeanza mwaka 2007 kilimo cha chai na tumefanya vizuri sana na mpaka wa pili kijiji chetu kimoja kikapata kitalu bora Kitaifa na tuliweza kuanza na vitalu 30 na sasa tumeshafika kupanda mashamba yenye ekari 100 na tuliambiwa

kwamba tunatakiwa tufikishe ekari mia tano ili tuweze kupata kiwanda, swali langu lilikuwa tunajua inachukua muda mrefu kupata wawekezaji wa kujenga kiwanda, uzoefu wa Kilolo umeonyesha, hivyo inahitaji kuanza mapema sana kutafuta wawekezaji wa kujenga kiwanda cha chai, tunaamini ifikapo mwaka 2012 tutakuwa tumefikisha ekari hizo zinazotakiwa 500, Serikali inatusaidiaje, tulitaka ufafanuzi mtatusaidiaje kuanza kutafuta wawekezaji wa kujenga kiwanda cha chai Ludewa?

**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli unapoanza kilimo cha chai lazima wakati huo huo uanze kufikiria kupata kiwanda sasa inachukua muda kadhaa hivi chai ile inaanza kutoa majani na majani yale yanatakiwa yanapovunwa yafikishwe kiwandani katika muda mfupi inavyowezekana. Ni kweli tunayo *experience* ya Kilolo na kwa hiyo, tunachojaribu kushauri hivi sasa ni kwamba wakulima wa chai na hasa kwa kweli wakulima wadogo wangeanza wakati huo wanapoanza kupanda chai waanze kuunda umoja wenye nguvu halafu baada ya hapo waanze kutafuta namna wanavyoweza kupata mikopo. Kilolo sasa hivi wana *process* mikopo kutoka *TID* kwa ajili ya kununua mitambo ambayo inaweza kufungwa kwenye kiwanda chao kwa sababu kilimo ni biashara na hawa wakulima wadogo wakiunga wanaweza wakapata vilevile mkopo wakajenga kiwanda chao kuliko kutegemea mwekezaji wa nje, akija mwekezaji wa nje sawa, lakini mahali ambapo hayupo mimi nadhani wakulima wanaweza wakawa wawekezaji wenyewe. Kule Kenya wakulima wadogo ndiyo wenye viwanda hata sisi tunaweza kuiga mfano wao. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Agricultural Mechanization* … … … sh. 497,850,000/=

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi kwenye kifungu hiki kuhusiana na *Indian credit* ya *40 million dollars* kwa ajili ya kununua matrekta, hapa pesa mlizoweka hazilingani na kwamba kuna ziada ya *40 million dollars* kutoka India kwa ajili ya *mechanization acquisition of tractors.* Naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHURIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko kwenye *sub vote* ipi kwa sababu hapa ni kifungu 2002. Sawa nimemwelewa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu miradi ya kuongeza thamani kwa mfano *Agro Processing* viwanda vidogo vidogo, kwa hiyo, ndiyo hiyo imetengewa shilingi milioni 497.

**MWENYEKITI:** Lakini sasa kuhusu hiyo pesa kutoka India kuna maelezo yoyote?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHURIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo pesa dola milioni 41 bado mchakato unaendelea na haujakamilika. Kuhusiana na yale matrekta ambayo yalikuwa yaagizwe kutoka India kwa mkopo kutoka *Exim Bank*, bado mchakato unaendelea kati ya Wizara ya Fedha na wadau wengine wanaohusika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *Administration and General*.................................sh. 0/=
Kifungu 3001 - *Research Development*..............sh. 11,351,242,000/=

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *sub-vote 3001* Kifungu kidogo zaidi ya 4458 *Stabex Coffee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma tulikuwa tunapata pesa hasa yale maeneo yanayolima Kahawa yalikuwa yanapata pesa ambazo zilikuwa zinasaidia sana katika kuendeleza miundombinu ya maeneo haya yanayolima Kahawa. Pia yalitusaidia sisi kujenga barabara kwa mfano ya kutoka njia panda ya Ruanda kwenda Idiwiri mpaka Nyimbiri, barabara hiyo ni nzuri na inapitika vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona fungu hili linakuwa halitengewi fedha je, Serikali pamoja na kwamba inawezekana wafadhili walikuwa wanatusaidia, kwa nini Serikali isiendeleze utaratibu huu wa kutenga fedha kwa maeneo yale yanayolima zao la Kahawa nchini kote ili maeneo hayo yaweze kufaidika na kwa maana hiyo usafirishaji wa zao la Kahawa uwe ni rahisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHURIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kusema kweli wafadhili hawakuahidi kutoa fedha katika mradi huu, lakini pia muda wake ulishakwisha. Sasa kwa sababu tuna *ASDP* ambayo ndiyo *umbrella* ya kutekeleza maendeleo yote ya kilimo kwa sasa yaani katika kutekeleza Kilimo Kwanza, namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba tuweze kuibua miradi hiyo kupitia programu ya *ASDP*.

.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 - *Cooperatives Development*..…………………….sh. 0/=

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Nsanzugwanko!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *unless* nimepotea ukurasa, lakini ninachozungumza ni hivi ile fedha ya *DADSP* ambayo nilikuwa nimeizungumzia Waziri amesema kwamba itaingizwa kwenye *commission* ya *cooperatives*. Sasa mimi hapa kwenye *development* siioni na kwenye hotuba yake *item*

*number* mbili ya kazi za Fedha za *DADPS* moja ya kazi hizo ni *promotion* ya *SACCOS* kwenye maeneo yanayohudumiwa na mfuko wa *DSP*…

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Baada ya kumaliza kwenye kitabu hiki hiki fungu 24 utakuta hiyo *Commission* ya Maendeleo ya Ushirika, ukurasa wa 21.

Kifungu 5001 - *National Food Security* ………….sh. 1,223,080,000/=
Kifungu 4002 - *Cooperative Micro*
*Finance Section*...............................................................sh. 48,400,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4005 - *Registration Service Section* ……….sh. 51,600,000/=

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo langu nataka tuelewane vizuri kwa sababu hizi fedha za *DADPS* zina matatizo kwenye maeneo ambayo sisi tunatekeleza miradi hii.

Nataka niwe *very clear DADPS* kwenye ile kasma ya *development* ambayo kuna *1.5 billion* kule tulikotoka ambako nilipotea kidogo katika ukurasa ule. Nataka niwe *clear* je, yale maeneo ambayo yanatekeleza mradi wa *DADPS* ikiwemo Kasulu, maana ukiangalia hapa hela ni kidogo sana iliyotengwa je, zile fedha kwa ajili ya *promotion na training* kwa ajili ya *SACCOS* kama ilivyoanishwa ukurasa wa 72 kwenye mfuko wa *DADPS* nataka tuwe *clear* na kwa nini hazikuwa *very clear* kwa *commission* ya *cooperatives*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama nimeeleweka.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHURIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko anachanganya hivi vifungu, hapa tuna *DADPS, DADPS* ina kazi zake na inafanya kazi na shughuli nyingi tu mojawapo ni ku-*promote* na ku-*invest* katika *agriculture* kama ilivyo *ASDP* ambayo nimeieleza. Lakini katika *investment* kwenye *agriculture SACCOS* ni *aspect* mojawapo ya kazi za *DADPS* lakini *commission* ndiyo yenyewe hasa inayosimamia ushirika *in general.* Sasa tusichanganye vitu viwili, hii *DADPS* ina ka-*element* kadogo ka-*SACCOS* kama *part* ya *promotion* ya *agriculture development* katika Wilaya 28 za Mikoa za Ziwa, lakini hii *commission* ndiyo imepewa kazi ya kusimamia *policy* zote zinazohusiana na mambo ya ushirika, *training na promotion.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FEDHA ZA KAWAIDA**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management Unit* …….............................................sh. 1,185,361,500/=
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit* ………….sh. 46,140,000/=
Kifungu 1003 - *Planning Monitoring and Evaluation Unit*……………...............................................sh. 92,656,800/=
Kifungu 1005 - *Legal Service Unit*...……………………sh. 57,350,000/=
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*…..sh. 43,770,000/=
Kifungu 1007 - *Management Information Unit*…...sh. 199,973,200/=
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*……………………..sh. 30,671,500/=
Kifungu 4001 - *Promotion Services Section* ………sh. 474,540,000/=

**MWENYEKITI:** Naona sasa Mheshimiwa Nsanzugwanko unayaona sasa.

Kifungu 4002 - *Cooperative Micro Finance Section*....................................................................sh. 303,502,000/=
Kifungu 4003 - *Cooperate Banking and Investment Section*………....................................................................sh. 286,230,000/=
Kifungu 4004 - *Cooperate Marketing and Inforamation Section*………..........................................sh. 283,110,000/=
Kifungu 4005 - *Registration Service Section*……..sh. 171,395,000/=
Kifungu 4006 - *Inspection and Supervision Services Section*………........................................…sh. 3,389,866,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kifungu kwa kifungu na kuikubali bila marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa jinsi hiyo naomba kutangaza rasmi kwamba Bunge limeidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2010/2011. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika zote na muda wetu unakaribia kabisa kuisha, kwa kuwa hakuna shughuli nyingine ya ziada mezani hapa nachukua fursa hii kuwapongeza sana na kwa ushirikiano mkubwa ambao tumekuwa nao katika kushughulikia Bajeti hii ya Wizara muhimu sana ya Kilimo, Chakula na Ushirika, tunawatakia kila la heri Wizara hii ambayo ndiyo tunaitegemea kabisa kwa uhai wa Taifa letu kwamba watatumia mafungu haya vizuri kabisa na matokeo yatakuwa mazuri kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Nachukua fursa hii basi kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.34 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 23 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*